

5 FEBRUARI, 2015
BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Tisa – Tarehe 5 Februari, 2015

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, leo sijamwona. Kwa hiyo tunaendelea na Maswali kwa Waziri Mkuu na atakayeanza ni Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vipindi tofauti vya Bunge Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Mussa Zungu na hata Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu wamekuwa wakiuliza swali kuhusiana na manyanyaso wanayoyapata wafanyabiashara Wadogo Wadogo pamoja na Mamalishe.

Kwa kipindi hicho chote umekuwa ukitoa maagizo na maelekezo, inavyoonekana mamlaka zinazosimamia hili jambo haziko tayari kutii amri yako.

5 FEBRUARI, 2015

Je, unawaambia nini Watanzania na Bunge hili kwa ujumla?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Murtaza Mangungu swali lake kama ifuatavyo:-

Suala hili la vijana wetu ambao tunawajua kama Wamachinga, kwanza nataka nikiri kwamba ni suala kubwa na ni tatizo kubwa na si la Jiji la Dar es Salaam tu, bali lipo karibu katika miji mingi. Kwa hiyo, ni jambo ambalo lazima twende nalo kwa kiwango ambacho tutakuwa na uhakika kwamba tunalipatia ufumbuzi wa kudumu.

Kwa hiyo, ni kweli kwamba mara kadhaa kuna maelekezo yametolewa yakatekelezwa sehemu na sehemu nyingine hayakutekelezwa kikamilifu kulingana na mazingira ya jambo lenyewe lilivyo.

Lakini dhamira ya kutaka kumaliza tatizo hili la Wamachinga bado ipo palepale na kwa bahati nzuri umeuliza wakati mzuri kwa sababu jana tu nimepata taarifa ambayo nimeandikiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ambayo wanaleta mapendekezo kwangu juu ya utaratibu ambao wanafikiri unaweza ukatatua tatizo hili ambalo lipo sehemu nyingi.

Nililoliona katika taarifa yao ni kwamba wao wamependekeza kwamba wataunda kakikosi kazi hivi ka kiofisi, kikosi hicho kitafanya kazi kupitia viongozi wa makundi mbalimbali ya Wamachinga hapa nchini, watakuwa wanakaa nao, wanakubaliana nao juu ya maeneo ambayo wanaona ni vema yakatumika kwa madhumuni hayo.

Watakubaliana vilevile juu ya muda muafaka wa kufanya hizo shughuli. Kikubwa nilichokiona katika maeleo yao wametaka sana suala la usafi katika maeneo ambayo shughuli zitaendeshwa lipewe kipaumbele.

5 FEBRUARI, 2015

Jambo ambalo mimi nimelikubali na wamamua kwamba wataanza na Jiji la Dar es Salaam watakutana na viongozi, watazungumza nao na uongozi kwa ujumla wakishakubaliana hilo basi wawekeane kabisa maelewano kwamba utaratibu huu sasa ndiyo utatumika na vyombo vyote vifahamu kwamba hayo ndiyo maafikiano.

Kwa hiyo, mimi naamini wakifanya kazi hiyo vizuri Mwanza na Arusha wakafanya hivyo inawezekana jambo hili likamalizika vizuri sana. Pengine niseme tu kwamba wengine mnaweza mkafikiri jambo hili ni la Kitanzania tu, hapana. Vijana hawa wapo sehemu nyingi kwa sababu ni mambo yanayotokanana ajira Ugumu wa kupata ajira kwa vijana wetu.

Lakini wakati mwingine hata nchi za nje, mimi nimekwenda huko nimekuta kuna kitu wanaita *Sunday Markets*. Kwa mfano, haina tofauti na hii. Unakuta ni watu wamekusanyika wanafanya biashara lakini kwa kipindi maalum na wakishamaliza wanaondoka.

Kwa hiyo, mimi nadhani nimekubaliana nao. Hivyo naamini Mheshimiwa Mangungu pengine jambo hili tunaweza sasa tukalipa sura tofauti kuliko huko tulikotoka.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri.

Kwa kipindi hiki cha mpito wakati hayo yakiendelea, je, uko tayari kutoa kauli ili unyanyasaji ambao unafanyika dhidi ya wafanyabiashara hao wadogowadogo pamoja na waendesha Pikipiki isimamishwe mara moja kwa maana kwamba sasa hivi wanyang'anywa mali zao, wanapelekwa Mahakamani, wanapigwa faini lakini zile mali zinataifishwa na hatujui kama mali hizo zinaingia katika mfuko wa Serikali au zinaingia katika mfuko wa nani.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, wazo ni zuri lakini mimi nafikiri wazo hili ambalo limetoka TAMISEMI mimi nadhani ni jema zaidi.

5 FEBRUARI, 2015

Ninachoweza kushauri ni kwamba madam Bunge linamalizika ndani ya siku mbili zijazo, zoezi hili lianze wiki ijayo yaani kukutana huku wafanye wiki inayokuja ili waweze kuanza utaratibu huu mapema kadri itakavyowezekana.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA:Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuanza kumwuliza swali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo ni mara ya nne ninasimama katika Bunge hili Tukufu, nikikuuliza swali lile lile linalohusiana na kufukuzwa Madiwani wangu watatu wa Manispaa ya Ilemela wa CHADEMA na sasa ni miaka miwili imepita na mara zote umekuwa ukinipa majibu yenye matumaini yasiyo kuwa na ukamilifu.

Hoja ya msingi ni uhalali wa kufukuzwa kwao kwa sababu moja tu kwamba hawakuhudhuria vikao vitatu vya kawaida. Mara ya mwisho kauli yako ulisema kwamba umeagiza jopo la Wanasheria ili waweze kuangalia uhalali na ukweli wa suala hili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala hili limechukua muda mrefu sana na miaka miwili ni mingi sana. Kwa niaba ya wananchi wa Ilemela, leo unawaambia nini kuhusiana na mustakabali wa Kata tatu hizi ambazo zimekosa uwakilishi kwa muda wa miaka miwili sasa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Kiwia nakubaliana na wewe kabisa, naomba radhi kama unaona tumechelewa sana. Lakini limetokana na tatizo lenyewe kwani lilikuwa ni la kisheria zaidi kuliko tulivyokuwa tumefikiria.

Ilibidi katika hatua za mwisho hapa tukakubaliana tukaunda jopo la Wanasheria ili kutupa tafsiri ya baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yanaleta utata. Bahati nzuri ile timu imemaliza kazi yake, wameleta kwangu na juzi nimesaini barua kwenda TAMISEMI nikitoa uamuzi wa mwisho juu ya jambo hili.

5 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, mimi nafikiri sasa limemalizika baada ya ushauri tulioupata kutoka kwa wanasheria.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na maelezo haya ambayo hayafanani na maelezo ya huko nyuma wakati tulipoandika barua ya kwanza na matokeo yake ikaishia kwa Mkuu wa Mkoa na haikufika kwa wahusika.

Naomba uwahakikishie wananchi wa Ilemela hususani wa Kata hizi tatu za Kirumba, Nyamanoro pamoja na Ilemela, ni lini maamuzi ambayo yamefikiwa yatawafikia ili tuweze kupata mustakabali na mazingira ya amani katika Jimbo letu la Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, hiyo barua nimeisaini juzi wakati nipo Dar es Salaam, inakwenda kwa Waziri wa Nchi TAMISEMI kama ilivyo kawaida. Kwa hiyo, ninachoweza kukuaminisha tu ni kwamba halitachukua muda mrefu kutoka TAMISEMI kwenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ili yeye sasa aweze kutoa taarifa kwa kwenye mamlaka inayohusika na wahusika waweze kujulishwa.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kukuza *democracy*, Tanzania imesifika na imefanya jambo zuri sana la kupigiwa mfano. Mwaka jana, Serikali imesifiwa sana kupitia Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba, iliporuhusu wajumbe wa Bunge hilo kupiga kura wakiwa nje ya nchi.

Kwa kuwa, mwaka huu tuna Uchaguzi wa Rais na Wabunge, na kwa kuwa jambo hili linakwenda vizuri sana na *principles* za kidunia za *Human Rights*, za *African Charter on Human Rights and Peoples Rights* za *United Nations* ambazo Tanzania imesaini.

5 FEBRUARI, 2015

Je, utaratibu gani au maandalizi gani yameshafanywa katika uchaguzi wa mwaka huu wa Rais na Wabunge kwamba Watanzania waliopo nje ya nchi ambao wamejiandikisha katika daftari la kupiga kura wataruhusiwa kupiga kura na mipango gani imetengenezwa?

SPIKA: Ahsante kwa kuuliza kwa kifupi, Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, swali zuri lakini sina hakika kama Mnyaa wale jamaa wakipiga kura kule kama utawakubalia maana naona mna tatizo nao sana.

Lakini jambo hili tumelipeleka kwenye Tume ya Uchaguzi ili wao waone ni utaratibu gani ambao utatumika ili kuwezesha ndugu zetu ambao wako nje sehemu mbalimbali kama Uarabuni, Ulaya, China na kadhalika ili naowaweze kushiriki katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Sasa tulisha-*attempt* huko siku za nyuma ilionekana kama kuna matatizo kidogo ya kitaalamu taalamu hivi na hasa unapokuwa sasa na utaratibu mpya ambao tutakwenda nao katika Kuandikisha Wapiga Kura ndiyo maana tumesema bora tuwaachie wao ili waone ni namna gani hili jambo wanaweza wakalisimamia.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Uchaguzi wa Rais ni wa Jamhuri nzima ya Tanzania kwa hiyo kuachia upande mmoja si suala zuri kwa sababu Tanzania ni nchi moja.

Na kwa kuwa, muda mchache uliobakia wa Mabunge. Je, jambo hili tutalifanya kisheria ambayo italetwa hapa Bungeni ili tufanikishe jambo hili?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sheria ya Uchaguzi ipo na imeweka utaratibu wa namna watu watakvoyoshiriki katika Upigaji wa Kura.

5 FEBRUARI, 2015

Suala hapa ni pale anapokuwa na Mpiga Kura hayupo nchini unamwekea utaratibu gani utakaomwezesha na yeye kushiriki katika Uchaguzi huu. Ndiyo maana nasema ni suala kimsingi linalopaswa kusimamiwa na Tume hizi mbili, ya Zanzibar na Tume ya Taifa ya Bara ili kuweka utaratibu. Itakuwa ni utaratibu wa kawaida tu ambao utawawezesha watu hawa kushiriki. Suala ni namna tu watakvoyofanya kwa sababu wakati wa Bunge la Katiba tuliweza kufanya hivyo ingawa kulikuwa na matatizo ya hapa na pale lakini iliwezekana.

Kwa hiyo, mimi naamini Tume inaweza kabisa ikaona ni utaratibu gani ambao hautaleti kikwazo, tunaweza tukautumia na tukawawezesha wananchi kushiriki.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kumwuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na tatizo la muda mrefu sana ambalo suala hili tumeleta ofisini kwako lakini mpaka sasa halijapata majibu nalo ni mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Chato na Wilaya ya Biharamulo hususani katika kijiji cha Nyantimpa.

Suala hilo limekuwa ni la muda mrefu Wataalamu wamekaa, tumeleta nyaraka ofisini kwako lakini halijapata ufumbuzi, jambo ambalo limepelekea hata kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa kupata utata mkubwa sana baada ya hicho kijiji kuonekana kipo katika Wilaya zote mbili kwa maana ya Chato na Biharamuro.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini kauli yako juu ya utatuzi wa mgogoro huu?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sikumbuki vizuri maana ofisi yangu ni kubwa, inawezekana ilikuja kwangu, inawezekana iko kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu lakini mimi nafikiri kubwa ni hoja uliyoisema madam Mawaziri wangu wapo mimi nadhani ngoja tuwaagize wao sasa ili

5 FEBRUARI, 2015

wajaribu kutafuta ufumbuzi wa hili jambo kwa sababu kama unavyosema ni suala la muda mrefu na si Chato na Biharamulo tu, bali najua yapo maeneo mengine ambayo bado tunahangaika nayo.

Lakini *specifically* kwa hili acha Waziri wa Nchi TAMISEMI na Waziri wa Ardhi waitafutie ufumbuzi kwa sababu si mpaka wenye utata mkubwa sana, kilichokuwa kinahitajika pale ni ku-verify ule mpaka kuuthibitisha ili tuweze kujua ni upande gani uko sehemu ya Wilaya gani na jambo hilo tuwe tumelizamaliza.

Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba wanafanya hiyo kazi mapema kadiri itakavyoweze kabla hatujafikia kwenye maeneo hayo ya Uchaguzi mwingine.

SPIKA: Siyo lazima maswali ya nyongeza kama kitu kimejitosheleza, haya Mheshimiwa Dkt. Mbassa!

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala tumelisisitiza mara nyingi sana kupitia vikao vyetu vya Halmashauri na juzi nilikuwa kwenye kikao cha *full council* tumeliongelea na hata kwenye kikao cha *RCC*. Lakini majibu yamekuwa ni hayo hayo na utekelezaji ngazi ya chini umekuwa haupo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sasa labda Mheshimiwa Waziri atuhakikishie ni baada ya muda gani litakuwa limekamilika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Hawezi kukuthibitishia hapa maana yake mimi ndiye naulizwa sasa ndiyo maana nimesema madamu yupo hapa na jambo lenyewe linajulikana, tuwape hiyo kazi waifanye imalizike na utakumbuka kuna wakati niliwahi kusema kwamba wakati mwingine na mimi huwa nashangaa sana kwa sababu Wilaya na Wilaya wapo

5 FEBRUARI, 2015

Maafisa wa Ardhi wenye utaalumu ambao wangeweza kwa dhamira moja kujaribu kutafsiri GLs matangazo ya Serikali yanasema nini unapokuja kwenye mpaka ndani ya maeneo hayo.

Lakini unakuta nao huwa wanatofautiana sana ndiyo maana inabidi tuje sasa Wizarani kuomba watoke Wataalamu huku kuja huko. *(Makofi)*

Mimi nafikiri tutalimaliza ndugu yangu. *(Makofi)*

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha inawapatia wananchi wake waishio vijijini maji kwa 75% na wale waishio mijini maji kwa 95%.

Je, azma hiyo imetekelezwa kwa kiasi gani?

SPIKA: Aisee! Hilo swali ni la kisekta kabisa, labda useme utaratibu ukoje maana yake, haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu labda umeelewa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli ni jambo la kisera lakini ni la kiutekelezaji zaidi na pengine lingejibiwa vizuri zaidi kama angekuwa ameulizwa Waziri wa Maji moja kwa moja.

Lakini ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Vicky Kamata ni kwamba Serikali ina mipango mizuri ambayo inaendelea kutekelezwa hapa nchini ambayo inatoa matumaini ya upatikanaji wa maji kwa sehemu kubwa ya Watanzania na ninaamini hata yeye Mheshimiwa Vicky Kamata, hili analijua kutokana na taarifa ambazo Wizaru wa Maji imekuwa ikizitoa mara kwa mara.

5 FEBRUARI, 2015

Sasa natambua kwamba kuna changamoto zake katika utekelezaji na sehemu kubwa ni za kibajeti, jambo ambalo wote tunalijua.

Lakini nataka nimhakikishie tu kwamba dhamira hiyo ipo, juhudi hizo zinaendelea na tutajitahidi kadri ya uwezo wetu wote kuona kwamba tunatoa huduma hiyo kwa kiasi cha kuridhisha kama ambavyo tulikuwa tumedhamiria. *(Makofi)*

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru kwa majibu mazuri.

Maelezo yako yamejitosheleza lakini ninaomba basi mpango huu utekelezwe kwa haraka ili kupunguza kero ya wanawake hasa waishio Geita kwani wamekuwa wakitaabika kwa muda mrefu na Serikali imekuwa ikisema mambo yaleyale.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba uongee chochote kuhusiana na wananchi wangu wa Geita wanaoteseka sana kwa tatizo la maji. *(Makofi)*

SPIKA: Naweza kulikataa mimi, tena Waziri aseme Waziri habari ya Geita? Jibu ukitaka Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, suala la Geita nalifahamu na Mheshimiwa Vicky Kamata bila shaka analijua vizuri zaidi.

Juhudi za kupeleka maji katika maeneo ya mji wa Geita zinaendelea, tulichelewa kidogo kwa sababu kulikuwa na matatizo kidogo na vikwazo vya fedha lakini kwa sasa nadhani Waziri wa Maji ameshalishughulikia vizuri.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie tu kwamba juhudi hizi nadhani zitazaa matunda mazuri kwa kushirikiana na mgodi wa Geita ambao nao wamekuwa ni wadau wazuri sana katika kupata ufumbuzi wa maji katika Wilaya ya Geita.

5 FEBRUARI, 2015

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu nimeingia hapa Bungeni nimekuwa na swali kuhusu vitalu katika Mkoa wa Kagera na hususani Wilaya ya Misenyi Jimbo la Nkenge.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi tunavyoongea....

SPIKA: Kuhusu nini?

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Kuhusu vitalu.

SPIKA: *Blocks!* Vitalu ni zile *blocks* ambazo wanapewa wawekezaji. Ni zile *blocks* ambazo walikuwa wamepewa Wawekezaji na matokeo yake kuna ugomvi katika Wilaya yetu. Ninadhani linaeleweka!

SPIKA: Hilo swali hebu uliza halafu tutaona, kama ni la kisekta litakataliwa.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ni la kisekta.

SPIKA: Kama ni la kisekta halihusiki.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: *No, no, no!*

SPIKA: Haya uliza swali.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, linaeleweka, ninaomba niulize.

SPIKA: Uliza.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, Wafugaji wa Ranchi.

5 FEBRUARI, 2015

SPIKA: Haya sasa tumeelewa maana vitalu, vitalu tu haiwezekani...! Haya uliza sasa!

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, haya ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nimekuwa nikikuuliza swali hili na leo limeingia katika sura nyingine. Juzi tu Mkuu wa Mkoa Mpya ametembelea Wilaya ya Misenyi na akaongea na wananchi wa Kata ya Kakunyu alichoamrisha ni kwamba, wale wananchi walioko kitalu Namba 17 wawe wameondoka ifikapo tarehe 30 na mwisho ni tarehe 15. Lakini suala lililopo na linalojulikana ni kwamba, wanatakiwa kulipwa fidia ya kuhamu maeneo yale.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, matokeo yake ni kwamba juzi tumepoteza Baba mmoja na Mama mmoja, kwa sababu kumbuka Wahaya wanalima *permanent crops* (mazao ya kudumu), lakini leo unawaambia waondoke waende kokote na hawana mahali pa kwenda, kutokana na ile shock tumepoteza Baba mmoja na Mama mmoja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unaweza kusitisha zoezi hilo mpaka kwanza watu walipwe fidia ndipo wahamishwe kutoka katika maeneo hayo?

SPIKA: Si unaona kumbe jambo lenyewe kubwa! Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, anachoulizia Mheshimiwa Assumpter Mshama ni mashamba ambayo yalikuwa ya NAFCO na baadaye Serikali ikafanya uamuzi wa kutoa maeneo haya kwa ajili ya wawekezaji. Katika kuyagawa ilibidi eneo hili kubwa ligawanywe katika maeneo madogo madogo ya mashamba kwa ajili ya ufugaji. Kwa hiyo wakapewa ili waweze kuyaendeleza.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli anachokisema Mama Mshama kwamba, katika baadhi ya maeneo haya kwa kuwa yalikuwa hayajatumika kwa muda mrefu wapo watu waliokuwemo katika maeneo hayo na uamuzi ulipokuwa umefanywa sasa, *specifically* analolizungumza baadhi ya maeneo Serikali iliona iyatoe kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na mengine tukawapa watu wengine.

Kwa hiyo, upande mmoja ni kweli anachokisema kwamba, watu waliokuwemo mle wamepewa maelekezo kwamba, waondoke na hoja ya Mbunge ni kwamba ni vizuri wandoke baada ya kulipwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nilifanyie kazi kidogo ili niweze kujua tatizo likoje maana inawezekana ni ya kisheria tu. Lakini ninataka nimhakikishie kwamba, tutapata ufumbuzi na tunaweza tukatoa maelekezo ya kiutawala baada ya kuwa nimeelewa jambo lenyewe lilivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Mshama swali la nyongeza.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakumbuka niliuliza mara nne hili swali na Waziri wa Ardhi aliyepita akasema kwamba, hizo *documents* za hao waliopewa eneo lile, yaani tuseme Hati amezipeleka kwa Mheshimiwa Rais ili zifutwe na zigaiwe upya kwa kuzingatia maeneo ambayo hayana watu.

Je, unaweza kutueleza ni nini kinaendelea katika hilo?

SPIKA: Ndiyo yale yale mambo yako ofisini kwa Waziri wa Ardhi. Ah! Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya nimwambie Mheshimiwa Mshama kwamba, sina jibu la hilo kwa sababu kama lilipelekwa kwa Rais ninachoweza kusema

5 FEBRUARI, 2015

tu labda ni kwamba, ni – *find out* kutoka kwenye ofisi inayohusika kwamba jambo hilo pengine liko katika hatua gani. Kwa sababu yakienda kwenye ngazi hiyo nyingine ni kwamba, yamekwenda kwenye ngazi hiyo nyingine na wakati mwingine si lazima na mimi nikajua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitajaribu ku-check tuone ni hatua gani imefikiwa.

SPIKA: Ahsante sana. Tuendeleo na swali linalofuata Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, uzoefu unaonesha kuwa maeneo mengi ya mipakani yanakabiliwa na changamoto ya raia wa kigeni kuishi nchini na kunufaika na stahili za Watanzania ikiwemo Kupiga Kura.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo hili?
(Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Josephine Genzabuke, lina ukweli kwa kiasi fulani, lakini ni lazima nikiri vilevile kwamba kwa upande wa Kigoma lina changamoto zake. Ninadhani na yeye analijua hilo. Kwa hiyo ni jambo ambalo ni lazima lifanyike kwa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, sisi ambacho tumekwishakubaliana kwa kweli ni kuendelea kutumia Idara ya Uhamiaji kufanya kazi yao inavyotakiwa na kwa utaratibu ambao utatuwezesha kutoingia katika mgogoro wa kuhisi watu ambao ni Watanzania wakafikiriwa wametoka nje kwa sababu mpaka wa Kigoma na nchi ya Burundi ni changamoto kubwa sana na uko mwingiliano mkubwa sana.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakubaliana naye lakini ni jambo ambalo ni lazima tulifanye kisheria ili tusije tukatoa uonevu kwa baadhi ya makundi ya watu. Lakini Uhamiaji wameelekezwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ameambiwa, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa ameambiwa hivyo hivyo, kwa sababu na sisi tuna changamoto zetu na Kongo, lakini ni lazima lifanyike kwa utaratibu.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni nchi yetu itaendelea na zoezi la kuandikisha watu ili kushiriki katika zoezi la Kupigia Kura Katiba Inayopendekezwa na Uchaguzi Mkuu ujao.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba, raia wa kigeni hawatapata fursa ya Kupiga Kura katika Uchaguzi huo? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema njia rahisi ingekuwa *operations* ambazo huwa tunafanya, lakini kila unapofanya operesheni wakati mwingine haizai matunda mazuri. Kigoma ninaifahamu na changamoto zake ninazijua na Mheshimiwa Mbunge anazijua. Kinachohitajika pale ni idara kufanya kazi ile kwa utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba, tutasimamia jambo hili vizuri ili tuweze kutenganisha makundi haya mawili kwa sababu wako kweli ambao ni Watanzania.

Lakini pia wako wengine ambao kwa sababu ya mahusiano ya karibu siyo Watanzania. Tumeiona hiyo na bahati nzuri nilifika mara ya mwisho Kigoma maeneo

5 FEBRUARI, 2015

mengine ni vigumu sana, ni kama unavyoona tu katika baadhi ya mipaka mingine. Eneo moja linahitaji tu uangalifu mkubwa ili tusije tukachukua hatua ambazo zinaonea watu wengine, lakini tutajitahidi kuhakikisha hilo halifanyiki.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Suzan Jerome Lyimo!

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndani ya Bunge hili na hata nje kumekuwa na taarifa na tumeambiwa kwamba, viongozi na wanasiasa wasitumie wanafunzi kushiriki katika masuala ya siasa hasa katika vyuo na shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na viongozi wa Mkoa wa Ruvuma wamewatumia wanafunzi wa Manispaa ya Songea kushiriki katika Maadhimisho ya miaka 38 ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Unatambua umuhimu wa elimu, lakini vilevile Chama cha Mapinduzi mnadai kwamba, mna wanachama zaidi ya milioni 10.

Je, ni kwanini msitumie wanachama wenu kwenye sherehe hizo mnaenda kutumia wanafunzi tena wa shule za msingi ambao hawajawa na maamuzi ya chama gani wanakitaka? *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Suzan utafikiri tulikuwa pamoja, nilijua swali hili ni lazima litaulizwa tu. Lakini unajua mtoto wa nyoka ni nyoka. Chama hiki kina mfumo wake ambao umeshuka mpaka kwenye ngazi ya kitu kinaitwa Chipukizi. Chipukizi hawa ni watoto ambao wamezaliwa kutokana na Wazazi wao Wana – CCM, ndiyo maana chama kiliwatumia, kwanza ilipendeza sana, ilipendeza sana, enhe! *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Sasa kama unavyosema maadam havijafikia hata umri wa kuingia katika masuala ya siasa, halina madhara lile rafiki yangu, kwa sababu bado wadogo mno! Wao walichokuwa wanafurahia pale ni ile *parade* na kuonekana wamepiga sare ile, basi. Kwa hiyo, sisi wengine tulikuwepo pale tulifikiri ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo, swali la nyongeza.

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali anayepaswa kusimamia utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kwamba, watoto hawa ni wadogo lakini utatambua kwamba, baadhi ya watoto hawa vilevile wazazi wao ni wa Vyama vya Upinzani.

Kwa hiyo, sikubalini na wewe kwamba, watoto hawa Wazazi wao ni wa Chama cha Mapinduzi. Lakini suala la msingi ni kwanini kuwe na *double standards* wakati watoto hawa lengo lao ni kusoma na siyo kufanya siasa? *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ah! labda niseme tu kwamba na mimi ninaheshimu sana maelezo ya Mama Suzan pale, lakini kiacheni chama na utaratibu wake waendeleo nao. Mimi sioni kama kuna tatizo kubwa kwa sababu mfumo ule ndivyo ulivyo kwenye chama hiki. Sasa ukisema leo tuanze kubishana juu ya jambo hili sidhani kama itakuwa ni halali sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa.

5 FEBRUARI, 2015

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza swali moja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwepo na matatizo makubwa sana nchini ya kuwalipa fidia wananchi ambao wanahitajika kuachia maeneo yao kwa maendeleo mbalimbali, lakini pia hata kwa upanuzi wa barabara.

Mfano mzuri ni barabara kubwa ambayo inatoka kwenye Jimbo la Segerea inaingia Jimbo la Ukonga na inaenda mpaka Chamanzi. Barabara hiyo ambayo itaitwa Barabara ya JK na Rais alienda kusaini mkataba wa ujenzi wake kule China mwaka jana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini mpaka sasa wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi wa barabara ile kwa sababu ni ndefu na pana sana, kwani ni barabara ya njia Sita, bado hawajajua hatima yao ya kulipwa fidia.

Je, sasa kama Kiongozi unayesimamia shughuli za Serikali unatoa maagizo gani kwa watendaji wa miradi mikubwa kama hiyo nchini kote kuweka utaratibu mzuri wa kuwalipa mapema watu wanaoachia maeneo yao kwa ajili ya maendeleo mbalimbali ya nchi ili waweze kulipwa mapema? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, tatizo la fidia kimsingi kwa kweli ni tatizo tu la uhaba wa fedha. Lakini msingi wake unaeleweka.

5 FEBRUARI, 2015

Kama anavyosema Mheshimiwa Mwaiposa, hivyo ndivyo inavyotakiwa kuwa, inatakiwa mtu anapohamishwa au anapoombwa apishe bila kuchelewa anapaswa kulipwa fedha yake.

Lakini kikwazo kikubwa kimekuwa ni tatizo la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya fidia.

Kwa hiyo, ninachoweza kumwahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, Serikali inalijua hili na tunaendelea kulifanyia kazi kwa maana kila fedha zinapopatikana kwenye maeneo mbalimbali ambayo tumeishatoa ahadi tunatoa fedha kwa ajili ya kuondoa hilo tatizo la fidia.

Kwa hiyo, ninadhani hata hiyo barabara yako tutaangalia tuone tumefikia hatua gani na tuone kama tunaweza tukapata fedha kwa ajili ya kulipia fidia hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Mwaiposa ahsante. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweza kujibu maswali. Ninawashukuru pia waliouliza maswali kwani leo mmeuliza maswali kwa kifupi, tumeweza kuwa na watu Tisa.

Kwa hiyo, imekuwa vizuri sana na hii ndiyo hatua tunayopenda. Siku nyingine wengine wanakuwa na maswali marefu na ubishi, basi tunajikuta tumeishia na maswali manne. Kwa hiyo, niwashukuru na muendeleo kuuliza maswali la kisera na siyo kisékta. Maswali ya kisékta yana wenyewe, lakini ya kisera Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lazima ajue tu.

Ninamshukuru Waziri Mkuu, pamoja na Wabunge. Tuendeleo Katibu!

5 FEBRUARI, 2015
MASWALI YA KAWAIDA

SPIKA: Maswali ya kawaida tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ignas Malocha, atauliza swali la kwanza.

Na. 98

Maombi ya kuanzisha Halmashauri Mpya

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kupitia Baraza la Madiwani ilijadili na kupitisha maombi ya kupatiwa Halmashauri mpya iitwayo Lyamba ya Mfipa, baada ya kutimiza vigezo vinavyotakiwa.

Je, ni lini Serikali itatoa kibali cha kuanzishwa kwa Halmashauri hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imekwishapokea maombi ya uanzishwaji wa Halmashauri mpya ya Wilaya ya Ziwa Rukwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Awali Halmashauri hii ilipendekezwa kuitwa Halmashauri ya Lyamba ya Mfipa, lakini kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilibadilisha jina hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inaendelea na uchambuzi wa maombi haya na maombi mengine yote yanayohusu uanzishwaji wa Halmashauri. Kama maombi haya yatakuwa yamekidhi vigezo vya uanzishwaji, Halmashauri hii itaanzishwa sambamba na Halmashauri zingine. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini vile vile ninampongeza kwa juhudi na uwajibikaji. Aliishafika katika Halmashauri hiyo na aliishajionea mwenyewe jiografia ya eneo lile ilivyo ya maporomoko kiasi kwamba, inaleta utata hata katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Kwa hiyo, ninatoa ombi kwake awe mmoja wa Mabalazi wa kunisaidia katika kuhakikisha Halmashauri hiyo inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina Kata 27, ni Kata 12 tu zenye Watendaji walioajiriwa. Vilevile ina vijiji 114, ni vijiji 72 tu ambavyo vina watendaji walioajiriwa, watendaji 42 hawajaajiriwa.

Halmashauri ilitoa maombi ya muda mrefu ya kuajiri watendaji hao toka Bajeti ya mwaka jana hawajapatiwa kibali cha ajira.

Je, ni lini Serikali itatoa kibali kwa Halmashauri dhidi ya maombi hayo ili kuwezesha usimamizi mzuri wa shughuli za maendeleo? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru kwamba ameishukuru Serikali na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba tuchukue shukrani hizo. Ni kweli nimekwenda mpaka kule, nimeliona eneo lenyewe na kama anavyosema hapa pamoja na wengine wale wote, hawa ni pamoja akina Mheshimiwa Paul Lwanji, Manyoni kule wameomba nafasi hizo.

5 FEBRUARI, 2015

Wote kwa pamoja tunajaribu kuyaangalia haya na wakikidhi vile vigezo ambavyo tumekuwa tunavieleza mara kwa mara hapa tuna hakika kwamba, tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu hii habari ya kukaimu. Sisi tunachofanya, sasa hivi kimoja kikubwa kilichofanyika ambacho ni maendeleo makubwa ni kuhakikisha kwamba, kada hii inayokwenda kwenye Watendaji wa Vijiji sasa imerudi katika Halmashauri zenyewe. Lakini vibali vyote vya wale watendaji wa kata na vijiji wote tunakwenda Ofisi ya Rais, Utumishi, pale ndipo tunapomalizia mambo yetu.

Sasa hivi tunavyozungumza hapa Halmashauri nyingi sana zimepewa vibali ninajua kwamba, havitatosheleza kwa maombi yaliyotolewa. Lakini nilitaka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitajibu swali lingine katika eneo hili na nitaeleza vizuri ni hatua gani ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, tutakachofanya hapa kwa maana ya hivi vijiji na kata ambazo amesema zinakaimiwa, tutafuatilia Ofisi ya Rais, Utumishi ili kuhakikisha kwamba wanapata nafasi hizo.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Suzan Kiwanga.

MHE. SUZAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Mji Mdogo wa Ifakara, ambao mpaka sasa hauna hadhi ya Mji Mdogo, licha ya kuwa na Vitongoji 33 na Wakazi wengi sana. Mpaka leo wanashindwa kukusanya mapato kwa sababu hawajapewa mamlaka kamili.

5 FEBRUARI, 2015

Je, ni lini sasa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itaupa mamlaka kamili Mji Mdogo wa Ifakara ili ukusanye mapato na kuweza kuupanga mji huo vizuri?

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Kiwanga, kama ifuatavyo:-

Kabla haijapata mamlaka kamili ya kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo ninadhani sijui anamaanisha nini kwa sababu hiyo mamlaka inayo mtendaji wake na tunavyokuwa na mamlaka ya Mji Mdogo inakuwa na Vitongoji. Kwa hiyo, ilivyo ndivyo mamlaka ya Mji Mdogo inavyopaswa kuwa na inaendeshwa kwa kutumia Bajeti ya Halmashauri Mama bado Mamlaka ya Mji Mdogo inaendelea kulelewa na Halmashauri Mama haiwezi kujitawala vile unavyotaka. Kwa hiyo jinsi ilivyo ndivyo Mamlaka ya Mji Mdogo inavyopaswa kuwa. (Makofi)

Na. 99

Ushuru wa Geti Kwenye Baadhi ya Halmashauri

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Baadhi ya Halmashauri zinaendelea kutoa ushuru wa geti na tayari kuna agizo na tangazo la Serikali Na.230 la Mwaka 2003 la kuzuia swala hilo.

(a) Je, Serikali inajua kwamba kitendo hicho ndiyo chanzo cha migogoro iliyopo katika baadhi ya Mikoa?

5 FEBRUARI, 2015

(b) Kama Serikali inajua tatizo hilo. Je, ni hatua gani zimechukuliwa ili kukomesha kitendo hicho?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ushuru wa mazao ni chanzo kimojawapo cha mapato ya Halmashauri ushuru huu unatozwa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 Sura Namba 290 (7) (1) (g) kama ilivyorekebisha na Sheria ya Fedha Namba 15 ya Mwaka 2010 ambayo haijafutwa na inaendelea kutumika hadi sasa, pamoja na Sheria ndogo ziliziwekwa na Halmashauri.

Hata hivyo kwa mujibu wa Sheria hiyo ushuru unaotowza mahali ambapo mazao yanazalishwa yaani (*payable at source*) na unatozwa kwa mnunuzi. Ninakubaliana kuwa Serikali ilinunua magezi yaliyokuwa yamewekwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru. Magezi yaliyoko kwa sasa ni yale ambayo yamewekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002.

Lengo la magezi haya ni kudhibiti utoro shaji wa nyara za Serikali yakiwemo meno ya tembo, mbao na vitendo vya ujangili vya aina yoyote ile katika Hifadhi za Taifa. Halmashauri au Mawakala wanaokusanya ushuru wa mazao ya Halmashauri wamekuwa wakitumia fursa hiyo ya uwepo wa magezi hayo kudhibiti na kukagua kama ushuru wa mazao yanayosafirishwa umelipwa huko yanakotoka.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, mnunuzi wa mazao Kisheria ndiye anayelipa ushuru wa mazao na kupewa stakabadhi ambayo itaonyesha na kuthibitisha kama amelipa ushuru mahali popote atakapokuwa anakaguliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo niliyotoa hapo juu hakuna Halmashauri inayotoza ushuru kinyume na Sheria zilizopo. Halmashauri zimekuwa zikishirikiana na Wizara ya Maliasi na Utalii kwa kutumia magezi yaliyowekwa kudhibiti wanunuzi wa mazao ambao wanakwepa kulipa ushuru wa mazao ambao upo Kisheria.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kuhimiza na kuhakikisha ushuru huo unalipwa na wanunuzi wa mazao ili kuimarisha mapato ya ndani ya Halmashauri zetu. *(Makofi)*

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza ninakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ameeleza kwa ufasaha na yanaeleweka lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kuna malalamiko yanayotokana na wananchi kwamba risiti zinapotolewa hazilingani na uwezo wa ule mzigo uliobebwa na mwananchi yule.

Je, Serikali haioni kuwa kufanya hivyo ni kutowatendea haki wananchi?

Kwa kuwa usafirishaji wa chakula katika eneo moja kwenda eneo lingine ni kuisadia Serikali kutawanya chakula nchini.

Je, ni kwa nini wanaosafirisha chakula ndani ya nchi hii huwa wanatozwa ushuru?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nieleze kwa kifupi sana jambo hili kwa sababu lina matatizo yake.

5 FEBRUARI, 2015

Haya magezi kama nilivyosema tunafanya hivyo, sisi kama Halmashauri tunachokifanya hapa ni kwamba huwezi kukimbizana na *Fuso* kule Mjini unakimbizana nalo unalifuata huku limekata kona unakwenda.

Sisi tunachofanya ni kwamba na sisi tuna *take advantage* kwa sababu ni sehemu ya Serikali tunakwenda kwenye magezi pale tunakwenda tuna check *Fuso* pale na risiti. Mheshimiwa Fakharia anazungumza habari ya kwamba wakati mwingine risitii zinatolewa ambazo hazilingani na kiasi kilichotolewa. Mimi nitaomba sana mtusaidie, kwa sababu hili ni jambo kubwa analisema Mheshimiwa Mbunge.

Kama kweli kuna mtu hapa analipa hela ameambiwa kwamba ni laki mbili zinatakiwa halafu anapewa risiti ya laki moja na nusu au laki moja haya ni mambo ambayo tunataka kuelezwa hapa tupate sisi na tuhushwe hapa mara moja na Halmashauri.

Sasa kuna mambo mengine na faini huko na vitu vingine vyote vinavyofanyika kule Halmashauri hizi tumepewa majukumu mengi kusomesha watoto, kujenga barabara, kuhakikisha Zahanati zinajengwa na miradi mbalimbali ambayo inatakiwa kufanya kazi. Hizi 10% ambazo zinazungumzwa hapa tunazipata kwenye *own source* ambazo tunazitungumzia hapa. Ndiyo maana ninamshukuru sana Mheshimiwa Fakharia kwamba anakubali na ameridhika na majibu ambayo tumetoa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali lingine ni hili la kusaidia kutawanya chakula mtu anatoka Ulanga pale anafika Kilombero anakwambia haya mahindi ni ya kwangu sisi mahindi hatutozi mpaka yanapokuwa yanahama kutoka kwa Mkulima yanakwenda kwa mchuuzi pale, ndipo unamwambia nipate 5% yangu au kulingana na Halmashauri ilivyopitisha pale anataka kutoa mahindi yale anataka kupeleka Kilosa au anataka kupeleka Morogoro huwezi kupambanua kwamba haya mahindi sasa hivi haya ni ya kwake mradi anahama mipaka ya Halmashuri tutamwambia atupatie cha kwetu.

5 FEBRUARI, 2015

Kwa sababu mahindi yale hata kama ana magunia milioni moja kama hayajatoka mikononi mwake huwezi kumtoza. Hili ndilo tatizo linalotokea hapa. Tunashindwa kupambanua sasa, sasa anazungumza habari ya kutawanya chakula inawezekana kabisa kuwa hawa wanatawanya chakula lakini wanaotawanya chakula wanafahamika na majina yao yanajulikana watakuwa pia na barua inayoonyesha kuwa huyu mtu ni wa kutawanya chakula.

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema tatizo tunalolipata hapa na changamoto tunazozipata hapa ni kwamba wakati mwingine unashindwa kupambanua kwa sababu watu wanakwepa mambo haya mimi nitaomba kama ana vielelezo hili tunalichukua na tunalifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba haki inatendeka. *(Makofi)*

SPIKA: Tunaendelea maana yake leo umekaa mbali na mic, kwa hiyo sauti haikuwa mbaya sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila. *(Makofi)*

Na. 100

**Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji Katika
Wilaya ya Kalambo**

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA aliuliza:-

Baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Rukwa zina Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata ambao wengi wao hawajaariwa ila wanakaimu katika nafasi hizo kwa kipindi kirefu cha kati ya miaka 3-4.

Je, Serikali haioni kuwa inapokuwa na Watumishi wasioajiriwa huku wakikaimu kwa muda ni kuwafanya wasiwajibike ipasavyo na hivyo kushindwa kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo husika?

5 FEBRUARI, 2015

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vijiji na Kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ambavyo vina watendaji wanaokaimu. Serikali imerudisha ajira za Watendaji wa Vijiji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Halmashauri zenyewe.....

SPIKA: Ninaona kuna mazungumzo, matembezi humu ndani ninaomba mtulie Mheshimiwa endelea.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, Serikali imerudisha ajira za Watendaji wa Vijiji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Halmashauri zenyewe zinajiri kada hii baada ya kupata kibali.

Aidha watendaji wa Kata, ajira zao zimeendelea kubaki katika sekretarieti ya ajira katika mwaka wa Fedha 2014/2015 nafasi 15 za Maafisa Watendaji wa Vijiji na nafasi 15 za Watendaji zilitengwa na kuombewa kibali kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetoa kibali cha kuajiri Watumishi hao kwa Mwaka huu wa Fedha. Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Watumishi hao ni shilingi milioni sitini na nane, laki nane ishirini na mia sita. Vilevile katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri Watendaji wa Vijiji 30 na Watendaji wa Kata 10.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha nafasi wazi zinajazwa na kuondokana na Watendaji wanaokaimu kwa muda mrefu.

5 FEBRUARI, 2015

Hatua hii itasaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Maendeleo kwenye maeneo yao. Halmashauri ya Wilaya inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Sekretarieti ya Ajira ili kupata kibali cha kuajiri Watumishi hao. (Makofi)

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya Watendaji wa Vijiji bado wana kaimu siyo wote walioajiriwa, wapo ambao bado wanakaimu na Watendaji wa Vijiji hawa wamekuwa wanashindwa hata kuitisha mikutano Mikuu ya Mwaka ili kusoma taarifa za Maendeleo ya Vijiji vyao. Lakini pia kusoma Mapato na Matumizi ya fedha wanazokusanya kwa sababu tu bado wanakaimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuajiri au kuajiri Watendaji wa Vijiji hawa wote ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi?

Swali la pili, kwa kuwa vibali vya Watendaji wa Kata bado havijatoka na kama vimetoka ni wachache tu. Serikali inatoa tamko gani kuhusu kutolewa vibali vyote kwa ajili ya Watendaji Kata ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa wa kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, kama ifuatavyo:-

5 FEBRUARI, 2015

Hivi vijiji ambavyo anavisema

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba usogee kwenye *mic*.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Vijiji hivi ambavyo vipo ni 111 na Kata zake ni Kata 22 na hizi Kata ambazo nimezisema hapa, sasa hivi tunazo Kata tano ambazo ni mpya na ambazo tunategemea kwamba hizi kwa maana ya maombi haya ambayo tumepeleka tutakuwa tumepata jawabu la jambo hili.

Lakini bado tutakuwa na Vijiji ambavyo vina watendaji wanaokaimu kwa sababu ni Halmashauri mpya, hii anayoizungumza hapa. Sasa anachoweza kufanaya hapa ni kwamba kila wakati na ndiyo maana ninazungumza habari ya Bajeti hapa.

Mheshimiwa Spika, ni lazima waingize katika Bajeti zao na waingie katika mtandao ili ianze kuji *reflect* kule na kuona kuwa hawa wandlipa *otherwise* watakwenda pale wata *gang up* wataanza tunataka haki zetu tunaonewa na mambo mengine ya namna ile ambayo ni *problem* hiyo sasa. Kwa hiyo *the bottom line is* ni lazima waingize katika mtandao na ni lazima waingize katika Bajeti na ndiyo maaana nimesema hapa kwamba kwenye mwaka 2014/2015 tayari hawa tumeshawaomba waingie katika Bajeti na hii ninaisema ni kwa ajili ya Halmashauri nyingine zote. (*Makofi*)

Sasa kuhusu hili la Mapato na Matumizi. Mapato na Matumizi ya Halmashauri ya Kijiji yanatakiwa yawe *pinned on the board* kila baada ya miezi mitatu kinachozungumzwa pale siyo mtu anakaimu pale. Kinachozungumzwa ni kwamba Serikali ya Kijiji iko pale wanakaa pale na baada ya miezi mitatu ni lazima waweke pale kwenye *board* ni Sheria inataka hivyo ni matakwa ya Sheria.

5 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwakumbusha na ninajua kuwa jambo hili Wabunge wamelizungumza hapa kwa muda mrefu na niseme kwa sababu kubwa kwa ajili ya msisitizo wanaowajibu wa kuhakikisha hela zinazokwenda kwenye Halmsahuri.

Pale ni hela za Serikali, ni hela zinazotoka kwa wananchi, ni hela ambazo zinatokana na nguvu yao na majina yao. Haiwezekani mtu mmoja akakaa pale akasema unajua Bwana mimi ninakaimu tu hapa. Kwa hiyo mimi siwezi kutoa taarifa ya Mapato na Matumizi, taarifa ya mapato na matumizi inatolewa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanaokaimu hizi nafasi za Watendaji wa Kata na Vijiji wengi wao ni walimu na kwa mantiki hiyo ina maana walimu wanaacha kazi zao za msingi za kufundisha watoto wetu wanakuwa wanafanya kazi za Uafisa Utendaji na hii inapelekea kuzorotesha kwa elimu.

Nilitaka kujua Serikali inafanya makusudi kuwakaimisha walimu na kutokuchukua hatua thabiti ya kutokuhakikisha kuwa inawaajiri hawa Maafisa Watendaji?

SPIKA: Unaulizwa wanafanya makusudi au vipi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kitu kimoja hapa tulishasema kabisa hii habari ya kumtoa mwalimu darasani au daktari na kwenda kumkaimisha kwenye kijiji kule. Hii habari Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Hawa Ghasia wamezuia hili jambo. Tulishazuia tukasema hatufanyi hivyo, ninasema usitikise kichwa, kwa sababu ninaeleza sasa nikieleza si ndiyo utaelewa na ukielewa si utapata jibu. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Ninachosema hapa ni kwamba huwezi ukamkaimisha mwalimu pale unakwenda kumchukua mratibu wa elimu wa Kata ndiyo unamwambia wewe utakuwa ni Mtendaji wa Kata hapa anayekaimu au unamchukua Mtendaji wa Kijiji unampeleka pale na kumwambia kuwa utakaimu pale. Sasa anisikilize vizuri Mheshimiwa Matiko.

Kama tunao walimu ambao wametoka madarasani pokea maelekezo huko waliko na mimi ninaomba unilettee majina hayo ili tuwaambie wenzetu kama imetokea hiyo mtulettee kwa sababu tunalo tatizo hapa la walimu ambao wanafundisha madarasani ambao hatuwezi kukubali.

Anayezungumzwa hapa ni Mratibu wa Elimu huyo ndiye anaweza kukaimishwa pale hili jambo siyo jambo ambalo tunalitaka. Sasa Geography ya kwetu ni ngumu unaweza ukaenda ndani kule Mwese, Mpanda huko katikati na nini, utakuta wametafuta wamefika mahali ndipo mambo kama haya anayosema Mheshimiwa Matiko, yanaweza kujitokeza, *its an fortunatully* lakini siyo makusudi.

SPIKA: Haya tuendeleo na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, atauliza swali hilo.

Na. 101

Askari Polisi Kujihusisha na Uhalifu

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH aliuliza:-

Kumejitokeza vitendo vya baadhi ya askari Polisi kuhusika na uhalifu wa wazi wa kutumia silaha.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya jambo hilo?

5 FEBRUARI, 2015

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Vitendo vya aina yoyote ile vya kihalifu havitakiwi kutendwa na mtu yoyote yule awe raia au askari. Aidha askari polisi ndiyo wenye dhamana ya kudhibiti uhalifu, kuimarisha hali ya amani na utulivu na ni jambo lisilokubalika kwa askari kujihusisha na vitendo hivyo. Kwa kuzingatia hayo Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua kali kwa askari wote wanaohibitika pasipo na shaka kuhusika na matukio ya uhalifu.

Serikali inatoa wito kwa askari wasio waadilifu wanaoharibu taswira nzuri ya Jeshi kwa kujihusisha na vitendo vya uhalifu waache mara moja. Serikali hii haitasita kuwachukulia hatua kali na za Kisheria ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi na kufikishwa Mahakamani, kama ilivyokwisha kufanywa kwa wenzao waliobainika kukiuka maadili ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH: Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini sasa ninaomba nimwulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya askari hao wanafahamika na raia wema.

Je, huoni kuna haja sasa ya kufungua ofisi maalum ya kuweza kuripoti askari hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba pale ambapo inaonekana wanaeleweka hawa watu kuwe na mahala ambapo wanatakiwa kuripotiwa. Katika Wilaya zote zimeundwa Kamati za Madili kwa ajili hii.

5 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, wanaofahamu lolote wanaweza kuchukua hatua hiyo. Hata Makao Makuu pia kuna kitengo cha Maadili kwa ajili ya kurekebisha tabia za wale ambao wanapotoka.

Wiki ya jana nilikuwa ninajibu swali la Usalama barabarani, nilitakiwa pia niwape namba ambayo kwa yule mtu ambaye ana taarifa yoyote ile ya askari au matukio mengine aripoti kwenye namba hiyo ya Wizara. Namba hii iko wazi masaa 24, kwa siku saba nayo ni 0685 777222. (Makofi)

SPIKA: Haya kama mmesikia shauri yenu na kama hamjasikia basi tena. Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ataulizwa swali linalofuata.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninajua umenisahau lakini umekusudia mimi nina hakika.

SPIKA: Ndiyo si umekaa hapo? Niliyemwita ni nani?

MBUNGE FULANI: Ni mimi.

SPIKA: Mheshimiwa Ali Khamis Seif, yuko wapi? Kama Ali Khamis Seif, asimame huyo niliyemwita asimame.

WABUNGE FULANI : Hayupo.

SPIKA: Haya uliza wewe mwenyewe basi.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Katika suala la dorioa haramu iliyofanywa na askari wa Zanzibar iliyopelekea kifo cha Askari Suleiman

5 FEBRUARI, 2015

Makame, ambaye inasemekana amepotea na hajaonekana mpaka leo. Ingawa siku yake ilipatikana juu na kupelekea marehemu mwingine ambaye ameuwawa askari PCF 7642 akionekana na jeraha la risasi.

Jambo ambalo limezua uvumi katika Mji wa Zanzibar kama ni tukio ambalo walikosana katika mgao haramu waliokwenda kuufanya.

Je, Serikali mpaka sasa kwa nini haijatoa tamko lolote?

MHE. HAROUB M. SHAMIS: Ilihali kukiwa na askari wengine watatu walioko hai, ambao kinachosadikiwa ni kwamba walikosana katika mgao na kupelekea askari hao kuuwa?

Mheshimiwa Waziri, unatoa tamko gani ambalo wanafamilia wa marehemu hawa mpaka sasa hawajui hatma ya ndugu yao aliyepotea na huyu aliyekufa? Tunaomba tamko la Serikali kuhusiana na tukio hili. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kama ifuatavyo:-

Nafikiri amenipa taarifa muhimu na hivi ndivyo tunavyotaka tuisaidiane katika kufanya kazi. Amezungumza kwamba kuna uvumi na sisi hatufanyi kazi kwa uvumi. Namwomba anipe taarifa kamili ili hili jambo kama lipo tulifanyie kazi, ili haki ionekane imetendeka na itendeke.

5 FEBRUARI, 2015

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

Na.102

Ununuzi wa Sare kwa Ajili ya Walinzi

MHE. KOMBO H. KOMBO aliluliza:-

Utaratibu wa kuwapatia sare walinzi wetu wa Usalama wa Raia na mali zao ni mzuri sana.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani juu ya manunuzi ya sare hizi na zinatoka wapi?

(b) Je, sare hizo hununuliwa kwa awamu ngapi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Kombo Hamisi Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kwa ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za manunuzi ya sare za polisi huzingatia kif.2(2)(d), cha Sheria ya Manunuzi Namba 21 ya Mwaka 2004. Wizara yenye dhamana ya Usalama wa Raia, huwasiliana na Mamlaka ya Kusimamia Manunuzi ya Umma (PPRA), ili kupanga orodha ya bidhaa za kijeshi zinazotakiwa kununuliwa ndani na nje ya nchi kwa njia ya muafaka ya manunuzi, yaani *method of procurement*.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu hukutana na Mamlaka hii kila mwaka wa fedha kutimiza matakwa ya sheria ya manunuzi, na kwamba katika mwaka 2012/2013

5 FEBRUARI, 2015

tulikutana kupanga utaratibu wa kununua mahitaji haya, zikiwemo sare za askari. Ambapo tulikubaliana kuwa sare za polisi na vifaa vyote vinunuliwe kwa utaratibu wa tenda zuio (*restricted tendering*), kwa sababu za kiusalama.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, kila mwaka wa fedha, Wizara hupanga Bajeti kwa ajili ya kununua sare za askari wote kwa awamu moja. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, lengo hilo hushindwa kufikiwa na hivyo kulazimu sare hizi kununuliwa kidogo kidogo kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa KomboHamisi Kombo!

MHE. KOMBO HAMISI KOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ni dhahiri kwamba Serikali haina uwezo wa kununua sare za Jeshi la Polisi, kwa kulinda heshimiwa ya jeshi hili, pamoja na kulinda usalama wa raia na mali zao.

Je, Serikali inapata wapi fedha za kununulia marungu, risasi, mabomu ya machozi, ya kuwapigia Viongozi wa Upinzani na wafuasi wao, pamoja na wamachinga kwa kauli ile ile ya piga tu?

Ni dhahiri kwamba kuna askari ambao wanavaa sare ambazo zinakidhi haja na kuna askari ambao wanavaa sare ambazo ni dhaifu na hazionyeshi heshima ya jeshi hili.

Je, ndani ya nchi yetu kuna *double standard* katika jeshi hili? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

5 FEBRUARI, 2015

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba, siyo kwamba Serikali haina uwezo wa kununua sare. Isipokuwa upatikanaji wa fedha unakuwa taratibu, na ndiyo maana tunanunua kwa awamu.

Nataka nimwambie Mheshimiwa Kombo kwamba katika kufanya kazi hizi, kitu cha kwanza ni kile ambacho kitahakikisha usalama wa kuvaa sare, kinatekelezwa mwanzo.

Kwa hiyo, suala la rungu maji ya kuwasha, maji nini, ni mambo ya *priority* ya kutaka usalama ili askari nao waweze kuvaa sare.

Mheshimiwa Spika, sare ambazo tunanunua ni sare tunakubaliana na tuna *zi-fest* kwa kiwango kikubwa zinatimiza haja. Pale ambapo hazitimizi, narudia kwamba ni suala la Bajeti, lakini bado wanavaa na bado heshima ya jeshi ipo palepale.

SPIKA: Mheshimiwa Chombo, swali la nyongeza.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nitamwuliza swali moja la nyongeza Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, sare za askari wetu kwa kiasi fulani dizaini yake ni rahisi sana kugijiza kwa watu wa kawaida.

Je, kuna mpango wowote wa Jeshi la Polisi kudizaini sare ambazo zinaonekana zinavutia na zina heshima kubwa kuliko hizi za sasa?

5 FEBRUARI, 2015

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, dunia ya siku hizi hakuna kitu ambacho hakigushiwi. Ikiwa kila kikigushiwa ubadilishe, basi utashindwa kudizaini.

Tunachoweza kufanya kwenye nguo zetu ni kuhakikisha kwamba zina alama ya kuonyesha, uhalali kutoka Serikalini. Heshimiwa ya Serikali itabaki, na hizi zimekuwa dizaini kwa kuweza kuweka heshima inayotakiwa. Wale ambao wanagushi, tutaendelea kuwafuatia, lakini dizaini zetu tutaziboresha tu pale ambapo haja ya kiulinzi itakuwepo.

SPIKA: Ahsante sana, tunaenda na Swali linalofuata, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, atauliza swali hilo.

Na. 103

Wanafunzi Wanaomaliza VETA Kukosa Ajira

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Wanafunzi wengi wanaomaliza VETA hukosa ajira na kushindwa kujijiri kwa kukosa mtaji au vifaa vya kufanyia ufundi wao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukopesa vifaa ili wajijiri wenyewe?

5 FEBRUARI, 2015

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kwa ufasaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna tatizo la kukosa ajira kwa wahitimu wa Vyuho na Taasisi mbalimbali za elimu, vikiwemo vile vinavyotoa elimu ya Ufundi Stadi hapa nchini. Ukosefu wa ajira unachangiwa kwa kiasi kikubwa na uchache wa viwanda katika Nyanja mbalimbali hapa nchini.

Pia, utafiti wa VETA/VET uliofanyika kufuatia shughuli za wahitimu, ulionyesha kuwa tatizo la ajira husababishwa na vijana waliohitimu elimu na mafunzo mbalimbali kushindwa kujajiri, kwa kukosa mitaji au vifaa vya kufanya kazi, ili kutumia ujuzi wao walioupata vyuoni.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya ufundi ustadi ambayo hufundishwa kwa nadharia na vitendo kwa lengo la kumwezesha mhitimu kupata ujuzi wa kujajiri na kuajiriwa.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali kupitia Wizara ya Kazi na Ajira, imetenga jumla ya shilingi bilioni tatu, kwa ajili ya utekelezaji wa *program* ya kukuza ajira. Kupitia *program* hii Serikali inatarajia, kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji.

5 FEBRUARI, 2015

Wahitimu wanachotakiwa kufanya ni kujiunga katika vikundi, na kuandaa andiko la mradi kwa ajili ya kuomba mikopo ya mitaji na ununuzi wa vitendea kazi.

Vilevile Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya, Miji na Majiji hutenga asilimia tano ya Bajeti yake kila mwaka kwa ajili ya mikopo kwa vijana, wakiweno wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi kutoka katika vyuo vya VETA.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha vijana wanaohitimu vyuo vya ufundi stadi wanaweza kujijiri, somo la elimu ya ujasiriamali linafundishwa, pamoja na masomo ya ufundi ustadi, kwa lengo la kuwapa stadi ya kujijiri na kuajiriwa. Somo hili huwaongezea wahitimu uwezo na mbinu za kuanzisha biashara, kutoa kazi yenye ubora, kutafuta masoko, umuhimu wa kuwa na vikundi na namna ya kupata mikopo. *(Makofi)*

Aidha, mada zinazohusu Taasisi za Fedha hutolewa kwa lengo la kuwaunganisha wahitimu hao na Taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Suzan Lyimo swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu lake la msingi amesema kwamba Halmashauri hutenga asilimia tano kwa ajili ya vijana.

5 FEBRUARI, 2015

Ni dhahiri kwamba katika ripoti ya LAAC, tumeona kwamba kwa mwaka 2013/2014, Halmashauri zilitakiwa kukusanya shilingi bilioni 270, kwa ajili ya vijana na akina mama. Lakini zimeweza kutoa bilioni saba tu, sawa na asilimia 2.6 tu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, utatumia miujiza gani kuhakikisha kwamba hiyo asilimia 98 iliyobaki, inapatikana ili hawa vijana waweze kupata ajira?

Kumejitokeza vyuo vingi sana vya ufundi binafsi, na vyuo hivi vinakuwa havijasajiliwa. Nimemsikiliza sana Mtendaji Mkuu wa NACTE, Dkt. Mkwera, akisema kwamba wamekuwa wakitumia diplomasia sana kuwaambia wamiliki wa vyuo hivi wavisajili lakini bado hawajavisajili.

Je, serikali haioni kwamba watoto hawa wanatapeliwa kwa sababu wanapomaliza katika vyuo hivyo hawapati vyeti na kwa maana hiyo hawawezi kupata ajira? Mnachukua hatua gani? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mpaka uitwe ndiyo usimame. Haya unaitwa sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kukiri kwanza kwamba, Halmashauri hazitoi ile asilimia tano. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kama alivyosema.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, niipongeze Manispaa ya Wilaya ya Temeke, ambayo imejaribu na imeweza kutoa milioni mia tatu kwa ajili ya mikopo kwa vijana wake na vikundi vya VETA.

Kwa hiyo, naomba ninapojibu swali hili, kuziamrisha Halmashauri zote, zifuate mfano wa Manispaa ya Temeke, ikiwepo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Same.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuu vya VETA ambavyo havijasajiliwa na vinatoa kozi, naomba niseme kwamba hayo ni makosa makubwa na kuanzia leo tutachukua hatua kali katika vyuo ambavyo vinafanya kitu kama hicho. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, swali la nyongeza.

MHE. OMARY AHMAD BADWEL: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeamua kujenga Vyuu vya VETA katika nchi nzima, lakini ujenzi wa vyuo hivyo vimekuwa ghali sana. Lakini Halmashauri ya Wilaya ya Bahi na Wizara ya Elimu ilikubalina na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ikatoa majengo yake yote yaliyokuwa Chuo cha Kilimo miaka minne iliyopita, na Naibu Waziri alienda kutembelea na alikiri kwamba majengo yale yanaweza kuanzishwa Chuo cha VETA.

Lakini hadi sasa miaka minne imepita, Wizara haijakiri kwanza kupokea majengo pamoja na kwamba Halmashauri imeipa. Lakini wala hawajarudi tena mpaka sasa katika Kijiji cha Kigwe ili tuanze kujenga ujenzi wa chuo hicho.

Sasa ni lini Serikali itayapokea hayo majengo na kuanza ujenzi katika Chuo cha VETA katika Wilaya ya Bahi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu. Waziri wa Elimu!

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omary Badwel, kama ifuatavyo:-

Nikiri kwamba changamoto nyingi zilizokuwepo pamoja na changamoto za Bajeti, jambo hilo hatukulifanyia kazi kwa ukamilifu. Nichukue hii taarifa ambayo Mheshimiwa ameitoa, ili kushirikiana na yeye kuangalia namna tunavyoweza kulitekeleza kwa mapema iwezekanavyo.

5 FEBRUARI, 2015

SPIKA: Ahsante sana. Tuendeleo na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, kwa niaba yake Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan. Kama tulivyosema Mheshimiwa Rita Mlaki, amefiwa na mama yake.

Na. 104

Sarafu ya Pamoja kwa Nchi za EAC

MHE. IDDI MOHAMED AZZAN (K.n.y. RITA LOUISE MLAKI)
aliuliza:-

Nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki, wako katika maandalizi ya kupitisha Mkataba wa kuweka sarafu ya pamoja na tayari baadhi ya Nchi Wanachama wameshapelekewa Mkataba huo kwenye Kamati za Bunge la Nchi husika, na baadhi nyingine tayari Mkataba umeshapitishwa tayari kupelekwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

(a) Je, nchi ya Tanzania iko katika hatua gani ya kupitisha Mkataba huo sehemu zote kabla haujaletwa Bungeni?

(b) Kwa kuzingatia kuwa Nchi Wanachama wa EAC zinatofautiana kiuchumi. Je, hilo suala la sarafu ya pamoja haliwezi kuziumiza zile nchi zenye uchumi hafifu kama ilivyokuwa kwa Nchi za Ulaya walipoanzisha sarafu ya pamoja *EURO*?

(c) Je, nchi yetu imejiandaa vipi kukabiliana na hali hiyo endapo ikitokea?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 25 Juni, 2014.

Kabla ya kuridhiwa kwa itifaki hiyo, Serikali ilitoa semina kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara tarehe 10 Juni, 2014 hapa Dodoma. Semina hiyo, ilifuatiwa na Semina ya Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo tarehe 22 Juni, 2014.

Aidha, Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kuridhia itifaki hiyo na mpaka kufikia hivi sasa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekwisha ridhia itifaki hiyo.

Mheshimiwa Spika, tofauti za kiuchumi zilizopo kwa sasa sio kikwazo cha kuanzisha umoja huo wa fedha. Kwani hata nchi ambazo zimefanikiwa kuunda umoja wa fedha, kama umoja huu uliopo kwa nchi za Afrika Magharibi na Umoja wa Fedha za nchi za Jumuiya Ulaya, Uchumi wao ulikuwa unatofautiana.

Suala la msingi ni kuhakikisha kwamba, hatua za awali zinabainishwa, zinatekelezwa na kuzingatwa, ili kujikinga na changamoto zinazoweza kujitokeza baada ya kuanzishwa kwa kutumia sarafu ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, imebainisha kipindi cha mpito, cha miaka kumi. Kwa nchi wanachama kuchukua hatua za kuboresha misingi, na mifumo yao ya kiuchumi ili kuweza kushabiana, na hivyo kuondoa tofauti za viashiria muhimu vya kiuchumi kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuandaa itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wanachama wamezingatia changamoto zilizojitokeza kwenye umoja wa fedha wa nchi za Ulaya.

5 FEBRUARI, 2015

Itifaki imeanisha mikakati na mbinu za kuzuia uwezekano wa kutokea kwa msukosuko wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na mfumo wa kutoa tahadhari ya chombo cha kusimamia utulivu wa sekta ya kifedha. Taasisi imara na huru za kusimamia takwimu na Taasisi ya kusimamia Utekelezaji wa Matakwa ya Itifaki wa Umoja wa kifedha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan, swali ya nyongeza.

MHE. IDDI MOHAMED AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo tu mawili.

Tunafahamu kwamba mfumo huu hauna tofauti sana na ule mfumo ambao umetumika kwenye nchi za Ulaya, ambayo Uingereza ilikataa kushiriki. Nilitaka kufahamu tu tahadhari ambazo Serikali imechukua, ili kulinda uchumi wetu. Kama ilivyofanya Uingereza kwenye Umoja wa nchi za Ulaya?

Yapo matatizo mbalimbali yametokea katika Jumuiya yetu, ikiwa ni pamoja na itifaki mbalimbali mpaka sasa nyingine hazijasainiwa. Lakini magari ya Tanzania kuziwa kuingia Kenya vitu kama hivyo.

Serikali imechukua tahadhari gani kabla ya kuanza mfumo huu wa sarafu moja, ili kuhakikisha kwamba hatujiingizi kwenye matatizo kama ambavyo imetokea kwenye nchi za Ulaya?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa kufuatilia suala hili na kuitaka Serikali kuchukua tahadhari kabla haijaingia kwenye hatua hizi.

5 FEBRUARI, 2014

Niseme tu moja ya tahadhari kubwa ambayo Serikali imechukua, mtakumbuka Tanzania imekuwa kinara wa kusimamia taratibu zile zote zilizowekwa katika kufikia makubaliano ya hatua zote nne zilizowekwa kwenda kwenye *East African Federation*. Hiyo ni moja ya hatua ya kutuhakikishia kwamba hatupati matatizo kama ya nchi nyingine zilizopata matatizo.

Vigezo vilivyowekwa katika viashiria vya msingi vya kiuchumi kabla ya kuamua; kwa mfano, mfumuko wa bei kuwa chini ya asilimia nane, utaona nchi kama Tanzania tumeweza kushusha mfumuko wa bei ambao ulikuwa zaidi ya asilimia 16 na kurudi mpaka chini ya asilimia 4.8.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha juu cha nakisi ya bajeti, hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali za Kibajeti, pamoja na vitu vingine ambavyo vinahusisha uwepo wa akiba ya fedha za kigeni, hii inafanywa kwa nchi zote wanachama; viashiria hivi vikishakuwa na utulivu, ni dhahiri kwamba uchumi mpana utaweza kuwa na ulinzi na hivyo hatuwezi tukapata matatizo ambayo walizipata zile nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua zilizochukuliwa, ametolea mfano wa kusema magari kuzuiwa. Nadhani yale mambo mengine ni ya kiutawala na ni mambo ya kimahusiano ambavyo kama historia yake ilivyo, Tanzania ni kinara wa kutengeneza mahusiano katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Afrika; ni mambo ambayo yanarekebishwa na hayawezi kuleta tatizo, hata mengine majibu tayari yalishatolewa kama vyombo vilivyoweza kuripoti katika siku za hivi karibuni.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ungependa kuongeza hapo? Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, tunaomba kama ungeongeza kuhusu magari yaliyozuiliwa kule Kenya.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kilichotokea ni kwamba kiasi cha mwezi mmoja uliopita,

5 FEBRUARI, 2014

Serikali ya Kenya ilizuia magari yanayochukua watalii kutoka na kuingia uwanja wa Jomo Kenyatta wasipokelewe na magari ya Tanzania, wachukuliwe na magari ya Kenya mpaka kilomita tano kutoka kwenye uwanja, halafu ndiyo magari ya Tanzania yawachukue kwa mara zote mbili. Yaani Watalii wanapomaliza ziara zao, basi wanaletwa mpaka kilomita tano kutoka uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta, na vivyo hivyo wakishuka wanachukuliwa kwanza na magari ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo halipendezi sana, lakini tuliwasiliana na wenzetu na baada ya muda Mheshimiwa Waziri wa Utalii alikwenda Nairobi na hali hiyo imesharekebishwa, lakini tatizo halijaisha. Tunaomba wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, wajihadhari. Wanachokitaka Kenya ni kuwezesha Watalii wanaokwenda Kenya baada ya kufika kule waingie katika mbuga hasa ya Serengeti ambayo ndiyo kivutio kikubwa maarufu hapa duniani, wao wakae Kenya, lakini wawe wanakuja Serengeti kupitia mbuga yao ya Masai Mara ambayo ni sehemu ambayo inaungana.

Mheshimiwa Spika, hilo lilizuiwa tangu mwaka 1985 na sababu ni dhahiri, kwa sababu wakiwa wanakaa Kenya na watalii wanaoshuka Jomo Kenyatta ili kuja Tanzania ni laki tatu na nusu. Ikiruhusiwa hiyo, hoteli zetu zitakuwa hazipati watalii, watakuwa wanashuka Kenya wanaingia Tanzania kuangalia wanyama na kurudi kulala Kenya, wanatuachia takataka na hakuna zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, kwa hali hiyo, tuna mkutano ambao utafanyika Arusha baada ya Bunge hili, tunajaribu kuangalia ni namna gani tutayalinda maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba katika haya mahusiano ya Afrika Mashariki kunatakiwa kuwa na tahadhari kubwa sana. Kwa mfano, sisi Wizara ya Uchukuzi tunaanza kuangalia jinsi ambavyo Shirika la Ndege la Kenya linatoza dola 700 safari ya Dar es Salaam - Nairobi kwenda na kurudi, ambayo ni zaidi ya nauli ya kwenda Dubai na wakati huo ile *Precision Air* imeshuka sana ufanisi. Kwa hiyo, ndege za Kenya

5 FEBRUARI, 2014

sasa zinatua mara nne Dar es Salaam kwa siku na kwa nauli hiyo, kitu ambacho hatukifurahii hata kidogo. Lakini yote haya tutayazungumza kwa pamoja ili kulinda maslahi ya nchi yetu. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa twende Wizara ya Maji, Mheshimiwa Gaudence Kayombo!

Na. 105

Tatizo Sugu la Maji - Mji wa Mbinga

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO aliuliza:-

Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa kwenye ziara yake huko Mbinga Julai, 2014 aliwaahidi wananchi kutatua tatizo sugu la maji kwenye Mji wa Mbinga:-

Je, ni lini tatizo hilo litakwisha.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la maji linalowakabili wananchi wa Mji wa Mbinga. Katika hatua za dharura za kuboresha huduma ya maji safi kwa Mji wa Mbinga, Serikali imetenga kiasi cha fedha Shilingi bilioni moja katika bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 ili kupanua mfumo wa maji safi katika Mji wa Mbinga. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukarabati mabomba yaliyochakaa, upanuzi wa mtandao wa maji na ununuzi wa dira za maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mpango wa muda mrefu wa kuwapatia maji Mji wa Mbinga. Kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni umeshakamilika. Mradi huu utatekelezwa katika awamu ya pili ya Mpango wa

5 FEBRUARI, 2014

Maendeleo wa Sekta ya Maji iliyoanza mwaka wa fedha 2014/2015. Mradi huu utakapotekelwa na kukamilika utatua tatizo sugu la maji kwenye Mji wa Mbinga.

SPIKA: Mheshimiwa Kayombo, swali la nyongeza!

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naipongeza Serikali kwa majibu mazuri na yenye matumaini kwa wananchi wa Mbinga. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Moja, Serikali imekiri kwamba imetenga kiasi cha Shilingi bilioni moja katika bajeti ya mwaka huu na sasa tuna miezi kama mitano tu mwaka wa fedha uishe na taarifa nilizonazo, hakuna fedha zilizoingia kule, na kwa sababu natambua tatizo; ni lini sasa Serikali itatusaidia kupeleka hizi fedha ili ziweze kufanya kazi na kutatua matatizo ya afya ya Mji wa Mbinga?

Pili, katika mradi wa vijiji kumi kule Mbinga, Vijiji vya Kihongo, Litoo na Mkako vilianza kidogo kufanya kazi na Wakandarasi walikuwa kule *site*, lakini kwa sababu ya ukosefu wa fedha miradi hii sasa imesimama na Wakandarasi hao wanatishia kuondoka. Ni lini pia wataokoa ili vijiji hivi viweze kupata maji ya kutosha?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba tumetenga hizo fedha na kwa sababu mwaka wa fedha haujaisha na Waziri wa fedha yupo hapa anasikia, nafikiri mara watakapotupa fedha, sisi tutapeleka fedha katika Mji wa Mbinga kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji anavyovitaja katika ujenzi, vipo katika 35%, 25% na 45%, lakini tayari tumeshapeleka Shilingi milioni 300 na wakati wowote kuna Shilingi milioni 168 ziko njiani zitafika Wilaya ya Mbinga.

5 FEBRUARI, 2014

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, anapaswa kuuliza swali hilo. Mheshimiwa Mkosamali umehama mahali pako! Umeenda kukaa pale pale, *ooh sorry!* Uliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Msigwa! (*Kicheko*)

Na. 106

Maazimio ya Tanzania Kutekeleza Makubaliano ya Kimataifa Kukomesha Ujangili

MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. MCH. PETER S. MSIGWA) aliuliza:-

Tatizo la upungufu wa Tembo katika Hifadhi za Taifa unatokana na ujangili na biashara haramu ya Nyara hata kuifanya Tanzania kujiweka maazimio ya kutekeleza makubaliano ya Kimataifa ya kukomesha tatizo hilo:-

Je, mpaka sasa Tanzania imetekeleza Maazimio ya makubaliano mangapi.

SPIKA: Ahsante. Huna haja ya kukaa pale anapokaa mwenyewe. Naibu Waziri, majibu! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kudhibiti ujangili na biashara haramu ya mazao ya maliasili, Tanzania imeridhia na kutekeleza mikataba minne ambayo ni *CITES*, *UNESCO*, *INTERPOL* na *LATF*.

Katika mikataba hiyo, maazimio mbalimbali yamewekwa ikiwa ni pamoja na kudhibiti ujangili na biashara ya wanyama walioko hatarini kutoweka, mfano, tembo;

5 FEBRUARI, 2014

kudhibiti ujangili unaovuka mipaka, kuhifadhi na kulinda maeneo ambayo yametambulika kuwa urithi wa dunia kwa mfano, pori la akiba *Selous*.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maazimio na mikataba ya Kimataifa, nchi yetu iliandaa mikutano miwili ya Kimataifa ya uhifadhi iliyofanyika hapa nchini na kuhusisha wadau mbalimbali wa maendeleo na mashirika mbalimbali ya uhifadhi ya Kimataifa.

Mikutano hiyo ilifanyika mwezi Mei na Novemba, 2014 katika Miji ya Dar es Salaam na Arusha. Katika Mkutano uliofanyika Arusha, nchi yetu iliridhia makubaliano maalum ya Kikanda ya kudhibiti uhalifu dhidi ya wanyamapori na ujangili unaovuka mipaka, nchi za Burundi, Kenya, Malawi, Msumbiji, Uganda, Zambia na Sudan Kusini. Aidha, mwezi Oktoba, 2014 Serikali ilizindua mkakati wa Kitaifa wa kuzia ujangili na biashara haramu ya wanyamapori. Pia ilikubali kuanzisha Mfuko wa Pamoja (*Basket Fund*) kuwezesha udhibiti wa ujangili na biashara haramu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2014, nchi yetu ilishiriki katika Mkutano maalum wa Hifadhi ya Wanyamapori uliofanyika London. Katika kikao hicho, Serikali iliridhia makubaliano ya mikakati ya uhifadhi wa tembo (*Elephant Protection Initiative*) na nchi za Gabon, Botswana, Chad na Ethiopia. Nchi yetu itaendea kutekeleza maazimio ya kikao cha London ikiwemo kuboresha *database* ya meno ya tembo na utunzaji wa kumbukumbu za meno ya tembo yaliyopo katika ghala kuu la nyara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Tanzania kuchukua hatua katika kutekeleza maazimio ya makubaliano ya Kimataifa kukomesha tatizo la ujangili, faida mbalimbali zimepatikana kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya Euro 30,000 na USD 100,000 zimetolewa na UNDP na kuwekwa katika mfuko wa *Basket Fund* kwa ajili ya kudhibiti ujangili;

5 FEBRUARI, 2014

(ii) USD 33,160 zilitolewa na *African Elephant Fund* kwa ajili ya mradi wa kuimarisha usimamizi wa sheria katika maeneo ya bandari na viwanja vya ndege.

(iii) Vifaa mbalimbali vya doria vilitolewa yakiwemo magari 21, *helicopter*, mahema, *binocular* na sare.

(iv) Watumishi zaidi ya 100 wamejengewa uwezo katika maeneo yanayohusu udhibiti wa ujangili kupitia mafunzo yaliyotolewa na *Interpol*, *Howard Buffet Foundation*, *TRAFFIC* na *LATF*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miakati ya Kimataifa kwa lengo la kudhibiti ujangili nchini. Aisha, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi, ukusanyaji na utumiaji wa taarifa za kiintelijensia kwa ajili ya kushirikisha wananchi na kuhusisha taasisi za ndani na nje ya nchi katika kudhibiti ujangili unaovuka mipaka.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali, maswali ya nyongeza!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Haya majibu hayajajibu swali. Swali linauliza, utekelezaji; sasa unapouliza utekelezaji wa mauaji ya tembo, unatakiwa ujibu kwamba tembo walikuwa wanauawa hivi, tumepunguza, sasa hivi wanauawa hivi. Swali ni kwamba, hizi hadithi za Mikutano na nini ziache, jibu hivi... (*Kicheko*)

Swali, mwaka 1978 tulikuwa na tembo 2,800,000, mmetueleza hizi habari za mikutano wamebaki maelfu. Yaani wamuawa kutoka kwenye mamilioni, wapo 55,000, au 33,000 sasa hivi. Sasa jibu, mtatekeleza lini kwa vitendo hii mikataba ya Kimataifa? Hiyo namba moja. (*Makofi*)

Pili, kwanini msizuie uwindaji wa utalii, watu wanaingia na silaha kwenye mapori ya akiba, Selous ndiyo ilikuwa inaongoza kwa ndovu, sasa hivi wameisha kwenye mapori ya akiba? Kwanini msipige marufuku uwindaji wa kitalii kwa

5 FEBRUARI, 2014

sababu unachangia kwa kiasi kikubwa uuaji wa tembo? Kwanini msifanye hivyo kuliko kuwa na hadithi, maelezo na nini? Tembo wanatoka mamilioni wanafika...

SPIKA: Umeshauliza swali, na wewe hayo mengine hayana haja! Yale uliyouliza yanatosha. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na tatizo kubwa la ujangili hapa nchini ndiyo maana Serikali yetu ikaamua kuingia mkataba na kutengeneza maazimio.

Kwa mfano, Azimio la *CITES* lilikuwa lina lengo la kuisaidia nchi kulinda wale wanyama adimu. Sisi kama Tanzania tulitengeneza *National Ivory Action Plan* ambayo kwa kiasi kikubwa imetusaidia. Sasa hivi tembo wameanza kuongezeka na *at the same time* uwindaji haramu umepungua katika nchi yetu kwa sababu taasisi mbalimbali zimekuwa zinatusaidia katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, pili, tulikuwa tuna tatizo kubwa sana *Selous* na lilisababisha mbuga yetu ya *Selous* kuingizwa kwenye *list endangered*, lakini nataka nikuhakikishie tu kwamba sasa hivi *Selous* tembo wameanza kuongezeka toka tumeingia *list endangered*.

Mwaka 2014 tulikuwa kwenye kikao cha Doha na tulikubaliana kupata misaada tutahakikisha baada ya miaka miwili tutatoka kwenye hii *list endangered*.

Vilevile tuna *Lusaka Agreement Task Force* ambayo inasaidia ujangili wa nje ambao unavuka ndani ya mipaka. Tunashirikiana na wenzetu vizuri na Makao Makuu ya *Task Force* haya yapo Nairobi. Hii *Basket Fund* tuliyoianzisha inatusaidia kupata hela na kutufasaidia kufanya shughuli mbalimbali katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mkosamali ni suala la kisheria. Suala la kuzuia uwindaji wa

5 FEBRUARI, 2014

tembo ni suala la kisheria ambalo tunatakiwa tukubaliane na kama sheria italetwa hapa tunaweza tukalishughulikia.

SPIKA: Jamani muda wangu umekwisha. Naomba niwatambue baadhi ya wageni waliopo humu ndani.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka Ubalozi wa Norway ambao ni Balozi wa Norway, Mheshimiwa Mrs. Hanne-Marie Kaarstad na Msaidizi wake Bi. Elisabeth Shamte Hansen, Mshauri wa masuala ya siasa. *You're welcome, on us to have you here and I hope you will enjoy being here in Dodoma with us. Thank you very much!*

Tunao Viongozi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii NSSF. Hawa ni Ndugu Cresencius Magori, Mkurugenzi wa *Operation NSSF*, yupo wapi? Yupo na Ndugu Celestine Ntagara, Kaimu Mkuu wa Sheria, NSSF. Nadhani watapata nafasi baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu ambao ni watoto anaowalea ambao ni Ndugu John Madaha, Ndugu Silvanus Ole-Samnwa, naomba wasimame watoto hawa walipo. Ahsante sana, tunashukuru.

Tunao Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Sylvestry Koka, kutoka Kenya wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Saimon Gicharu ambaye ni *Chairman and Founder of Mount Kenya University*, yupo wapi ndugu yetu huyu, ahsanteni sana, karibuni sana, ni wageni wetu wote mnakaribiwa sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, ambao ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Wanging'ombe, Ndugu Edson Msigwa, naomba asimame alipo, yupo pale. Yupo Katibu wa CCM Wilaya ya Wanging'ombe, Ndugu Jumanne Kapinga, ahsante, karibu sana. Tuna Mjumbe wa Halmashauri Kuu *(NEC)* Ndugu Nebichad Msigwa, ule Mkoa wote Wajumbe wa *NEC* wote

5 FEBRUARI, 2014

wanaitwa Msigwa. Yupu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wanging'ombe, Ndugu Anthony Mahatwa, ahsante! Yupu Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa wa Njombe, Mheshimiwa Mama Lwila, yeye hajaonekana. *(Makofi)*

Wapo Viongozi wengine wa Wilaya na Kata katika Wilaya ya Wanging'ombe naomba wote wasimame. Alah, kumbe wengine wako pale! Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri amekaribisha wageni wake wote hao. Ahsanteni sana, karibuni sana. Mnamwona Naibu Waziri anavyohenya hapa, ndiyo maneno yenyewe yanavyokuwa. Kwa hiyo, msiseme hamumwoni kama asivyoonekana mtu mwingine, basi ndiyo hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Grace Kiwelu, hawa ni Ndugu Boniface Mbanda, Mwenyekiti wa BAVICHA, Jimbo la Vunjo. Yupu wapi huyu ndugu yetu? Aah yuko pale, ahsante, karibu sana. Tuna ndugu Helga Mchomvu. Huyu ni Mheshimiwa Diwani, Halmashauri ya Hai na Katibu wa BAWACHA, Mkoa wa Kilimanjaro. Naomba asimame alipo. Yuko wapi? Alaa, yuko pale upande huu. Ahsanteni sana, karibu. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa John Mnyika, ambaye ni Ndugu Mohamed Mtoi Sheng'ombe. Huyu ni Mratibu wa Kanda Taifa, CHADEMA. Yuko wapi Bwana Sheng'ombe? Aah yuko upande huu hapa. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, ambaye ni Ndugu Mchungaji Amos Chideni, kutoka Kanisa Anglican Igunga. Yuko wapi Mchungaji? Ahsante, naye yuko hapa. Tunaomba Wachungaji mfanye kazi ya kuombea nchi hii, tuweze kuvuka.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Clara Mwatuka, ambaye ni Ndugu George Mwatuka, mume wake. Yuko wapi Mzee Mwatuka? Ahsante sana, tumefurahi kukuona, ahsante sana. Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, kutoka Jimbo la Igalula, Tabora, ametajwa kwa majina tu, hata sijui vyeo vyao. Kwa sababu wametajwa kwa

5 FEBRUARI, 2014

majina, naomba wageni wa Mheshimiwa Eng. Mfutakamba, wote wasimame walipo. Yuko hapa Mama Mariam Mfutakamba Kahabi, yuko Amina Hussein Kahabi, Shani Tandiko, Halima Kombo, Kuruthumu Kombo, Mrisho Sinundo na Mzee Mohamed Janja. Ahsanteni sana. Karibuni sana muwe pamoja nasi. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu ambao ni vijana 55 kutoka Wilaya ya Hanang waliokuja Dodoma kwa ajili ya mafunzo ya ujasiriamali. Naomba wenyewe wote hawa wasimame walipo. Eeh ndiyo nyie! Ahsanteni sana, wajasiriamali, tunawashukuru sana. Naomba mwendele vizuri. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale ambaye ni Mwinjilisti, Cecil Simbaulanga, yuko Mwinjilisti Samson Bulegi, naomba musimame. Yupo Mwinjilisti Eliteli Kakobelo, yuko Mwinjilisti Shadrack Mwasonya na yuko Mchungaji Elia Mwauza. Ahaa, ahsante Wachungaji. Kama nilivyoomba pale, ni lazima tusali kwa nguvu na tuikabidhi nchi mikononi mwa Mungu aweze kufanya kile kinachompendeza. Ahsanteni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu ambao ni Mchungaji Stephen Sinda, kutoka Kata Kikiyo Singida Mashariki. Naomba asimame Mchungaji alipo. Yuko Ustadhi Ismail Mohamed kutoka Kata ya Kikio Singida Mashariki. Yuko Ndugu John Missanga, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkinyo na yuko Ndugu Balali Lissu Mugwayi, mdogo wake. Karibuni sana na Viongozi wa Dini walioko hapo, naomba muiombe nchi, Mungu aiweke pale ambapo inampendeza.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Janeth Mbene, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye ni Ndugu Filomen Molel, Kamanda wa Vijana wa CCM, Mkoa wa Arusha. Yuko wapi huyu? Halafu yuko na Mkurugenzi wa Kampuni ya *Monaban Trading and Farming Company*. Wako wapi? Ndiye huyo huyo! Ahsante, karibu sana. Sijakuona, karibuni sana. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2014

Kuna wageni 19 wa Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Selemani Jafo, ambao ni wanafunzi wagonjwa wa Kampuni Acashia, mgodi wa Bulyankulu wakiongozwa na Kiongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa migodi na madini, Ndugu Benjamin Daudi Doto.

Naomba hawa vijana wetu wasimame walipo, kama wapo. Sasa Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Maige muwapeleke kwa wanaohusika kusudi waweze kuonekana. Sidhani kama wamekuja kuangalia Bunge tu, naona wana shughuli yao.

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Esther Matiko, ambao ni Ndugu Mary Nyagabona, huyu ni Mwenyekiti wa BAWACHA, Tarime. Yuko wapi? Aah, yuko upande huu hapa. Yuko Godliver Masamaki, Mwenyekiti wa BAWICHA, Bunda. Yuko wapi? Yuko sehemu ile ya nyuma.

Halafu yuko Ndugu Edna Ingeleza, Mwenyekiti wa BAWACHA, Serengeti; yuko na Ndugu Miriam Chacha, Mwenyekiti wa BAWACHA, Musoma Mjini. Kwa hiyo, Wenyeviti wote hawa karibuni sana, tunawatakia kazi njema ya kuwaendeleza akina mama.

Tuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni, wako wanafunzi 15 kutoka Chuo cha St. John Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Israel Edga aliyekuwa Spika wa Bunge la Vijana, lililofanyika mwezi Desemba, 2014 na Katibu wa Bunge hilo Bi. Mary Chacha. Naomba msimame mlipo na Maspika wastaafu, basi tena! Ahsante, karibuni sana. Karibuni sana, tuwatakia kazi njema shuleni, someni kwa bidii. *(Makofi)*

Tunao Wanafunzi 100 na Walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Msalato Dodoma. Naomba wasimame hao wa Msalato Dodoma. Ahaa, okay, ahsante. Karibuni sana! Shule ile ni ya wadada, kwa hiyo, msome kwa bidii sana muweze kuvuka viwango vile tuwe na Shule ya mfano. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2014

Tuna Wanafunzi wengine 130 na Walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Kiwanja cha Ndege, Dodoma; na hawa wasimame walipo. Watakuwa wamekosa nafasi, tutawaona baadaye. Okay karibuni sana wageni wengine wote ambao mko hapa. Bunge letu kila mtu anaweza kuja kulitembelea akiwa na nafasi.

Naomba nitoe matangazo ya kazi za leo. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi Namba 229.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 8.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 227. Wale 29, hawa 27!

Halafu nimeombwa na Katibu wa Wabunge Wanawake wa CHADEMA ambaye ni Mheshimiwa Pauline Gekul, anaomba niwatangazie kuwa kutakuwa na Kikao cha Wabunge Wanawake wa CHADEMA leo Ukumbi wa Msekwa 'C' mara tu baada ya kusitishwa kwa Bunge saa 7.00.

Halafu yupo Katibu wa Waheshimiwa Wabunge wa CCM kule Zanzibar, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kutoka Zanzibar kuwa kutakuwa na Kikao muhimu leo siku ya Alhamisi saa 7.00 mchana baada Kikao cha Bunge kuahirishwa chumba Na. 231.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mwongozo kidogo!

SPIKA: Wee kaa tu. Unisikilize mimi. Katibu!

5 FEBRUARI, 2014

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii na
Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii**

SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali, siyo ndiyo Waziri aah.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) na nisiisome ili kuokoa muda.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu amehalalisha jambo ambalo ni kinyume na haki za binadamu ndiyo maana nimesimama hapa. Hapa tuna barua ambazo Mkuu wa Mkoa alimwandikia Afisa Elimu kuwalazimisha vijana wa *Songea Boys* na *Songea Girls* wavae sare za CCM na Walimu waende kule kwa lazima. *(Makofi)*

Sasa hili jambo ni kinyume na haki za binadamu na ni kinyume kwa nchi ambayo inafuata mifumo ya kidemokrasia. Huwezi kuwalazimisha watu wafanye...

SPIKA: Mwongozo!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mwongozi wangu ni kwamba Waziri Mkuu ufute kauli hapa. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa wewe huo ni mwongozo, ni amri, ni ushauri?

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Naomba mwongozo wako umwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aje afute kauli, ili watu wasilazimishwe.

MBUNGE FULANI: Hajui sheria huyo!

5 FEBRUARI, 2014

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Watu wasilazimishwe kufanya shughuli za kisiasa wakiwa hawataki, kuingizwa kwenye Vyama ambavyo hawataki. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, ahsante. Mwongozo wangu, simlazimishi. Haya tunaendelea, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto! *(Kicheko/Makofi)*

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, si unasoma hotuba? Alah, ooh nimesoma. Hii ni sababu ya Mheshimiwa Mkosamali! *(Kicheko)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Samahani Waziri, unisamehe sana. Inaanza Kamati ya Maendeleo ya Jamii halafu atakuja Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Kabla hajasoma, naomba Mheshimiwa Mheshimiwa Mwenyekiti aje anipokee. *(Makofi/Vigelegele)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Kidawa Hamid Saleh)
Alikalia Kiti*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naomba kuanza kwa kuwashukuruni kwa kunipa imani yenu na kunichagua kuwa Mwenyekiti wenu wa Bunge. Naomba tupeane ushirikiano kwa sababu kazi hii ni yetu sote. Asanteni sana. Katibu! Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, karibu. *(Makofi)*

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyekiti Mungu, kwa kunipa fursa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kusoma taarifa ya Kamati Bunge ya Maendeleo ya Jamii ya kazi katika kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niruhusu nikupongeze wewe binafsi na Mheshimiwa Ledian Mung'ong'o kwa kuteuliwa kuwa Viongozi, Wenyeviti wa kusaidia shughuli za kuendesha Bunge letu hili Tukufu.

5 FEBRUARI, 2014

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafanya hivyo kwa sababu Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama amekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa muda mrefu sana, kwa hiyo, Kamati yangu inatambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika uendeshaji wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, Kanuni ya 117(5), naomba sasa kutoa taarifa ya shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2014 hadi 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati hii ni kama yalivyo majukumu ya Kamati nyingine na yameorodheshwa vizuri ukurasa wa pili wa taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni hizo pia, majukumu ya Kamati hii kama ambavyo yameorodheshwa, Kamati yangu inasimamia Wizara tatu; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; na Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambazo zimetekelezwa na Kamati yangu; kwanza ni kujadili bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/2015. Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 Aprili, hadi tarehe 4 Mei, 2014 kwa lengo la kupitia na kuchambua makadirio na mapato na matumizi ya Wizara inayozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara husika Kamati iliona changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo inazozisimamia kutokana na ukosefu wa fedha kutoka Hazina. Kwa kifupi Wizara kutopewa fedha kwa wakati imepelekea Wizara hizo kutotekeleza majukumu yake kwa

5 FEBRUARI, 2014

wakati kama ambavyo takwimu zinajionyesha kwenye Jedwali katika vitabu ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano. Katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ilitengewa Shilingi bilioni 16.6 na Bunge hili, lakini hadi tunaenda kukutana na Wizara hii ni kiasi cha Shilingi bilioni 4.3 tu sawa na asilimia 26, ndicho kilikuwa kimepokelewa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtiririko huo, unaweza kuona namna ambavyo bajeti katika kila Wizara inavyopata fedha kiasi kidogo sana ikilinganishwa na majukumu yaliyopaswa kutekelezwa ambapo fedha hizo kidogo hazitolewi pia kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari 2015, Kamati imepokea na kuchambua Miswada ya Sheria ifuatayo:-

Mosi, Muswada wa Binafsi wa Kuundwa Baraza la Vijana la Taifa wa Mwaka 2013. Kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Spika aliiikabidhi Kamati yangu kazi ya kupitia, kuchambua na kujadili Muswada Binafsi wa Kuundwa kwa Baraza la Vijana wa Mwaka 2015, Muswada au hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi hii, Kamati ilitoa fursa kwa wadau wote muhimu kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu Muswada huo. Baada ya kupitia kwa kina na kupata maoni ya wadau, mtoa hoja pamoja na maoni ya Serikali kuhusu Muswada huo Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao:-

Kwanza Kamati ilimpongeza mtoa hoja kwa kuona umuhimu wa kuundwa kwa Baraza la Vijana la Taifa lenye lengo mahususi la kuwaunganisha vijana wote nchini ili kuweza kuratibu shughuli zao za kiuchumi na za kijamii. Kamati

5 FEBRUARI, 2014

iliurejeshwa Muswada huo kwa Spika ili mtoa hoja aweze kuuboresha zaidi kwa kushirikiana na wadau, aidha kutoa fursa kwa wadau wengi nchini kuweza kushirikishwa kutoa maoni yao, hasa wadau walioko pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wachache ambao wengi wao ni wa Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Nchini, wa mwaka 2014 (*The Non Citizens (Employment Regulation) Act, 2014*), unakusudia kutunga Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni ya Mwaka 2014 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa ajira za wageni nchini.

Sheria hiyo itaweka mamlaka moja itakayoratibu na kurahisisha upatikanaji wa vibali vya ajira za wageni kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji, kudhibiti ajira za wageni zisizo rasmi na kuongeza uwajibikaji katika soko la ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetekeleza vyema jukumu la kupokea maelezo ya Serikali pamoja na maoni ya wadau, ilijadili na kuchambua Muswada kwa kuzingatia maoni ya wadau na Serikali ili kuboresha Muswada huu. Kamati imemaliza kazi na itatoa maoni na mapendekezo yake pindi Muswada huu utakapowasilishwa hapa Bungeni kwa ajili ya mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria Mbalimbali wa mwaka 2014 katika kitabu ambacho mmekabidhiwa ukurasa wa sita kwa mujibu wa karatasi niliyonayo hapa, mnaweza mkaona. Naomba taarifa yote hii iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Pili katika moja ya majukumu yake inaitaka Kamati kufuatilia taarifa za utendaji za Wizara inazozisimamia. Aidha, Kamati inao wajibu wa kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hiyo kwa mujibu wa lbara ya 63(3) (b) ya Katiba ya nchi yetu.

5 FEBRUARI, 2014

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetekeleza majukumu ya kuzifuatilia Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo katika maeneo yaliyopo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama ifuatavyo:-

Mosi, Benki ya Wanawake Tanzania ambayo ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wanawake kiuchumi na kuwawezesha kupata mikopo kwa riba na gharama nafuu kwa ajili ya kukuza mitaji yao ya kibiashara.

Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu kwani, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alielekeza kwamba Benki hii itakuwa ikipatiwa fedha kiasi cha Shilingi bilioni mbili kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kujengea uwezo Benki hii kuweza kujiendesha kibiashara kwa mujibu wa masharti ya Benki Kuu ambapo inaitaka Benki hii kujiendesha kibiashara pindi inapofikisha mtaji wa Shilingi bilioni 15. Kwa hiyo, Benki hii imeshindwa kujiendesha kibiashara kwa sasa kwa sababu ina mtaji wa Shilingi bilioni 8.7 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kutoa fedha Shilingi bilioni mbili kwa Benki hii, kwani kiasi ambacho kilitengwa mwaka 2012/2013 ni Shilingi bilioni 1.3, ndicho kilichotolewa na kiasi cha Shilingi milioni 700 hakikutolewa. Mwaka 2013/2014 kiasi cha Shilingi milioni 450 tu ndicho kilitolewa kati ya Shilingi bilioni mbili. Kwa hiyo, Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatengwa ili Benki hii izeze kukidhi mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hajjaridhishwa na utendaji wa Serikali katika kuimarisha Benki ambayo ni msaada mkubwa kwa wanawake wengi hasa wa vijijini. Aidha, Benki hii imeshindwa kuwafikia wanawake wengi wa vijijini kutokana na kuwa na mtaji mdogo kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

5 FEBRUARI, 2014

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ulinzishwa kutokana na Azimio la Bunge lililopitishwa Agosti, 1993 kwa mujibu wa Kifungu 17(1) cha Sheria ya *Exchaquer* na *Audit Ordinance Number 21* ya mwaka 1961 kama mojawapo ya mikakati ya kuwawezesha wanawake kujiimarisha na kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mfuko huu ni kuwawezesha wanawake wote walio katika Halmashauri kwa kuwakopesha fedha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na kupambana na umasikini kwa kuunda vikundi na kupatiwa mikopo. Imekuwa ni kawaida kwa Halmashauri nyingi nchini kutozingatia Sheria mbalimbali ikiwemo kutoa fedha kwa 5% ya mapato yao kwa ajili ya maendeleo ya wanawake. Kamati inasikitishwa na kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Halmashauri ambazo hazitengi 5% kama Sheria inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaipongeza Halmashauri ya Mji wa Korogwe na Halmashauri nyingine ambazo zimekuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa zimekuwa na utamaduni wa kutenga kiasi hicho cha fedha na kutumika kama kilivyokusudiwa. Kamati ilifanya ziara maeneo hayo na kujionea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu, hasa katika ngazi ya Kata na Vijiji, ingawa Taarifa ambazo tumezipokea mbele ya Kamati ni kwamba, kila mwaka wahitimu 4,900 wanahitimu katika Vyuo mbalimbali vya Maendeleo ya Jamii. Kuna upungufu wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wapatao 2,045.

Kwa hiyo, Kamati inaona umuhimu wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii kama chachu ya maendeleo katika Halmashauri. Hivyo, Serikali ione umuhimu kwa kutoa ajira kwa wahitimu hawa wa Vyuo mbalimbali vya Maendeleo ya Jamii, iwe kama ambavyo inafanyika kwa Walimu nchini. Wanapohitimu mchakato wao siyo mkubwa katika kupata

5 FEBRUARI, 2014

ajira. Kwa hiyo, ifanyike hivyo hivyo kwa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchakato wa kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu inapatikana katika Taarifa yetu na mtajisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu wa maagizo katika maeneo yaliyopo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira limekuwa ni tatizo sugu siyo tu kwenye nchi yetu bali duniani kote, hasa kwa vijana kutokana na fursa rasmi za ajira kutokuwepo. Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 3 Mei, 2014, Wizara iliieleza Kamati kuwa imeandaa programu ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu na kuibua fursa za ajira kwa vijana wapatao 840,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa utekelezaji wa programu ya kukuza ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa itachangia kupunguza umasikini nchini kama ilivyoainishwa katika Programu ya MKUKUTA II na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, yaani ile *Vision 2025* na kuwa mafunzo hayo yawafikie walengwa kwa kuanzia kada ya elimu ya chini hadi elimu ya juu kwa lengo la kuwanufaisha vijana wote nchini. Kamati inashauri fursa hizo za ajira zielekezwe pia kwa vijana wa vijijini ambao wanapenda kujajiri katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Mkapu aliwahi kusema kwamba, "Mtaji wa Masikini ni Nguvu zake." Kwa hiyo, vijana wa maeneo ya Vijijini kwa kutumia nguvu zao wakiwezesha mitaji, wanaweza kujajiri katika kilimo na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza programu mbalimbali za maendeleo, Wizara ilitengeka Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuanza utekelezaji kwa mwaka wa fedha

5 FEBRUARI, 2014

2014/2015. Kamati inapenda kufahamu kutoka Serikalini juu ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji. Aidha, Kamati inampongeza Mkuu wa Mkoa wa Geita, Ndugu Fatma Mwasa; Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Ndugu Mwantumu Mahiza na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Ndugu Yahaya Nawanda kwa kuongoza kwa mfano na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana katika maeneo yao. Kamati yangu inawataka Viongozi wa ngazi mbalimbali nao kuiga mfano huu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro ya Wafanyakazi. Pamoja na kuwepo kwa Sheria zinazosimamia masuala ya kazi na ajira nchini kama vile Sheria Na. 6 na Na. 7 zote za mwaka 2004, bado kumekuwepo na migogoro mingi sehemu za kazi kama vile kwenye migodi, viwanda, makampuni na mashirika mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua migogoro hiyo sehemu za kazi, Wizara ilifanya jumla ya kaguzi 1,712 kupitia OSHA katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Ukaguzi huo uligundua kwamba baadhi ya wafanyakazi hawana mikataba ya kudumu ya ajira, wanafanyishwa kazi kwa saa nyingi zaidi kinyume na Sheria na utaratibu, hawapewi likizo na hawalipwi kima cha chini cha mshahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika kushughulikia tatizo hili ambalo ni sugu. Serikali ilieleze Bunge hili kwa nini kumekuwa na kuachishwa kazi hovyoy kwa wafanyakazi wengi hasa wa migodini hasa katika Mgodini wa Bulyanhulu kule Kahama. Kamati yangu imekutana na Wafanyakazi zaidi ya 30 pale Dar es Salaam, lakini zaidi ya 20 hapa Dodoma kutoka kwenye Mgodini wa Bulyanhulu, Wengi wao wakiwa na afya dhaifu, wameachishwa kazi, hawalipwi stahiki zao, kwa hiyo, Serikali katika hili itueleze ni kwa nini mgodi huu umekuwa na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pensheni ya Wazee. Wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote kwa kuwa wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema,

5 FEBRUARI, 2014

malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati ilishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.

Aidha, katika kikao cha Kamati, Wizara ilitoa maelezo kuwa Wizara ilikamilisha Rasimu ya Mpango wa Pensheni kwa Wazee mwezi Septemba, 2013 ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za uzoefu kutoka nchi nyingine na kuandaa mapendekezo ya mfumo wa pensheni kwa wazee kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo kutoka nchi zilizotembelewa na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Pensheni kwa Wazee kuweza kutungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lifahamu ajenda hii imeishia wapi? Matibabu kwa wazee, ulinzi wao pia unaratibiwa na nani? Kama Serikali haina mpango wa kutekeleza jambo hili ni vyema ikasema ukweli kuliko kuendelea kusuasua kama ilivyo hivi sasa. Ni vema tuseme ukweli Watanzania waelewe kwamba hakuna pensheni kwa wazee kuliko kuendelea kuwapa moyo wananchi na Watanzania Wazee hawa, jambo ambalo litakuwa siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa maagizo katika Wizara Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kuangalia Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC). Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni chombo cha habari cha Umma kinachomiliki mitambo ya Redio na Televisheni iliyoko maeneo mbalimbali ya nchi. Moja ya majukumu ya kuanzishwa kwa Shirika hili ni kuhakikisha kuwa matangazo ya Redio na Televisheni yanasikika nchi nzima na yanakuwa hewani kwa saa 24.

5 FEBRUARI, 2014

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji, *TBC*, mpaka sasa limeshindwa kukamilisha ujenzi wa jengo ambalo jiwe la msingi liliwekwa tarehe 10 Aprili, 1995 na Rais Mstaafu, Mzee Mwinyi. Hadi leo ni zaidi ya miaka 20 jengo lile ambalo lingetumika kama *Administrative Block* halijakamilika, hakuna dalili yoyote. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali itueleze imekwama nini? Kwa miaka 20 kwa nini jambo hili halimalizwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taswira ya *TBC* haifanani na taswira ya vyombo vingine vya Umma. Hata ukienda Kenya, *South Africa* na maeneo mengine kama Ethiopia Kamati yangu imefika, taswira ya chombo hiki bado hailingani na hali halisi na taswira halisi na heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uandishi wa Habari ni taaluma muhimu sana duniani, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya Waandishi wa Habari kupigwa, kunyanyaswa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kamati yangu inaitaka Serikali kukomesha vitendo hivi haramu, na hivyo azimio la kuletwa Muswada wa Habari ni moja kati ya kilio kikubwa cha Kamati yangu na tunashukuru na tunaipongeza Serikali kwamba, Muswada huo utakuja kwenye Bunge la mwezi wa Nne.

Tunaipongeza Serikali na tunataka iendeele kushirikiana na Waandishi wa Habari kwani na wao wamekuwa ni mchango mkubwa katika kuleta utulivu na amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Nchini Tanzania ulianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kutoa mikopo midogo midogo yenye gharama nafuu itakayowawezesha vijana kujijiri wenyewe.

Suala la kuwawezesha vijana kujijiri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa na hii ni kutokana na ukweli kwamba vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Ukweli ni kwamba vijana ndio kundi kubwa katika jamii. Tafizo kubwa katika kuwawezesha vijana

5 FEBRUARI, 2014

ni ukosefu wa rasilimali fedha ambayo ingetumika kutoa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali na ufuatiliaji wa shughuli za vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwaendeleza vijana kwani kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitenga Shilingi bilioni sita kwa ajili ya mikopo ya vikundi kwa vijana vya uzalishaji mali; maeneo mbalimbali Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yenu mtashuhudia. Hadi kufikia Machi, 2014 kati ya hizo Shilingi bilioni sita, Serikali ilikuwa imetoa Shilingi bilioni mbili. Kamati inaitaka Serikali sasa kutoa Shilingi bilioni nne zilizobaki ili vijana waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyopo chini ya Wizara inazosisimamia ili kujiridhisha na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba tarehe 30/01/2014 na kufanya ukaguzi wa kina na kupokea taarifa ya utekelezaji na maendeleo ya Chuo. Kamati ilipata pia taarifa ya mafanikio pamoja na chagamoto zinazokikabili Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Chuo hicho kiliweza kukarabatiwa miundombinu yake ya maji safi na salama, kuchimba visima virefu, kukarabati mabweni na nyumba sita za kuishi watumishi, ujenzi wa maktaba ya Chuo, kuweka mifumo ya umeme, kuendeleza watumishi wake na kukusanya na kuendelea na kazi ya kukusanya maduhuli. Kwa hiyo, Kamati yangu iliridhika sana na iliipongeza sana Serikali kwa kukijali Chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Kamati iliridhika na maendeleo ya Chuo hiki, lakini kuna tatizo kubwa la mgogoro baina ya Chuo Cha Rungemba na Kijiji ambacho Chuo hiki kipo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kutueleza kwa kuwa Kamati ilitoa maelekezo kwa Serikali kutaka mgogoro huu umalizwe. Ni imani yangu kwamba Bunge hili litaelezwa

5 FEBRUARI, 2014

namna gani mgogoro huu wa zaidi ya miaka 25 umechukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha tarehe 31 Januari, 2014 na kuelezwa juu ya mafanikio ya Chuo ikiwemo kuongezeka kwa kiwango cha udahili wa wanafunzi. Aidha, tangu Chuo kianze kimeweza kutoa mafunzo ya maendeleo ya jamii na jumla ya wahitimu 1,556 waliweza kukamilisha masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya ongezeko hilo la wanafunzi mwaka hadi mwaka, Chuo kinakumbana na changamoto nyingi ikiwemo matatizo ya watumishi kutokulipwa madai yao mbalimbali kwa zaidi ya miaka minne na wengine kutokupandishwa madaraja yao kwa muda mrefu. Aidha, kiwango cha fedha kinachorudishwa Chuoni kutokana na fedha zinazopokelewa kwenye *Retention Account* ni kidogo sana na kiasi hicho kidogo hakirudishwi kwa wakati na hivyo kukwamisha shughuli za uendeshaji wa Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hiki hakina usafiri, kina Wanachuo wengi, wakipatikana wagonjwa nini kitaendelea pale? Kwa hiyo, tuliishauri Serikali kuhakikisha kwamba kwa kushirikiana na TRA, katika Taarifa yetu, pia tuliandika katika bajeti iliyopita kwamba kiombewe magari; yako magari mengi huko Bandarini Serikali inashika, watu wamekimbia kodi ili yaweze kusambazwa katika Vyuho hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Oktoba, 2014 Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilitembelea miradi inayosimamiwa na Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) iliyo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ambayo ni mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi, mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni na mradi wa mji wa kisasa (*Dege Eco Village*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi unaotekelezwa na Shirika hili la

5 FEBRUARI, 2014

NSSF ulikaguliwa katika ziara iliyofanyika tarehe 28 Oktoba, 2014. Katika ziara hiyo, Kamati ilijionea na kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo na kushuhudia baadhi ya nyumba zikiwa zimeanza kutumika kwa wananchi waliokidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilitembelea Mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni ambapo ujenzi wake ulianza rasmi mwaka 2012 chini ya Mkandarasi wa *China Railways Construction Engineering Group* ikishirikiana na Kampuni ya *China Major Bridge Engineering Co. Ltd*, zote kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), limetakiwa kuwekeza katika mradi huu asilimia 60 ya gharama zote, yaani Shilingi bilioni 248 au Dola milioni 143.5 sawa na Shilingi bilioni 248. Serikali ilikuwa imeji-*commit* kuwekeza asilimia 40 katika utekelezaji wa mradi huu. Lakini pia Serikali ilikuwa imeji-*commit* kuwalipa wale wote ambao wangeondolewa kupisha ujenzi wa mradi huo wa daraja la Kigamboni. Lakini hadi hivi leo Serikali haijatoa asilimia 40 iliyoahidi, lakini pia haijawalipa wale ambao wameondolewa pale wakiitaka *NSSF* kuwalipa wale watu. Kwa hiyo, asilimia 100 yote sasa inafadhiliwa na *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kamati imeishauri Serikali kwa kuwa sasa *NSSF* inaidai Serikali zaidi ya Shilingi bilioni 811 na kwa mujibu wa makubaliano yao, ilitakiwa ifikapo mwaka 2014 Serikali iwe imetoa Shilingi bilioni 301, tunaishauri Serikali kutoa fedha hizo ili *NSSF* iweze kutekeleza majukumu yake. Kama Serikali isipofanya hivyo, miradi ya ujenzi wa Kijiji cha Bunge itakwama, ujenzi wa Ofisi za Wabunge Majimboni, utakwama, ujenzi wa Mji wa kisasa wa *Dege Eco Village* utakwama, lakini pia ujenzi wa Hospitali ya Apollo, Kigamboni utakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPF* nao wanaidai Serikali zaidi ya Shilingi bilioni 236 kutokana na dhamana ambayo waliingia kwenye ujenzi wa Jengo la Bunge ambalo tumo hii leo, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, hali kadhalika. Kutokana na changamoto hizo, mifuko hii inashindwa

5 FEBRUARI, 2014

kuboresha maslahi ya wanachama wake, kwa sababu fedha wanazotumia kuwekeza ni fedha ambazo ni michango ya wanachama. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali iweze kuzingatia na kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitia pia Mradi wa Kituo cha kurushia matangazo ya redio, ambayo kwenye Taarifa inasomeka, pale eneo la Mafifi Gangilonga, Iringa. Kwa hiyo, huduma za redio na *television* kule Iringa zimeongezwa sana kutokana na kuanzwa kwa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea Mradi wa kuhamisha mitambo ya kurushia matangazo (*FM Transmitter*) kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kwenda Mlima Kola. Kutokana na hivyo, imeongeza zaidi usikivu wa redio katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Wilaya ya Temeke. Kamati ilipata fursa ya kukutana na Kikundi cha Sokoine *Youth Development* kilichokopeshwa Shilingi milioni tano. Wanafanya kazi ya kulima matikiti kule na Kamati iliridhishwa na kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea kikundi cha *Waungwana Youth Family*, ambacho nacho kilikopeshwa fedha Shilingi milioni tano. Wanarejesha vizuri na Kamati iliwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati yangu ilifurahishwa sana na kikundi cha *African Legends* ambao wao ni vijana wasomi waliomaliza Vyuo Vikuu. Wameanzisha mgahawa wao. Vijana wale wanahudumia wateja wao wenyewe na baada ya kazi hizo, wanafanya kazi zinazoambatana na taaluma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kamati yangu iliwapongeza sana na iliomba Serikali iwaongeze kiasi cha mkopo zaidi ili waweze kutimiza malengo yao kama walivyokusudia. Tunaipongeza Serikali kwa kuwakopesha vijana wale Shilingi milioni saba.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Mashine za Kielektroniki Uwanja wa Taifa. Kamati yangu ilifanya *TFF* kwa kushirikiana na *CRDB* wameanzisha mfumo mpya viwanja vyetu vya michezo kufunga mashine za kielektroniki. Kamati yangu iliona mfumo ule hajjaridhika kwa sababu elektroniki haionekani inaonekana ni *manual*. Kwa hiyo tiketi zinanunuliwa mkononi, kwenye magari, kwa hiyo ufanisi wa mfumo huu umekuwa ni dhaifu.

Kamati yangu imeshauri wadau wanaohusika *TFF* kupitia Wizara inayohusika *CRDB* lakini wamiliki wa viwanja hivyo huwezi kuingia mkataba wa kufunga mashine za elektroniki kwenye viwanja ambavyo si mali yako, halafu wenyewe hawapo kwenye mkataba. Viwanja mali ya CCM ninyi mnaingia mkataba mnaendesha hamjui wenyewe wadau wakubwa ambao ni klabu zenyewe hazimo kwenye mkataba, kwa hiyo hapa tuliona ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, Kamati yangu imeomba Serikali ifuatilie jambo hili ili kupitia mfumo ule na Kamati haipingi matumizi ya elektroniki kwa sababu ndiko dunia inakoelekea sasa. Kamati inachosema jambo hili liboreshwe ili kuweze kupatikana ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati sasa. Baada ya kueleza hayo kwa muhtasari na naamini taarifa yangu yote haya mtayaona kwenye vitabu mlivyokabidhiwa, sasa niende kupitia mapendekezo, maoni na ushauri wa Kamati. Kwanza Kamati inapendekeza kuwa Serikali ihakikishe fedha kwa Wizara hizi zitolewe kwa wakati na kwa kiwango kilichopitishwa. Wizara ya Maendeleo ya jamii mwaka jana wamepata shilingi bilioni nne kwenye bilioni kumi na sita, kwa hiyo tunaona jambo hili ni tafizo kubwa. Kwa hiyo, kama Bunge ilipitisha bilioni kumi na sita kwanza ni fedha ndogo, sasa angalau fedha hizo bilioni kumi na sita zitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuhusu benki ya Wanawake Kamati inaitaka Serikali kutoa kiasi chote cha fedha ambacho hakikupelekwa kwenye benki ya wanawake ili kuifanya benki hii kujijendesha kibiashara na kuwafikia

5 FEBRUARI, 2015

wanawake wengi popote walipo nchini. Kamati pia inapendekeza kuwa Halmashauri zote nchini ambazo hazitengi asilimia tano (5%) ya wanawake na asilimia tano (5%) ya vijana ziorodheshwe na zichukuliwe hatua kali na kuzitambua Halmashauri zinazofanya vizuri kama ile Halmashauri ya Mji wa Korogwe, hata Halmashauri ya Lindi ili wapewe pongezi zao, ni motisha kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna tatizo kubwa la ajira nchini na kwa kuwa inabainika wazi kuwa mfumo wetu wa elimu unasababisha wahitimu wengi kutegemea kuajiriwa Serikalini badala ya kujajiri, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuangalia upya mfumo utakaowawezesha vijana wanapohitimu kuweza kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mapendekezo haya yote yanasomeka vizuri. Mwisho naliomba Bunge lako kuipokea, kujadili, kuiboresha na kuikubali taarifa hii pamoja na maoni na mapendekezo tuliyoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. MUSTAFA H. MKULO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII KWA KIPINDI CHA
KUANZIA MACHI, 2014 HADI JANUARI, 2015 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, Kanuni ya 117(15), naomba kutoa

5 FEBRUARI, 2015

taarifa ya shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2014 hadi Januari 2015.

1.1 MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Pili, Kanuni ya 6(7), Kamati ya Maendeleo ya Jamii itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- a) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;
- b) Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; na
- c) Wizara ya Kazi na Ajira.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni hizo yafuatayo ni majukumu ya Kamati Maendeleo ya Jamii;

- i. Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;
- ii. Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iii. Kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iv. Kushughulikia Taarifa za utendaji kazi za Wizara hizo; na
- v. Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

SEHEMU YA PILI

2.0. KAZI ZILIZOTEKELEZWA

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, Kanuni ya 117(7) Kamati ya Maendeleo ya Jamii imefanya kazi ya kujadili Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015, kuchambua na kujadili Miswada ya Sheria iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kufuatilia taarifa za utendaji kazi wa Wizara inazozisimamia na kufanya ziara za kukagua miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara zilizopo chini ya Kamati hii.

5 FEBRUARI, 2015

2.1 KUJADILI BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 Aprili hadi tarehe 4 Mei, 2014 kwa lengo la kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara inazosisimamia.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara husika, Kamati iliona changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazosisimamia kutokana na ukosefu wa fedha kutoka Hazina. Kwa kifupi Wizara kutopewa fedha kwa wakati imepelekea Wizara hizo kutotekeleza majukumu yao kwa wakati kama takwimu zinavyosomeka kwenye jedwali hapo chini:-

Jedwali Na. 1

MWAKA	WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO			WIZARA YA KAZI NA AJIRA			WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO		
	Kiasi Kilicho - idhini-shwa	Kiasi Kilicho-tolewa	Asilimia %	Kiasi Kilicho-idhini-shwa	Kiasi Kilicho-tolewa	Asilimia %	Kiasi Kilicho - idhini-shwa	Kiasi Kilicho-tolewa	Asilimia %
2013/2014	Bilioni 17.3	Bilioni 5.3	28	Bilioni 13.3	Bilioni 9.9	74	Bilioni 35.6	Bilioni 28.4	80
2014/2015	Bilioni 16.6	Bilioni 4.3	26	Bilioni 17.6	Bilioni 6.1	34	Bilioni 36.6	Bilioni 14.7	40

Mheshimiwa Spika, kwa mtiririko huo unaweza kuona namna ambavyo bajeti katika kila Wizara inavyopata fedha kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa ambapo fedha hizo kidogo hazitolewi kwa wakati.

2.2 MISWADA YA SHERIA

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati imepokea na kuchambua Miswada ya Sheria ifuatayo:-

5 FEBRUARI, 2015

a) Muswada wa Binafsi wa Kuundwa Baraza la Vijana la Taifa wa Mwaka 2013;

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013 uliikabidhi Kamati yangu kazi ya kupitia, kuchambua na kujadili Muswada Binafsi wa Kuundwa Baraza la Vijana la Taifa wa Mwaka 2013 wa Mhe. John Mnyika, Mb, unaohusu kuundwa kwa Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi hii Kamati ilitoa fursa kwa wadau wote muhimu kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu Muswada huo. Baada ya kupitia kwa kina na kupata maoni ya wadau, mtoa hoja pamoja na maoni ya Serikali kuhusu Muswada huo Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimpongeza mtoa hoja kwa kuona umuhimu wa kuundwa kwa Baraza la Vijana la Taifa lenye lengo mahsusi la kuwaunganisha vijana wote nchini ili kuweza kuratibu shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Kamati iliurejesha Muswada huo kwa Spika ili mtoa hoja aweze kuuboresha zaidi kwa kushirikiana na wadau, aidha kutoa muda wa kutosha kwa vijana kutoa maoni kwa uwazi na kwa wingi zaidi.

b) Muswada wa Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Nchini, 2014 (*The Non Citizens (Employment Regulation) Act, 2014*;

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni ya Mwaka 2014 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa ajira za wageni nchini. Sheria hiyo itaweka mamlaka moja itakayoratibu na kurahisisha upatikanaji wa vibali vya ajira za wageni kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji, kudhibiti ajira za wageni zisizo rasmi na kuongeza uwajibikaji katika soko la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetekeleza vyema jukumu la kupokea maelezo ya Serikali pamoja na maoni ya wadau,

5 FEBRUARI, 2015

ilijadili na kuchambua Muswada kwa kuzingatia maoni ya wadau na Serikali ili kuboresha Muswada huu. Kamati imemaliza kazi na itatoa maoni na mapendekezo yake pindi Muswada utakapowasilishwa Bungeni.

c) Muswada wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2014 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Act, 2014.*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na wadau na kujadili vipengele mbalimbali vya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2014. Aidha, Kamati imemaliza kuchambua na kujadili Muswada huu na imetoa maoni na mapendekezo yake kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo itawasilisha maoni yake ya jumla kuhusu Muswada huo.

2.3 UFUATILIAJI WA TAARIFA ZA UTENDAJI ZA WIZARA

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Pili katika moja ya majukumu yake inaitaka Kamati kufuatilia taarifa za utendaji za Wizara inazosisimamia. Aidha, Kamati ina wajibu kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetekeleza majukumu ya kuzifuatilia Wizara kama ifuatavyo:-

2.3.1 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ufuatiliaji wa utendaji na utekelezaji wa maagizo katika maeneo yaliyopo chini ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

i. Benki ya Wanawake Tanzania

Mheshimiwa Spika, Benki hii ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha

5 FEBRUARI, 2015

kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara. Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu.

Wakati Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, akielezea dhumuni la kuanzishwa kwa Benki hii alisema Serikali itatoa jumla ya **shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=)** kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha benki hii kuimarika kimtaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na mwaka 2011/2012 Benki ya Wanawake ilipokea kiasi cha **shilingi 2,000,000,000/=** kama ilivyoelekezwa. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 kiasi cha **shilingi 1,300,000,000/=** tu ndiyo kilitolewa na kiasi cha **shilingi 700,000,000/=** bado hakijatolewa na Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 kiasi cha **shilingi 450,000,000/=** tu ndiyo kimetolewa na Serikali na kiasi cha **shilingi 1,550,000,000/=** bado hakijatolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Tangu Benki ianzishwe mpaka sasa ni kiasi cha **shilingi 8,746,053,000/=** tu ndiyo kilichopo kama mtaji, na kufutia Sheria za Benki Kuu ya Tanzania ili Benki iweze kujiendesha kibiashara inapaswa iwe na mtaji kuanzia **shilingi 15,000,000,000/=**.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na utendaji wa Serikali katika kuimarisha Benki ambayo ni msaada mkubwa kwa wanawake wengi hasa wa vijijini, aidha Benki hii imeshindwa kuwafikia wanawake wengi wa vijijini kutokana na kuwa na mtaji mdogo.

ii. Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu ulinzishwa kutokana na Azimio la Bunge lililopitishwa Agosti, 1993 kwa mujibu wa Kifungu 17(1) cha Sheria ya *Exchaquer and Audit Ordinance (Cap. 439) No. 21* ya mwaka 1961 kama mojawapo ya mikakati ya kuwawezesha wanawake kujiimarisha na kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, Dhamira ya Mfuko huu ni kuwawezesha wanawake wote walio katika Halmashauri kwa kuwakopesha fedha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na kupambana na umaskini kwa kuunda vikundi na kupatiwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Imekuwa ni kawaida kwa Halmashauri nyingi kutozingatia sheria inazozitaka kutenga asilimia tano (5%) ya mapato yao kwa ajili ya maendeleo ya wanawake, Kamati inasikitishwa na kuitaka Serikali kuchukua hatua dhidi ya Halmashauri ambazo hazitengi asilimia tano kama Sheria inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Halmashauri ya Mji Korogwe na Halmashauri nyingine ambazo zimekuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa zimekuwa na utamaduni wa kutenga kiasi hicho cha fedha na kutumika kama kilivyokusudiwa.

iii. Ajira kwa Wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

Mheshimiwa Spika, Kuna upungufu mkubwa wa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika Halmashauri na hasa katika kata kwa idadi ya 2,045 licha ya kwamba vyuo vyetu vinaendelea kutoa wastani wa idadi ya wahitimu 4,900 kila mwaka. Kamati bado inaona umuhimu wa wataalamu wa maendeleo ya jamii kama chachu ya maendeleo katika Halmashauri, hivyo Serikali ione umuhimu wa kutoa ajira hizo. Aidha wahitimu wanapomaliza masomo yao waajiriwe moja kwa moja kama ilivyo kwa walimu.

iv. Mchakato wa kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Chuo kujitegemea uliwasilishwa kwa Waziri wa Elimu ambaye ana dhamana ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi vilivyo chini ya Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE). Baada ya Waziri wa Elimu kuridhia na kusaini, Muswada ulipelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri, uandishi wa kisheria na uchapaji.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada ulichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 9 la Tarehe 25/01/2013 kwa jina la *Tengeru Institute of Community Development (Establishment Order, 2013)*. Muswada wa kukibadilisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru ili kujiendesha kama Taasisi ya Elimu ya Juu uliletwa Bungeni, tunaipongeza Serikali kwa kukamilisha mchakato huu.

2.3.2 Wizara ya Kazi na Ajira

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ufuatiliaji wa utendaji na utekelezaji wa maagizo katika maeneo yaliyopo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira kama ifuatavyo:-

i. Tatizo la Ajira

Mheshimiwa Spika, Suala la ajira limekuwa ni tatizo sugu hasa kwa vijana kutokana na fursa rasmi za ajira kutokuwepo. Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 3 Mei, 2014 Wizara iliieleza Kamati kuwa wameandaa programu ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu na kuibua fursa za ajira 840,000.

Kamati inaona kuwa utekelezaji wa programu ya kukuza ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa itachangia kupunguza umaskini nchini kama ilivyoainishwa katika Programu ya MKUKUTA II na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na kuwa mafunzo hayo yawafikie walengwa kwa kuanzia na kada ya elimu ya chini hadi elimu ya juu kwa lengo la kuwanufaisha vijana wote. Kamati inashauri fursa hizo za ajira zielekezwe pia kwa vijana wa vijijini ambao wanapenda kujijiri katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza programu mbalimbali za maendeleo Wizara imetengewa **shilingi 3,000,000,000/=** kwa ajili ya kuanza utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kamati inapenda kufahamu kutoka Serikalini juu ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, aidha Kamati inampongeza Mkuu wa Mkoa wa Geita Ndugu Fatma

5 FEBRUARI, 2015

Mwasa, Mkuu wa Mkoa wa Lindi Ndugu Mwantumu Mahiza na Mkuu wa Wilaya ya Iramba Ndugu Yahaya Nawanda kwa kuongoza kwa mfano na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana. Viongozi wengine waige mfano wao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Wizara sasa kulieleza Bunge hili utekelezaji wa mpango huo.

ii. Migogoro ya Wafanyakazi

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuwepo kwa sheria zinazosimamia masuala ya kazi na ajira nchini kama vile Sheria Namba 6 na 7 zote za mwaka 2004 bado kumekuwepo na migogoro mingi sehemu za kazi kama vile katika migodi, viwanda, makampuni na mashirika.

Mheshimiwa Spika, Katika kutatua migogoro hiyo sehemu za kazi, Wizara ilifanya jumla ya kaguzi 1,712 katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Katika ukaguzi huo iligundulika kwamba baadhi ya wafanyakazi hawana mikataba ya ajira; wanafanyishwa kazi kwa saa nyingi zaidi; hawapewi likizo na hawalipwi kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika kushughulikia tatizo hili ambalo ni sugu, Serikali ilieleze Bunge ni kwa nini kumekuwa na kuachishwa kazi hovyoya kwa wafanyakazi wa migodini hasa katika Migodi wa Bulyanhulu, Kahama bila kulipwa stahili yao.

iii. Pensheni ya Wazee

Mheshimiwa Spika, Wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote kwa kuwa wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati ilishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa

5 FEBRUARI, 2015

Wazee. Aidha, katika kikao cha Kamati, Wizara ilitoa maelezo kuwa Wizara ilikamilisha Rasimu ya Mpango wa Pensheni kwa Wazee mwezi Septemba, 2013 ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za uzoefu kutoka nchi nyingine na kuandaa mapendekezo ya mfumo wa pensheni ya wazee kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo kutoka katika nchi zilizotembelewa na kuleta Bungeni Muswada ili Sheria ya Pensheni kwa Wazee kuweza kutungwa. Bunge lifahamu ajenda hii imeishia wapi na matibabu kwa wazee na ulinzi wao unaratibiwa vipi? Kama Serikali haina mpango wa kutekeleza jambo hili ni vyema ikasema ukweli kuliko kuendelea kusuasua kama ilivyo sasa.

2.3.3 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifuatilia utendaji na utekelezaji wa maagizo katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

i. Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni chombo cha habari cha umma kinachomiliki mitambo ya Redio na Televisheni iliyopo maeneo mbalimbali ya nchi. Moja ya majukumu ya kuanzishwa kwa Shirika hili ni kuhakikisha kuwa matangazo ya Redio na Televisheni yanasikika nchi nzima na yanakuwa hewani kwa saa ishirini na nne (24).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) mpaka sasa limeshindwa kukamilisha ujenzi wa jengo ambalo jiwe la msingi liliwekwa tarehe 10 Aprili, 1995 na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi. Awali jengo hilo lilikuwa likitengewa fedha za ujenzi katika mfuko wa maendeleo lakini baadaye fungu hilo lilisitishwa. Kamati ingependa kupata maelezo kupitia bunge lako tukufu juu ya usitishwaji wa fedha hizi kwani ni fedheha kubwa kwa chombo hiki kuwa na miundombinu chakavu na isiyo lingana na taswira ya nchi yetu.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, Katika kushughulikia kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo, Menejimenti ya TBC ilifanya makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupatiwa mkopo kwa utaratibu wa kudhaminiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Wizara ya Fedha imeshindwa kutoa tamko la kudhamini mkopo huo kwa asilimia mia moja na kuahidi kutoa dhamana ya asilimia 75 tu, Bunge hili lielezwe sasa ni lini jengo hili litakamilika.

ii. Taaluma ya Habari

Mheshimiwa Spika, Uandishi wa Habari ni taaluma muhimu sana duniani, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya Waandishi wa Habari kupigwa, kunyanyaswa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Kamati yangu inaitaka Serikali kukomesha vitendo hivi haramu, na hivyo azimio la kuletwa kwa Muswada wa Habari ni moja kati ya kilio kikubwa na cha muda mrefu cha Kamati hii.

iii. Maendeleo ya Mfuko wa Vijana

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Tanzania ulianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kutoa mikopo midogo midogo yenye gharama nafuu itakayowawezesha vijana kujijiri wenyewe. Suala la kuwawezesha vijana kujijiri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa na hii ni kutokana na ukweli kwamba vijana ndiyo nguzo na nguvu kazi ya Taifa na ukweli kwamba vijana ndiyo kundi kubwa katika jamii. Tatizo kubwa katika kuwawezesha vijana ni ukosefu wa rasilimali fedha ambayo ingetumika kutoa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali na ufuatiliaji wa shughuli za vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwaendeleza vijana kwani mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitenga **shilingi 6,100,000,000/=** kwa ajili ya mikopo ya vikundi kwa vijana vya uzalishaji mali. Hadi kufikia Machi, 2014 **shilingi 2,000,000,000/=** zilitolewa na kutumika.

5 FEBRUARI, 2015

Pamoja na hayo, Kamati inaitaka Serikali kupeleka fedha zote zilizosalia ili kuifanya Wizara kuweza kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka huo kwani Kamati inaamini fedha hizi ni kidogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya vijana ambao hawana ajira.

2.4 ZIARA ZA KAMATI

2.4.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyopo chini ya Wizara inazosisimamia ili kujiridhisha na utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

2.4.2 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza moja ya majukumu yake Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

i. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba tarehe 30/01/2014 na kufanya ukaguzi wa kina na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maendeleo ya Chuo. Aidha Kamati ilipata pia taarifa ya mafanikio pamoja na chagamoto inazozikabili Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, Chuo kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kilikarabati miundombinu ya maji safi na salama kwa kuchimba kisima kirefu, kukarabati mabweni matatu na nyumba sita za kuishi watumishi, ujenzi wa maktaba ya chuo, kuweka mfumo wa umeme wa jua (*solar*), kuendeleza watumishi watano (5) kitaaluma kati yao watumishi wawili Shahada ya Uzamili, wawili Stashahada na mmoja mafunzo ya dereva mahiri pamoja na kuweza kukusanya maduhuli tangu mfumo wa *retention* kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kinakabiliwa na changamoto ya mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha

5 FEBRUARI, 2015

Rungemba na Chuo katika eneo lenye hekta 250. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Kamati ya Ardhi ya Wilaya tarehe 6/9/1989 iliridhia ugawaji wa eneo hilo kwa ajili ya matumizi ya chuo na kupatiwa ramani ya upimaji yenye usajili Na. 31195 wa tarehe 12/12/1990.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa tangu kupimwa kwa eneo hilo kumekuwa na mgogoro usioisha licha ya juhudi za uongozi wa Mkoa na Wilaya kuendelea kutafuta suluhu ya mgogoro huu. Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu hatua zilizochukuliwa katika kumaliza mgogoro huo wa muda mrefu.

ii. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha tarehe 31 Januari, 2014 na kueleza juu ya mafanikio ya chuo ikiwemo kuongezeka kwa kiwango cha udahili wa wanafunzi kutoka 112 mwaka 2009 hadi 651. Aidha, tangu chuo kianze kutoa mafunzo ya maendeleo ya jamii mwaka 2009 hadi 2013 kimetoa jumla ya wahitimu 1556.

Mheshimiwa Spika, mbali ya ongezeko hilo la wanafunzi mwaka hadi mwaka, chuo kinakumbana na changamoto nyingi ikiwemo matatizo ya watumishi kutokulipwa madai yao mbalimbali kwa zaidi ya miaka minne na wengine kutokupandishwa madaraja kwa muda mrefu. Aidha, kiwango cha fedha kinachorudishwa chuoni kutokana na fedha zinazopelekwa kwenye *Retention Account* ni kidogo sana na kiasi hicho kidogo hakirudishwi kwa wakati na hivyo kukwamisha shughuli za uendeshaji wa chuo. Wizara iliahidi kulishughulikia tatizo hili, leo ni vyema Bunge lako lielezwe hatua zilizochukuliwa na Serikali.

2.4.3 Wizara ya Kazi na Ajira

Mheshimiwa Spika, Tarehe 28 Oktoba, 2014 Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilitembelea miradi inayosimamiwa na Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) iliyo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ambayo ni mradi wa ujenzi wa

5 FEBRUARI, 2015

nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi, mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni na mradi wa mji wa kisasa *Dege Eco Village*.

i. Mradi wa nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi

Mheshimiwa Spika, Mradi wa nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi unaotekelezwa na Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulikaguliwa katika ziara iliyofanywa tarehe 28 Oktoba, 2014. Katika ziara hiyo Kamati ilijionea na kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo na kushuhudia kwamba baadhi ya nyumba hizo zimeanza kutumika kwa makazi ya wananchi waliokidhi vigezo.

ii. Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigamboni

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea Mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambapo ujenzi wake ulianza rasmi mwaka 2012 chini ya mkandarasi *China Railway Construction Engineering Group* ikishirikiana na Kampuni ya *China Major Bridge Engineering Co. Ltd* zote za kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) limewekeza asilimia sitini (60%) ya gharama za ujenzi ambapo asilimia arobaini (40%) iliyobaki inatolewa na Serikali ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kulipia fidia kwa maeneo yaliyoathirika wakati wa utekelezaji wa mradi huu. Gharama za ujenzi zimeelezewa kuwa ni Dola za Kimarekani (US\$) 143.5 milioni sawa na **shilingi bilioni 248**. Aidha, ujenzi wa daraja hilo unakadiriwa kukamilika katika kipindi cha mwezi Juni 2015. Kamati iliridhika na maendeleo ya mradi na inaamini kwamba ifikapo mwezi Juni 2015 mradi utakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Hadi sasa NSSF imeendelea kuchukua hatua na juhudi za kuunusuru mradi huu kwani ahadi ya Serikali kuchangia 40% katika Mradi huu hajiatekelezwa. Kwa kufanya hivyo kuna uhatarishi wa utekelezaji wa mradi huu

5 FEBRUARI, 2015

kwa wakati, mkandarasi anadai fedha zake. Serikali pia iliahidi kuwalipa fidia wananchi ili kupisha mradi huu jambo ambalo halijafanyika. NSSF imeelemewa, Serikali timizeni ahadi yenu.

a) Madeni ya NSSF kwa Serikali

Mheshimiwa Spika, NSSF inaidai Serikali jumla ya **shilingi bilioni 811**, kati ya fedha hizo ilitakiwa Serikali iwe imeshalipa **shilingi bilioni 301** hadi kufikia tarehe 14 Novemba, 2014. Kutokana na Serikali kutotekeleza ahadi yake kwa NSSF upo uwezekano mkubwa kwa miradi ifuatayo kuathirika:-

- i. Mradi wa Ujenzi wa Kijiji cha Bunge;
- ii. Ujenzi wa Ofisi za Wabunge Majimboni;
- iii. Ujenzi wa Mji wa Kisasa wa *Dege Eco Village*; na
- iv. Ujenzi wa Hospitali ya Appolo Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kutoa kiasi cha fedha **shilingi bilioni 301** kwa NSSF ili kuinusuru miradi hiyo. Hali itakuwa mbaya.

b) Madeni ya PPF kwa Serikali

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2014 Mfuko wa Pensheni wa PPF unaidai Serikali shilingi **236,259,921.84/=** za Kitanzania. Fedha hizi ni pamoja na zile zilizogharamia:-

- i. Ujenzi wa Jengo la Bunge, Dodoma; na
- ii. Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Arusha.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na changamoto hiyo Mifuko hii inashindwa kuboresha maslahi ya wanachama wake, Serikali ilipe deni hili mapema iwezekanavyo.

iii. Mradi wa Mji wa Kisasa wa Dege Eco Village

Mheshimiwa Spika, Mradi wa mji wa kisasa wa *Dege Eco Village* uliopo katika mji wa Kigamboni jijini Dar es Salaam ni

5 FEBRUARI, 2015

mradi ambao utakuza na kuongeza hadhi kwa jiji la Dar es Salaam. Aidha, mradi huo unaashiria kukuza mji wa Kigamboni kwani utaongeza nyumba za kisasa zenye mpangilio madhubuti ambao ndani yake utakuwa na huduma zote muhimu kama zahanati, shule, maduka, vituo vya mabasi na kadhalika. Kazi ya ujenzi wa mradi huu inaendelea.

2.4.4 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Mheshimiwa Spika, Tarehe 29 Januari hadi 05 Februari, 2014 Kamati yako ilitembelea Mradi wa Vituo vya kurushia Matangazo ya Redio Mafifi, Iringa na Kola Hill, Morogoro vyenye thamani ya **shilingi 200,000,000/=** (milioni mia mbili) kwa pamoja.

i. Mradi wa kituo cha kurushia matangazo ya redio (FM Radio Transmitting Station) Mafifi Gangilonga, Iringa

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni kati ya miradi mikubwa ya kufunga mitambo ya kurushia matangazo katika vituo tisa (9). Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2010 kwa lengo la kupanua usikivu katika maeneo ambayo hayakuwa na huduma hiyo ya kupata matangazo ya redio. Maeneo mengine yaliyonufaika na mradi huu ni Mkoa wa Manyara, Morogoro, Moshi, Mpanda, Newala, Shinyanga, Songea na Tunduru.

Mheshimiwa Spika, Manufaa ya mradi huu ni pamoja na kupata matangazo ya redio kwa ubora zaidi, ambapo matangazo hayo yanapatikana katika masafa ya FM-TBC Taifa (107.1MHz) na TBC FM (96.2MHz), pia kuongezeka usikivu kwa matangazo ya TBC kwani kwa sasa yanasikika katika maeneo mengi zaidi nje ya mji wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa jitihada za kuboresha mfumo wa mawasiliano katika mji wa Iringa na Morogoro

5 FEBRUARI, 2015

ambayo inapelekea wananchi wengi wa maeneo hayo kupata matangazo ya redio na televisheni kwa urahisi.

ii. Mradi wa kuhamisha Mitambo ya kurushia matangazo (FM Transmitter) kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Morogoro kwenda Mlima Kola

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mradi huu ni mwendelezo wa mradi ambao awali uliwekwa kwa lengo la kupata matangazo ya redio katika eneo la Morogoro Mjini. Kutokana na ufinyu wa bajeti uliokuwepo kwa wakati huo mradi huu ulianza katika jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa mwaka 2010. Aidha, baada ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu ilibainika kuwa eneo bora litakaloweza mitambo hiyo kufungwa na kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi ni Mlima Kola.

iii. Ziara ya Kamati kutembelea Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Wilaya ya Temeke

Mheshimiwa Spika, Tarehe 19 Januari, 2015 Kamati ilifanya ziara ya kukagua Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulio chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliyopo katika Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam. Katika ziara hiyo miradi iliyotembelewa ni kikundi cha *Sokoine Youth Development*, *Waungwana Youth Family* pamoja na kikundi cha *African Legends*.

a) Sokoine Youth Development

Mheshimiwa Spika, kikundi hiki cha vijana kinajishughulisha na shughuli za kilimo cha umwagiliaji, ambapo wanalima matikitiki maji, mapasheni, mbogamboga na ufugaji wa kuku na bata, katika eneo la Kata ya Somangila, Kigamboni. Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana imeweza kutoa mkopo wa kiasi cha **shilingi 5,000,000/=** (milioni tano) kwa ajili ya maendeleo ya miradi ya kikundi hicho na marejesho yao kwa mwezi ni **shilingi 250,000** (laki mbili na elfu hamsini) na mpaka Kamati inafanya ziara vijana hawa

5 FEBRUARI, 2015

wamesharushisha **shilingi 500,000/=** (laki tano). Tunawapongeza vijana hawa.

b) Waungwana Youth Family

Mheshimiwa Spika, Kikundi hiki kinajishughulisha na mradi wa saloni ya kunyoa nywele pamoja na muziki wa kizazi kipyaa (*bongo flavour*) kwa kutunga nyimbo, kutoa santuri na kuziua ambapo wanapatikana katika Kata ya Sandali eneo la Temeke. Kikundi hiki kiliweza kukopeshwa jumla ya kiasi cha **shilingi 5,000,000/=** (milioni tano) na marejesho yao kwa kila mwezi yameanza kwa kiasi cha **shilingi 250,000/=** (laki mbili na elfu hamsini). Hadi Kamati inafanya ziara marejesho ya jumla yalikuwa ya **shilingi 500,000/=** (laki tano) yamefanyika.

c) African Legends

Mheshimiwa Spika, Kikundi hiki kinajihusisha na mradi wa mgahawa unaotoa huduma ya chakula, huduma ya stationery pamoja na ufundi wa kompyuta katika eneo la Kigamboni. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo uliweza kuwakopesha vijana hao kiasi cha **shilingi 7,000,000/=** (milioni saba) ikiwa marejesho yake kwa mwezi yameanza kwa kiasi cha **shilingi 350,000/=** (laki tatu na elfu hamsini), mpaka Kamati inafanya ziara yake marejesho ya jumla ya **shilingi 700,000/=** (laki saba) yalikuwafanyika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kutimiza wajibu wake kwa kusimamia fedha za mfuko wa vijana na kuhakikisha zimewafikia walengwa ambazo zimewasaidia wahusika kutimiza malengo yao ya kujikwamua kiuchumi.

Aidha Kamati inawapongeza vijana wa kikundi cha African Legends ambao wamehitimu elimu ya juu ngazi ya shahada katika vyuo vikuu vya hapa nchini na kuwa mfano wa kuigwa kwa vijana wengine wa Kitanzania kwa kuamua. Tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Wilaya ya Temeke, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mheshimiwa Abas Mtemvu, Mbunge

5 FEBRUARI, 2015

wa Jimbo la Temeke kwa ushirikiano wao mkubwa wanautoa kwa vijana hawa.

iv. Ukaguzi wa Mashine za Ki-elektroniki – Uwanja wa Taifa Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara tarehe 19 Januari, 2015 na kukagua jinsi mashine za Ki-elektroniki katika Uwanja wa Taifa kuona jinsi mashine hizo zinavyofanya kazi. Wajumbe walijionea jinsi watazamaji wa mchezo wa mpira wa miguu wanavyoingia kwa njia ya kawaida tofauti na maelezo kuwa wanatumia kadi za mfumo wa ki-elektroniki. Aidha, mfumo huo umethibitika kuwa hautumiki na Kamati haijaridhishwa na utaratibu wa ukataji tiketi unaotumika sasa. Kamati inaitaka Serikali kuitisha kikao cha wadau yaani Benki ya CRDB, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), wamiliki wa viwanja na klabu ili kuupitia upya mkataba na kuuangalia mfumo mzima wa uendeshaji.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI

Kutokana na Taarifa niliyowasilisha, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

- 3.1 Kamati inapendekeza kuwa Serikali ihakikishe fedha zinazotengwa kwa Wizara hizi zitolewe kwa wakati na kwa kiwango kilichopitishwa na Bunge.
- 3.2 **Mheshimiwa Spika,** Tangu Benki ya wanawake ianzishwe ni kiasi cha shilingi 8,746,053,000/= tu ndiyo kilichopo kama mtaji hadi hivi sasa tofauti na Sheria za Benki Kuu ya Tanzania inavyotaka kwamba ili Benki iweze kujiendesha kibiashara inapaswa iwe na mtaji kuanzia shilingi 15,000,000,000/=. Kamati inaitaka Serikali kutoa kiasi chote cha fedha ambacho hakikupelekwa kwenye Benki ya Wanawake ili kuifanya Benki hii kujiendesha kibiashara na kuwafikia wanawake wengi popote walipo hapa nchini.
- 3.3 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kuwa Halmashauri zote nchini ambazo hazitengi asilimia

5 FEBRUARI, 2015

tano (5%) ya wanawake na asilimia tano (5%) ya vijana ziorodheshwe na zichukuliwe hatua kali.

- 3.4 Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa kuna tatizo kubwa la ajira nchini na kwa kuwa inabainika wazi kuwa mfumo wetu wa elimu unasababisha wahitimu wengi kutegemea kuajiriwa Serikalini badala ya kujajiri, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iangalie mfumo bora utakawawezesha vijana kujajiri badala ya kusubiri kuajiriwa na Serikali kama ilivyo sasa.
- 3.5 Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa kuna kusuasua kwa ukamilishwaji wa jengo la shirika la utangazaji la Taifa (TBC) na kwa kuwa tayari menejimenti ya TBC ilishafanya makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupatiwa mkopo ambao Wizara ya Fedha iliahidi kudhamini kwa 75% ingawa haijatekeleza, Kamati inapendekeza kuwa Serikali ishughulikie haraka kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo lililochukua muda mrefu wa takriban miaka 20 kwani kwa kutokamilika kwa jengo hilo ni fedheha kwa Taifa.
- 3.6 Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa mgogoro wa ardhi baina Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba na Kijiji cha Rungemba umekuwa ni wa muda mrefu takriba miaka 25, Kamati inapendekeza kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kumaliza mgogoro wa ardhi kati ya Chuo cha Rungemba na wananchi.
- 3.7 Mheshimiwa Spika,** Kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika Halmashauri na hasa katika kata kwa idadi ya 2,045 licha ya kwamba vyyo vyetu vinaendelea kutoa wastani wa idadi ya wahitimu 4,900 kila mwaka. Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iajiri wataalamu wa maendeleo ya jamii moja kwa moja

5 FEBRUARI, 2015

wamalizapo masomo kama inavyofanyika kwa ajira za walimu.

- 3.8 Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kurudisha mfumo wa zamani wa fedha za maduhuli zinazokusanywa kupelekwa Hazina Ndogo (*retention at the source*) badala ya kutumia mfumo wa sasa (*retention account*) ambao una matatizo makubwa yanayopelekea Vyuho kushindwa kujiendesha.
- 3.9 Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa baada ya Kamati kutembelea uwanja wa Taifa na kutoridhishwa na mfumo wa ukataji tiketi kwa njia kielektroniki ulivyo hivi sasa, Kamati inaitaka Serikali kuangalia upya mfumo mzima wa ukataji tiketi wa Kielektroniki ili kuongeza mapato.
- 3.10 Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uinaidai Serikali jumla ya **shilingi bilioni 811 na kwa kuwa shilingi bilioni 301** ya fedha hizo zilitakiwa kulipwa hadi kufikia tarehe 14 Novemba, 2014, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuilipa NSSF kiasi cha shilingi bilioni 301 kama walivyokubaliana.
- 3.11 Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2014 Mfuko wa Pensheni wa PPF unaidai Serikali shilingi **236,259,921.84/=** za Kitanzania Kamati inapendekeza kwa Serikali kuulipa Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) fedha hizi ili mfuko huu utekeleze majukumu yake ipasavyo.

SEHEMU YA NNE

4.0 MWISHO

Mheshimiwa Spika, Natumia fursa hii kwa mara nyingine tena kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha

5 FEBRUARI, 2015

vikao vya Bunge. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Sophia Mattayo Simba, (Mb) Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, (Mb) Waziri wa Kazi na Ajira na Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara, (Mb) Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa ushirikiano mkubwa waliutoa kwa Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake.

Aidha, napenda kuwashukuru pia Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, (Mb) Naibu Waziri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, (Mb) Naibu Waziri Wizara ya Kazi na Ajira na Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, (Mb) Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru Ndugu Anna T. Maembe, Katibu Mkuu na Ndugu Nuru H. M. Milao, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Ndugu Erick Francis Shifindi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na Ajira; Ndugu Sihaba Nkinga, Katibu Mkuu na Profesa Elisante Ole-Gabriel, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, pamoja na Wakuu Idara, Vitengo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizi, kwa ushirikiano mzuri waliouonesha kwa Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao kwangu katika kipindi chote cha uongozi wangu kwa kuwa mawazo na ushauri wao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Naomba sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina:-

1. Mhe. Saidi Mohamed Mtanda, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Capt. John D. Komba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mb- Mjumbe

5 FEBRUARI, 2015

5. Mhe. Nasib Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Salum Halfan Barwany, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka, Mb- Mjumbe
9. Mhe. Salvatory Naluyaga Macheleli, Mb- Mjumbe
10. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb- Mjumbe
11. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agness Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Juma Othman Ali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jaddy Simai Jaddy, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Philip Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb -Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah akisaidiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndugu Theonest Ruhilabake, Makatibu wa Kamati, Ndugu Aziza Makwai na Ndugu Hanifa Masaninga, Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John kwa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati na pia kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mwisho naliomba Bunge lako Tukufu kuipokea, kuijadili na kuiboresha taarifa hii pamoja na maoni na mapendekezo yote.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Saidi Mohamed Mtanda, Mb

MWENYEKITI

5 FEBRUARI, 2015
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII
FEBRUARI, 2015**

MWENYEKITI: sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta karibu!

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KWA KIPINDI CHA
KUANZIA MACHI, 2014 HADI JANUARI, 2015
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

MHE. MARGARET S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nawashukuru wapiga kura wanawake wa Mkoa wa Tabora kwa ushirikiano wao wanaonipa. Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na pia wewe mwenyewe Mheshimiwa Kidawa Saleh kwa nafasi zenu mlizopewa mkioneshwa wanawake wanaweza hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba *Hansard* ichukue taarifa ya Kamati ya kudumu kama ilivyowasilishwa mezani kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika kipindi cha Mwezi Januari, 2014 hadi Januari, 2015, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Taarifa ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu matatu ikiwemo utangulizi, shughuli zilizotekelezwa na Kamati, maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, ni Kushughulikia bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati,

5 FEBRUARI, 2015

kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge chini ya Wizara hizo, kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo, kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara na kufuatilia Utekelezaji wa shughuli unaofanywa na Wizara husika kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii imeorodheshwa katika ukurasa wa tatu hadi nne wa taarifa yetu. Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa uliowezesha kupatikana kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa na Kamati zimeelezwa wazi kabisa na kwa kirefu kutoka ukurasa wa nne hadi ishirini na tisa, maoni na mapendekezo katika maeneo yote yaliyofanyiwa kazi katika kutekeleza shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na ilifanya vikao mbalimbali na wizara kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Wizara husika kwa miongozo na sera mbalimbali. Aidha Kamati ilichambua Miswada ya Sheria pamoja na kujadili maazimio ya Bunge, kuhudhuria semina na mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kuchambua hoja mbalimbali. Hali kadhalika, Kamati ilijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo Ufundi na Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii kwa mwaka 2014/2015 na kutoa Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti hizo kama zilivyojadiliwa na maoni yalitolewa katika Mkutano wa 15 wa Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao kati ya Kamati na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, jambo mojawapo kubwa lililojadiliwa ni Sera Mpya ya Elimu ambapo Kamati ilihimiza uzinduzi wa sera hii mapema iwezekanavyo. Kamati

5 FEBRUARI, 2015

pia ilijadili Mfumo wa Elimu nchini na umuhimu wa kuangalia upya mfumo wa elimu huu ili uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanyia kazi dhana ya matokeo makubwa sasa katika Sekta ya Elimu, huwezi kuepuka suala la kuhudumia Walimu jambo ambalo ni muhimu sana ili kuhakikisha Walimu wanapata haki zao kwa wakati, kupewa posho za mazingira magumu pamoja na mafunzo kazini ili wafanye kazi yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata fursa ya kujadili hatua zilizofikia katika kuunda Tume ya Utumishi wa Walimu Nchini yaani *Teachers Service Commission*. Taarifa ya Serikali ilieleza kwamba Tume hii ilitarajiwa kuzinduliwa mapema iwezekanavyo katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuhudumia Walimu wapatao zaidi ya laki mbili na sabini na sita kwa takwimu tulizopewa na TAMISEMI, chombo kimoja hakika kitasaidia kutatua kero nyingi za Walimu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Celina Kombani, ambaye angekuwepo ningefurahi angesikia yeye mwenyewe jinsi tunavyompongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko kubwa la taasisi za elimu nchini kwa mfano shule za msingi sasa hivi ni zaidi ya kumi na sita elfu, za Sekondari ni zaidi ya elfu nne, vyo vya ualimu ni zaidi ya mia moja thelathini na mbili. Taasisi hizi ni nyingi mno kiasi ambacho kuna umuhimu wa kuwa na ukaguzi imara na wa uhakika ili elimu itolewayo viwango vyake vijulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tulilionani ni muhimu sana ni mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Suala hili tuliliangalia sana kwa undani na hasa kuangalia kigezo cha uwezo wa familia ambacho tumeona ni muhimu sana kuzingatiwa ili kuwalenga wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato duni.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliona umuhimu wa kuimarisha lugha za kufundishia na kujifunzia, aidha, kuweka mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia kwa watu wenye mahitaji maalum jambo ambalo ni muhimu sana. Uboreshwaji wa shughuli za Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi yaani *NACTE* na kuwezesha pia *VETA* kutoa mafunzo zaidi ya ufundi kwa idadi kubwa ya vijana wanaokosa fursa ya maendeleo ya kuendelea na elimu ya juu, jambo ambalo litawasaidia kwa suala la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea miradi na taasisi mbalimbali za elimu ambapo ilikagua, ilitoa maoni na ushauri ambazo zinapatikana kwa uwazi zaidi ukurasa wa nne hadi ukurasa wa ishirini na tisa wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii suala la Bajeti ya Wizara hii lilijadiliwa kwa kina sana na hasa katika kuhimiza Serikali kuongeza bajeti katika Sekta ya Afya mwaka hadi mwaka ili kufikia asilimia 15 kama ilivyokubaliwa katika Azimio la Abuja la mwaka 2011. Bajeti katika sekta ya afya ikiongezeka itawezesha kuongeza ubora wa utoaji huduma za afya hususan suala zima la upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa kupitia Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa bajeti hii kutawezesha pia Taasisi za Matibabu ya Saratani *Ocean Road*, taasisi ya *MOI*, Kitengo cha Matibabu ya Moyo Muhimbili na Kitengo cha Matibabu ya Figo Muhimbili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, suala la utoaji wa Huduma kwa Mama na Mtoto na Huduma za Uzazi wa Mpango pia litaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watumishi katika sekta ya afya hususan katika maeneo ya pembezoni ulijadiliwa kwa kina na Kamati iliitaka Serikali kulitafutia ufumbuzi suala hili mapema iwezekanavyo. Kwa mfano mdogo tu, Wilaya ya Urambo ina zahanati 20, lakini katika zahanati hizi 20, ni zahanati sita tu ambazo zina *Clinical Officers* na kila zahanati inatakiwa iwe na *Clinical Officer*

5 FEBRUARI, 2015

mmoja au Afisa Tabibu. Kwa hiyo, ukiangalia kati ya 20 kwa hiyo ni sita tu ambazo zina *clinical officers*, huo ni mfano mmoja wapo wa uhaba wa watumishi katika Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii hasa katika maeneo ya pembezoni. Kamati pia ilijadili umuhimu wa serikali kuanzisha utoaji wa huduma za bima ya afya kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha kifedha idara ya ustawi wa jamii kulijadiliwa na Kamati iliona umuhimu wa Serikali kufanya uamuzi wa kuhamisha idara ya ustawi kuitoa kule iliko Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iende katika Ofisi za Waziri Mkuu yenye uwezo wa kuziagiza Wizara nyingine kuhudumia watu wenye mahitaji maalum kulingana na majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia Miswada ya Sheria mbalimbali ikiwemo Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Kemia wa Mwaka 2014, Muswada wa Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2014 na aidha Kamati ilijadili Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Utafiti wa Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutoa maoni na mapendekezo yake katika Mkutano wa 16 na 17 wa Bunge la Kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati. Kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu jambo kubwa ni Sera mpya ya Elimu. Uzinduzi wa Sera ya Elimu Kamati inasema ufanyike mapema iwezekanavyo ikiwemo kuweka mikakati ya utekelezaji wake. Kamati inasisitiza na kushauri yaani inasisitiza ushauri kwamba vyombo vya msingi katika utoaji wa elimu ambavyo ni Baraza la Mifihani Tanzania, Taasisi ya Elimu Tanzania na Ukaguzi wa Elimu vilindwe na viwezeshe kuendelea 2kuwa Mamlaka huru zinazojitegemea katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu nchini Serikali ichukue hatua za makusudi mapema iwezekanavyo, kuboresha mfumo wa utoaji wa elimu nchini ili kuweza kuzingatia mendeleo ya sayansi na teknolojia yanayoimarika

5 FEBRUARI, 2015

siku hadi siku. Hatua hii ni ya msingi katika kufikia maendeleo ya sekta mbalimbali ikiwemo maendeleo ya uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commission*). Pamoja na kupongeza Serikali kwa kusudio la kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu katika mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati inashauri kuwa, Serikali iangalie uwezekano wa Tume hii pia kupewa jukumu la kusajili Walimu wote nchini ikiwa ni pamoja wafanyakazi katika shule zisizo za Serikali. Hatua hii ni muhimu katika kutambua Walimu wote na kuweka kiwango cha msingi cha kutoa huduma kwa Walimu wote nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugatuaji wa sekta ya elimu nchini. Jukumu la utoaji mafunzo kazini kwa Walimu lisimamiwe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuweka utaratibu mahususi wa kuendeleza Walimu kitaaluma ili kukabiliana na changamoto za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ndani ya mfumo wa elimu nchini. Serikali inapoleta mabadiliko yoyote katika utoaji wa elimu nchini, ni muhimu Serikali iwashirikishe wadau pamoja na kuelimisha jamii kuhusu mabadiliko yanayotokea kabla ya utekelezaji ili kuepukana na mikanganyiko mbalimbali ambayo huwa inajitokeza. Mfano ni hivi karibuni mabadiliko yaliyofanyika katika Upangaji wa Alama za Ufaulu na Utunuku wa Madaraja katika Matokeo ya Mitihani ya Elimu ya Sekondari na pia hata ile utaratibu uliotumika haraka wa kubadili mafunzo ya cheti cha Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine ni utoaji wa mkopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Pamoja na utaratibu unaotumiwa na Bodi katika kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuzingatia masomo ya vipaumbele, suala la kulenga wanafunzi wanaotoka katika familia duni lizingatiwe. Serikali itumie mikakati ya makusudi kukusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa tangu mwaka

5 FEBRUARI, 2015

1991. Kamati inapendekeza Serikali kuona uwezekano wa wanufaika wa mikopo kufunga mkataba maalum na kuitumikia nchi katika maeneo mbalimbali kwa kipindi maalum na pia kupewa motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa elimu nchini. Kamati inasisitiza kwamba Serikali iimarishe na kuwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi zaidi kwa kusimamia viwango vya elimu inayotolewa nchini sambamba na ongezeko la taasisi mbalimbali zinazotoa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia. Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iimarishe lugha za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia Sera ya Elimu katika kutoa mafunzo kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu nchini ili kukabiliana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia kwa wenye mahitaji maalum. Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu kwa watu wenye mahitaji maalum kwa kutenga fedha za kutosha. Aidha, Serikali itoe mwongozo wa Kitaifa kuhusu ujenzi wa miundombinu ya shele na vyuo. Usajili wa shule uzungatie mahitaji ya kundi hili muhimu la watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Elimu la Ufundi (*National Council for Technical Education - NACTE*). Ili kukabiliana na changamoto ya ongezeko la vyuo vinavyotoa Elimu ya Ufundi bila kuzingatia vigezo vilivyowekwa na *NACTE*. Kamati inapendekeza kuwa Sheria ya Baraza la Elimu ya Ufundi ifanyiwe maboresho ya kupewa mamlaka zaidi kuchukua hatua ikiwemo kuvifungia vyuo ambavyo vinatoa mafunzo bila kupata ithibati kutoka *NACTE*.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya mazingira magumu kwa Walimu. Ili kuimarisha utoaji wa elimu hususan katika maeneo ya pembezoni, Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ili kuwafanya wabaki katika mazingira ya kazi na kuipenda taaluma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya VETA. Fedha za kuendeshea mafunzo ya ufundi yaani *Skills Development Levy* inayopelekwa kuhudumia mafunzo ya ufundi chini ya VETA iongezwe kutoka asilimia mbili hadi asilimia nne ili kuwezesha VETA kufanya kazi kikamilifu na pia kuweza kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) katika kutoa huduma ya mafunzo hayo muhimu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Baada ya Kamati kutafakari kwa kina kuhusu mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika ziara za Kamati katika kukagua shughuli za miradi ya maendeleo, Kamati inashauri fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati pia ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali ufanyike kwa kutumia kandarasi za VETA, Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa ili kuweza kutekeleza jukumu hilo kikamilifu na kwa uadilifu. Hatua hii ni muhimu katika kuokoa miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, jambo la kwanza ni bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutokidhi Azimio la Abuja. Tanzania iliridhia Azimio la Umoja wa Nchi za Afrika la Abuja mwaka 2001 linaloelekeza nchi wanachama kuwa ifikapo mwaka 2015 bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya afya ifikie asilimia 15 ya bajeti ya Serikali. Takwimu zinaonesha kwamba bajeti zinazotengwa katika sekta ya afya nchini hazikidhi Azimio hilo Kamati inashauri kwamba Serikali ijizatiti katika kuongeza vyanzo zaidi vya mapato ya ndani ili kuweza kufikia

5 FEBRUARI, 2015

asilimia 15 ya bajeti yake kama katika sekta ya afya kama walivyokubaliana. (Makofi)

Mheshimiwa Mweyekiti, kuhusu Bohari ya Dawa (*Medical Stores Department*), ili kuwezesha MSD na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali na vituo vya afya, Serikali ilipe deni lake kwa MSD lililofikia hadi kufikia Desemba 14 bilioni 93.3 ili tuweze kukabiliana na upungufu wa dawa vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali na vituo vya afya nchini. Aidha, fedha bajeti ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, vitolewe na Hazina katika mkupuo mmoja ili kumaliza tatizo la urasimu katika ununuzi na usambazaji dawa na vifaa tiba. Hali kadhalika Bunge lione umuhimu wa kutunga sheria maalum itakayoweka utaratibu maalum wa fedha za MSD kutengwa na kupelekwa moja kwa moja kama ilivyo fedha za ujenzi wa barabara.

Kuhusu Taasisi ya matibabu ya Saratani *Ocean Road*, Serikali ichukue hatua za makusudi za kudumu ili kuhakikisha kwamba mashine za tiba ya mionzi katika taasisi hii zifanye kazi wote. Aidha, hospitali ya rufaa za kanda ziweshwe kivifaa na wataalam wa kutoa huduma za msingi za matibabu hayo. Hospitali za Wilaya zijengewe uwezo wa kutoa huduma za awali za matibabu husika hatua hii itawezesha kupunguza msongamano wa wagonjwa katika taasisi hii.

Kuhusu Kitengo cha Matibabu ya Moyo Muhimbili, baada ya Kamati kukagua upatikanaji wa huduma za kipimo maalum za matibabu ya moyo kwa njia ya upasuaji kitiwacho *blood gas analyzer* ambayo hukodiwa kutoa huduma hii ikilinganishwa na ununuzi wake kwa lengo la kuepuka mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya uundaji wake. Kamati inashauri kwamba, Serikali iendelee kutoa huduma hii muhimu ili kupunguza gharama kwa Serikali kuhudumia matibabu hayo nje nchi. Aidha, Serikali iongeze kasi ya uwezeshaji kitengo hiki kuwa taasisi inayojitegemea ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu (Muhimbili MOI); Serikali iwekeze katika kununua

5 FEBRUARI, 2015

mashine za kisasa za uchunguzi. Kuweka vifaa na samani kwenye jengo jipya la *MOI* awamu ya tatu. Hatua hii itawezesha kupunguza changamoto ya msongamano wa wagonjwa pamoja na rufaa za matibabu nje ya nchi kwa upande wa mifupa, mgongo, nyonga na mishipa ya fahamu.

Kuhusu Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto na Huduma ya Mzazi wa Mpango, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango kwa asilimia 60 ya wanawake walio katika umri wa kupata mtoto ifikapo mwaka 2015, Serikali itenge fedha kuwezesha kufikia angalau asilimia ishirini ya mahitaji ya huduma za uzazi wa mpango nchini. Aidha, Halmashauri nazo zitenge fedha kuwezesha upatikanaji wa huduma hizo ikiwemo upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia kwa akinamama. Serikali iendelee kuhamasisha matumizi bora ya huduma ya uzazi wa mpango hususan katika maeneo ya vijijini.

Kuhusu Huduma ya Bima ya Afya kwa wananchi wote, Serikali iharakishe kukamilika kwa mpango maalum utakaowezesha upatikanaji wa huduma za Bima ya Taifa ya Afya kwa wananchi wote ikiwemo wasio na kipato ili waweze kupata huduma za afya nchini.

Kuhusu upatikanaji wa watumishi wa sekta ya afya katika maeneo ya pembezoni, Serikali iweke utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba wahitimu wa mafunzo katika taaluma za sekta ya afya, kwa udhamini wa Serikali watumike kutoa huduma za afya katika maeneo ya pembezoni kwa muda maalum. Aidha, motisha maalum itolewe kuwezesha watumishi wanaofanya kazi katika maeneo ya pembezoni waendeleo kubaki katika utumishi huo. Aidha, Serikali ifanye utaratibu wa kuaajiri watumishi katika sekta ya afya kwa kuwapata wanaotoka maeneo ya pembezoni na kuwaendelea kimafunzo.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa kuwa utolewaji wa huduma mbalimbali za jamii kwa watu wenye ulemavu ni sekta mtambuka, Idara ya Ustawi wa Jamii ifikiriwe kuhamishwa na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa ina mamlaka ya kutoa maelekezo kwa Wizara zote kutoa huduma kulingana na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo. Hatua inayopendekezwa itawezesha kuleta ufanisi katika upatikanaji wa huduma kama afya, elimu, ulinzi, miundombinu na sheria nyinginezo kwa kundi hili lenye mahitaji maalum.

Matumizi ya teknolojia ya *electronic* kukusanya maduhuli katika Taasisi za Wizara; ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato katika taasisi za Serikali ikiwemo taasisi za utoaji wa huduma za afya zikiwemo Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Mifupa yaani *MOI*, Serikali ichukue juhudi za makusudi za kutumia mfumo wa kisasa wa kieletroniki kukusanya maduhuli hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa majukumu yake katika kipindi cha mwezi Januari, 2014 hadi Januari, 2015. Naomba pia kuwashukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Seif Ali Rashid, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi Jamii Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe na aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Jenista Muhagama kwa kuipatia Kamati ushirikiano mzuri wakati wote katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuteuliwa katika nafasi hiyo muhimu kwa kuimarisha utolewaji wa elimu nchini. *(Makofi)*

Vile vile nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili zinazosimamiwa na Kamati hii pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa kazi nzuri wanayoifanya.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kasilillah kwa msada mkubwa waliotupatia na wanaoendelea kutupatia Kamati yetu wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. Hali kadhalika namshukuru Katibu wa Kamati, ndugu Happyness Ndalu, Chacha Nyakega na Stella Mlambo kwa kuihudumia vyema Kamati hii Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KWA KIPINDI CHA
KUANZIA MACHI, 2014 HADI JANUARI, 2015
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0: UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, naomba kuwasilisha Taarifa kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika kipindi cha Mwezi Januari 2014 hadi Januari 2015, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, kifungu cha 6(6) na kifungu cha 7(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati

5 FEBRUARI, 2015

hii ni kusimamia shughuli za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:

- i) Kushughulikia bajeti za Wizara zinazo simamiwa na Kamati,
- ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge chini ya Wizara hizo,
- iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo,
- iv) Kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara,
- v) Kufuatilia Utekelezaji wa shughuli unaofanywa na Wizara husika kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

1.2 Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii walioteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013 ni wafuatao:-

1. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb, - Mwenyekiti
2. Stephan H. Ngonyani, Mb - M/Mwenyekiti
2. Mhe. Zabein Mhaji Mhita, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb - "
4. Mhe. Agripina Z. Buyogera, Mb - "
5. Mhe. Faki Haji Makame, Mb - "
6. Mhe. Christowaja Gerson Mtinda, Mb - "
7. Mhe. Riziki Omari Juma, Mb - "
8. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje, Mb - "
9. Mhe. Antony G. Mbassa, Mb - "
10. Mhe. Ali Juma Haji, Mb - "
11. Mhe. Juma Sururu Juma, Mb - "
12. Mhe. Gregory George Teu, Mb - "

5 FEBRUARI, 2015

13. Mhe. Abia Muhama Nyabakari, Mb - “
14. Mhe. Salome D. Mwambu, Mb - “
15. Mhe. Mohamed Gulam Dewji, Mb - “
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - “
17. Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mb - “
18. Mhe. Asnain Muhamed Murji, Mb - “
19. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - “
20. Mhe. Abdulaziz Muhamed Aboud, Mb - “

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

2.1 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

2.1.1 Kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo Ufundi kwa mwaka 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Bunge liliidhinisha jumla ya **sh. 799,020,389,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii yalitolewa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi.

2.1.2 Vikao na Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utendaji kazi wa Wizara na taasisi zake, Kamati ilijadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kama ifuatavyo:

i) Sera Mpya ya Elimu ya Mwaka 2014

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali kuhusu muundo na hatua zilizofikiwa katika uundaji wa Sera Mpya ya Elimu nchini ilieleza kwamba rasimu ya sera imekamilika katika hatua zake na inasubiri uzinduzi rasmi. Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Vyombo vya msingi katika utoaji wa elimu nchini ikiwa ni pamoja na Baraza la Mitihani Tanzania (*National Examination Council of Tanzania -NECTA*) Taasisi ya Elimu Tanzania (*Tanzania Institute of*

5 FEBRUARI, 2015

Education -TIE), na Ukaguzi wa Elimu nchini vilindwe, kwa kuviwezesha kuendelea kuwa mamlaka kamili zinazojitegemea kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

- b) Baada ya Uzinduzi rasmi wa Sera ya Elimu, Serikali iandae mkakati madhubuti wa utekelezaji wa Sera hiyo mapema iwezekanavyo katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za utoaji wa elimu nchini.

ii) Uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (*Teachers Service Commission*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusudio la kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu nchini katika mwaka mpya wa fedha 2015/2016. Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Serikali iharakishe zoezi hili muhimu katika kukabiliana na adha zinazowakabili walimu nchini. Hatua hii itarejesha hadhi ya taaluma ya ualimu nchini, amasa kwa walimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- b) Serikali iangalie uwezekano wa Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na mambo mengine kuwa na jukumu la kusajili walimu wote nchini ikiwemo watakaofanya kazi katika shule binafsi/ zisizo za Serikali. Hatua hii ni muhimu katika kuwatambua walimu wote na kuweka viwango vya msingi vya kuhudumia walimu nchini.

iii) Ugatuuji wa Usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Elimu nchini

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kupeleka madaraka na huduma kwa wananchi kwa kupitia dhana ya ugatuuji, kuhusu utoaji wa elimu nchini, Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Utoaji mafunzo kazini kwa walimu usimamiwe na kutolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuweka utaratibu mahususi wa kuendeleza walimu kitaaluma nchini, ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

5 FEBRUARI, 2015

- b) Fedha zinazotengwa na Serikali kuhudumia miradi ya MEM na MMES nchini zisimamiwe kikamilifu kutekeleza majukumu yake kwa wakati. Uzoefu unaonesha kwamba wakati mwingine fedha hizi hurejeshwa Hazina baada ya muda wa matumizi yake kupita. Kukamilika kwa miradi husika ni kichocheo muhimu katika kuboresha utoaji wa elimu nchini.

iv) Mfumo wa Usahihishaji, Utunuku na Utoaji matokeo ya Kidato cha IV na VI nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa ya Wizara kuhusu upangaji wa alama za ufaulu na utunuku wa madaraja katika Mitihani ya elimu ya Sekondari nchini. Kamati inashauri kwamba, panapokuwepo na mabadiliko mbalimbali katika utoaji wa elimu nchini ni muhimu Serikali kushirikisha wadau pamoja na kuelimisha jamii kuhusu mabadiliko hayo ili kuepukana na mikanganyiko mbalimbali inayoweza kujitokeza.

v) Utoaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa ya Serikali ya kutenga kiasi kikubwa cha fedha kuhudumia Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini mwaka hadi mwaka kwa lengo la kupata wataalamu mbalimbali ikiwemo wa sekta ya elimu, kumekuwepo na upungufu wa watumishi (wataalamu) katika sekta hii hususan katika maeneo ya pembezoni. Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Serikali ibuni utaratibu maalumu utakaowezesha wahitimu wanufaika wa mikopo kufunga mkataba maalumu wa kutumikia nchi katika maeneo mbalimbali nchini kwa kipindi maalumu.
- b) Pamoja na utaratibu unaotumiwa na Bodi kutoa mikopo kwa kuzingatia masomo ya vipaumbele,

5 FEBRUARI, 2015

suala la uwezekanao wa kulenga wanafunzi wanaotoka katika familia duni pia lizingatiwe.

- c) ili kuwezesha kuinua uwezo wa Serikali kutoa mikopo kwa idadi kubwa ya wahitaji Serikali iendelee kuchukua juhudi za makusudi kuongeza makusanyo ya Mikopo iliyokwisha tolewa tangu mwaka 1991.

2.1.3. Kujadili sheria mbalimbali

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishiriki kujadili na kutoa maoni yake katika Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Miswada ya sheria mbalimbali:

a) *Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 3, 2013*, ambao moja ya sehemu yake ilikuwa na maudhui ya kuboresha utoaji wa mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Kamati inashauri kwamba Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ibainishe lengo mahususi la utungwaji wa Sheria hii ambayo ni kuwawezesha wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia mafunzo ya elimu ya juu kupata mkopo kwa ajili ya mafunzo hayo.

b) *Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Elimu (The Education Fund Act) cap 412*

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha marekebisho ya Sheria hii kinachoeleza kwamba vyanzo vya fedha vya Mfuko wa Elimu viwe sawa na vile vya VETA, Kamati inasisitiza kwamba juhudi za makusudi zichukuliwe mapema iwezekanavyo kuwezesha Mfuko huu kuwa na vyanzo endelevu vya fedha.

2.1.5 Ziara za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikiwemo kukagua utekelezaji wa shughuli za miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

i) **Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari MMES katika Shule ya Sekondari Naliendele Mkoani Mtwara.**

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikagua utekelezaji wa shughuli za mradi wa ujenzi wa majengo ya shule ikiwemo ujenzi wa matundu 08 ya vyoo, Tanki la maji, na Maabara 1 na ukarabati wa madarasa 6, nyumba 1 ya mwalimu. Kamati ilibaini upungufu ufuatao ikiwemo: Shimo la jumla la kuhifadhi uchafu la choo kuwa na kina kifupi na limeambatanishwa na matundu ya vyoo, Ukarabati hafifu wa nyumba ya mwalimu unaojumuisha ukosefu wa dari, nyavu za mbu hafifu na vyumba vidogo vya kulala, mkanganyiko katika matumizi ya ramani ya ujenzi wa meza za maabara inayojengwa na Ukosefu wa uzio na mpaka wa eneo la shule. Kamati inashauri kwamba:

- i) Kitengo cha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kijiimarisha katika utekelezaji wa majukumu yake,
- ii) Miongozo ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya shule ikiwemo madarasa, vyoo, maabara n.k. inayotolewa na Wizara izingatiwe. Aidha ni muhimu kuangalia upya miongozo hiyo ili iendane na hali halisi ya mazingira na mahitaji wa shule,
- iii) Wizara ishirikiane na Halmashauri za miji husika katika kufutulia maendeleo ya ujenzi wa miradi mbalimbali katika maeneo yao.
- iv) Uwepo mkakati wa makusudi wa kutambua mipaka ya maeneo ya shule nchini ikiwemo kuzungusha uzio kwa kupanda miti katika mipaka husika.

ii) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari katika Shule ya Sekondari Mikindani Mkoani Mtwara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikagua utekelezaji wa shughuli za mradi wa ujenzi wa miundombinu ya shule ujenzi wa maabara 1, matundu 08 ya vyoo, tanki la maji na ukarabati wa madarasa 5, nyumba 1 ya mwalimu na stoo. Mafanikio yafuatayo yaliidhirika:

- i) Ukarabati wa madarasa 5 umefanyika katika kiwango cha kuridhisha

5 FEBRUARI, 2015

- ii) Ujenzi wa matundu ya vyoo ikiwemo uwepo wa shimo la jumla la kuhifadhi uchafu umefanyika katika kiwango cha kuridhisha
- iii) Ukarabati wa nyumba ya mwalimu unaridhisha

Aidha, Kamati ilibaini upungufu ufuatao ikiwemo mkanganyiko katika matumizi ya ramani ya ujenzi wa meza za maabara inayojengwa, nguzo ya Tanki la maji ina kimo kifupi na ukosefu wa mpaka na uzio wa eneo la shule.

Kamati inashauri ifuatavyo:

- i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iwe na Sera ya matengenezo na marekebisho ili kuwezesha ukarabati wa majengo ya shule mara kwa mara.
- ii) Kitengo cha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kijijimarisha katika utekelezaji wa majukumu yake,
- iii) Miongozo ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya shule ikiwemo madarasa, vyoo, maabara n.k. inayotolewa na Wizara izingatiwe. Aidha ni muhimu kuangalia upya miongozo hiyo ili iendane na hali halisi ya mazingira na mahitaji wa shule,
- iv) Uwepo mkakati wa makusudi wa kutambua mipaka ya maeneo ya shule nchini ikiwemo kuzungusha uzio kwa kupanda miti katika mipaka husika.

iii) Mradi wa Ukarabati wa Maktaba ya Mkoa wa Mtwara

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara ilionesha kwamba Tathimini ya ukarabati uliofanyika mwaka 2011 ni sh. **mil 80**. Fedha iliyotolewa na Wizara kwa ajili ya ukarabati wa maktaba 3 (maktaba ya Musoma, Mtwara na Tanga) ni sh. **mil.100** ambayo haitoshelezi. Hata hivyo Wizara imefanya Tathimini Upya ya ukarabati huo na mchakato wa takwimu unafanyiwa kazi. Changamoto zifuatazo zilibainika.

- i) uhitaji mkubwa wa ukarabati wa maktaba husika ikiwemo ujenzi wa paa, uhitaji wa mwanga, mfumo wa maji taka na vyoo.

5 FEBRUARI, 2015

- ii) Eneo dogo la jengo la maktaba ikilinganishwa na uhitaji wa huduma hiyo mkoani Mtwara
- iii) Fedha iliyotolewa haitoshelezi zoezi zima la ukarabati.

Kamati inashauri ifuatavyo:

- i) Zoezi la kufanya tathmini mpya ya gharama za ukarabati wa jengo hilo ukamilike,
- ii) Wizara ijipange kujenga maktaba nyingine kubwa itakayotosheleza mahitaji,
- iii) Sera ya matengenezo na marekebisho itumike ili kuwezesha ukarabati wa majengo ya Serikali mara kwa mara.
- iv) Serikali ihimise matumizi ya maktaba kwa wananchi kwa kuandaa mkakati wa kitaifa endelevu wa kusoma vitabu.

iv) Mradi wa Uimarishaji Elimu ya Msingi MEM School Wash Programme katika Shule ya Msingi Chikwaya- Mtwara Vijijini

Mheshimiwa Spika Kamati ilikagua shughuli za Mradi zikiwemo kuboresha usafi wa mazingira, ujenzi na matumizi ya choo, matumizi ya maji ya kuvuna, na upatikanaji wa lishe shuleni. Mradi umehusisha ujenzi wa matundu 10 ya vyoo, na tanki 1 la kuvuna maji. Mradi umekamilika na umegharimu jumla ya sh. **8, 079,500.00.**

Yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo:

- i) Uhitaji wa kimarisha usafi na kutibu maji katika kisima cha kuvuna maji
- ii) Uhitaji wa usalama wa choo kutokana na ramani ya milango ya choo kuelekea porini,
- iii) ukosefu wa uzio wa shule

Pamoja na pongezi kwa Serikali kwa kuwezesha upatikanaji lishe shuleni, Kamati inashauri ifuatavyo:

- i). Ramani ya ujenzi wa Milango ya choo irekebishwe kuhakikisha usalama wa wanafunzi,
- ii). Kisima cha maji ya kuvuna kiboreshwe kuwezesha usalama wa matumizi ya maji hayo ikiwemo kutibu maji husika,

5 FEBRUARI, 2015

- iii). Mipaka ya shule itambuliwe rasmi na kuweka uzio wa shule
- iv.) Muongozo wa Wizara kuhusu ramani za ujenzi wa shule uzingatie suala la uvunaji wa maji ya mvua.

v) **Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Ualimu Kitangali – Mtwara**

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa bweni la ghorofa 1 litakalolaza wanachuo 160, ununuzi wa vitanda 80 na makabati 80, ununuzi wa tanki la maji, kutengeneza Mfumo wa maji taka na kufanya *Land scapping*. Mradi unagharimu sh. milioni **800** ambazo zimekwisha tolewa.

Hata hivyo Serikali ilitenga sh. **bilioni 4** kwenye bajeti ya Maendeleo katika mwaka 2013/2014 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vyuo vya ualimu nchini ambapo hadi kufikia mwezi Februari 2014 Wizara ilipokea sh. **Milioni 800** sawa na 20% na hivyo kupangwa kutekeleza Mradi wa Chuo cha Ualimu Kitangali. Aidha Kamati ilipata fursa ya kutembelea mabweni ya wanafunzi, bwalo la chakula, madarasa, na eneo la ujenzi wa bweni la ghorofa moja la wanafunzi na kubaini changamoto zifuatazo:

- i) Madarasa chakavu
- ii) Wazabuni kutolipwa kwa wakati
- iii) Pampu ya maji kuharibika
- iv) Mabweni chakavu
- v) Nyumba za walimu haziridhishi
- vi) Ukosefu wa maktaba ya chuo
- viii) Mradi wa ujenzi wa bweni la wanafunzi haujaanza kutekelezwa ingawa fedha sh. **milioni 800** zimetolewa

Kamati inashauri ifuatavyo:

- i) Kazi ya ujenzi wa bweni la wanafunzi ianze mapema iwezekanavyo
- ii) Utaratibu wa ukarabati wa vyuo ufanyike kwa kukarabati Chuo kimoja na kukamilisha badala ya kugawa fedha kwa vyuo mbalimbali na hivyo kutokuwa na tija katika ukarabati husika.
- iii) Serikali itoe fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati.

5 FEBRUARI, 2015

vi) **Mradi wa Ukuzaji Ajira kupitia Elimu na Mafunzo ya Ufundi stadi wa VETA Mkoani Mtwara.**

Mheshimiwa Spika Mradi huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu na unagharimu jumla ya shilingi **bilioni 2.3**. Kamati inashauri kwamba Serikali ijipange kufadhili mradi huu ulioonesha mafanikio makubwa, kupitia TPDC baada ya ufadhili wa kampuni ya British gas kumaliza muda wake.

vii) **Mradi wa TEA wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kukagua mradi huu inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu kwa ufanisi ikiwemo kurejesha mkopo kwa wakati. Pamoja na pongezi hizi imebainika kwamba kwa mwaka 2013/2014 kati ya tengeo la sh. Bilioni **49.5** zilizo dhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya TEA sh. Bilioni **5.0** zimepokelewa. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

viii) **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ADEM-Bagamoyo.**

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii kamati ilibaini changamoto mbalimbali ikiwemo matumizi ya wahitimu wa mafunzo ya uongozi wa elimu na mgogoro wa mpaka kati ya chuo na Kanisa. Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Uteuzi wa viongozi mbalimbali katika sekta ya elimu uzingatie Mafunzo ya Uongozi wa Elimu.
- b) Serikali itatue mgogoro wa mipaka uliopo kati ya wakala na kanisa.

ix) **Maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilipata fursa ya kuhudhuria Maadhimisho ya wiki ya elimu nchini yaliyofanyika katika Viwanja vya Jamhuri mjini Dodoma. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha maadhimisho haya kwani yatatoa fursa kwa wadau mbalimbali wa elimu kushiriki, kutafakari, kutathimini na kubuni mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha hali ya utolewaji wa elimu nchini. Ili kufanikisha suala hili, Kamati

5 FEBRUARI, 2015

inashauri kwamba shughuli zinazotekelezwa katika kipindi hiki ziboreshwe ili zilenge katika kuinua kiwango cha elimu nchini.

x) **Mfumo wa Elimu nchini**

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba elimu itolewayo nchini kwa kiasi kikubwa imekuwa ikitolewa kwa nadharia kuliko vitendo hatua inayosababisha kuwaandaa wahitimu katika ajira za kuajiriwa badala ya kujajiri. Maendeleo ya uchumi kwa sasa yanahitaji wahitimu kutengeneza ajira mbalimbali kutokana na mafunzo ya nadharia na vitendo. Hivyo Kamati inashauri kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti mapema iwezekanavyo kuboresha utoaji wa elimu ili kulenga maendeleo ya sayansi na teknolojia kuendana na maendeleo ya uchumi yaliyopo nchini na duniani kwa ujumla.

2.2 WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

2.2.1 Kujadili Kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliidhinisha jumla ya Sh. 622,952,923,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Afya na usta wa jamii kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara yalitolewa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi.

2.2.2 Vikao na Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utendaji kazi wa Wizara, Kamati ilifanya vikao mbalimbali ili kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Tasisi zake.

i) Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiwekea utaratibu wa kupata Taarifa ya Robo Mwaka ya Usambazaji wa Dawa, Vifaa Tiba

5 FEBRUARI, 2015

na Vitendanishi nchini kutoka MSD. Deni kubwa la Serikali kwa MSD la sh. **Bilioni 93.3** (Disemba 2014) linachangia kwa kiasi kikubwa upungufu wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini. Hali hii inasababisha kero na usumbufu mkubwa kwa watoa huduma na wagonjwa nchini. Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Serikali ichukue hatua za makusudi kumaliza deni lake kwa MSD.
- b) Serikali itoe tamko kuhusu deni lake kwa MSD kabla ya kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016
- c) Kiwango cha Bajeti ya Sekta ya Afya kilichopendekezwa na Azimio la Abuja la mwaka 2001 kizingatiwe.

ii) Upatikanaji wa Bima ya Afya kwa wananchi wote

Mheshimiwa Spika, imedhihirika kwamba umekuwepo uhitaji mkubwa wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) katika kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote. Ili kutekeleza suala hili muhimu Kamati inapendekeza kwamba Serikali iandae Mpango Maalumu utakaowezesha upatikanaji wa huduma za Bima ya Taifa ya afya kwa wananchi wote ikiwemo wasio na kipato kuweza kupata huduma za afya nchini.

iii) Kitengo cha Matibabu ya Figo Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya kitengo hichi, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali zinazokikabili kitengo hiki muhimu ikiwemo upungufu wa vifaa tiba na vitendanishi, pamoja na upungufu wa mashine za kusafishia damu ikilinganishwa na mahitaji. Kamati inashauri kwamba Serikali iendelee kuongeza idadi ya mashine za kusafishia damu ili kukabiliana na msongamano wa watu wahitaji wa huduma hii.

2.2.3. Kujadili Sheria na Maazimio ya Bunge

- i) Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Utafiti wa Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Protocol on*

5 FEBRUARI, 2015

the Establishment of the East African Health Research Commission)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo yake kuhusu Azimio hili la Bunge katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge la Kumi.

ii) Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Kemia wa Mwaka 2014 (*The Chemist professionals Bill, 2014*) na Muswada wa Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2014 (*The Government Chemistry Laboratory Bill*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imepata fursa ya kutafakari na kujadili miswada husika ambayo maoni yake yanasubiri kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu.

2.2.4 Ziara za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika taasisi mbalimbali za Wizara hii ikiwemo shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kama ifuatavyo:

i) Mradi wa Upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Hospitali ya Wilaya ya Masasi – Mkomaindo

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kutembelea Hospitali hii, inaipongeza Serikali kwa juhudi zilizochukuliwa kuwezesha upatikanaji wa dawa na vitendanishi kwa kutumia mbia mwenza wa MSD katika kutoa huduma za upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Aidha, Kamati ilibaini kwamba Chumba cha Hospitali cha kuhifadhi dawa ni kidogo, Upungufu katika takwimu za MSD za usambazaji dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa hospitali ya Mkomaindo, uwepo wa changamoto ya malipo ya utoaji wa huduma ya Mfuko wa Taifa wa Huduma ya Afya (NHIF) na Ukosefu wa taarifa za usambazaji dawa kwa wadau mbalimbali ikiwemo madiwani na wagonjwa. Kamati inashauri ifuatavyo:

5 FEBRUARI, 2015

- a) Serikali ifikirie kuanzisha mbia mwenza wa MSD katika kusambazaji wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi ili kuruhu ushindani utakaoleta ufanisi kama ilivyothibitika katika Hospitali ya Mkomaindo.
- b) MSD ifanye uhakiki wa takwimu za usambazaji wa dawa, vifaa tiba nchini ili kuwa na taarifa sahihi. Aidha Chumba cha kuhifadhi dawa cha hospitali kiboreshwe kuwa na mazingira rafiki.
- c) Taarifa za mapokezi ya dawa katika hospitali au kituo cha afya ziwekwe kwenye mbao za matangazo za Hospitali ili kuwafikia wadau.
- d) NHIF itumie mfumo wa kieletroniki katika utoaji huduma zake ikiwemo malipo kwa watoa huduma.

ii) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini (Mtwara) 2013/2014

Mheshimiwa Spika, Mradi huu wa ni wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje OPD awamu ya pili ambayo gharama yake ni sh. **4,23,972,575** (2009). Ujenzi wa OPD awamu ya kwanza unajumuisha kujenga *substructure, framed structure* pamoja na ngazi kwa gharama ya sh. **1,684,761,756.00** baada ya Kamati kutembelea eneo la ujenzi wa Hospitali husika, ilibaini yafuatayo:

- i) Ujenzi wa jengo husika haujaanza kutekelezwa ingawa fedha sh. Milioni **235** zimetolewa.
- ii) Fedha za utekelezaji wa mradi husika kutotolewa kwa wakati
- iii) Mkandarasi ameanza kutekeleza shughuli za awali ikiwemo kusafisha eneo, kujenga kempu ingawa hafifu za wafanyakazi n.k.

Kamati inashauri ifuatavyo:

- i) taarifa ya Utekelezaji wa Mradi huu iboreshwe kuonesha hali halisi ya hatua za utekelezaji wa mradi
- ii) Ujenzi wa Jengo husika uanze mara moja.

iii) Mradi wa Ununuzi wa Samani katika Mahabusu ya Watoto Mtwara 2013/14

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea mradi huu uliotengewa sh. milioni 40 kununua samani zikiwemo vitanda, makabati na kubaini yafuatayo:

- a) Uhitaji wa uzio wa mahabusu mapema iwezekanavyo ikiwemo kutambua mipaka ya eneo husika.
- b) Ukarabati wa majengo husika hususan katika suala la nyavu za mbu,
- c) Ukosefu wa miundombinu kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Kamati inashauri ifuatavyo:

- i) Serikali ibadili matumizi ya fedha zilizotolewa sh. milioni 40 kuwezesha ujenzi wa uzio wa mahabusu hiyo.
- ii) Ujenzi huu uzingatie miundombinu kwa watu wenye mahitaji maalumu.
- iii) Ukarabati ufanyike kwa kuweka umeme kabla ya ununuzi wa samani

iv) **Kituo cha makazi ya wazee na watu wenye ulemavu – Nunge kilichopo Kigamboni Dar es Salaam.**

Mheshimiwa Spika, katika ziara ya Kamati kituoni hapa ilibainika kwamba miundombinu muhimu ikiwemo mfumo wa umemena majengo ni chakavu, ukosefu wa uzio katika eneo la makazi umesababisha uvamizi wa raia katika eneo la kituo. Kamati inashauri kwamba hatua za haraka zichukuliwe kukarabati miundombinu husika. Aidha juhudi za makusudi zichukuliwe kupima na kutambua mipaka ya eneo la kituo pamoja na ujenzi wa uzio wake. Hatua hii itawezesha kumaliza mgogogro uliopo baina ya kituo na wakazi wanaozunguka eneo hilo.

v) **Vituo vya kukabiliana na Ugonjwa wa Ebola katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Mwalimu Nyerere na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea vituo hivi ili kukagua hatua zilizochukuliwa kukabiliana na Ugonjwa

5 FEBRUARI, 2015

wa Ebola nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua za haraka zilizochukuliwa kukabiliana na uwezekano wa mlipuko wa Ugonjwa wa Ebola nchini. Hata hivyo Kamati inashauri ifuatavyo:

a) Serikali ichukue hatua madhubuti kudhibiti uwezekano wa uingizwaji wa ugonjwa huu maeneo ya mipakani (njia za panya).

b) Elimu kwa umma kuhusu kujikinga na ugonjwa huu itolewe kupitia vyombo mbalimbali vya habari elimu ya nyumba kwa nyumba inayoweza kutolewa na maafisa wa afya kwa kushirikiana na wajumbe wa Kamati za Afya za mitaa.

vi) **Taasisi ya Matibabu ya Saratani Ocean Road**

Mheshimiwa Spika, matibabu ya Saratani kwa kutumia mashine za mionzi ni huduma muhimu sana inayotumiwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa Saratani nchini. Mashine za mionzi (idadi 2) zimekuwa zikiharibika mara kwa mara hali inayosababisha uhitaji mkubwa wa huduma na usumbufu kwa wagonjwa. Kamati ilipotembela Taasisi hii ilishuhudia zoezi la ukarabati wa mashine ya mionzi (Equinox 100) baada ya kuwasili kwa kifaa muhimu kiitwacho Chanzo cha Mionzi kutoka Canada. Mashine hizi zimekuwa zikifanya kazi kwa muda mrefu, hali inayosababishwa na uwepo wa msongamano wa wagonjwa wahitaji wa huduma hii. Kamati inashauri kwamba Serikali iendelee kuboresha upatikanaji wa huduma za Matibabu ya Mionzi, kwa kufikiria kuongeza mashine nyingine ya mionzi. Aidha, fedha kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) zitolewe kwa wakati ili kuwezesha pamoja na manunuzi ya dawa, ukarabati wa mashine za mionzi.

vii) **Taasisi ya Matibabu ya Moyo Muhimbili**

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii pamoja na mambo mengine, Kamati ilikagua upatikanaji wa huduma za kipimo maalumu cha matibabu ya Moyo kwa njia ya upasuaji kiitwacho *Arterial Blood Gas (Blood Gas Analyser)*. Taarifa ya Serikali ilieleza kwamba utaratibu unaotumika wa kukodi kifaa hiki, ni wa mafanikio makubwa ikilinganishwa na ununuzi wake. Hii inatokana mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya uundaji wa mashine pamoja na gharama za

5 FEBRUARI, 2015

kufanya matengenezo yake. Kamati inashauri serikali iendelee kutoa huduma hii muhimu ili kupunguza gharama kwa Serikali kuhudumia matibabu haya nje ya nchi.

viii) Taasisi ya Tiba ya Mifupa na magonjwa ya Mishipa ya fahamu Muhimbili (MOI)

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati ililenga kukagua hali ya vitendea kazi na mazingira ya utendaji kazi ya Taasisi. Kamati ilibaini kwamba vifaa vya upasuaji na mashine kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU) ni chakavu. Aidha, taasisi inakabiliwa na changamoto ya ongezeko la wagonjwa wa ndani na nje na hivyo kuathiri utoaji wa huduma mbalimbali ikiwemo dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Taasisi hii pia inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji finyu (chini ya asilimia 50) wa fedha za matumizi mengineyo (OC). Kamati inashauri ifuatavyo:

- a) Serikali kupitia TAMISEMI kuwezesha wataalamu wa taasisi utoa huduma za matibabu ya mifupa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa za Ilala, Mwananyamala, temeke, Tumbi na morogoro hatua itakayoweza kupunguza idadi msongamano katika taasisi hii.
- b) Serikali iwekeze katika kununua mashine za kisasa za uchunguzi, kuweka vifaa na samani kwenye jengo jipya katika *MOI Phase II*. Hatua hii itawezesha kupunguza rufaa za nje ya nchi kwa upande wa mifupa, mgongo, nyonga na mishipa ya fahamu.

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo na uchambuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati, maoni na mapendekezo ya kamati yanatolewa kama ifuatavyo:

4.1 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

4.1.1 Sera mpya ya Elimu

Uzinduzi wa Sera hii ufanyike mapema iwezekanavyo ikiwemo kuweka mikakati ya utekelezaji wake. Aidha, Vyombo vya

5 FEBRUARI, 2015

Msingi katika utoaji wa elimu ambavyo ni Baraza la Mitihani Tanzania (*National Examination Council of Tanzania- NECTA*) , Taasisi ya Elimu Tanzania (Tanzania Institute of Education- TIE) na Ukaguzi wa Elimu vilindwe, na viwezeshwe kuendelea kuwa Mamlaka huru zinazojitegemea katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

4.1.2 Mfumo wa Elimu nchini

Serikali ichukue hatua za makusudi mapema iwezekanavyo, kuboresha mfumo wa utoaji wa elimu nchini ili kuweza kuzingatia mwendeleo ya sayansi na teknolojia yanayoimarika siku hadi siku. Hatua hii ni ya msingi katika kufikia maendeleo ya sekta mbalimbali ikiwemo maendeleo ya uchumi kwa ujumla.

4.1.3 Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commission*)

Pamoja na pongezi kwa Serikali kwa kusudio la kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu katika mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa Tume hii pia kupewa jukumu la kusajili Walimu wote nchini ikiwa ni pamoja na wanaofanya kazi katika shule binafsi/ zisizo za Serikali. Hatua hii ni muhimu katika kuwatambua walimu wote na kuweka kiwango cha msingi cha kutoa huduma kwa walimu nchini.

4.1.4 Ugatuzaji wa Sekta ya Elimu nchini

Jukumu la utoaji mafunzo kazini kwa walimu lisimamiwe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuweka utaratibu mahususi wa kuendeleza Walimu kitaaluma ili kukabiliana na changamoto za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

4.1.5 Mabadiliko ndani ya Mfumo wa Elimu nchini

Serikali inapoleta mabadiliko yoyote katika utoaji wa elimu nchini, ni muhimu iwashirikishe wadau pamoja na kuelimisha jamii kuhusu mabadiliko husika kabla ya utekelezaji ili

5 FEBRUARI, 2015

kuepukana na mikanganyiko mbalimbali ambayo huwa inajitokeza. Mfano mabadiliko yaliyofanyika katika Upangaji wa Alama za Ufaulu na Utunuku Madaraja katika Matokeo ya Mitihani ya Elimu ya Sekondari.

4.1.6 Utoaji wa Mkopo kwa Wanafunzi wa ya Elimu ya Juu

Pamoja na utaratibu unaotumiwa na Bodi katika kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuzingatia masomo ya vipaumbele, suala la kulenga wanafunzi wanaotoka katika familia duni lizingatiwe. Serikali itumie mikakati ya makusudi kukusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa tangu mwaka 1991. Kamati inapendekeza Serikali kuona uwezekano wa wanufaika wa mikopo kufunga mkataba maalum wa kuitumikia nchi katika maeneo mbali mbali kwa kipindi maalum.

4.1.7. Ukaguzi wa Elimu nchini

Kamati inasisitiza kwamba Serikali iimarisha na kuiwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi kwa kusimamia viwango vya Elimu inayotolewa nchini sambamba na ongezeko la taasisi mbalimbali zinazotoa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

4.1.8 Lugha za kufundishia na kujifunzia.

Kamati inapendekeza kwamba Serikali iimarisha lugha za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia Sera ya Elimu katika kutoa mafunzo kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu nchini ili kukabiliana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

4.1.9 Mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia kwa Wenye Mahitaji Maalum

Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu kwa watu wenye mahitaji maalumu kwa kutenga fedha za kutosha. Aidha Serikali itoe mwongozo wa

5 FEBRUARI, 2015

kitaifa kuhusu ujenzi wa miundombinu ya shele na vyuo. Usajili wa shule uzungatie mahitaji ya kundi hili muhimu la watu wenye mahitaji maalumu.

4.1.10 Baraza la Elimu ya Ufundi (National Council for Technical Education - NACTE)

Ili kukabiliana na changamoto ya ongezeko la vyuo vinavyotoa Elimu ya Ufundi bila kuzingatia vigezo vilivyowekwa na NACTE, Kamati inapendekeza kuwa Sheria ya Baraza la Elimu ya Ufundi ifanyiwe maboresho ya kupewa mamlaka zaidi kuchukua hatua ikiwemo kuvifungia vyuo ambavyo vinatoa mafunzo bila kupata ithibati kutoka NACTE.

4.1.11 Posho ya Mazingira Magumu kwa Walimu.

Ili kuimarisha utoaji wa elimu hususan katika nmaeneo ya pembezoni, Serikali ikamilishe mapema iwezekanavyo mchakato wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ili kuwafanya wabaki katika mazingira ya kazi ikiwemo kuipenda taaluma yao.

4.1.12 Utekelezaji wa Majukumu ya VETA

Fedha za kuendeshea mafunzo ya ufundi (*Skills Development Levy*) inayopelekwa kuhudumia mafunzo ya ufundi chini ya VETA iongezwe kutoka asilimia **2** hadi asilimia **4** ili kuwezesha VETA kufanya kazi kikamilifu na pia kuweza kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDC*) kutoa huduma ya Mafunzo hayo muhimu kwa ufanisi.

4.1.13 Utekelezaji wa Miradi Maendeleo nchini.

Baada ya Kamati kutafakari kwa kina kuhusu mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika ziara za Kamati kukagua

5 FEBRUARI, 2015

shughuli za miradi ya maendeleo, inatoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:

i) Fedha za utekelezaji wa miradi maendeleo zitolewe kwa wakati.

ii) Ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali ufanyike kwa kutumia kandarasi za VETA, Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa ili kuweza kutekeleza jukumu hilo kikamilifu na kwa uadilifu. Hatua hii ni muhimu katika kuokoa miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya kiwango.

4.2. WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

4.2.1 Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutokidhi Azimio la Abuja.

Tanzania iliridhia Azimio la Umoja wa Nchi za Afrika la Abuja Mwaka 2001 linaloelekeza nchi wanachama kuwa ifikapo mwaka 2015 Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya ifikie asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali. Takwimu zinaonesha kwamba bajeti zinazotengwa katika Sekta ya Afya nchini hazikidhi Azimio hilo. Kamati inashauri kwamba Serikali ijizatifi katika kuongeza vyanzo zaidi vya mapato ya ndani ili kuweza kufikia 15% ya bajeti yake katika sekta ya afya nchini.

4.2.2 Bohari Kuu ya Dawa, (Medical Stores Department)

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha MSD kununua na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Hospitali na Vituo vya Afya, Serikali ilipe deni lake kwa MSD lililofikia takribani sh. **Bilioni 93.3** (Desemba 2014) ili kukabiliana na upungufu wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi katika hospitali na vituo vya afya nchini.

Aidha, fedha ya bajeti ya Ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi zitolewe na Hazina katika Mkupuo Mmoja ili kumaliza tatizo la urasimu katika ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa tiba. Hali kadhalika Bunge lione umuhimu wa kutunga sheria maalumu itakayoweka utaratibu maalum wa

5 FEBRUARI, 2015

fedha za MSD kutengwa na kupelekwa moja kwa moja kama ilivyo fedha za ujenzi wa barabara.

4.2.3 Taasisi ya Matibabu ya Saratani Ocean Road

Serikali ichukue hatua za makusudi za kudumu ili kuhakikisha kwamba mashine za tiba ya mionzi katika taasisi hii zinafanya kazi wakati wote. Aidha, Hospitali za Rufaa za Kanda ziwezeshe kivifaa na wataalamu kutoa huduma za msingi za matibabu hayo na Hospitali za Wilaya zijengewe uwezo wa kutoa huduma za awali za matibabu husika. Hatua hii itawezesha kupunguza msongamano wa wagonjwa katika taasisi hii.

4.2.4 Kitengo cha Matibabu ya Moyo Muhimbili

Baada ya Kamati kukagua upatikanaji wa huduma za kipimo maalumu cha matibabu ya Moyo kwa njia ya upasuaji kiiitwacho *Arterial Blood Gas (Blood Gas Analyser) ambacho* hukodishwa kutoa huduma hii ikilinganishwa na ununuzi wake kwa lengo la kuepuka mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya uundaji wake, inashauri kwamba Serikali iendelee kutoa huduma hii muhimu ili kupunguza gharama kwa Serikali kwa kuhudumia matibabu haya nje ya nchi. Aidha Serikali iongeze kasi ya kuwezesha kitengo hiki kuwa Taasisi inayojitegemea ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

4.2.5 Taasisi ya Tiba ya Mifupa na magonjwa ya Mishipa ya fahamu Muhimbili (MOI)

Serikali iwekeze katika kununua mashine za kisasa za uchunguzi, kuweka vifaa na samani kwenye jengo jipya katika *MOI Phase III*. Hatua hii itawezesha kupunguza changamoto ya msongamano wa wagonjwa pamoja na rufaa za matibabu nje ya nchi kwa upande wa mifupa, mgongo, nyonga na mishipa ya fahamu.

4.2.6 Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto, na huduma ya Uzazi wa Mpango.

Ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu upatikanaji wa huduma za Uzazi wa Mpango kwa asilimia 60 ya wanawake walio katika umri wa kupata mtoto ifikapo Mwaka

5 FEBRUARI, 2015

2015, Serikali itenge fedha kuwezesha kufikia angalau asilimia 20 ya mahitaji ya huduma ya Uzazi wa Mpango nchini. Aidha, Halmashauri zitenge fedha kuwezesha upatikanaji wa huduma hizo ikiwemo upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia kwa kinamama. Serikali iendeele kuhamasisha matumizi bora ya huduma ya uzazi wa mpango hususan katika maeneo ya vijijini.

4.2.7 Huduma ya Bima ya Afya kwa wananchi wote

Serikali iharakishe kukamilika kwa Mpango Maalumu utakaowezesha upatikanaji wa huduma za Bima ya Taifa ya afya kwa wananchi wote ikiwemo wasio na kipato ili waweze kupata huduma za afya nchini.

4.2.8 Upatikanaji wa watumishi wa Sekta ya Afya katika maeneo ya pembezoni

Serikali iweke utaratibu maalumu wa kuhakikisha kwamba wahitimu wa mafunzo katika taaluma za sekta ya afya kwa udamini wa Serikali watumike kutoa huduma za afya katika maeneo ya pembezoni kwa muda maalumu. Aidha, motisha maalum itolewe kuwezesha watumishi wanaofanya kazi katika maeneo ya pembezoni waendeele kubaki katika utumishi huo. Aidha, Serikali ifanye utaratibu wa kuajiri watumishi katika sekta ya afya kwa kuwapata wanaotoka maeneo ya pembezoni na kuwaendeeleza kimafunzo.

4.2.9 Idara ya Ustawi wa Jamii

Kwa kuwa utolewaji wa huduma mbali mbali za jamii kwa Watu Wenye Ulemavu ni sekta Mtambuka, Idara ya Ustawi wa Jamii ifikiriwe kuhamishiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa ina mamlaka ya kutoa maelekezo kwa Wizara zote kutoa huduma kulingana na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo. Hatua inayopendekezwa itawezesha kuleta ufanisi katika upatikanaji wa huduma kama afya, elimu, ulinzi, miundombinu, sheria na nyinginezo kwa kundi hili muhimu.

4.2.10 Matumizi ya Teknolojia ya Elektroniki kukusanya maduhuli katika Taasisi za Wizara.

5 FEBRUARI, 2015

Ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato katika taasisi za Serikali ikiwemo taasisi za utoaji huduma za afya zikiwemo Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali (*Chief Government Chemist*) na Taasisi ya Mifupa MOI, Serikali ichukue juhudi za makusudi za kutumia Mfumo wa Kisasa wa Kielektroniki kukusanya maduhuli hayo.

5.0 HITIMISHO


Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu yake katika Kipindi cha wa mwezi Januari 2014 hadi Januari 2015.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Dkt. Seif Ali Rashid (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Dkt. Kebwe Steven Kebwe (Mb) na aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama (Mb) kwa kuipatia Kamati ushirikiano mzuri wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Anna Kilango Malechela (Mb), Naibu wa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuteuliwa katika nafasi hiyo muhimu kuimarisha utolewaji wa elimu nchini. Vile vile nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dk. Thomas D. Kashililah, kwa msaada mkubwa walioipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake. Hali kadhalika ninamshukuru Katibu wa Kamati ndugu Happiness Ndalu, Chacha Nyakega na Stella Mlambo kwa kuihudumia vyema Kamati.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.



Margaret Simwanza Sitta (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII

05 Februari, 2015

MWENYEKITI: Sasa Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuwaita wachangiaji wa asubuhi ya leo naomba niwatambue wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Kabaka, kama ifuatavyo:-

Ndugu Hezron Kaaya, Naibu Katibu Mkuu *TUCTA*, nao wataja naomba wasimame. Ndugu Mathias Mjema, Katibu Mkuu *COTWU*; Ndugu Erasto Kiwele, Katibu Mkuu *TURAW*; Ndugu Johns Majura Katibu Mkuu Msaidizi *TUICO*, wako pale; Ndugu Jonathan Peresi, Katibu Mkuu Msaidizi *TUICO*; Ndugu Kibwana Njaa, Naibu Katibu Mkuu *TALGWU*; Ndugu Ramadhani Mwendwa, Katibu wa Kanda ya Kati *RAAW* na Katibu wa *TUCTA* Dodoma; Ndugu Peniela Perina Msilu Katibu wa Kanda ya Kati *TUICO*; Ndugu Abdul Mkama mwakilishi wa wafanyakazi *TANESCO*; Ndugu Ernest Mwakikoti, mwakilishi wa wafanyakazi *TANESCO*; Ndugu Janeth Siveso, mwakilishi wa wafanyakazi *TANESCO*; vilevile na Ndugu Kasambala, Mwanasheria *TRAWU*, ahsateni sana na karibuni katika ukumbi wenu.

Baada ya kusema hayo, nitawaita wachangiaji tunaanza na wale ambao hawajachangia kabisa, tunaanza na Mheshimiwa Ritta Kabati, karibu Mheshimiwa!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kuchangia mjadala huu wa Taarifa za Kamati ya Maendeleo

5 FEBRUARI, 2015

ya Jamii na Huduma za Jamii. Nianze kwanza na kukupongeza wewe Mwenyekiti kwa kuchaguliwa kwako kuwa Mwenyekiti wa Kamati wa Bunge na pia Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, tunaamini kwamba wanawake tunaweza, hamtatuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizi zilizopo katika taarifa hii ambazo zimewasilishwa hapa kwa kweli zinapata bajeti finyu sana ukilinganisha na changamoto nyingi sana ambazo zipo katika Wizara zao. Ningeomba Serikali iangalie kwa uangalifu na izingatie itoe bajeti yake kwa kiwango kikubwa na kwa wakati ili kusiwepo na maandamano, kusiwepo na matatizo ambayo yanasababishia hata Serikali yetu kupata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kutembelea Chuo cha Maendeleo cha Lungemba, kwa kweli chuo hiki pamoja na kuwa changamoto nyingi lakini iko changamoto ya muda mrefu inayohusiana na mpaka kati ya Serikali ya Kijiji na chuo hicho. Sasa ni vema tukapata maelezo ya kina ni nini mkakati wa kumaliza mgogoro huo kwa sababu umekuwa wa muda mrefu sana kiasi kwamba hata hiki chuo kinashindwa kufanya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu Mfuko wa Akinamama na Vijana zile asilimia kumi ambazo zinatakiwa zitengwe katika Halmashauri zetu. Pamoja na Serikali kuweka sheria ya kutenga asilimia kumi ya mapato ya ndani ili waweze kukopesha vijana na akinamama lakini bado Halmashauri nyingi sana zimekuwa hazitekelezi hili agizo. Sasa ni hatua gani Halmashauri hizi zinachukuliwa kwa sababu hii ni kudumaza kabisa akinamama na vijana, tulikuwa tunategemea kwamba hii mikopo ingeweza kuwasaidia kujikwamua na wangeweza kufanya shughuli za kimaendeleo na za kijamii ili waweze kujikwamua katika maisha yao. Ningeomba kwa kweli hili tupewe maelezo na tujue kwamba hizi Halmashauri zinachukuliwa hatua gani. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Sambamba na hilo pia ningependa kujua ule Mfuko wa Vijana ambayo Wizara hii inayoshughulika na vijana je, vijana wangapi wameshafaidika na huo Mfuko, je ni elimu kiasi gani hawa vijana wanapatiwa ili kupata uelewa wa kuweza kuufikia huo Mfuko? Kwa sababu mara nyingi sana tumekuwa tukitenga Mifuko hata hizo asilimia tano watu hawana uelewa wa jinsi ya kufikia hiyo Mifuko. Kwa hiyo, leo hii ni vizuri wakaelimishwa vizuri zaidi ili kila mtu atendewe haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu Benki ya Wanawake, kwa kweli niwapongeze sana Benki hii Wanawake pamoja na ufinyu mkubwa kabisa wa bajeti wamejitahidi angalau wameanza sasa kufungua vituo vya kukopesha kwa baadhi ya mikoa ukiwepo hata Mkoa wetu wa Iringa, sasa hivi kuna kituo ambacho kimeanza kuwakopesha akinamama japokuwa kidogo kidogo na hakijaweza kufikisha huko kijiji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile pesa ambazo zilitengwa bilioni 15, Serikali si ilikuwa imeahidi, je, zimefikia wapi? Hebu naomba tuwapeni kipaumbele benki hii ili iweze kufikia, wafungue matawi kabisa sio vituo na ziweze kuwafikia mpaka vijijini kabisa. Tunaamini kwamba Kamati imetoa maelekezo mazuri na ushauri mzuri kama utazingatiwa na Serikali basi tunaamini kwamba hii Benki ya Wanawake itaendelea na itafanya kazi yake vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze pia kuhusiana na mkataba wa kulinda haki za wafanyakazi wa majumbani umefikia wapi? Mimi ni mdau kwa sababu najua kuna nguvu kazi kubwa sana inatoka katika Mkoa wangu wa Iringa wameajiriwa kwenye kufanya kazi za ndani. Sasa ni muda mrefu sana huu mkataba tuliahidiwa kwamba ungeletwa hapa Bungeni ili tuuridhie kisheria. Sasa ni lini utaletwa kwa sababu kuna mikataba mingi sana tunaambiwa kwamba italetwa, lakini haitetwi. Matokeo yake hawa wasichana wa kazi au wavulana wa kazi wamekuwa wakinyanyasika, wakifanyiwa matendo mabaya sana kama siyo binadamu. Mishahara yao haieleweki wanalipwa kiasi gani. Kwa hiyo, tunaomba jamani hili lizingatiwe, tuweze

5 FEBRUARI, 2015

kuridhia huu mkataba ili wafanyakazi watendewe haki, wawe kama waajiriwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba nieleze kuhusu Waandishi wa Habari, nao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana. Wamiliki wa vyombo hivi wengine hawawapatii mikataba, wengine hawako hata katika Mifuko ya Jamii, hawawakatii bima za maisha, hawawakatii bima za afya.

MJUMBE FULANI: Ni kweli.

MHE. RITTA E. KABATI: Sasa naomba kujua ni lini Muswada wa Sheria hii utaletwa hapa Bungeni ili na wao wafanye kazi vizuri, kwa sababu tunaona kwamba wao ndiyo wamekuwa wakitusaidia pia kueneza habari zetu, na Katiba mpya najua wataitangaza vizuri sana. Kwa hiyo, leo semeni vizuri ili Waandishi wa Habari wafanye kazi kwa moyo kuhakikisha kwamba Katiba mpya inapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu deni la MSD. Kwa kweli Kamati imelizungumzia kwa undani sana na hili deni limekuwa likizungumziwa sana hii Kamati muda mrefu la bilioni 93, je, mpaka sasa hivi limefikia wapi toka Serikali imesema kwamba imeanza kulilipa? Pia naomba Serikali iangalie namna ya kudhibiti yale madawa yanayopelekwa katika mahospitali yetu, je, yanafikishwa kweli? Kwa nini kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa madawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya nchini? Tunaomba pia hii iangaliwe na kuwepo mkakati wa kuhakikisha kwamba hayasainiwi madawa hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna fedha zilizotolewa na wafadhili kwa ajili ya kununua vifaa vya kujifungulia wanawake, yaani *delivery kit*, bilioni tatu, inasemekana pesa hizo zilibadilishwa matumizi ni kwa nini? Ni imani yangu kuwa vifaa hivyo ndivyo vingeweza kusaidia sana kupunguza tatizo la akinamama na watoto. Kwa hiyo, ningomba maelezo ya kina ya Serikali kutokana na hilo inaonesha kwamba labda bado hatuthaminiwi sana sisi wanawake, naomba hili liangaliwe na tuambiwe kabisa.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa pia ufumbuzi wa mkakati uliotolewa na Serikali kuhusiana na madeni ya Walimu nchini, kwa sababu nimesikia kwenye vyombo vya habari tetesi kwamba wanataka kufanya mgomo mkubwa. Sasa kama tusipoangalia, hebu lielezeni vizuri ili tujue kwamba yale madeni ya Walimu sasa yamefikia wapi, maana yake tuliambiwa mengine yalikuwa ni hewa, hayakuwa ya ukweli, basi yafafanuliwe vizuri ili kusiwepo na malalamiko. Pia tuambiwe kuhusiana na mikopo ya wanafunzi kwa sababu bado kuna maeneo mengine ile ya vyyo vikuu bado wamekuwa wakilalamika lalamika kwamba hawatendewi haki sana, hawapati kwa wakati, kwa hiyo, naomba pia hili nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa pia Serikali iangalie na ituambie hii mikopo ambayo inachukua katika Mifuko ya Jamii, kwa kweli kuna Mifuko ya Jamii kama *NSSF*, *PPF* imekuwa ikikopesha Serikali, lakini bado wanakuwa hawalipwi, hii ni fedha ya wafanyakazi. Sasa kukopa bila kulipa hii Mifuko baadaye itakufa. Ningeomba kwa kweli tupatiwe majibu ambayo yataisaidia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nielezee kuhusu viwanja vya wazi (*open space*) vilitengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata haki ya kushiriki michezo, lakini kuna vingine vilivamiwa yakajengwa majumba. Sasa je, Halmashauri zetu zinasemaje kuhusiana na hilo na tuliambiwa kwamba kama vingine watu walipewa wakajenga majumba, zitabomolewa, lakini tunaona bado vijana hawatendewi haki, hawana sehemu za michezo na ndiyo hivyo kwamba michezo inawasaidia kukuza akili vijana wetu. Sasa siku zote tukiwa tunaambiwa maneno, tunaambiwa maneno ambayo hayatekelezeki, tunakuwa sisi Wabunge kama vile hatuisimamii Serikali na kuishauri. Tunaomba yale ambayo tunakuwa tunawaambia basi tuletewe majibu yale ili wananchi waone kweli tunawatendea haki. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabisa nizungumzie kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na ukatili kwa wanawake, umekuwa mkubwa mno, watoto wanabakwa, vijana wetu wanafanyiwa vitendo vya kikatili, akinamama wanapigwa, mateso makubwa, vikongwe wanauawa, watu wenye ulemavu wa ngozi wamekuwa kila siku wanauwawa, lakini hata akishikwa na kidhibiti hivi anakuwa anasema kwamba kesi inachunguzwa kesi inachunguzwa. Sasa huo uchunguzi ni upi wakati tumemshika kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi wahukumiwe na sheria kali itumike, kwa sababu hata hizi kesi za ubakaji sasa hivi liringa zimekuwa kwa kiasi kikubwa sana, kiasi kwamba, kesi haziishi na wale waliobakwa ndiyo wanapewa haki, wale watoto waliobakwa wameathirika kisaikolojia, hatujui hata mama ameathirika, watoto wameathirika kisaikolojia kwa sababu mtoto akishabakwa kwa kweli hata darasani hafanyi vizuri. Tunaomba Serikali yetu iangalie huu ukatili ambao wanawake wamekuwa wakifanyiwa kwa muda mrefu na watoto wetu wakipata shida. Juzi tu Dar es Salaam kuna tukio limetokea la ubakaji wa yule mtoto anabakwa mbele na nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba kabisa na naomba watendaji wanaohusika na Wizara hii waangalie na watutolee taarifa na mkakati gani unachukuliwa kuhakikisha kwamba watu hawanyanyaswi kijinsia na hata watu ambao wanashindwa kupata msaada wa kisheria wanasaidiwa, kwa sababu tunaona kwamba haya mashirika yanayosaidia kisheria vijijini kabisa kule hayapo, yapo tu mijini. Sasa unaona akinamama wakienda kufanya ziara na kuwatembelea, matatizo ni hayo, mirathi bado, msifikirie kwamba yamekwisha, bado watu wananyanyasika kuhusiana na mirathi. Naomba kwa kweli sisi kama Wabunge wa Viti Maalum...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

5 FEBRUARI, 2015

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa pili ndugu Al-Shaymaa Kwegyir, atafuatiwa na *Captain* Komba na Mheshimiwa Nassib Suleiman ajiandae!

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda kukupongeza wewe kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili, hongera sana na pia nampongeza mama Ledian Mng'ong'o kwa kupata nafasi hiyo pia. Nawapongezeni sana hongereni akinamama tunaweza sana. *(Makofi)*

Pili, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mama Margaret Sitta, Mwalimu wangu, mama yangu nakupongeza sana kwa kazi nzuri ya kuongoza Kamati ya Huduma ya Jamii, ama kweli mnafanya kazi nzuri. Pia, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, hongera sana kaka yangu kwa kazi nzuri ya kuongoza kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida yangu nikisimama mnajua najikita sana kwenye nini, nyote mnajua, maana huwa nadiriki kutoa machozi kwa kundi hilo, kundi hilo muhimu la watu wenye ulemavu. Waheshimiwa Wabunge, mnaposimama jaribuni kuzungumzia na hili kundi, halina wasemaji, hakuna kabisa wasemaji wa hili kundi. Nikongea mimi ataongea mama Mkanga, asipoongea mama Mkanga wawili watatu wataongea, lakini Waheshimiwa Wabunge jamani, na Kamati. Isiposema Kamati ujue basi hakuna atakayezungumza na Mheshimiwa Barwany pia anajikita sana kwa masuala haya ya watu wenye ulemavu.

Naomba Waheshimiwa Wabunge tuwasemee, hili kundi ni kundi muhimu sana, hakuna mtu asiyeguswa kwa

5 FEBRUARI, 2015

njia moja au nyingine na masuala ya ulemavu. Kuna ulemavu unaoonekana na kuna ulemavu mwingine hauonekani, hatuujui, kwa hiyo wote ni kundi hilo hilo, tuwe pamoja, tuseme pamoja, tupige kelele pamoja kuwasaidia kundi hili, wana changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naanza na changamoto za elimu. Kwenye suala la elimu kundi hili wana matatizo makubwa kwenye masuala ya mazingira, mazingira rafiki ya utoaji wa elimu kwa makundi haya. Makundi haya yako kama kumi, utoaji wao wa elimu unahitajika uwe maalum mno wa aina ya pekee hasa ukizingatia maumbile na mienendo tofauti tofauti, kuhusiana na ulemavu kila mmoja aliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na ulemavu mmoja wapo ambao una changamoto, walemavu wa viungo wana changamoto kubwa kwenye suala la miundombinu. Nalipongeza sana Bunge hili kwenye Bunge la Katiba waliweka sawa miundombinu, imekuwa rafiki mno kwa watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, natoa msisitizo na napendekeza kwamba, majengo yanayojengwa nchini watie msisitizo mkubwa kwenye miundombinu ili kuwapa wepesi watu wenye ulemavu wa viungo kuwa na wao rafiki na maeneo ya majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi lingine la watu wenye ulemavu wa ngozi kama nilivyo mimi. Watu wenye ulemavu wa ngozi wana changamoto ya uoni. Wanapokuwa kwenye masuala ya elimu wanahitaji mapenzi makubwa na mahaba makubwa kutoka kwa Walimu. Walimu wanatakiwa wawe na mapenzi, wawasaidie na wao wanataka wapate elimu, bila ya kupata mahaba na mapenzi kutoka kwa Walimu ujue tayari wana *give up*, wanaona kwamba mimi sifai kuendelea na masomo. Akikosa uoni tayari anashindwa kuendelea na masomo, anakata tama, matokeo yake anakuwa na maisha magumu katika maisha yake yote, kwa sababu hana na elimu ndiyo kila kitu, asiseme mtu kuhusu hilo. Elimu ndiyo kitu cha muhimu.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi mengine nizungumzie viziwi. Viziwi kwa kweli nimewasemea sana humu ndani kuhusu kupata habari, lakini nashukuru sasa hivi *TBC* nawapongeza sana, walemavu viziwi wanapata taarifa Bunge linavyoendelea. Sasa hivi na wao wanakuwa *up-to-date* na masuala yanayoendelea ndani ya Bunge la Jamhuri, nawapongeza sana *TBC* kwa kuweka lugha ya alama kwenye TV. Aidha, nasema kwamba Serikali itoe mwongozo wa Kitaifa, itoe mwongozo kabisa kuhusiana na masuala haya. Serikali iwe na mkakati kuhusiana na masuala haya kwa makundi yote ya watu wenye ulemavu kwenye mpango wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye elimu napenda kuzungumzia, kuna Kitengo cha Elimu pale Wizarani kiko chini ya Kamishna. Kitengo kile cha elimu cha watu wenye ulemavu sina uhakika ningepomba au napendekeza Kitengo hiki kiwe Idara inayojitegemea. Mheshimiwa Waziri anasikia kwamba iwe Idara Maalum inayoshughulikia masuala ya walemavu peke yake, isiwe kwamba inaenda kwa Kamishna, ikiwa ni idara peke yake itasaidia sana kufuatilia kwenye vyuo, kwenye masuala ya watu wenye ulemavu yote watakuwa wana idara yao, ukienda Wizarani unajua *straight* unakwenda kwenye kitengo kile kuzungumzia suala la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita sasa kwenye masuala ya afya. Nimeshawahi kuzungumzia suala la afya katika Bunge hili, nimezungumzia kuhusu Bima ya Afya. Inasemekana kwamba watu wenye ulemavu wanapewa matibabu bure, si kweli, matibabu bure hayo hayapo. Watu wenye ulemavu wanakwenda hospitali, matibabu anafika anaelekezwa aende akanunue dawa duka fulani. Madawa hakuna, nikizingatia pia na watendaji ni wachache kwenye hospitali, hilo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipatiwe majibu haya matibabu bure ni kweli yapo au ni kauli tu inazungumzwa kwamba kuna matibabu bure kwa watu wenye ulemavu. Naomba hili suala kwa sababu kuna

5 FEBRUARI, 2015

makundi ya watu wale *dhoful-hali*, wana hali ngumu, hawana uwezo, Serikali itafute mkakati maalum wa kuweza kusaidia watu wenye kipato cha chini kwenye suala la Bima ya Afya. Kamati wamezungumzia, nawaunga mkono kwa hilo pendekezo walilotoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kitengo cha Ustawi wa Jamii. Hilo ndiyo bomu, bomu kabisa, Ustawi wa Jamii wanasema kwamba watu wenye ulemavu wako chini ya Ustawi wa Jamii. Nimezungumza sana humu kwenye Bunge karibu kila Bunge la Bajeti nimezungumzia, Kitengo cha Ustawi wa Jamii kihamishiwe kwa Waziri Mkuu, wahamishiwe kwa Waziri Mkuu masuala ya watu wenye ulemavu ni mtambuka, tunaingia Wizara zote, kila Wizara masuala ya ulemavu yanaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na nawaunga mkono Kamati, wamelitoa hili lifanyiwe kazi, ni masuala mtambuka ya watu wenye ulemavu yako mle, wapelekwe kwa Waziri Mkuu na nimeshamwambia Waziri Mkuu mara kadhaa alifikirie hili, kwamba watu wenye ulemavu waingie kwenye masuala hayo, kwa sababu kuna Wizara nyingi, Miundombinu, Elimu, Afya, Ulinzi, Sheria vyote hivyo masuala ya watu wenye ulemavu yanapitia humo kwa hiyo ni masuala mtambuka. Pia, Ustawi wa Jamii bajeti yao ndogo, waongezewe bajeti na ukarabati wa miundiombinu pia ni muhimu kwenye vyo vya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la ajira. Ajira kwa watu wenye ulemavu ni tatizo, mtu akiwa mlemavu hata kama amesoma ana vyeti vyake, akienda kuomba kazi anapigwa teke, kisa ulemavu. Sasa ulemavu jamani ndiyo kichwani kule nako kumelemaa? Kichwani hakujalemaa, kichwani akili ipo, anaweza akawa ni mlemavu lakini ana akili na anaweza akafanya kazi. Kwa hiyo suala la ajira tuna asimilia tatu ya kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumeshalizingumza sana humu ndani, halijafanyiwa kazi, hatujasikia kauli kwa wanaotoa ajira, waambiwe na Serikali wafanye nini. Serikali

5 FEBRUARI, 2015

itoe tamko leo, naomba mtoe tamko kuhusiana na ajira kwa watu wenye ulemavu, wanakosa gani? Mtu amesoma, ana *masters*, mwingine ni daktari ana ulemavu eti kisa ulemavu wake, kwa kweli siyo haki kabisa. Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ningependa nilizungumzie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nizungumzie kuhusu Saratani. Jana ilikuwa ni siku ya Saratani Kimataifa na kauli mbiu ilikuwa Kuzuia Saratani Inawezekana, ni kitu kinachowezekana, inawezekana kabisa, Saratani ni changamoto kwa watu wenye Ulemavu wa Ngozi tunapata Saratani ya Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimkuta mgonjwa mwenye Saratani ya Ngozi lazima kama wewe ni mtu mwenye huruma utatokwa machozi. Saratani ni mbaya sana na inasababishwa na jua, jua likimpata mtu mwenye ulemavu wa ngozi kwa kipindi kirefu anapata Kansa ya Ngozi, kwa kweli imeshaua wengi, mara nyingi tunasafirisha maiti kutoka *Ocean Road* kurudisha Mikoani, mashahidi wapo, tumesafirisha pamoja maiti hizo. Wanakuja wako kwenye *critical situation*, matokeo yake wanafikia kifo na kusafirishwa. Kwa hili tatizo Serikali wanajua, pesa zitafutwe ili kusudi kudhibiti. Pesa zikipatikana ni rahisi sana kushughulikia tatizo hili la Saratani, ni ugonjwa mbaya sana ambao ni katika magonjwa ambayo yasiyoambukiza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni kengele ya pili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa ni ya pili.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata hii nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimemwita Mheshimiwa Komba, Mheshimiwa Nassib na Felister Bura wajiandae!

5 FEBRUARI, 2015

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hizi Kamati mbili, lakini kabla sijachangia kuna jambo ambalo linazungumza humu linapotosha maana, naomba nilinyooshe vizuri. Sherehe za miaka 38 ya CCM zimefana sana. Wanazungumza hapa akina Suzan kwamba eti tulichukua watoto, wale watoto waliambiwa waombe wenyewe kwa upenzi wao na jioni saa kumi, baada ya masomo yao ndiyo walikuwa wanafanya gwaride lile na siyo wakati wa kazi, hata sherehe yenyewe imefanyika siku ya Jumapili ambayo siyo siku ya kazi. Hizi zote ni chuki tu. *(Makofi)*

Kwanza Suzan Lyimo, ama sijui Vicent Nyerere niwaulize hapa, CHADEMA ilizaliwa lini hawana majibu, hawajui lini Chama chao kimezaliwa, hawa wote wa CUF hawa hawajui lini, mimi nafikiri anayejua kuzaliwa CHADEMA... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa changia hoja, Mheshimiwa changia hoja!

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Naam!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najibu kwanza hili ili lisilete mchanganyiko. Tulishinda vizuri, tulifanya vizuri nawasubiri mvua zile za masika Mwezi wa Kumi mwaka huu, wanaringia asilimia ishirini, tangu Nyerere asilimia shirini, hiyo hiyo ishirini wameungana ishirini, utaishinda CCM wewe? chezea CCM wewe? *(Makofi/Vicheko)*

Sasa nirudi kwenye maada... *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Nikae chini?

MWENYEKITI: Ndiyo kaa chini Mheshimiwa Komba!

5 FEBRUARI, 2015

MHE. VICENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa tu napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Komba kwamba hata CCM ilizaliwa tarehe tano mwezi wa Pili lakini kwa sababu imepoteza kumbukumbu walifanya sherehe tarehe moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komba unapokea taarifa hiyo?

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Naipokea huo ni umbumbu wake tu, CCM haiwezi kufanya sherehe siku ya kazi, ndiyo maana tukarudisha Jumapili ili watu wote waone, tungefanya siku ya kazi mngelalamika pia hivyo hivyo. Kwa hiyo, tumewajua kwa kulalamika, tumewajua kwa kusema uongo. CCM imefanya tarehe ile kwa sababu si siku ya kazi. Hiyo nambari one hiyo! *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Endelea na mada.

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Tunaendelea bwana. Sasa niende kwenye hoja hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana na jinsi Serikali hii ya CCM sikivu inavyotoa pesa kwa Wizara ya Kazi halafu isitimize. Mmetoa shilingi bilioni kumi na saba, lakini hapa wamepata shilingi bilioni sita tu. Wizara ya Maendeleo shilingi bilioni kumi na sita, wamepata shilingi bilioni nne tu. Wizara ya Kazi shilingi bilioni therathini na sita wamepata shilingi bilioni kumi na nne tu. Sasa naomba kwa hili, mengi mazuri mnafanya lakini kwa hili lazima niwaseme kidogo, mrekebishe hii kitu.

Ya pili nipongeze Benki ya Wanawake....

TAARIFA

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Taarifa gani tena? Wanani katisha katisha vipi hawa!

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Mheshimiwa mwache aendelee, endelea Mheshimiwa Komba. *(Makofi)*

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Sawasawa, kaa chini!

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nikimaliza...

WABUNGE: Kaa chini! *(Makofi)*

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Kaa chini niendelee!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kti ndiyo kinasema nani atoe taarifa na nani aendelee. Mheshimiwa Komba endelea huna haki ya kumwambia wewe kaa chini.

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Taarifa yangu aipeleke Polisi, sasa naendelea! *(Makofi)*

Benki ya Wanawake, ninashukuru sana Benki ya Wanawake kwa uongozi wake, menejimenti yake, Mama Chacha anafanya kazi usiku na mchana, lakini tafizo anakosa vitendo. Yule mwanamke alichaguliwa kweli kweli, hata mimi hapa niseme kabisa kwa upande wangu, kanipa mkopo wa pikipiki 300 nimepeleka kwenye vijiji huko. Benki changa lakini inaweza kukopesha miradi mbalimbali tena kwa riba nafuu kuliko benki zingine, kwa hiyo nawapongeza sana, lakini naomba Serikali itimize wajibu wake wa kutoa shilingi bilioni mbili kila mwaka, ili benki ya wanawake iweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Halmashauri zote za Wilaya, hili jambo si mchezo la wanawake kupata asilimia tano na vijana kupata asilimia tano, kwa sababu haya ndiyo makundi ya maendeleo ya nchi yetu. Ukimwelimisha

5 FEBRUARI, 2015

mwanamke umeelimisha Taifa. Sasa leo mwanamke unamnyima hata ile ambayo imetungwa na sheria, hii ni dhambi, naomba Halmashauri, naomba Waziri wa Tamisemi afuatilie na atoe adhabu kwa Halmashauri ambazo hazifanyi vizuri katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, leo nipongeze tu daraja la Kigamboni. Nawashukuru sana Serikali na NSSF kutotegemea hela za nje ni hela zenu wenyewe za ndani, leo ukienda pale darajani unafurahi. Nakumbuka miaka ya 80 kuna Mwalimu mmoja anaitwa sijui Mwalimu nani, Boti la wanafunzi lilipinduka halafu akawa anazama ndani anaokoa wanafunzi anawatoa nje pale Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kumaliza mtoto wa mwisho yeye mwenyewe akafa ndani ya maji, akaokoa wanafunzi, wakati wa Getrude Mongella akiwa katika Wizara ile. Kwa hiyo naomba sana Watanzania watambue Serikali yetu imefanya jambo kubwa kweli, vifo vingi vimetokea pale lakini baada ya mwezi wa Sita mwakani, Kigamboni na Dar es Salaam patakuwa peponi kabisa, peponi kabisa, oye oye kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kusema mengi, mmefanya mengi bwana, mengi mengi, naomba Serikali yetu isivunjike moyo, mbele kwa mbele, tutafika tu, hakuna kihelehele. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Nassib, atafuatiwa na Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Christowaja una nafasi ya kuchangia yale utayaeleza katika nafasi yako.

Mheshimiwa Christowaja Mtinda, naomba ukae chini.

5 FEBRUARI, 2015

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza tumshukuru Mungu sana mwingi wa rehema kwa neema zake nyingi sana juu yetu.

Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na kadhalika nimshukuru Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Said Mtanda na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa *Captain* Komba, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi katika ajira. Hivi sasa kama mnavyoelewa, nchi yetu imekabiliwa na tatizo kubwa sana la ajira, ajira ya vijana. Maelfu ya wahitimu wanamaliza vyuo vikuu, wanamaliza taasisi, wanamaliza *form six*, *form four* na hata *form two* na kuingia katika soko la ajira. Wengi wao hawa au kwa wachache sana ndiyo wanaopata ajira ya kuajiriwa, lakini wengi wanabakia katika mitaa wanazurura, hawana kazi. Hili ni tatizo kubwa sana na hatua thabiti lazima zichukuliwe ili kuliondoshwa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia za kuondosha tatizo hili ni tatu, ya kwanza ni kuweka mazingira mazuri wezeshi ili hawa vijana waweze kujajiri. La pili, kuondosha fikra potofu, au mawazo potofu, kwa hawa wahitimu wote, kwamba watakapomaliza kusoma, watapata ajira. Na la tatu, ni kupatikana mikopo yenye riba nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yakifanyika, basi nafikiri tatizo la ajira litapungua. Kama wenzangu mara nyingi walivyosema, kwamba hili tatizo la ajira, sawasawa na bomu, ambalo wakati wowote linaweza likalipuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mifano mizuri ambayo Kamati yangu ilipotembelea Halmashauri ya Temeke waliona. Wizara ya Habari, Vijana na Utamaduni wakishirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, walitoa milioni 17 kuipatia *Temeke Youth SACCOS*. SACCOS hii, iliwakopesha vikundi vitatu na vikundi hivi viliweza kufanya vizuri sana na ni mfano mzuri kwa Tanzania nzima.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi cha kwanza ni *Sokoine Youth* ambao walipewa milioni tano na wao wanafanya kilimo cha umwagiliaji. Wanalima matikiti maji, wanalima mbogamboga, mapesheni, vilevile wanafuga kuku na bata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfani mzuri kwa sababu kwa muda ambao wamekopeshwa fedha hizi, wameweza kulipa kwa wakati marejesho na vilevile hali ya maisha yao imekuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi cha pili ni *Waungwana Youth Family*, ambao hawa pia walipewa milioni tano, wanajishughulisha na mambo ya saluni na muziki wa kizazi kipyaa, na hawa vilevile wameweza kuboresha hali zao na kadhalika wamerejesho marejesho yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi cha mwisho kabisa ambacho ningependa kukizungumzia ni *African Regan's*, ambao hawa walipata mkopo wa milioni saba. Katika mkopo huu wameanzisha *restaurant*, wanalisha chakula kwa wanafunzi wenzi wao wa vyuo, lakini vilevile wanajishughulisha na *stationery* na kadhalika wanafanya kazi za *consultation* na kutengeneza *computers*.

Hawa ni wataalam ambao wamemaliza *degree*, baada ya kumaliza *degree* hawakutegemea kazi za kuajiriwa, lakini badala yake, wameweza kujajiri wenyewe kwa kufungua mgahawa wao, kupika, kufanya kazi za *stationery* na vilevile kufanya mambo mengine ya kuweza kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifano mitatu ni somo tosha kwa Halmashauri na Wizara kuweza kuiga na kuweza kupeleka katika Halmashauri nyinginezo na kuweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hawa wamefanya vizuri, wamelipa na maisha yao yamebadilika.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitajikita zaidi katika ajira, na sasa hivi nitaazungumzia namna gani vibali vya ajira vinavyotolewa vibaya na Serikali kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumesikia, kwamba zaidi ya wachina 300 wameingia nchini na hawa wachina 300 wamekwenda Dangote katika kiwanda cha saluji na wanafanya kazi. Kwa kweli wengi kati ya hao ujuzi wao upo nchini, lakini wamefika hapa wanaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni vijana ambao wametoka Nepal na India, walipewa vibali kuja kufanya kazi hapa, baadaye ikagundulika wanafanya kazi za ukahaba na kazi nyinginezo ambazo hazifai. Wote hawa walipata vibali vya kuingia nchini kuja kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tunaona sisi waziwazi, kwamba katika miji yetu mikubwa kuna wageni wengi sana ambao wanafanya kazi ambazo Watanzania wangeweza kufanya. Kazi za kuuza viatu, maduka ya kuuza *stationery* na mambo mengine kama hayo, Watanzania wanaweza wakafanya, lakini wamepewa kibali na wako nchini wanafanya kazi kama hizo.

Sasa watu wetu wengi wapo hawana ajira, ingekuwa hivi vibali vinadhhibitiwa vizuri na Wizara ya Kazi na nyinginezo ambazo zinatoa vibali, basi kazi zingeweza kupatikana kwa Watanzania.

Kwa hiyo, ningetaka Wizara ya Kazi itakapokuja hapa, ilete majibu kwa masuala haya ambayo yametokezea, watu ambao wamekamatwa na hao wengine ambao nimewataja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa hivi habari ya *TBC*; *TBC* ilipangiwa kupewa bilioni sita mwaka huu ili kuboresha *TBC*. Kwa sababu kama unavyojua tuna uchaguzi mwaka huu, lakini kadhalika kuna kura ya maoni ya Katiba. Bila kuiboresha *TBC*, watahindwa kufanya kazi zao vizuri.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inasikitisha sana, kwamba mpaka sasa hivi wamepewa bilioni mbili. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha, wawaongezee fedha, bilioni nne zilizobakia ili waweze kukamilisha kazi hiyo ambayo wanataka kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nitazungumzia deni la *NSSF*, inaidai Serikali zaidi ya bilioni 800. Shirika hili linashindwa kufanya kazi zake vizuri, linashindwa kuboresha maisha ya wafanyakazi wake kutokana na mkopo ambao Serikali haijalipa.

Vilevile *PPF* inaidai Serikali zaidi ya bilioni 239, nao vilevile wako taabani, wanashindwa kufanya kazi za maendeleo, wanashindwa kuboresha maisha ya wafanyakazi wao kutokana na Serikali kwamba hailipi deni hili. Kwa hiyo, naomba Serikali watakapokuja kujibu hapa, watuambie mipango gani ipo ambayo itaweza kufanywa ili kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bura, utajijandaa Mheshimiwa Christowaja!

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze kwa kupata nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili, lakini pia niwapongeze Mawaziri wanaohusika na Kamati ambazo zinajadiliwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuunge mkono sana dada yangu Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na hata nimpongeze pia ndugu yangu Mheshimiwa Said Mtanda, mdogo wangu kwa taarifa zao nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, pendekezo la Kamati kuhusu kuhakikisha kwamba taasisi za elimu zinaimarishwa sasa na hasa Baraza la Mitihani.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani limefanya kazi nzuri kwa kipindi kirefu. Zamani kulikuwa na vyeti *fake* kibao mitaani na watu walikuwa wanapata kazi kwa elimu ambayo haiwahusu, wengine madaktari, lakini hawakusomea udaktari. Wengine waliitwa wana *PhD*, lakini hawakuwa na *PhD*. Kwa hiyo, tumeona udhibiti wa Baraza la Mitihani jinsi linavyosaidia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Ninawasihi na ninaisihi Serikali yetu kwamba, wawasaidie Baraza la Mitihani kujiimarisha na kama kuna changamoto ambazo zinalikabili Baraza la Mitihani, basi Serikali ione namna ya kulisaidia Baraza la Mitihani. *(Makofi)*

Nilipata fununu kipindi fulani kwamba Baraza hili lilitaka kuvunjwa, lakini litavunjwaje hata Kamati inayohusika haina taarifa? Litavunjwaje kama Bunge lako tukufu halina taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Baraza hili, wapewe vitendea kazi, wapewe fedha za kutosha ili liweze kuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Idara ya Ukaguzi, kila bajeti inapofika, Idara ya Ukaguzi tunaipigia kelele sana. Katika Halmashauri yangu ya Manispaa ya Dodoma hawana hata ofisi, hawana gari la kukagua shule, kwa hiyo, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Serikali ingewasaidia Idara ya Ukaguzi kujiimarisha, na kama haiwezekani, basi iwe Wakala kama Kamati ilivyopendekeza kwamba Idara ya Ukaguzi iwe Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia sana suala la vazi la Taifa kwa muda mrefu. Nashangaa kwamba Serikali hii iko kimya na kila wakati, kila mwaka tunazungumzia suala la vazi la Taifa, lakini sijawahi kuona. Utambulisho wa Taifa la Mtanzania, mbali ya Kiswahili, kuna wakati Wizara ilileta pendekezo na nini kwamba tuwe na vazi la Taifa na

5 FEBRUARI, 2015

linajadiliwa kila mwaka, lakini sijawahi kuona kwamba hitimisho la vazi la Taifa liko wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Kamati hasa ya Maendeleo ya Jamii, kwa kutembelea wajasiliamali vijana waliomaliza vyuo vikuu. Kamati na imetaja baadhi ya makundi ya vijana ambao wameamua kujijiri, na mimi nina makundi ninayoyafahamu na kundi moja linaitwa *Rabican*, mwenyekiti wake anaitwa James Ezekiel, na wameanza kilimo, wamelima maharage ekari 50 na wanategemea kupata zaidi shilingi ya milioni 60 kwa kuvuna mara moja, msimu mmoja. Kwa hiyo, nina imani kwamba vijana wakiwezesha wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasomi sasa hivi wameamua kijijiri. Nimefurahi sana kwamba wasomi wana mgahawa na wanahudumu wenyewe na baadaye wanatumia taaluma zao. Hawa ambao kampuni hii ya *Rabican* ambao wameanzisha, wanafunzi kutoka *DUCE* wako watano, wameamua kujijili katika kilimo na wamefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba, wameambiwa na maafisa kilimo kwamba hawatapata chini ya milioni 50. Hawajawezeshwa, walikwenda kwenye dirisha la kilimo kule Dar es Salaam, hawakupata fedha kwa ajili ya mkopo na wameambiwa wawe na dhamana. Hawa watoto wadogo waliomaliza vyuo vikuu wana dhamana ya nini, hawana ardhi, hawana nyumba, hawana magari, hawana kitu chochote, lakini wameambiwa wawe na dhamana ya kupeleka benki ndiyo wapate mkopo! Kwa hiyo, hawa vijana wametembea wakiombaomba fedha kwa ajili ya kupata mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa na mfuko wa vijana unaoeleweka, wasingehangaika kutafuta fedha mitaani. Wangepata fedha kupitia kwenye Halmashauri zetu. Lakini kwa sababu Halmashauri zote hawajali kutenga ile asilimia tano, ndiyo maana hata vijana hawa wanaomaliza

5 FEBRUARI, 2015

vyuo vikuu, wanatangatanga tu kutafuta mtaji, hawana dhamana, hawana nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri sasa, na leo naomba Serikali ituambie, tangu huu mfuko uanzishwe, umekua kiasi gani? Kwa sababu tunasema tu mfuko wa vijana na wanawake, mfuko wa vijana na wanawake, huu mfuko haukui? Ungekuwa unakua, hawa vijana wanaomaliza vyuo vikuu wala wasingehangaika kwenda benki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombab Serikali ituambie, huu mfuko sasa hivi umekua kwa kiasi gani na vijana watakaomaliza vyuo vikuu mwezi wa Juni mwaka huu, tuwambie kwamba fedha zipo katika Halmashauri zao, waende wakapate mikopo kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linahuzunisha kwamba bilioni 15 zimeshindikana kupelekwa benki ya wanawake. Benki ya wanawake ni msaada mkubwa kwa wanawake walioko vijijini. Benki nyingi ziko mijini hawataki kwenda vijini na kwa sababu mkopaji wao ni Serikali Kuu, kwa hiyo wamebaki mijini. Lakini benki ya wanawake imekwenda hata vijijini. Bajeti ijayo tunaomba bilioni 15 ambazo zinatakiwa kupelekwa benki ya wanawake zipelekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la *TBC* lina miaka 20 halijakamilika, umri wa mtoto ambaye yuko chuo kikuu kwa sasa! Sijui Serikali inapata kigugumizi gani kuidhamini *TBC* ambayo ni *TV* ya Taifa ipate kuonekana kwa Watanzania wote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumizie suala la asasi za kiraia. Tusipoweka udhibiti katika asasi za kiraia ambao wamechukua watoto wa mitaani kama mtaji, wale watoto wengine wanalala kwenye maeneo machafu, maeneo yasiyoeleweka, lakini fedha zinakwenda kwa ajili ya wale watoto kuwahudumia.

5 FEBRUARI, 2015

Serikali ifanye tathimini na tuambiwe kwamba tathimini ya mwisho ilifanyika lini kuangalia taasisi ambazo wanasema kwamba wanahudumia watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna posho ya mazingira magumu, imezungumzwa kwa walimu tu, kwani manesi hawapo kwenye mazingira magumu! Manesi wanaoishi kwenye maeneo ambayo ni *remote areas*, watazamwe kwa jicho lingine. Na hata kwa madaktari na wafanyakazi wengine ambao wanafanya kazi katika mazingira ambayo ni *remote areas*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie suala la wasanii, wasanii ambao nyimbo zao ambazo zipo kwenye milio ya simu, je, wanapata haki zao? Tunataka kujua, kama wanapata haki zao, kwa sababu siku hizi milio ya simu wameweka nyimbo za wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia tatizo la watoto ambao baba zao wamewakimbia. Wamezalishwa watoto wetu mitaani, lakini akina baba hawatunzi watoto wao, wamewaacha watoto wao. Sheria wakienda ustawi wa jamii, wanaambiwa ni shilingi mia tu kumhudumia mtoto mmoja. Shilingi mia unanunua nini hata andazi hakuna la shilingi mia. Lakini watoto wapo, Wabunge ndiyo tunatafutwa, mtoto wangu baba yake kamkimbia, ukimpeleka ustawi wa jamii, sheria hairuhusu zaidi ya shilingi mia, sijui ni shilingi mia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kuna haja ya kurekebisha sheria na hata wale ambao hawazai na watoto wa shule, lakini wanazaa na wanawake na kuwatelekeza watoto wao, Serikali iweke sheria ya kuhakikisha kwamba wale watoto wanatunzwa inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la MSD, bilioni 93. Tunategemea dawa kutoka MSD, hata zahanati zetu za vijijini wanategemea hizo dawa kutoa MSD.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni fedha za wanachama zinazoliwa na Serikali, hawataki kutoa fedha zile walizozikopa kutoka mifuko ya hifadhi ya jamii, wazilipe. Kwa sababu riba inayolipwa kwa wanachama wetu inatokana na fedha za uwekezaji. Kwa hiyo,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bura, muda wako umekwisha.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuita Mheshimiwa Christowaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Lyimo, kukiwa na muda atazungumza mMheshimiwa Machali.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa ku-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Naunga mkono taarifa iliyoletwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, zote kabisa naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na taarifa yangu ambayo nilitaka kumpa Mheshimiwa Komba kwamba, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inafanya kazi kwa kanuni na taratibu na sheria zilizowekwa na nchi hii. Walimu na wanafunzi hawaruhusiwi na wala hawana ruhusa ya kushiriki katika sherehe za chama chochote cha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barua hapa, pamoja na miongozo kutolewa asubuhi na kupuuzwa, barua hii imetoka kwa Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa ya Songea kwenda kwa Wakuu wa Shule za sekondari zifuatazo, za sekondari, siyo za msingi:-

5 FEBRUARI, 2015

Shule ya Sekondari ya Songea Boys, Songea Girls, Matogoro, Mashujaa, Matarawe na Mfaranyaki, shule sita za sekondari. Anawaabia walimu, watumishi na wasio walimu, wanafunzi, sote lazima, LAZIMA. Hiyo LAZIMA ni ya herufi kubwa, kuhudhuria hizo sherehe za sikukuu sijui ya kuazimisha maiaka mingapi ya Chama Cha Mapinduzi. Hili ni agizo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haikubaliki na wala hatuwezi kufurahia jambo hili, ni uvunjaji wa Katiba ya nchi, haikubaliki hata siku moja. Ndiyo maana wanafunzi wa shule za sekondari na shule za msingi za Serikali, wanafeli. (Makofi)

Hapa hakuna wanafunzi wa shule za *private*, hata wanafunzi wa shule yako hawaendi kwenye sherehe za namna hiyo. Una shule, hawaendi wanafunzi wa *private*, wanakwenda wanafunzi wa shule za Serikali tu, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo linatakiwa litolewe ufumbuzi na lifanyiwe tafakuri ya hali ya juu. Waziri wa Elimu na Naibu Waziri mko hapa, hatutaki kusikia fena. Wala hizo halaiki za kuwapeleka wanafunzi, eti baada ya masomo, sio sawa. Baada ya masomo mwanafunzi anatakiwa kufanya *assignment* na kupumzika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye mchango, Sera ya Elimu inasema kwamba mwanafunzi aosome siku 196 kwa mwaka; hizo ni kuondoa *public holidays*, ukiondoa likizo zao fupi na ndefu, ukiondoa Jumamosi na Jumapili. Siku 196 mwanafunzi anatakiwa awe darasani anasoma. Siku za mapumziko anatakiwa afanye *assignment*, afue nguo zake, apumzike, aende kwenye michezo *a-refresh*, sio kwenda kwenye halaiki, haikubaliki. Na hii kwa kweli Chama Cha Mapinduzi mnaaibisha Sera ya Elimu na mnaaibisha elimu nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mchango wangu. Kuna matatizo makubwa sana kwenye mfumo wa elimu, tuna matatizo makubwa sana. Pamoja na Wizara kusema mnajitahidi, mnataka kuongeza walimu wa sayansi

5 FEBRUARI, 2015

kwenye ngazi za chini, sekondari na elimu ya msingi, na juzi hapa, Bunge la juzi la Novemba tumepitisha Muswada wa Mabadiliko Mbalimbali ya Sheria ambao uliruhusu Bodi ya Mikopo kutoa mkopo kwa ajili ya hao wanafunzi mliotumbia wako 5,000 wanaochukua sayansi kwa ajili ya shule za sekondari na cheti kwa ajili ya shule za msingi, wengi wao tuliambiwa wako UDOM na wengine wako Korogwe na vyuo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, hawa wanafunzi, pamoja na kupitisha hiyo sheria, mimi kama Mjumbe wa Kamati tulihakikishiwa pesa zipo; kulikoni wanafunzi wa UDOM wakaandamana kudai pesa zao? Sikukubaliana na majibu ambayo tuliyapata kwa sababu sisi tuna wadogo zetu, tuna wanafunzi ambao ni watoto zetu wanasoma pale, wanasema hawakupewa zile pesa. Pesa ziko wapi?

Kwa nini mtie hasira wanafunzi mpaka waamue kuandamana barabarani, halafu matokeo yake muwapige mabomu, muwachukue kama vile ni wafungwa, wakati Serikali hamjapeleka hela? Kwa nini hazina mnatutenda hivi? Kwa nini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi mnawaonea wanafunzi wanyonge? Hebu mkae mjitafakari. *(Makofi)*

Waziri wa Elimu umekuwa Waziri miaka yote tangu mimi nimekuwa Mbunge hapa, Wizara hii imefanikiwa kubadilishiwa Manaibu Waziri mara tatu, imefanikiwa, nasema fanikio hilo.

Naomba mfanye uchunguzi wa dhati, hawa wanafunzi wa sayansi ambao tunawataka, je, kweli wako 5000? Tuliambiwa UDOM wako 2,177, tuliambiwa Korogwe wako 77, tukaambiwa, tena sio wale wa Diploma, ni wale ambao wanasoma Shahada, wamemaliza UDOM, waliposikia mkopo wakaenda Korogwe. Hili lina ukweli kiasi gani? Kama ni kweli hizo pesa ziko wapi? Kuna siri gani hapa? Tusifanye siasa kwenye elimu kila siku nasema, mimi ni mwalimu, tusifanye siasa kwenye elimu, tusitake kuonesha tumefanikiwa wakati tunarudi nyuma. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo, juzi na jana hapa mmetoa maagizo, mmetoa matamko kuziambia shule za *private* wasikaririsha wanafunzi, wasifukuze, sijui wasikatae wanafunzi, eti alama za 30. Nani *private* atachukua mwanafunzi mwenye alama za 30? Hamjui kama ninyi mmeifanya elimu iwe ni biashara?

Private schools hazipewi ruzuku na Serikali, ni biashara *per se*, mtu anatafuta bidhaa bora, anapeleka mwanafunzi kupata *quality* ya elimu, hatuangukii *quantity* pale. Hata mzazi wa leo hawezi kumpeleka mwanafunzi wake au mwanae kwenye shule ambayo ina alama 30, hakuna, tusidanganyane hapa. Hayo maagizo, sijui amri, sijui nini havifanikiwi, *unless otherwise* muamue kufufua elimu yetu ambayo mmeidororesha miaka nenda rudi ili shule zetu za Serikali zifanye vizuri kama tulivyokuwa mwanzo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesoma shule ya Serikali, kila siku namsifia mwalimu wangu Mheshimiwa Mkanga hapa, ni mwalimu wangu, amenifundisha *form five* na *form six* Kilakala, *form one* mpaka *form four* nimesoma Msalato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeona wanafunzi wa Msalato, nimefurahi sana. Mimi ni *product* ya Msalato, tumesoma shule nzuri sana. Elimu ilikuwa nzuri sana, yemekwenda wapi hayo mazuri ya elimu? Tusifanye siasa, siasa inatawala ndiyo maana leo mnawaagiza wanafunzi kuhudhuria eti sherehe za CCM. *Never*, hatuwezi kukubaliana, yaishe. Sio sawa sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije afya. Kwenye Afya naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati. Deni la MSD, sasa hivi tunavyozungumza deni ambalo ni jipya ni bilioni 93.3. Serikali inakopa tu, inakopa tu, inakopa tu. Hivi hamjui kwamba hawa wanawake wa vijijini wanaowapigia kura ndio hawapati dawa? Hamjui kwamba akina mama wajawazito na watoto ndio wahanga wakubwa wa hii ya ninyi kukopa kopa huko MSD na kutokulipa?

5 FEBRUARI, 2015

Sisi hatuwezi kwenda kusimama kwa wanawake, hawana hata Aspirini, anapokwenda hospitali hata vifaa vya kujifungulia anavyotakiwa kupewa bure, anabeba kwenye begi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukubaliana, Serikali mlipe deni. Mlituomba tupitisha bajeti ya Wizara ya Afya, tukapitisha kwa makubaliano kwamba mtalipa deni, hamlipi! Deni mlilolipa ni la zamani, mmelipa bilioni 30.7 out of bilioni 40.4 ambalo lilikuwa limehakikiwa mpaka Juni, 2012. Aibu kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Hakuna afya bora hapo, mlipe deni hilo. Hiyo afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makaimu kila mahala, yaani kila idara watu wanakaimu tu, hata huyu Mkurugenzi wa MSD hata kama ni mbaya, lakini anakaimu *for three years now*, miaka mitatu mtu anakaimu, hivi atafanyaje kazi huyu? Kama mbaya si mumuweke mwingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anakaimu miaka mitatu, mnategemeaje atafanya kazi? Na ni idara nyingi za Serikali wanakaimu. Wanakaimu, wanakaimu. Hizi Wizara mbili hizi zimezidi kwa kukaimu. Hebu mlifuatilie na mliangalie. Sasa sisi tumechoka, kila tukija kukutana na Wizara, wanakaimu, wanakaimu, utendaji kazi sifuri, hakuna kila mahali ni sifuri, hiyo hatuwezi kukubali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwapa pole waalimu na kuwapongeza kwa kazi wanayoifanya. Wametangaza mgomo, lakini najua hawatagoma, wakitaka kugoma Jaji ataitisha *Court Injunction* hata saa tatu za usiku, watanyamazishwa watakwenda kufundisha. Lakini mgomo wa waalimu uko kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi wanafunzi wanakipata cha moto. Mgomo wa mwalimu hamchapi mwanafunzi fimbo, anakwenda darasani kwa sababu kitengo cha ukaguzi ni sifuri, anafundisha moja jumlisha moja ni kumi na moja, mbili jumlisha mbili ishirini na mbili, tatu toa

5 FEBRUARI, 2015

tatu tatu. Hiyo ndiyo adhabu ambayo wanafunzi wetu wanapewa.

Hebu angalieni, hawa walimu muwape motisha ili waweze kutulia, wasiende kule kufundisha shule za *private*. Hawa ndio mnaowapa mikopo asilimia mia moja, lakini leo wako *private schools* na wanafanya vizuri, ndiyo matunda ambayo tunajivuni sasa hivi kwenye *private schools*, ni waalimu hao mnaowapa mikopo. Kwa nini mmeshindwa kuwa-retain? Kwa nini msiwape motisha wabaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walimu wa Sayansi hawajatoka mbinguni kwenye shule za *private*, ndio hao hao ambao wanatoka kwenye shule za Serikali, ndio mnaowapa mikopo asilimia mia moja, lakini hawabaki kufundisha. Shule zenu hazifanyi vizuri, Wizara ya Elimu hamuwapi motisha walimu. Wapeni motisha walimu wabaki kufundisha, tuna walimu wengi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukururu sana. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Nimemwita Mheshimiwa Susan Lyimo na nadhani atakuwa ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii, wengine watakuja jioni.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukururu sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia hoja muhimu zilizo mbele yetu, ya Wizara ya Elimu na nitajikita zaidi kwenye masuala ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumwambia Mheshimiwa Komba kwamba shule au wanafunzi wanapokuwa shuleni Jumamosi au Jumapili maana yake wanajiandaa kwa *programs* mbalimbali kwa *assignment*, na kwa maana hiyo haijapangwa Jumamosi au Jumapili kupumzika kwa maana ya kutosoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia kuhusiana na suala hili; ni wazi mfumo

5 FEBRUARI, 2015

wetu wa elimu umeporomoka na elimu ya Tanzania imeporomoka na imeporomoshwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuhakikisha kwamba watoto hawa wanafanyishwa mambo ambayo yako nje ya utaratibu wa elimu. Namshangaa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu anapobariki masuala haya ya kwamba watoto waende kwenye siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, au Serikali, yeye ndiye Serikali hapa Bungeni; anapojibu maswali hovyo hovyo ya kuonesha kabisa upendeleo na kutokuelewa maana ya elimu, tunapeleka Taifa kaburini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema mazungumzo hayo, imesikitisha na Tanzania nzima imeona ni jinsi gani nchi hii isivyokuwa na viongozi wenye uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuchangia. Katika taarifa ya Kamati halijazungumzwa jambo kubwa sana ambalo ni la muhimu, suala zima la migogoro katika vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba migogoro mingi inaletwa na suala la mikopo, lakini sasa hivi limejitokeza jambo kubwa sana la mitaala katika vyuo vya elimu ya juu. Natambua ya kwamba Tume ya Vyuo Vikuu ndiyo ambayo inasimamia ithibati za vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapoongea wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *IMTU* wako nyumbani kwa takriban mwaka mzima. Wamefuatilia jambo hili lakini na kwa masikitiko makubwa niseme Serikali kupitia Wizara ya Elimu na taasisi zake zimeshindwa kabisa kutatua tatizo la *IMTU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, watoto hawa walikuwa kwenye *program* ambayo tayari ilikuwa imepitishwa na *TCU*, *TCU* wamekuja kuifuta baada ya wanafunzi hao kuwa darasani. Wanafunzi hao

5 FEBRUARI, 2015

wamehangaika mpaka kwa Waziri Mkuu lakini suala lao bado liko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la Chuo cha Mtakatifu Joseph Branch ya Arusha. Ni jambo la aibu kwamba nimeongea na Mheshimiwa Waziri wa Elimu haelewi utaratibu wa chuo kile kwamba chuo kile usipofikisha asilimia 85 ya *attendance* mwanafunzi anafukuzwa chuo. Hiki ni chuo au shule ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza kuna wanafunzi wa chuo kile takriban 84 wako nyumbani kwa sababu za ugonjwa na hivyo wameshindwa kufikisha asilimia 85 ya *attendance* ya darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni bovu ni baya kwa sababu watoto hawa ni wale ambao Serikali na sisi wote tunajua kwamba tuna tatizo kubwa sana la walimu wa masomo ya sayansi. Chuo hiki kilijidavua kwamba kinaweza kuchukua wanafunzi, kiliwachukua, lakini matokeo yake wanafunzi wale wanapata matatizo makubwa, Serikali inajua, imewaachia Wahindi wale wanaendelea kuendesha kile chuo kama vile wako India.

Naomba Serikali pamoja na Kamati ihakikishe kwamba watoto wale wanatendewa haki, wale ambao wako nje ya masomo warudishwe masomoni kwa sababu tayari Serikali ilishawapatia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mwanafunzi wa kike anapata ujauzito au anaugua anaambiwa asisome kwa sababu haingii darasani, hili halikubaliki. Na naomba, kama utaratibu huo upo tuambiwe, lakini mimi ninavyojua kama mfanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwanafunzi wa chuo kikuu ni mtu mzima na anaweza kupata mimba, au kuolewa au kuo *as long as* ni mwanafunzi wa chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Kampala International University*. Chuo hiki nacho kina matatizo yale

5 FEBRUARI, 2015

yale. Tanzania ninavyojua, TCU kazi yake ni kutoa ithibati lakini baada ya kuhakikisha kwamba *program* zinazofundishwa ziko sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongea hapa ninajua *program* ya udaktari inachukua miaka mitano na *programs* nyingine za *pharmacy* zinachukua miaka minne. Lakini kwa Chuo Kikuu cha Kampala wameongeza *program* ya udaktari inakuwa miaka mitano na nusu na *program* nyingine miaka minne na nusu badala ya minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo haitambui huo nusu mwaka, nimeenda mpaka TCU, wamesema watalishughulikia, lakini mpaka leo bado ni tatizo, na ninavyoongea wanafunzi takriban 20 wameomba kuondoka kwenye chuo kile, tayari wame-*postpone* masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kadhia hii, naiomba au naitaka Serikali kupitia TCU kuhakikisha kwamba *programs* za vyuo vya elimu ya juu zinakuwa na ulinganifu, kwa maana ya kwamba kama ni *medicine* ni miaka mitano iwe mitano, kama ni sita iwe sita na si sehemu nyingine inakuwa mitano sehemu nyingine inakuwa mitano na nusu; hii inaleta kuwakanganya wanafunzi, lakini vile vile kutokujua nani atawalipia ada hiyo ya muda wa nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la ukaguzi. Nashukuru kwamba Kamati imeliona. Lakini jambo hili la wakaguzi kuwa wakala limezungumzwa siku nyingi, na Mheshimiwa Rais alipokwenda Mbeya mwaka 2013 alitoa agizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nashindwa kuelewa nchi hii, inaongozwa kwa misingi gani! Kwa sababu kama Rais wa nchi ametoa agizo mwaka mmoja/miaka miwili, leo Kamati inalileta tena kama pendekezo. Tunashindwa kuelewa huu ni utawala wa namna gani! Kwa nini kama Rais alishatoa agizo, miaka miwili imepita, bado wakala huyo hajafanya kazi na haijaanzishwa.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baya zaidi tunajua umuhimu mkubwa wa ukaguzi. Mpaka leo ninavyoongea tunatambua kwamba baadhi ya kanda ambazo zinatakiwa zikakague hawana magari, wanapata shilingi milioni nne, hawawezi kukagua kabisa, wamekuwa ombaomba. Kwa hiyo maana yake ndiyo sababu ukienda madarasani, sio shule ya msingi sio shule za sekondari, walimu hawapo madarasani, walimu watu wengine wanafanya biashara kwa sababu hakuna kitengo cha ukaguzi hakipewi fedha, hakijawa wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kitengo hiki, kama ni wakala, uanze mara moja kama lilivyokuwa agizo la Rais ili kuhakikisha elimu ya Tanzania inakwenda kama ambavyo tunataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuko hapa Dodoma, nimeenda kwenye Shule ya Msingi Nkuhungu, shule yenye wanafunzi 3,170 imefungwa kwa sababu haina matundu ya vyoo ya kutosha; hiyo ni shule iko kwenye Manispaa ya Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ambayo inatakiwa iwe na matundu 130, leo ina matundu 12, kwa hiyo Afisa Elimu ameenda ameifunga; halafu leo tunasema shule za *private* zisiwepo au zisifanye biashara. Hivi, kama shule nzima, watoto 3000 na wako nyumbani kwa sababu ya vyoo, unategemea watoto wafauluje, ukiongezea na CCM kuwapeleka kwenye halaiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema na vizuri kuhakikisha kwamba watoto wanasoma hawakai nyumbani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana na namheshimu sana Mheshimiwa Susan Lyimo, naomba tu kumpa taarifa kwamba, wakati Serikali ikitoa

5 FEBRUARI, 2015

taarifa zake Bungeni kuhusiana na shule binafsi, haikusema kwamba shule binafsi zitafungwa kama anavyochangia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuliweka hilo sawa sawa na kumpa hiyo taarifa. Serikali ilikuwa inazungumzia shule binafsi kufuata utaratibu wa kisheria na kikanuni katika kuendesha shughuli zake, na Serikali haikusema itafunga shule binafsi katika nchi yetu ya Tanzania. Naomba kumpa tu hiyo taarifa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Lyimo endelea.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa kwa sababu hata juzi hapa Bungeni Naibu Waziri alisema, kwa hiyo, naendelea.

Naomba nimalizie kwa kusema kwamba, kama tutaendelea na utaratibu huu wa kutokufuatilia shule hizi kutokana na kitengo cha ukaguzi kutofanya kazi, shule za *private* zitaendelea kutoa *cost* kubwa kwa sababu shule za Serikali zimeshindwa kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha kwamba wanatoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Asilimia tano kwa ajili ya wanawake na vijana: Katika nchi hii tuna makundi makubwa matatu yenye matatizo, nayo ni vijana, wanawake na wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee ni watu ambao wanakuwa hata wanahudumia familia za wenye UKIMWI, kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali vile vile iangalie ni jinsi gani wazee nao watafikiriwa katika asilimia tano ili wao waweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahsante. Waheshimiwa, muda wetu wa asubuhi umemalizika. Sasa kabla ya kusitisha kikao cha Bunge, naomba nitoe matangazo mawili.

Moja, wale watu wa *Unit Trust of Tanzania* bado wanaendelea na maonesho na wanaomba Waheshimiwa muendeleo kutembelea hapo kwenye eneo la maegesho ya magari.

Pili nisome majina ya ambao watachangia jioni. Tukiingia tu tutaanza na Mheshimiwa Machali, atafuatiwa na Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Mwaiposa, Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Salum Khalfan Barwan, wengine watatangaziwa baadaye tukiingia.

Sasa naomba nitishe kikao cha Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaanza. Mwenyekiti aliyeongoza Bunge asubuhi, ameacha majina. Tunaanza na Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia Taarifa hizi za Kamati ambazo ziliwasilishwa leo asubuhi za Kamati ya Huduma za Jamii na pia Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwa sehemu kubwa nakubaliana na maelezo mengi ambayo yameweza kutolewa na Wenyeviti wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ningependa kuanza na hili linalohusiana na *TBC*. Ni ajabu pengine kuona

5 FEBRUARI, 2015

majengo yakiwa hayajakamilika kwa zaidi ya miaka 20 kama ambavyo imeripotwa na Kamati.

Naiomba hebu Serikali ijiulize, kumekuwa kuna tatizo gani la kutokukamilisha majengo ya Shirika la Utangazaji (TBC) hapa nchini kwa zaidi ya miaka 20! Hivi kuna *seriousness* kweli kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba watu hawa wanakuwa na majengo ambayo yanawawezesha kuwa mahali pazuri na mahali pa usalama kwa ajili ya uendaji wa kazi zao? Tunaiomba Serikali itueleze ni jinsi gani ambavyo iko *serious* kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kuwa tunawatetea TBC, waweze kupata majengo ambayo mazuri, tuwaombe pia Watangazaji wa TBC, waache kufanya kazi kwa namna ambavyo inaonyesha misingi ya upendeleo na ubaguzi, hasa miongoni mwa vyama vya siasa.

Haya jinsi gani ambavyo mmekuwa mnafanya, kuna wakati umefika watu wengine tunatafsiri kwamba chombo hiki ni kama mali ya CCM. Mambo mengine ambayo wakati mwingine yanaonesha kwamba yanavihusu vyama vingine, mmekuwa mnafanya, mnakuwa kama vile mko *biased*. Hii inawezekana mnapewa maelekezo.

Mkurugenzi wa TBC naamini utapata *message* hii, kama Mawaziri wanakuwa wanakupatia maelekezo ya kukibeba Chama Cha Mapinduzi, unakosea sana kwa sababu hujui kesho ni nani atakayekuwa Serikalini. Angalia usije ukakuta kesho kwamba UKAWA kwa sababu ndio mpango mzima kwa hivi sasa, ukajikuta kwamba pengine kesho tutakushughulikia kwa mujibu wa sheria. Hatutaki watu ambao wako *biased* kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuhakikishe kwamba *principal of natural justice* zinazingatiwa kuhakikisha kwamba chombo hiki kitende haki kwa watu wote, kwa sababu tunalipa kodi, hawalipi kodi CCM peke yao, wanalipa kodi Wapinzani.

5 FEBRUARI, 2015

Kuna vipindi vizuri mmeondoa kama *This Week in Perspective*, leo hakuna ambapo kulikuwa kuna fursa ya kuweza kuwaalika watu kama Jenerali Ulimwengu na watu mbalimbali ambao wamekuwa wanachambua vitu vya msingi. Mmeondoa vipindi vya maana mnataka nini?

Serikali kamilisheni majengo haya wapate maeneo mzuri na mahala pa kufanyia kazi, lakini maslahi yao pia muangalia. Na wao waache kuweza kutekeleza maagizo ambayo tunasema kwamba hayana maana katika ujenzi na ustawi wa demokrasia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya eneo hilo naomba nizungumzie kidogo kuhusiana na *component* ya elimu. Sekta ya elimu hapa nchi inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Moja ya eneo ambalo linasababisha elimu ya nchi yetu kuweza kuyumba ni kwa sababu walimu wamekatishwa tamaa.

Walimu wamekuwa wanadai madai ya aina mbalimbali. Wanadai fedha za matibabu, wanadai fedha za uhamisho, wanadai fedha za masomo, wanadai fedha kwa ajili ya kupandishwa madaaja, wamepandishwa madaraja pengine hata mishahara haijarekebishwa. Mmewatelekeza, mnawakatisha tamaa, matokeo yake, tatizo ambalo linakuja kulikumba Taifa, ndicho kile ambacho amekieleza Mheshimiwa Christowaja, kwamba badala ya mwalimu aingie darasani, afundishe moja kujumlisha moja ni mbili, atawambia wanafunzi moja kujumlisha moja ni kumi na moja, kwa sababu wamekata tamaa. Na pengine kwa sababu kunakuwa kuna wanafunzi ambao uelewa wao ni mdogo kulingana na kiwango kile, wataamini kwa sababu tu mwalimu amesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko chini ukienda kwenye Halmshauri mbalimbali, baadhi ya Maafisa Elimu wamekuwa ni Miungu watu. Walimu wanandika barua za madai na wakiambatanisha na vielelezo, lakini matokeo yake Afisa Elimu hawezi kuweka *comment* yoyote kwamba huyu hili deni lilipwe au lisilipwe.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza na imefika mahali, wanapokuwa wanafanya uhakiki na Chama cha Walimu kwa mfano katika Jimbo langu la Kasulu Mjini, ile Kamati ambayo imekuwa inashughulikia madeni au madai ya walimu wanashindwa wafikie uamuzi gani, kwa sababu Afisa Elimu hakuweza ku-*comment* chochote kwamba madai haya ya Mwalimu X yalipwe au yasilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali, ni lini upuuzi huu ambao umekuwa unafanywa na baadhi ya watendaji wa Serikali, Maafisa Elimu pamoja na Wakurugenzi, wataacha *arrogance* na hivyo kuwapuuzi walimu, kutokuandika chochote kwenye barua zao wanapokuwa wanadai stahiki zao mbalimbali na hatimaye waweze kulipwa?

Nitaiomba kauli ya Serikali ni lini upuuzi huu utaachwa, kwa sababu ni upuuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaandika madai yake, ameambatanisha vielelezo, pengine alikuwa ni mgonjwa, alikuwa masomoni, alihamishwa, au anadai madai mengine ambayo ni stahili zake labda za kupandishwa cheo. Lakini hakuna kitu chochote ambacho kinaandikwa kwenye barua ya mwalimu, mwalimu anatabika sana.

Nitaomba nipate kauli ya Serikali, ni lini matatizo ya walimu hawa, ambayo yanatokana na uzembe au chuki za baadhi ya Maafisa Elimu ambao wanakuwa wanawagandamiza na hatimaye walimu wamekosa stahiki zao na wanazidi kukata tamaa. Kwa sababu hawa ndiyo ambao tunawategemea watusaidie kama Taifa kuhakikisha wanatoa elimu iliyo bora na siyo *just* elimu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, jambo la tatu ambalo ningelipenda kulizungumzia ni suala la uundaji wa Tume ya Utumishi ya Walimu (*Teachers Service Commission – TSC*). Tume hii ilikuwepo japokuwa ilikuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali huko nyuma.

5 FEBRUARI, 2015

Ni imani yangu, kama ambavyo naungana kabisa na Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Margaret S. Sitta, ambayo yenyewe imeona kwamba kuna haja ya kuwa na Tume ya Utumishi ya Walimu ambayo itaweza kushughulikia matatizo ya walimu ili kuhakikisha tunapunguza mlolongo wa walimu kushughulikiwa na Wizara zaidi ya nne, matokeo yake imekuwa ni usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu yuko TAMISEMI, mwalimu yuko Utumishi, Mwalimu yuko Wizara ya Fedha, Mwalimu sijui yuko Wizara ya Kazi na Afjira. Huu usumbufu, yuko Wizara ya Elimu. Huu usumbufu mnauongeza makusudi, ili kusudi Mwalimu akiambiwa jambo hili, aambiwe liko TAMISEMI, liko Wizara ya Elimu, liko Ofisi ya Rais, Utumishi, liko Wizara ya Elimu. Mmefanya makusudi ili mwalimu anapofuatilia stahiki zake mbalimbali akate tamaa kwa sababu hana uwezo wa kufika huko. Mishahara mnawalipa kidogo.

Sasa tunaomba mtueleze ni sababu gani zinazopelekea kucheleweshwa kuanzishwa kwa chombo hiki, wala chombo hiki hakihitaji Katiba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ilipokuwa TSC huko zamani baadaye mlirekebisha na kuja kuifanya kuwa (*Teachers Service Department – TSD*), hakukutokea mabadiliko ya Kikatiba mpaka kuja kuitoa kwenye kuwa TSC na kuja kuwa TSD. Tunaomba kauli ya Serikali, mtuambie ni lini chombo hiki kitarejea ili kumpunguzi mwalimu mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda siyo rafiki, naomba nizungumzie, kwanza niipongeze Serikali kwa kubali kwamba kuwe na shule mbalimbali za Kata, hili ni jambo jema.

Sasa tunapokuja kwenye ku-measure kwamba *quantitatively* au *qualitatively*, tunakuja kuona kweli kwenye ujenzi wa madarasa mmefanikiwa, mmejenga madarasa

5 FEBRUARI, 2015

mengi chini ya *quantitative approach*, ni kweli madarasa yapo. Lakini, kuwepo kwa madarasa ambayo ni mengi bila ya kuwa na vitendea kazi, hatuwezi tukapata *quality education* (hatuwezi tukapata elimu ambayo ni bora). Tunapokuja kupima vigezo vya elimu inatolewa ambayo ni bora, sasa vitabu nenda shuleni ni janga, nenda kaangalie miundombinu kama madawani, watoto wanakaa chini ni majanga.

Mtuambie, mna mpango gani kama Serikali wa kuhakikisha changamoto ambazo zinajitokeza hivi sasa zinakwisha...

MWNEYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Profesa Kahigi, ajiandae Mheshimiwa Mwaiposa.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Kwanza, nianze kuzipongeza Kamati zote Mbili; Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa Taarifa nzuri. Kamati hizi zote zinahusika na maeneo ambayo yanamgusa kila mwananchi hapa Tanzania.

Kamati ya Huduma za Jamii, inahusika na elimu, inahusika na afya, inahusika na ustawi wa jamii. Kamati ya Maendeleo, inahusika na maendeleo kwa ujumla, inahusika na masuala ya akinamama, masuala ya kazi, masuala ya ajira, na hayo yote yanamhusu kila mwananchi. Kati ya haya yote, elimu na afya ni mambo ya msingi zaidi. Bila elimu hakuna maendeleo na bila afya hakuna haya yote ambayo yanawezekana. Lakini kwa babati mbaya bajeti ambazo zinatengwa kwa ajil ya elimu na afya, za chini sana. Na hata kile ambacho kinatengwa, lile tengeo, siyo lote linalofika kunakohusika. Naomba suala hili Serikali ilianganalie.

Zamani kulikuwa na programu nzuri sana za afya, za Mtu ni Afya, na nyinginezo, siku hizi hazipo. Naomba Serikali ianganalie bajeti ya afya na bajeti ya elimu. Nchi zote ambazo

5 FEBRUARI, 2015

zimeendelea, viashiria vya maendeleo viko katika maeneo haya mawili, elimu na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kwa kuchangia katika maeneo machache. Nakubaliana na karibu yote ambayo yamesemwa katika Kamati ya Huduma za Jamii, kwa sababu mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati hiyo na nakubaliana na karibu yote yaliyosemwa katika taarifa ya Maendeleo ya Jamii, kwa sababu pia yanahusiana na maeneo ambayo mimi ni mdau, maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwanza katika suala la vyombo vya msingi katika utoaji wa elimu, jambo ambalo limeongelewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, leo asubuhi. Vyombo hivi ni Baraza la Mitihani, Taasisi ya Elimu na Ukaguzi wa Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wazo mwanzoni lililoanza Wizarani kwamba vyombo hivi viwe chini ya Kamishina Mkuu. Wazo hili lilianzaanza halafu badaye tukalisikiasikia kwenye Kamati, tukawa tunashanga sana tunajiliza, iweje vyombo hivi ambavyo viko katika kila nchi na ni huru, vianze kuingiliwa uhuru wake, hii elimu kweli itakuwa salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuepoke suala hili. Vyombo hivi viendeleo kuwa huru. Tukianza kuviingilia, siasa zitaanza kuingilia, ndio yale yale ambayo yalikuwa yanasemwa asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuchangia katika suala zima la elimu ya juu. Elimu ya juu kabla haijaunganishwa na hizi elimu zote katika Wizara moja, ilikuwa inajitegemea pamoja na sayansi na teknolojia. Wakati ule mimi nikiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nilikuwa naona kweli usimamizi wa elimu ya juu ulikuwa ni mzuri. Sasa hivi kwa hakika usimamizi wa elimu ya juu umeteteroka. *(Makofi)*

Leo asubuhi tumesikia mifano kwamba, kuna matatizo *IMTU*, wanafunzi wamekaa nje ya chuo mwaka

5 FEBRUARI, 2015

mzima, mmesikia kwamba kwenye Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph huko Arusha kuna matatizo na mmesikia suala lingine ambalo amelieleza Mheshimiwa Susan Lyimo kuhusu matatizo ambayo yako kwenye elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafahamu matatizo mengi sana katika elimu ya juu. Tatizo mojawapo ni upungufu wa wahadhiri. Ninyi mnazungumza hapa kuhusu upungufu wa walimu kwenye shule za msingi na shule za sekondari, lakini kwenye vyuo vikuu kuna upungufu mkubwa sana wa wahadhiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya ubora wa elimu kwenye vyuo vikuu vimeshuka. Kuna tatizo zima la mafunzo ya umahiri na uzamivu kwenye vyuo vikuu. Vyuo vikuu vingi sana vimeruhusiwa kuanzishwa bila kuwa na uhakikisho kwamba wangeweza kutoa elimu ya shahada ya mwanzo, halafu shahada ya umahiri na shahada ya uzamivu.

Sasa hivi viko vyuo vikuu viachache tu, navyo ni vya Serikali na vingine vichache vya mashirika ya dini ambavyo vinaweza kutoa shahada ya umahiri. Lakini, vyuo vingine vyote, viko zaidi ya 40, vyuo vikuu vingine vyote kwa kweli viko hoi. Utakuta watu wenye shahada ya kwanza wanafundisha shahada ya kwanza. Hiyo kwa kweli hairuhusiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza, kwa hakika, kwa sababu tuko katika kipindi cha mpito, elimu ya juu isimamiwe vizuri ili hapo baadaye tuwe na elimu ya juu iliyo bora, kwa kweli ingefaa iwe katika Wizara inayojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuchangia kuhusiana na Tume ya Walimu. Nizungumze kwa ufupi kwamba, tunashukuru Serikali hili jambo imeliona na inalifanyia kazi. Kwa kweli, tunahitaji chombo ambacho kinajitegemea ambacho kinawahudumia walimu. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hicho kilikuwepo, lakini katika nchi hii kuna majabu sana yanayotokea. Katika awamu ya Kwanza, taasisi nzuri sana zilianzishwa na zikatengenezwa vizuri. Awamu ya pili vile vile, awamu ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kuna watu wachache wachache wakija tu, tena hasa katika Wizara hii ya Elimu ina tatizo moja, mtu anakuja na wazo lake la ajabu bila hata kulipitisha na likajadiliwa, anaanzisha tu. Sasa ndivyo ilivyotokea, kulikuwa kuna *Teachers Service Commission*, ikapoteapotea, ikaundwa katika Idara. Jambo la ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kenya wanayo inafanya kazi vizuri sana, na hakuna malalamiko kule Kenya. Tumefika kule. Hakuna malalamiko ambayo yamejaa. Hapa ni lukuki, kila siku kuna maswali hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba Serikali imeliona hilo na ilifanyie kazi haraka ili matatizo haya ya walimu ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu yaishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie kidogo kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia. Suala hili limegubikwa kwa muda mrefu katika kitu ambacho tunakiita utovu wa uelewa na upotoshaji. Kwa muda mrefu watu wamekuwa wakidhani kwamba Kiswahili hakiwezi kutumika kwenye ngazi za juu sana kufundishia. Hawajiulizi hii lugha ya Kiingereza ilikuwaje hapo mwanzoni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tumeisoma historia ya Kiingereza, tunajua kwamba lugha ya Kiingereza ilikuwa ni lugha ya mitaani tu. Ila Waingereza walijenga kwa uzalendo na kuifikisha hapo ilipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba angalau huku kwenye Bunge sasa hivi Miswada itakuwa inaletwa kwa Kiingereza na kwa Kiswahili. Hiyo ni hatua. Sasa tuendele hata huko kwingine, masomo yawe yanatolewa ama kwa Kiingereza ama au kwa Kiswahili, kwenye vyo viko. Na hiyo Sera...

5 FEBRUARI, 2015
(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji
kumalizika)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru!

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwaiposa, ajiandae Mheshimiwa Sara Msafiri.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi na mimi niungane na wenzangu kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati hizi kwa kutuletea taarifa ya utendaji nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda ulivyo mfupi mimi nitajikita zaidi kwenye Bohari Kuu ya Dawa, nitazungumzia Benki ya Wanawake, nitazungumzia *pension* ya wazee na kama nitapata nafasi nitaongea kuhusu sera mpya ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari Kuu ya Dawa ni chombo muhimu sana hapa nchini, ndicho kinachotegemewa kusambaza dawa nchi nzima. Lakini tumeshuhudia kwamba mwaka uliopita chombo hiki kilipata tatizo la upungufu wa dawa na sababu zake ukisoma kwenye kitabu ambacho kimeandaliwa na Kamati ni kutokana na deni kubwa la Serikali ambalo bado hawajalipa, deni la shilingi bilioni 93.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki ni muhimu sana kama nilivyosema. Katika hospitali nyingi na katika zahanati dawa zimekosekana kwa kipindi kirefu na tatizo kubwa linapatikana kwa wazee kwa sababu wazee hawapati dawa, watoto ambao wako chini ya umri wa miaka mitano hawapati dawa, lakini hata wananchi wenyewe hawapati dawa wanakwenda kupata matibabu na inawabidi wakanunue dawa kwa bei mbaya sana katika maduka ya dawa ya watu binafsi.

Naiomba sana Serikali na ninaomba sana Bunge hili liendelee kuisimamia Serikali na kuilazimisha kwamba ilipe deni hili ili wananchi waweze kupata dawa. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati na vituo vya afya vinavyoathirika ni ambavyo vipo pembezoni mwa Jiji kama zile ambazo zipo katika Jimbo la Ukonga, kuna zahanati moja ipo Kitunda, Msongola, Pugu, Gongo la Mboto, Singiziwa na mahali pengine na hasa ukizingatia kwamba sasa zahanati hizi na vituo vya afya viko mbali sana na Hospitali ya Rufaa. Kwa hiyo, dawa muhimu zinapokosekana katika maeneo ya wananchi kunakuwepo na tatizo kubwa sana la kuwasafirisha wagonjwa kutoka katika maeneo yao kwenda katika Hospitali za Rufaa.

Lakini yapo matatizo mengine nadhani ambayo Bohari Kuu ya Dawa yenyewe bado haijaweza kuyadibiti. Sijui Serikali inadhifiti namna gani usambazaji wa hizi dawa. Mimi nina hisia kubwa kwamba zipo dawa nyingi ambazo zinapotelea njiani au zipo dawa nyingi ambazo zinapelekwa hospitali lakini watendaji wa hospitali au zahanati wanaziua kwa maduka ya watu binafsi au katika hospitali za watu binafsi. Naomba sana Serikali iwe na mrejeshonyuma kufuatilia kwamba dawa zinazotoka Bohari Kuu basi zinakwenda moja kwa moja kufika kwenye hospitali husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Benki ya Wanawake. Kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu, Bibi Margareth Chacha kwani amekuwa muhimili mkubwa sana katika hii benki, ni benki ambayo imesaidia sana wanawake kwa kiwango kikubwa lakini hata vijana kwa kiwango kikubwa. Lakini unaposoma taarifa iliyowasilishwa na Kamati unakuta kwamba bado Serikali ina deni kubwa kwa benki hii. Iliyahidi kutoa shilingi bilioni mbili kila mwaka lakini mpaka sasa Serikali imetoa mwaka mmoja tu kikamilifu. Benki hii ilikuwa inatakiwa kuwa na shilingi bilioni 15 kama mtaji wa Benki lakini mpaka sasa kuna shilingi bilioni nane tu. Nawaomba sana Serikali ihakikishe kwamba inapeleka fedha hizi ili benki hii iweze kuendelea kupanuka na kuendelea kuwa na matawi yake nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia niseme Serikali iangalie utaratibu mzuri hata kama inawezekana zile 10% ambazo kila Manispaa inapaswa kutenga kwa pato la

5 FEBRUARI, 2015

Manispaa kwa mwaka kwa ajili ya wanawake na watoto basi fedha hizi zipelekwe kwenye Benki ya Wanawake na vijana ili waweze kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba kwanza fedha hizi Manispaa nyingi hazitengi, lakini nyingine zinatenga zinakwenda kwenye njia ambayo si halali na Manispaa nina uhakika hakuna watu wenye uzoefu wa mikopo. Kwa hiyo, mikopo hii ikipewa vikundi ni kwamba inaishia moja kwa moja, haizunguki kwa ajili ya kuja kusaidia vijana wengine maana yake hairudishwi.

Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba kuna sababu sasa ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakwenda kwenye Benki ya Wanawake ili waweze kukopeshwa wanawake na vijana kwenye Benki hiyo hiyo, nadhani benki itakuwa na uzoefu mkubwa wa kufuatilia mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushauri hilo naomba niende kwenye pensheni za wazee. Ni mara nyingi nimekuwa nasimama katika Bunge lako Tukufu na nimezungumzia leo ni mara yangu ya tatu kama siyo ya nne kuzungumzia umuhimu wa wazee kupewa pensheni zao.

Mimi niseme tu kwamba wazee ni kundi muhimu sana katika nchi hii, ndiyo walioifikisha nchi hii kiuchumi hapa tulipo, lakini ndiyo wanaoishi na wajukuu waliofiwa na wazazi wao aidha kwa UKIMWI au kwa magonjwa mengine. Lakini wazee hawa ni washauri wazuri sana katika familia na jamii na Taifa kwa ujumla, kwa hiyo kama tutawawezesha wazee kuna uwezekano mkubwa sana wa kupunguza watoto wanaorandaranda mitaani kwa sababu ya kukosa ulinzi, lakini ushauri na utunzaji kwa sababu wazazi wao wamefariki.

Kamati imeeleza kuwa Wizara sasa hivi imekwishakukamilisha rasimu ya mpango wa pensheni kwa wazee tangu mwaka 2013. Naomba sasa hiyo rasimu ije Bungeni ili tuweze kuitungia sheria ili mara moja wazee

5 FEBRUARI, 2015

waweze kupewa pensheni zao ili Taifa hili liweze kuondokana na malalamiko na laana za wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wanapokuwa wanalalamika siyo jambo zuri kwa Taifa kama Tanzania. Nawaomba sana tuondoe malalamiko na manung'uniko ya wazee ili tuweze kupata baraka zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee sera mpya ya elimu ya mwaka 2014. Niipongeze Serikali kwamba imekuja na mkakati huu, lakini naomba sana sera hii sasa ianze kutumika. Hii sera ikianza kutumika itasaidia sana kupambana na changamoto nyingi za elimu ambazo zipo nchini. Sera imekamilika na inasubiri sasa kuzinduliwa kama waliyosema Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii kama itazinduliwa na kuanza kufanya kazi kama inavyosema kwamba itanza kuzinduliwa mwaka 2015/2016 itasaidia sana Serikali lakini itasaidia sana zoezi hilo kuendelea kutatua matatizo ya wananchi. Pia itasaidia kukuza elimu nchini baada ya walimu kuridhika na mpango wa maisha yao na malipo yao yote, lakini itasaidia kuondoa migogoro ya muda mrefu ya Serikali na walimu, itasaidia pia kujua na kufuatilia na kutatua kwa haraka sana matatizo ya walimu kwa sababu yanakua yanajulikana, lakini pia itarudisha hadhi ya walimu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu kupata haki zao ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwaiposa ahsante, kengele ya pili. Mheshimiwa Sara Msafiri, ajiandae Mheshimiwa Barwany.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Taarifa za Kamati mbili zilizowasilishwa Bungeni.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niongelee kuhusu madeni ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii ambayo inaidai Serikali. Haya madeni ni makubwa sana, tunaona kwamba Serikali inadauwa na Mashirika ya Hifadhi za Jamii jumla ya shilingi trilioni 1.8. Fedha hii ni nyingi sana na hizi fedha ni fedha za wafanyakazi yaani watumishi ambao wanakatwa fedha zao ili muda utakapofika wa kustaafu waweze kupata akiba ya uzeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye Shirika la NSSF linaidai Serikali jumla ya shilingi bilioni 811 na Serikali walishaingia makubaliano kwamba itakapofika tarehe 14 Novemba, 2014 wawe wameshalipa shilingi bilioni 301; lakini cha kusikitisha mpaka sasa Serikali haijalipa fedha hizo. Tunajua kwamba haya mashirika yanafanya uwekezaji kwa sababu kile kidogo anachochangia mtumishi leo, thamani ya pesa atakapofikia umri wa kustaafu itabadilika kwa hiyo lazima wafanye uwekezaji ili muda utakapofika wa kustaafu mtumishi wa umma aweze kulipwa mafao yake kulingana na thamani ya pesa ya kipindi husika. Kwa hiyo, kama Serikali itayakopa mashirika sasa na itashindwa kutekeleza makubaliano ya kurejesha hizo fedha moja kwa moja tunaona kwamba watumishi wataathirika siku watakapofikia umri wa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni kama leo tunavyoongelea tunatafuta bima kwa ajili ya wazee. Kimsingi ni kwamba kulikuwa hakuna mifumo kipindi hicho wazee wakiwa watumishi na ndiyo maana leo sasa wamestaafu wanapata shida na Serikali inatafuta namna yoyote ya kuangalia namna ya kuwa-*accommodate*. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba mikataba yote wanayoingia na Mashirika ya Hifadhi za Jamii wawe wanatekeleza ili haya mashirika yaweze kufanya uwekezaji.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa NSSF Dkt. Ramadhani Dau, kwani amejitahidi sana kufanya uwekezaji mkubwa sana kupitia taasisi yake na kuna miradi mikubwa mingi tu, kwa mfano kuna mradi wa kujenga Hospitali ya Apollo - Kigamboni, tunajua kwamba

5 FEBRUARI, 2015

Serikali inatumia fedha nyingi sana kwenda kuwatibia wagonjwa India. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hospitali hii ikijengwa kwanza itasaidia Watanzania ambao hawana uwezo wa kwenda kutibiwa India watatibiwa hapa hapa, lakini vilevile Serikali itaweza ku-save fedha kwa sababu ni gharama kubwa inatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa vile watumishi wengi ni vijana kwa hiyo tusipowatengenezea mazingira mazuri ya kustaafu sasa hivi kupitia pesa yao kidogo wanayochanga kama akiba ya uzeeni tutazalisha bomu lingine huko mbele, sasa hivi tuna bomu la ajira kwa vijana. Kwa hiyo, haya mashirika yanahitahidi sana kuhakikisha kwamba hata zile sekta binafsi ziweze kuingia kwenye mashirika ya NSSF na mengineyo ya huduma za jamii. Kwa hiyo, tusipotengeneza mfumo mzuri wa kurejesha hizi fedha kama Serikali na kuyawezesha mashirika ya huduma za kijamii ziweze kuwekeza huko mbele tutakapokwenda kutakuwa na mtafaruku mkubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa itafute njia yoyote ile kuhakikisha inarejesha shilingi triloni 1.8 ambayo imekopa kutoka kwenye taasisi hizi za huduma ya mifuko ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena niongelee mfuko wa vijana na mfuko wa wanawake. Huu mfuko wa vijana na wanawake umeongelewa kwenye Kamati nyingi. Kamati ya Serikali za Mitaa imeongelea hii mifuko na Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio la Bunge la mwaka 1993 ndiyo lilipitisha hii mifuko iwepo, lakini sasa hivi ni miaka 22 imepita lakini utekelezaji wake unasuasua, Halmashauri hazitekelezi kutenga ile 5% ya vijana na 5% ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tu kutokana na taarifa ya Serikali za Mitaa tuliyoiona juzi makusanyo ya Halmashauri zote 140 Tanzania zilikusanya shilingi bilioni 270 na wangetenga 10% ambapo 5% ni vijana na 5% nyingine ni wanawake ina maana shilingi bilioni 27 zingewekezwa kwenye mifuko hii. Lakini cha kusikitisha ni kwamba ni shilingi

5 FEBRUARI, 2015

bilioni saba tu ndiyo ilitengwa na baadhi ya Halmashauri ambapo ni sawasawa na 7% tu. Kwa hiyo, unaona kwamba 83% ya Halmashauri hakuna utekelezaji wowote wa mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umefika sasa hivi Serikali ichukue hatua kwa sababu akina mama wengi wako huko vijijini, hizi huduma za kibenki tumeona taarifa ya jana iliyosomwa na Kamati ya Viwanda na Biashara ni 14% ya Watanzania ndiyo wanakopeshwa kwenye mabenki na hawa wako mijini, hawako vijijini na benki siyo rafiki kwa wakulima ambao ni Watanzania wengi ambao wanashiriki kwenye kilimo ni karibu 75%. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa ichukue juhudi za makusudi kwamba kila Halmashauri ihakikishe inatenga hizi fedha kwa ajili ya vijana na akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Benki ya Wanawake, nia ya kuanzisha benki ilikuwa nzuri na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishatoa agizo kwamba kila mwaka Benki ya Wanawake itengewe shilingi bilioni mbili, lakini cha kusikitisha kadri mwaka wa bejeti unavyokwenda kila mwaka pesa ya Benki ya Wanawake inashuka. Mwaka 2013 na 2014 Benki ya Wanawake badala ya kupewa shilingi bilioni mbili ilipewa shilingi milioni 450 tu, kwa kweli Serikali imetuangusha sana na imemuangusha Mkurugenzi ambaye ni mwanamke Mama Margareth Chacha, sisi kwa kweli imetuangusha na tunaiomba Serikali ifanye utaratibu wa kuhakikisha inakuza mtaji wa Benki hii kwa sababu hata sheria za Benki Kuu ya Tanzania ili benki iendelee inahitajika iwe na si chini ya shilingi bilioni 15; lakini benki yetu mpaka sasa ina shilingi bilioni saba tu. Kwa hiyo, hii benki itakufa na yale malengo yaliyowekwa ya kuwafikia wanawake vijijini na wilayani hayatawafikia na benki itabaki kuwa benki ya watu wa Dar es Salaam na benki ya watu wachache kwa sababu mtaji ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na kusisitiza tena kwamba Serikali ilipe madeni inayodaiwa na mashirika ya huduma za jamii. Ahsante sana. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Anafuata Mheshimiwa Barwany, ajiandae Mheshimiwa Msabaha.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuchangia Kamati zetu hizi mbili.

Kwanza nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa Wenyeviti kwa mawasilisho mazuri kabisa ya hoja muhimu ambazo tayari kama Bunge tulitaraji kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuungana na Mbunge mwenzangu Mama Al-Shaymaa kwa hoja ambazo ameziwasilisha katika Bunge letu hususani katika eneo la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumepiga kelele sana katika Bunge hili, tumewaeleza Watanzania kupitia hili Bunge na Serikali kwa jumla mahitaji gani muhimu ambayo tayari kama watu wenye ulemavu wanahitaji ndani ya Taifa lao. Lakini tuna mwaka wa nne sasa bado zimekuwa ngonjera tu kwetu, bado matarajio yetu kama watu wenye ulemavu hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baya zaidi ni kwamba sasa ndani ya Bunge watu wenye ulemavu tupo kadhaa ambao tunatoa hoja juu ya wenzetu waliokuwa nje lakini pamoja na yote haya bado Serikali hata sisi kutuonea aibu wenzenu kwamba imefika mahali sasa tuwasaidie wenzetu hawa katika hoja zao ili watu ambao wanawategemea katika kutoa hoja ndani ya Bunge hili basi waone kwamba tunawawakilisha wenzetu vizuri waliokuwa nje ya Bunge hili, lakini bado Serikali imekuwa kiziwi na pofu juu ya hoja zetu hizi kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia mengi hapa katika suala zima la uwajibikaji wa Serikali katika maeneo ya watu wenye ulemavu, lakini hili kitengo cha watu wenye ulemavu ambacho kipo katika Wizara ya Afya imezungumzwa pia kwamba ni eneo moja tu la afya ambalo

5 FEBRUARI, 2015

tayari linazungumziwa na kuhitajika lishughulikiwe. Lakini kuna maeneo mengi ambayo tunahitaji sasa watu wenye ulemavu washughulikie katika Wizara nyingine kama vile elimu, ajira na mambo mengine. Lakini kwa muda mrefu tumeitaka Serikali kitengo hiki cha watu wenye ulemavu kihamishwe sasa kutoka katika Wizara ya Afya kiende katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo tayari kutakuwa na Wizara kadhaa katika maeneo yale ili kila Wizara ichukue jukumu lake namna gani inaweza kusaidia kundi hili ambalo lina mahitaji makubwa kabisa ili kuweka uwiano wa kimaisha ndani ya Taifa moja yaani Taifa la Watanzania. Miaka 53 bado tukiendelea kuwa na matabaka ya watu wenye uwezo mzuri kiuchumi, kielimu na kiafya bado tutakuwa tunaendeleza tabaka letu na haina maana sasa kusema kwamba Taifa hili linajenga usawa, umoja na hali ambayo kila mtu analitegemea Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ukosekanaji wa dawa katika hospitali zetu. Ni kweli kuna madeni makubwa ambayo tayari Serikali inadaiwa na MSD, lakini siyo Mkutano huu tu wa Bunge, bali katika Mikutano mingine ya Bunge pia tumejaribu kuielezea hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna eneo moja ambalo tayari linazungumziwa. Tunaambiwa kwamba wagonjwa wanakwenda hospitali wanaambiwa dawa hakuna, lakini mzigo ambao tayari umetikwa katika hospitali zetu kwa mujibu wa sera ambazo zimetolewa kwamba makundi ambayo yanahitaji kupewa msamaha ndani ya hospitali zetu yanabeba idadi kubwa ya mahitaji ya dawa hizo katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukisema kwamba, mama mjamzito, watoto na wazee wote wanahitaji msaada katika hospitali hizo na unapopeleka fungu katika hospitali zile ili wananchi wasaidiwe, inaonekana dawa katika hospitali zetu hazipo kwa sababu mzigo wa msamaha unakuwa mkubwa katika hospitali hizo kiasi kikubwa inapelekea uwezo wa hospitali kuwa na dawa za kutosha ka jamii ya jumla unakuwa ni mdogo sana.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia zaidi ya asilimia 60 ya msamaha katika hospitali zetu ni makundi haya matatu; watoto, akina mama na wazee. Sasa tunaitaka Serikali iangalie ni namna gani msamaha huu unakwenda kufidiwa ili hospitali zetu sasa ziwe na uwezo wa kukidhi haja ya dawa katika hospitali zetu. Unaposema kwamba tayari dawa hakuna lakini ni katika mazingira gani? Msaada mkubwa umetolewa na dawa nyingi zimekwenda bila malipo na matokeo yake ni kwamba wananchi wengine wa kawaida wanakosa huduma ya dawa katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa Serikali ikafikiria upya kwamba msamaha huo mpya ambao unatolewa angalau uongezwe tena ili hili liwe kundi maalum ambalo litakuwa na fungu maalum kwa ajili ya misamaha na huduma nyingine ziweze kupatikana katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa hapa ni tatizo la ajira katika nchi yetu. Ni kweli ni tatizo kubwa, vijana ambao wamemaliza vyuo vikuu na shule sasa ni wengi, wanahitaji ajira ktika Taifa lao. Lakini kwa namna moja au nyingine kuna ajira katika maeneo mawili; sekta binafsi na sekta ya umma. Bado katika sekta binafsi Serikali haijaangalia kwa ukaribu zaidi kuona ni taratibu na kanuni gani zinatumika ili kuwafanya wafanyakazi hawa ambao wameajiriwa katika sekta binafsi wabaki salama. Kuna manyanyaso makubwa, ukiukwaji mkubwa wa taratibu za ajira katika maeneo mbalimbali kama kwenye migodi huko na maeneo mengine ya ajira binafsi kiasi cha hata mtu kujivunia kwamba hii sekta binafsi ni sehemu ya ajira katika nchi yetu bado watu wanaamini kwa asilimia ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kwamba wala hii ajira binafsi si rasmi katika Taifa hili. Tumeambiwa sasa hivi tumeishakwenda katika *private sector* kiasi kwamba, sasa tunahitaji ajira binafsi iweze kusimamiwa vizuri ili wananchi wetu waweze kufaidi matunda.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa juu ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kubwa zaidi hapa ni uingiliaji wa Serikali katika mifuko hii. Tunataka tujue sheria zikoje hapa? Imefikia mahali kwamba Serikali inaweza tu kukwapua kwapua katika mifuko hii kila mara, mara inadaiwa bilioni hizi huku, mara bilioni hizi huku, kila inapoonekana kuna fedha basi tayari Serikali imejiingiza katika ukwapuaji wa fedha hizo kiasi kwamba wananchi wetu wanakata tamaa na kujjuliza hivi tutakapostaafu tutapata fedha zetu sisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni kadhaa za fedha zinadaiwa kutoka Serikalini, hivyo ni lazima tuziangalie upya tena sheria zetu ili kubaini ni mamlaka gani ya Serikali ambayo yameiruhusu kwenda kuchukua fedha katika mifuko hiyo? Je, inachukua kwa mujibu wa sheria? Sisi tunachoamini ni dhamana tu ambayo Serikali imepewa kuisimamia mifuko ile na siyo kwenda kuchukua fedha. Mifuko hii bado si salama kabisa. Tunapoambiwa kwamba madeni ya Serikali kwenye mfuko wa NSSF ni mengi inatushitusha kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mradi wa Kigamboni, Serikali na NSSF walikubaliana waingie katika ubia na Serikali itoe zaidi ya asilimia 40, lakini mpaka leo bado Serikali hajitoe ile asilimia 40. Inaonekana kwamba kwa ujumla asilimia 100 yote itatolewa kupitia NSSF. Kama hivyo ndivyo basi Mkataba utenguliwe ili NSSF imiliki asilimia 100 ya mradi ule kuliko ambavyo iko sasa, tunaambiwa Serikali itachangia asilimia 40 lakini bado inaonekana hajifanya hivyo.

Mwisho ni pensheni ya wazee. Imezungumzwa hapa, suala la wazee nalo ni muhimu sana. Sisi tusingekuwa hapa kama wazee wasingekuwepo. Ahsante!

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msabaha.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nipate kuchangia Kamati hizi mbili; Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana mama yangu, Mheshimiwa Sofia Simba anavyofanya kazi katika Wizara isiyo na fedha kwa sababu Wizara hii imesahaulika. Mkumbuke Wizara hii ndiyo inayobeba jamii ambayo inatupigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, mimi nimekuwa na kipaumbele katika kutetea watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu, watoto hawa wamesahaulika. Mikoa mikubwa kama Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam na Arusha, watoto hawa wanaongezeka kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi ni kwamba watoto hawa wanatumika katika dawa za kulevya na hata usiku wanatumika kufanya uhalifu katika nyumba. Sasa kama Serikali ya CCM ni sikivu, ninaiomba itenge bajeti ya kutosha ili tunusuru watoto wetu hawa ambao ni Taifa la leo na wala si la kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wa dini. Kama nilivyouliza swali la nyongeza hapa Bungeni, viongozi wa dini wamekuwa msaada mkubwa sana kwa Serikali kwa kulea watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mengi, jamani mtakubali amekuwa mdau mkubwa kwa watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi. Wote ni walemavu watarajiwa, lakini Mzee huyu amekuwa akijitahidi sana kulishughulikia kundi lile na anajua mwenyewe anavyohangaika anapata *lotions* wanapaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tuangalie na niwaulize Wabunge wenzangu, hivi mlishakwenda hospitali ya *Ocean Road*?

Ninaomba mfike katika hospitali ile. Ninaomba kabisa Serikali kwa makusudi iingalie hospitali ile. Bhakhresa amejitolea anawalisha wagonjwa katika hospitali ile na pia wapo baadhi ya watu wanapeleka vifaa vya kuwahudumia wagonjwa wale, lakini navyo vimekuwa vinaporwa au kuchukuliwa.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mashine za mionzi pale, wale wanawake wanateseka jamani hasa wenye ulemavu wa ngozi. Ukienda kuwaangalia mwenyewe utasikitika na kama unakula nyama unaweza ukakaa mwaka mzima bila kula nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Serikali tunasema kweli ni sikivu, kwa nini haiwajali watu katika huduma ya afya? Kwa nini sisi kama viongozi tunakimbilia India kwenda kutibiwa? Hawa Watanzania wasio na uwezo wa kwenda kutibiwa India hospitali zetu tunaziboreshaje? Hospitali nyingi hazina dawa kwa ajili ya maradhi sugu ya moyo, saratani na Watanzania wengi ni maskini na hawawezi kwenda India. Tuhakikishe bajeti ya Wizara ya Afya inatengwa kukidhi afya ya Watanzania, siyo tunatenga bajeti ya kufurahishana huku, Wabunge tunakaa tunapitisha bajeti ambayo haifikii malengo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala hili la ajira, limekuwa kizungumkuti. Leo tunaambiwa kuna *panya road*, ninasema kama hawa vijana wa *panya road*, wangewezeshwa vizuri kwenye mikoa kama ya Ruvuma, Sumbawanga Mbeya na ile mingine ambayo inalima vizuri, wakawezeshwa kwa kupewa mikopo nafuu isiyo na riba, ingewasaidia. Lakini ukiangalia vijana hawa bado hawajawezeshwa na wote wanakimbilia Dar es Salaam wanakuwa wamachinga; wanauza vichupi na mwisho wa habari vile vichupi wanapokonywa au kuporwa na Jiji, na mtaji unakufa. Kwa nini mnawanyanyasa vijana hawa badala ya kuwatafutia ajira za kudumu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta hata vijana ambao ni wasanii, wana vipaji lakini Serikali ambayo imekuwa inasema ni sikivu, vipaji vya vijana hawa hamviendelezi. Utakuta vijana wamejiajiri wenyewe, lakini hamuwezi kuwaendeleza. Sasa unaona kuna *panya road*, sijui kuna nini, ninasema itakapofika 2015 vijana watawahukumu kwenye daftari la kupiga kura, na ndiyo maana mnakataa kuwaandikisha kwenye daftari la kupiga kura. (*Makofi*)

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam vijana wapewe kipaumbele na watengewe sehemu kabisa ambazo kama wana biashara zao ndogo ndogo wazifanye katika hali ya usalama na utulivu. Ukija kwa akina mama ntilie (mama lishe) Serikali itenge fungu la kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa tuna Benki ya Wanawake, hii Benki ya Wanawake ni kwa namna gani imenufaisha wanawake? Mimi ninaona wanawake wa pembezoni hawajanufaika na benki hii. Hata baadhi ya wanawake wa mijini nao hawajanufaika kwani wengi wanakopa kutoka *PRIDE* na mwishowe wanachukuliwa vitu vyao. Inafikia hatua sufuria za hawa mama ntilie (mama lishe) zinachukuliwa na kuuzwa. Tunasema kama kweli Mheshimiwa Rais ana dhati ya kusaidia Benki hii ya Wanawake, ahakikishe fedha hizi zinafika kwa walengwa siyo zinaishia kwa watu wachache au wa mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wanaokwenda kukopa *PRIDE* utashangaa mtu anakwambia nimeenda kukopa mkopo na hata sikopesheki. Baada ya muda yule mama anahangaika kwa kuuza chakula chake ili angalau apate fedha za kurejesha mkopo, basi lile lile sufuria lake linachukuliwa. Hivi hiyo ndiyo maana ya Serikali kusema ni sikivu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala lingine, suala la wanafunzi. Shule hizi za Serikali ni kweli wote tunajua tumesoma humu na pia hatutazidharau, lakini ni namna gani mnaziboresha shule hizi? Mkienda shule za pembezoni mnakuta watoto wanaandika kwenye mavumbi, majengo ni machakavu, miundombinu na mazingira ya walimu ni magumu. Walimu wanahangaika na kuuza vitumbua...

MBUNGE FULANI: Na ubuyu!

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa leo tuna Mawaziri saba na muda wao ni huu huu. Jana tulikubaliana tuwape muda mchache, lakini inaelekea majibu yenu Serikali ndiyo inayo. Kwa hiyo, msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Esther Matiko, dakika tano wewe na dakika tano Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa sababu tayari nilikuwa nimeshakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanza kuchangia hizo hoja mbili. Kwanza kabisa nielezee masikitiko yangu kwa majibu ya Waziri Mkuu leo asubuhi na ninaomba Wizara husika ilichukulie hili suala kwa umuhimu wake.

Kwanza kitendo cha Waziri Mkuu, kutuambia kwamba mtoto wa nyoka ni nyoka na kwamba wale watoto wote baba zao ni wana CCM, kwa maana wale watoto wote wa chipukizi au shule za msingi walioenda kwenye ule Mkutano wa CCM wazazi wao wote ni CCM, anatakiwa awaombe radhi Watanzania. Lakini pia mzazi anaweza kuwa CCM na siyo lazima mtoto awe CCM. Hii inaonesha umakini wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina *double standard*. Kama mnafuatilia ikitokea watu wanadai haki shuleni au katika vyuo vikuu na mfano mdogo tu ni wa UDOM mwezi jana, walikuwa wanadai haki ya kutopewa fedha zao ambazo ni kweli Hazina ilikuwa haijawalipa, lakini kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilihisi labda baadhi ya wanafunzi wale wako Upinzani, watoto walipigwa, wakavunjwa miguu na wengine wamefukuzwa hadi chuo. Baadaye ikaja kudhihirika kwamba ni ukweli Hazina au Serikali hii haijawalipa wale wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali wanawalazimisha wanafunzi wa sekondari za Songea, tena

5 FEBRUARI, 2015

kwa kuwaambia msipokuja mtapewa adhabu watumishi na walimu, halafu cha zaidi wakawadanganya kwamba watawalipa fedha. Wametuingia muwalipe fedha zao mlizowaahidi. Lakini mwisho msisahau kuna ule usemi unaosema; "kula CCM, kulala Upinzani (UKAWA)."

Kwa hiyo, ninyi endeleeni kuwadanganya kwamba mtawapa fedha mwisho wa siku uchaguzi mkuu utaeleza. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia deni la MSD la shilingi bilioni 93. Wakati wa Bajeti Mheshimiwa Cecilia alizungumzia sana hili na ni uhalisia kwamba Watanzania wengi wanakufa hospitalini kwa kutopata dawa, Watanzania wengi wanakufa huko vijijini hatuna dawa kwenye vituo vya afya na *dispensary* na miundombinu ni mibovu. Leo hii Serikali ya Chama cha Mapainduzi haioni umuhimu wa afya kwa kulipa deni la shilingi bilioni 93 wakati huo huo mkifuatilia hata hizi taarifa zetu za PAC na LAAC, kuna mianya mingi sana ya upotevu wa fedha. Mngeweza kudhibiti zile fedha mkalipa angalau hili deni la MSD mkawasaidia Watanzania, maana ukiumwa hautaenda kazini na uchumi unazidi kuzorota. Serikali mjaribu kudhibiti maeneo muhimu, fedha za nchi (makusanyo ya kodi yawepo), mboreshe miundombinu ya hospitalini na lipeni deni la dawa.

Mheshimiwa Spika, kuna *scandal* nyingine ya *Ocean Road*. Kuna fedha zilitolewa shilingi milioni 333 kwa ajili ya kununuliwa mashine mbili za ndugu zetu wanaokuwa na ugonjwa wa kansa. Sisi wanawake tunaathirika sana lakini na wenzetu wenye ulemavu wa ngozi. Ikaonekana kwamba hakuna sehemu ya kuhifadhi hizi mashine, wakabadili matumizi yake kwamba ni bora wajenge. Mkandarasi akapatikana ameishia kukwangua tu lile eneo, fedha hazionekani zimeenda wapi. Muone aibu! Mnaiba hadi fedha ambazo zinakwenda kutibu akina mama wanaouguu kansa na ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi. Waoneeni huruma Watanzania. Tunataka tupate majibu hizi shilingi milioni 333 zimekwenda wapi, mtupatie majibu yenye uhalisia. (Makofi)

5 FEBRUARI, 2015
Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Wewe za kwako ni dakika tano tu! Mheshimiwa Mbasa.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru walau kwa hizi dakika chache zilizobaki na ninaomba kuongelea suala zima la MSD.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MSD kimekuwa ni chombo ambacho kimekuwa kikifanya kazi bila ya kuwa na mpinzani. Pamoja na kuidai Serikali fedha nyingi sana lakini chombo hiki kimekuwa kikifanya kazi kwa uzembe mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati za Huduma za Jamii, tumekuwa tukitembelea pale MSD mara nyingi lakini utendaji kwa kweli unasuasua. Niunge mkono maazimio ya Kamati na Wajumbe wengi ambao wamechangia, leo hii kuwe na mbia wa MSD. MSD ishindanishwe na chombo kingine ili tuweze kupata ufanisi na ufaulu wa huduma zinazotolewa na MSD. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda Hospitali ya Mkomaindo na *challenge* tuliyoiona pale ni kwamba hawana chumba cha kutosha kwa ajili ya kutunzia dawa, lakini dawa zinapatikana kwa wingi, kwa sababu hawa watu wawili watakapofanya kazi pamoja kila mmoja anajitahidi soko lile alitendee haki na asiendeele kukosa pesa ile. Leo hii imefikia wakati muafaka sasa wananchi waweze kupata huduma bora, lakini wataipata pale MSD itakapokuwa imebadilisha *modalities* za utendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata tatizo kubwa sana katika ununuzi wa dawa. Leo hii dawa zinazoagizwa kutoka kituoni ili waweze kuzi-compile na MSD iweze kuagiza inahitaji muda wa kutosha. Tanzania yetu uwezo wa kutengeneza

5 FEBRUARI, 2015

dawa ni asilimia 20 tu na asilimia 80 tunategemea dawa kutoka nje. Lakini kadri ulimwengu unavyoendelea na teknolojia nayo inabadilika. Juzi tumeenda katika Taasisi ya Moyo pale Muhimbili tukakuta kuna hii mashine ambayo inahitaji vitendanishi na vitendanishi vile ndiyo vinavyotegemea aina ya mashine iweze kufanya kazi, lakini wakienda MSD hakuna na mpaka waagize viletwe hapa nchini tayari muda wake unakuwa umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe Serikali ianagalie uwezekano wa kuwa na mbinu mbadala kwa hizi vitendanishi vinavyohitajika haraka iweze kutoa mwanya ili hizi taasisi ziweze kuagiza moja kwa moja, hivyo vitendanishi vipatikane, mashine hizi zifanye kazi kwa uhakika na watu wetu wapate huduma iliyo bora. Ni kweli kabisa kuwa hospitali zetu zina uwezo wa kuhudumia Watanzania wenzetu, siyo kila mmoja ni lazima aende India au Afrika ya Kusini, lakini vitendanishi vikipatikana pale kazi hii itafanyika kwa uzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la makazi ya wazee. Tumekuwa tukitembelea makazi mbalimbali ya wazee na walemavu lakini hali inatisha sana. Wazee hawa wamekuwa wakitengewa bajeti kidogo na hata hiyo bajeti inayotengwa haiendi. Pale Sukamahela unakuta wazee wale wamekaa barabarani mchana kutwa, hawana cha kujifunika, jua linawapiga ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuombe makazi haya ya wazee yaangaliwe kwa ukaribu sana. Siyo kwamba hawa wazee kuzeeka imekuwa ni laana kwao, hapana? Siyo kwamba wazee kuzeeka basi wanatumikia adhabu ya yale waliyoyatenda huko nyuma. Tuombe Serikali iwaangalie kupitia Wizara husika na Wakurugenzi wasikae ofisini, tafadhali sana tembeeleni hawa wazee muone shida walizo nazo. Chakula hawana, maji hakuna na nyumba zenyewe zimekuwa za hovy hovy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayotengwa kwenda kukarabati zile nyumba haionekani imefanya kazi gani.

5 FEBRUARI, 2015

Inasikitisha kama Wazee hawa ambao ndiyo wamefanya Taifa hili kufika mahala hapa tunawaenzi katika mtindo huu hakika hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la uanzishwaji wa Maduka ya Dawa Baridi. Kumekuwa na kasi kubwa ya kuongezeka kwa haya maduka ya Dawa Baridi sehemu mbalimbali za viunga vya miji yetu. Lakini cha kushangaza unashindwa kuelewa haya maduka yanayofunguliwa je, wataalamu wanatosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti,....

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Rage.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa nasikitishwa na wachangiaji wengi wamekuwa wakilaumu juu ya hii Mifuko hawaoni jinsi Mifuko yetu inavyofanya kazi nzuri sana, kwa mfano hivi sasa Shirika la *NSSF* limeingia...

MWENYEKITI: Hii ni Taarifa au siyo ulisema ni Taarifa.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Ni Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama umefuatilia vyombo vya habari Shirika la *NSSF* limeingia mkataba na Real Madrid kujenga kitu kinaitwa *Football Academy* jambo ambalo litaoko na kubadili heshima ya nchi yetu, *NSSF* wametenga bilioni 16 lakini bado unakuta watu wananalalamika tu kwamba haya mashirika hayasaidii sijui wanataka wasaidiwe namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna mashindano ya *AFCON* yanaendelea huko timu za Kusini mwa Sahara hazishiriki...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Rage ninakushukuru kwa taarifa ahsante sana.

5 FEBRUARI, 2015

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunarudi Serikalini kwa majibu na tuna Mawaziri kama saba tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi dakika tano.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza nianze tu kwamba tu jamani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya vitu vingi sana siyo ya kuibeza na mwenye macho haambiwi tazama upande wa barabara, upande wa miundombinu mbalimbali, umeme na kadhalika jamani Watanzania wanaona na Watanzania wanawaona mnavyosema uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye chombo cha walimu. Walimu walikuwa na kero mbalimbali, walikuwa na kero kuhusu muundo wao wa utumishi. Ninapenda kukuarifu kwamba muundo wa utumishi wa walimu umehuishwa na umeanza rasmi kuanzia tarehe 1/7/2014. Kwa hiyo mwalimu akianza toka ngazi ya chini anaenda mpaka anafikia ngazi ya juu na hichi ndicho kilikuwa moja kati ya vilio vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha pili kilikuwa ni chombo kimoja cha walimu sasa hivi ninapenda kuliarifu Bunge lako kwamba chombo hiki tayari kimeshapita katika ngazi mbalimbali na Serikali imekubali na kitaanza rasmi tarehe 1/7/2015 na sasa hivi tuko kwenye bajeti na kukiunda chombo hiki kuangalia mahusiano na vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye madeni ya walimu, mwaka 2006 madeni ya walimu yalikuwa ni shilingi bilioni 166. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi madeni yanayohusiana na mishahara kwa mfano kuanzia Julai mpaka sasa hivi tumelipa shilingi bilioni 16 kwa walimu, madeni ambayo yamehakikiwa ni shilingi bilioni sita, madeni ambayo sasa hivi ambayo hatujayahakiki ni bilioni tatu jamani tumepiga hatua na sasa hivi kuanzia mwaka huu walimu watakuwa wanapata *promotion* kwa wakati.

5 FEBRUARI, 2015

Kwa hiyo, madeni haya tumeyahakiki pamoja na walimu wenyewe, uhakiki wetu ulikuwa ni shirikishi. Kwa hiyo hata mikutano walimu pamoja na Serikali mwaka uliopita tumefanya mikutano saba na tumehakiki madeni tukishirikiana na walimu wenyewe hilo wanalifahamu tuko pamoja nao, tunaelewana nao na kero zao tumezitatua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *incentives* zingine za wafanyakazi mbalimbali sasa hivi imeanzishwa *Utumishi Housing* yaani nyumba kwa ajili ya watumishi wote bila ya kubagua kwa hiyo hiyo *Utumishi Housing* tunajenga nyumba kwa bei nafuu ili tuweze kuwauzia walimu na watumishi wengine kwa bei nafuu na sasa hivi tumeshaanza Mikoa mbalimbali kwa mfano kwa Dar es Salaam wameshapata viwanja wanaanza kujenga, Morogoro na sehemu mbalimbali tutajenga nyumba ili kuwamotisha walimu pamoja na watumishi mbalimbali.

Kwa hiyo, madeni kwa ujumla ya wafanyakazi mpaka sasa hivi tunachodaiwa sisi Serikali yanayohusiana na mishahara ni shilingi bilioni tisa tu na ambayo yako kwenye *que* kwa watumishi wote ni shilingi bilioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya kazi kubwa na baada ya muda madeni yanayohusiana na watumishi yaani mishahara kwa kuwa yanaingizwa kwenye *system* moja kwa moja hakutakuwa na mrundikano wala malimbikizo tena ya madeni ya walimu. Sasa tunataka kufika *stage* baada ya kumaliza hii kazi tunataka kuangalia huo mfumo wetu wa taarifa za wafanyakazi kama utaweza kuingiza likizo za wafanyakazi wake ili iwe kama *first charge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tumewaagiza taasisi zote kwamba jamani likizo iwe ni *first charge*, *first charge* maana yake ni nini? Iwe kama tunavyolipa mishahara, tuiweke kipaumbele iwe *first charge* ili iwe inalipwa kwa wakati. Kwa hiyo, waajiri wote wanatakiwa kuiweka likizo ambazo zenye malimbikizo sana yaani OC waiweke kama *first charge* kama

5 FEBRUARI, 2015

ilivyo kwenye mishahara hilo tumeshatoa agizo kwa waajiri wote ili waweze kulichukua hili jambo kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe wito tu kwa Kamati zote, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tayari imeshakuja Utumishi kuangalia ule mfumo wetu wa *Human Capital Management Information System*. Mimi niwaombe tu Kamati zingine kama mna muda mje pale Utumishi ili tuwaonyeshe huo mfumo unavyofanya kazi na mtaona kwamba baada ya muda suala la malimbikizo ya mishahara utakuwa ni historia kwa sababu mtajionea ni jinsi gani tunavyoingiza kwa wakati na tunavyotekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya ajira na vibali; mimi niwaagize tu waajiri wote sasa hivi tunatengeneza bajeti ya *personal emolment* na sasa hivi bajeti hiyo inafanyika kwa njia ya *electronic*, iwapo hutaziweka nafasi hizi kwenye mfumo wetu haitawezekana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Seif dakika 10.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi nianze kwanza kupongeza Kamati zilizowasilisha na vilevile kutoa pongezi kwa Wajumbe wote walioshiriki kuchangia mawasilisho ya Kamati hizi, nitoe tu kwa muhtasari kwamba Wizara yangu itakamilisha majibu ya hoja zilizowasilishwa kwa maandishi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzipata kwa maandishi kwa sababu hoja zote hazitakuwa rahisi kuzizungumzia ndani ya dakika kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninataanza upesi kuzungumzia eneo la bajeti. Kusema kweli ni kwamba nchi zote hasa hizi za Kiafrika ambazo ziliridhia kutekeleza mpango wa *Abuja Declaration* kwamba bajeti za afya zifikie 15%, ni nchi chache sana ambazo zimefikia na hazifiki zaidi ya tatu na kusema kweli hizi zinaenda sambamba na uhalisia wa nchi zote hizi za Afrika ya kwamba bajeti zake zinategemea

5 FEBRUARI, 2015

sana vipaumbele vya changamoto walizokuwa nazo za kimaendeleo ambazo ni za kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtakumbuka eneo la maji ni muhimu, eneo la miundombinu ni muhimu, eneo la nishati ni muhimu, eneo la afya ni muhimu, eneo la elimu ni muhimu na kwa namna yoyote ile kufikia 15% siyo kitu chepesi katika bajeti kwa maana hiyo ni vyema turidhie hapa tulipo na tuiombe Serikali, na sisi wote kwa pamoja tuweze kuona umuhimu wa kuongeza uchangiaji na kutafuta njia mbadala za kuwezesha upatikanaji wa huduma zetu za afya.

Katika eneo hili tulichokifanya kwa uhalisia na kutambua kwamba kufikia 15% siyo rahisi tumetayarisha mpango mkakati wa kupata fedha kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za afya na katika eneo hili mojawapo ni bima ya afya, na nyingine ni bima ya afya ya jamii na vilevile kuongeza uwezo wetu wa matumizi ya rasilimali tunazozitumia katika utoaji wa huduma za afya, lakini vilevile na udhibiti wa mapato na hii kikukweli katika kuongeza udhibiti kwa kutumia mifumo sahihi mapato katika vituo vyetu yameongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano Hospitali ya Rufaa ya Mbeya kabla ya kuweka mifumo sahihi ilikuwa ikikusanya wastani wa shilingi milioni 60 kwa mwezi, lakini baada ya kuweka mifumo sahihi Hospitali ile ya Rufaa ya Mbeya sasa hivi inakusanya wastani wa shilingi milioni 500 mpaka milioni 600 kwa mwezi na kwa namna hiyo inadhihirisha kabisa kwamba kwa kuweka mifumo sahihi changamoto nyingi katika utoaji wa huduma za afya zinaweza zikadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumeshakamilisha mkakati wa kupata fedha au kuwa na njia mbadala za upatikanaji wa fedha ili kuweza kutoa huduma za afya nchi nzima na mkakati huo tumewasilisha na kesho utakuwa unawasilishwa kwa Kamati ya Huduma za Jamii ili waweze kutoa mapendekezo yao na baadaye kuweza kuendelea mbele ili iweze kukamilika.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upesiupesi juu ya deni la MSD na ni kweli kwamba Serikali inadaiwa na MSD, lakini MSD ni sehe u ya Serikali pia. Deni hili lipo katika hatua mbalimbali, cha kwanza kulikuwa na deni la bilioni 40 ambalo tulishalifanyia uhakiki na Serikali imeshalipa wastani wa shilingi bilioni 30.7. Na deni lingine lililobakia linafanyiwa uhakiki na uhakiki huu utakuwa umekamilika ndani ya wiki sita zinazofuata ili baada ya kukamilika kwake Serikali iweze kuanza tena kutenga fedha na kulilipa hili deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nielezee kidogo kuhusu deni. Cha kwanza kabisa ni kwamba 80% ya deni hili linatokana na ufadhili ambalo MSD inatumia fedha zake kugomboa vifaa pamoja na dawa zinazokuja kwa programu maalum kwa mfano kama mpango wa chanjo. Kwa hiyo, katika kugombia chanjo, kuzitunza na kuzisafirisha deni hili ndo limefanya iweze kutokea na siyo sababu ya ununuzi wa dawa ambazo zinaenda kwenye matumizi moja kwa moja kwenye vituo vyetu vya tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha msingi kuhusu deni hili ni kwamba Serikali itaendelea kuzifanyia uhakiki na baada ya pale kuweza kulipa kwa awamu na tutajitahidi kwa namna inavyowezekana tuweze kulilipa hili deni, lakini niweze kutoa angalizo katika eneo hili upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu vya tiba mpaka sasa hivi changamoto zilizopo zinazozungumzwa siyo za uhalisia. Kwa taarifa tulizokuwa nazo sisi kwenye maeneo mengi ya vituo vyetu hapa nchini bado wanazo dawa za kutosha hadi mwisho wa mwezi huu wa tatu na katika tafsiri hiyo inaonyesha utofauti kati ya maeneo ambayo kuna udhibiti na usimamizi wa matumizi ya dawa na maeneo ambayo hakuna udhibiti na usimamizi wa matumizi ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna Wilaya katika Mkoa wa Singida ambazo mpaka hivi sasa hawana lalamika lolote kuhusu tatizo la dawa, kwa mfano Iramba, Igunga, Tanga, Tabora wananchi wakiwa wanasimamia vituo vyao vya kutolea huduma, zile Kamati za vituo zinafanya kazi vizuri, dawa zinapofika pale wanazihakiki

5 FEBRUARI, 2015

kwamba zimetua na zimefika na wanazisimamia kuhakikisha zinatumika kituoni pale na tukiendelea kudhibiti wizi dawa zipo za kutosha na kuhakikisha kuwa huduma zetu zinaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda nizungumzie eneo la *Ocean Road*. Ni kweli kwamba katika kipindi cha nyuma tulikuwa na tatizo la mashine la tiba ya mionzi ambazo baadhi yake zilikuwa hazifanyi kazi. Lakini baada ya pale Serikali imeshughulikia tumepata fedha, tumeagiza vyombo vinavyotakiwa kutumika na kuweza kuvifunga katika mashine hizo na hivi leo ninafuraha kabisa kusema kwamba mashine zote nne katika kituo kile cha Saratani cha *Ocean Road* zinafanya kazi. *(Makofi)*

Lakini pia katika kufanya kazi kwake huko bado tutaendelea kufanya kila kinachowezekana ili tuweze kununua mashine za kisasa ambazo zitakuwa na uwezo wa kutibu maradhi haya kwa wagonjwa wengi zaidi. Ndugu zangu mashine hizi hazinunuliwi kwa milioni 300, milioni 500 au bilioni moja mashine hizi gharama yake inazidi bilioni nane kununua mashine moja, kwa hiyo kwa namna ambayo tumepata milioni 300 halafu zimetumika kwa kununulia mashine siyo kweli au kwamba hizo milioni 300 zilitlewa kwa ajili ya kununulia mashine siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nizungumzie kuhusu eneo la utoaji wa huduma hizi. Kimsingi na kwa ujumla wake Serikali yetu imejitahidi kwa kiwango kikubwa sana, tuna kituo cha kisasa kikubwa ambacho kimetumia fedha nyingi za Serikali katika kituo cha utoaji huduma za matibabu ya moyo na hivi sasa tuko katika hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba upatikaji wa vifaa vinavyohitajika kutumika wakati wa kutoa matibabu ya moyo viendeleo kupatikana katika kituo hicho na wataalam wetu waweze kuongeza uwezo na ujuzi wa kuweza kufanya upasuaji huu na kwa hakika katika kipindi fulani kitakachofuata tutakuwa na uwezo mkubwa wa kutibu magonjwa haya ya moyo na kuweza kuzuia watu ambao wanahitaji kwenda kutibiwa kule nje, badala ya kutumia gharama hizo kwenda nje gharama hizo

5 FEBRUARI, 2015

zinaweza zikapunguzwa kwa matibabu hayo kupatikana ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upesi upesi kuhusu Kitengo cha *MOI*. Katika kitengo hiki kwa kweli tumefanya kazi nzuri pale, ni wajibu wetu kuisifia Serikali kwa kiwango kikubwa ambacho tumefikia. Jengo kubwa la kisasa limejengwa lenye uwezo wa kuchukua vitanda 240 lenye uwezo wa kuwa na *theatre* nane, lina *oxygen plant* pale pale chini katika hilo jengo, ni jengo la kisasa kwa hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni tano kama zitakuwa zimepatikana zitaweza kununua angalau asilimia 50 ya vifaa ambavyo vinahitajika katika jengo hilo. Lakini bado hatua za Serikali zinaendelea na mazungumzo na Bima ya Afya ili fedha ziweze kupatikana kwa mkupuo wa mara moja ili vifaa hivyo viweze kupatikana kwa jengo hilo na huduma ziweze kutolewa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu eneo la Ustawi wa Jamii upesi upesi ili niweze ku-cover maeneo karibu yote ya msingi. Eneo la Ustawi wa Jamii ni kweli kwamba kumekuwa na mapendekezo ambayo yanahitaji eneo au idara hii ihamie Wizara...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kabaka.

WAZIRI KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Kwanza ninaomba niishukuru Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii kwa mawasilisho mazuri, pamoja na waliochangia hoja hii.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi hoja hii ime-cover Wizara yetu katika maeneo matatu makubwa. La kwanza lilikuwa suala la upatikanaji wa ajira, hasa zilizo katika sekta rasmi, lakini pia kulikuwa na suala la migogoro ya kazi pamoja na suala la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na hili suala la ajira. Kimsingi suala la ajira hasa iliyo rasmi kwa kweli ni matokeo ya uchumi. Kama uchumi ni mzuri, ajira zitapatikana na vijana wataajiriwa kwa wingi na kama uchumi ni hafifu ajira zitakuwa chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini ambacho tunakifanya katika Serikali yetu? Sisi tumetengeneza programu kubwa tu ambayo tulisema tutaajiri zaidi ya vijana 840,000 katika miaka hii mitatu na ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa miaka mitano wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu hii tuna *components* tatu, *component* ya kwanza ni kuwatambua vijana wetu walipo na vijana wako zaidi mikoani ingawa wengine wanakimbia kuja Dar es Salaam. Lakini *component* ya pili ni kutoa elimu ya ujasiriamali kwa hawa vijana kusudi wajue ni nini maana ya kufanya shughuli za kujiajiri wenyewe pamoja na kwamba wana elimu yao kwani wengine ni wale ambao wamemaliza vyo viko na *component* ya tatu ni kuwawezesha sasa kujiajiri kwa maana ya mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuona umuhimu kwamba, vijana hawa zaidi wako mikoani tarehe 12 Novemba, tuliwaita Wakuu wa Mikoa yote nchi nzima hapa Dodoma na wote walifika. Kongamano hilo lilifunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na tukawakabidhi programu hii kwa maana ya kuwatambua vijana katika maeneo yao kupitia Halmashauri na Wilaya zao, lakini pia kuwatengea maeneo ya kufanyia shughuli zao na hatimaye waweze kupata mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaji hii inaweza kutokana na *own sources* za Halmashauri, lakini kama nilivyosema sisi

5 FEBRUARI, 2015

Wizara katika programu hii tulikuwa tumeandaa programu ambayo tuliomba na kutengewa shilingi bilioni tatu na Serikali, bahati mbaya fedha hii hatujaipata lakini tumewakabidhi Wakuu wa Mikoa kwamba sasa watekeleze hili na tukawekeana na tukasainiana mkataba, watakuwa wanazalisha hizi ajira, wanatoa taarifa kwetu na sisi tunatoa taarifa kwamba tumezalisha ajira kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuongea zaidi kwa sababu muda ni mfupi, lakini pia lilijitokeza suala la ajira kwa walemavu ambalo aliongea kwa uchungu sana Mheshimiwa Al-Shaymaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba asilimia tatu ya waajiriwa wanatakiwa wawe waajiriwa wenye ulemavu. Suala hili katika sekta iliyo rasmi kwa maana ajira katika sekta ya umma hazina matatizo. Katika sekta binafsi inawezekana kuna matatizo kidogo, lakini labda nitoe taarifa tu kwamba kupitia Shirikisho la ATE, waajiri wameshapewa hii taarifa na nitoe taarifa tu kwamba hospitali yetu ya CCBRT ndiyo inayoongoza na imeshapata zawadi katika kuajiri watu wenye ulemavu kwa wingi na wamezidi kiasi cha asilimia tatu.

Lakini Shirika la Posta pia ni Kampuni au ni Idara ambayo inaaajiri watu wenye ulemavu kwa wingi na tunawapongeza sana, lakini tunawaomba waajiri wengine binafsi kwa kweli wafanye hii, kwa sababu sio ombi wanatakiwa waajiri zaidi ya asilimia tatu ya waajiriwa wao hao watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nassib alizungumzia akasema vibali vinavyotolewa, vinatolewa kiholela. Lakini Mheshimiwa Nassib ni Mjumbe wa Kamati yetu. Suala hili tumeshaliongea na tukasema ndiyo maana tunaleta Sheria mpya ya Vibali vya Kazi kwa sababu vibali hivyo vimekuwa na mamlaka tofauti. Hata hao wafanyakazi wa *Dangote*, taarifa niliitoa katika Kamati ambayo yeye ametaja hapa na kwamba kutokana na hiyo ndiyo maana

5 FEBRUARI, 2015

tunataka sasa tu *centralize* suala la utoaji wa vibali vya wageni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyojua Kamati yetu inajua kwamba sheria hii imeiva, ilikuwa iletwe Bungeni sasa hivi, lakini kutokana na ratiba haikuweza kuletwa, basi mwezi wa tatu ikiletwa naomba tuiptishe kusudi tuweze kupunguza wimbi la wafanyakazi wageni ambao wanaingia katika nchi yetu bila utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii limezungumzwa hapa. Kwa kweli mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ni Mifuko ya hifadhi ya jamii maana inasaidia sana maendeleo ya jamii na huduma za jamii, kwa maana ya eneo la afya, masuala ya utawala kwa mfano ndani katika hili jengo letu la Bunge, masuala ya elimu - UDOM, masuala ya kilimo kwa mfano *Kagera Sugar* na pia vikundi vya kilimo kama tunavyofahamu vya wakulima wadogo wadogo.

Lakini tunasema pia wanawekeza katika majengo na miundombinu, na hii yote ni kuboresha mafao ya wafanyakazi, kwa sababu mfumo uliopo katika hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni mfumo wa bima. Kwa hiyo, muajiriwa mfanyakazi anapojiunga na mfuko anaambiwa wewe utapewa kifurushi fulani. Mfuko ukipata hasara, yule mwajiriwa ama mwanachama atapewa kifurushi kile kile hatapungukiwa. Kwa hiyo, wanawekeza kusudi waweze kuongeza mafao kwa wanachama wao. Katika kanuni mpya ambazo zilizotolewa na *SSRA* mifuko hii yote kwa kweli imeongeza *pension* za watumishi wao, za wanachama wao, mfuko *NSSF* na wa *PPF* na tume-*harmonize* sasa mifuko yote inatoa *pension* ambayo ipo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumzia kuhusu migogoro ya wafanyakazi, ni kweli! Wamezungumzia suala la waliofukuzwa Bulyanhulu, tunao hapa wengine, lakini tunasema, sisi Wizara ya Kazi na Ajira kwanza tuna maeneo mawili. Kuna suala la kufukuzwa kwa sababu unaumwa ambalo halikubaliki, lakini kuna suala la kufukuzwa bila

5 FEBRUARI, 2015

taratibu. Kama umefukuzwa bila taratibu, mahala pako ni CMA na kama umefukuzwa kwa sababu ya kuugua, lazima uenda OSHA. Tunachowaomba wale waajiri ni kutoa barua kwamba huyu ninamuondoa kwa sababu hii na kama ni kwa sababu ya ugonjwa, lazima umtobie kwanza huyu muajiriwa kusudi kabla ya kumrudisha kazini ahakikishe kwamba ana afya ambayo inastahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hautoshi, lakini naomba nikubaliane na Kamati yangu kuhusiana na maoni yao ambayo kwa kweli wanataka Serikali tuongeze pesa katika bajeti, tutashukuru ikiwa hivyo, lakini tunajua sungura ni mdogo. Lakini tunatumaini kwamba hii fedha ya maendeleo bilioni tatu ambayo tumeitenga kwa ajili ya programu ya ajira ya vijana itapatikana kabla ya mwisho wa mwaka kuisha. Lakini pia umezungumzia suala la...

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sophia Simba.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie taarifa ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru sana kwa taarifa yao na kuwapongeza kwa kazi kubwa ambayo wanafanya katika kutushauri na kutuelekeza katika shughuli zetu na kutusimamia Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kutoa taarifa kidogo tu kuwafahamisha wananchi kuhusu yaliyojiri kwenye Mkutano uliopita wa Umoja wa Wakuu wa Nchi za Afrika huko Addis Ababa ambao Wakuu wa Nchi walitamka (*wali-declare*) kwamba mwaka huu 2015 ni mwaka wa uwezeshwaji na maendeleo ya wanawake, kuelekea kwenye ajenda ya Afrika ya miaka 2063,

5 FEBRUARI, 2015

ni ajenda ya miaka 50 ya kuhakikisha kwamba Afrika inabadilika, inakuwa Afrika ambayo tunaitaka iwe. Afrika moja, Afrika isiyokuwa na migogoro, lakini Afrika iliyokuwa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mazungumzo hayo, tumewekwa kuwa namba moja, tumepewa mwaka huu wanawake kwa sababu imeonekana kwamba wanawake na vijana ndiyo *drivers* wakubwa katika ajenda ile. Kwa hiyo, ni vyema mkilielewa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo napenda niwaarifu kabla sijasahau kwamba kila mwaka tunakuwa na maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi na tumekuwa kila mwaka, kila Mkoa unaadhimisha maadhimisho hayo kimkoa na kila baada ya miaka mitano tunaadhimisha Kitaifa. Kwa hiyo, mwaka huu maadhimisho ya siku ya mwanamke duniani yataadhimishwa Kitaifa katika Mkoa wa Morogoro tarehe 8 Machi na kauli mbiu itakuwa; "Uwezeshwaji wa Wanawake, Tekeleza Wakati ni Sasa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niwafahamishe hilo kwa sababu tayari tumeshapewa mwaka huu wa uwezeshwaji, lakini bado na kauli mbiu inasema, uwezeshaji na niseme tu, kila mtu hapa anazungumzia uwezeshaji. Uwezeshaji wa wanawake upo katika sehemu nyingi, maji yakifika kijijini ni uwezeshaji wa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepiga hatua, huduma za afya zimefika sehemu mbalimbali. Afya ya uzazi, matibabu kwa watoto na huduma ya afya kwa ujumla lile ni jambo la jinsia, anayeangaika ni mwanamke, huo ni uwezeshaji. Kwa hiyo, Taifa letu limefika mbali kwenye uwezeshwaji, kijamii, kisiasa wote tunajua tumefika wapi, tunangojea 50/50 na mipango tunajua inaenda vizuri, tunatengeneza utaratibu 50/50 itakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pia kwenye uchumi, sote tunajua Serikali imekuwa ikijitahidi kutuwezesha kiuchumi kina mama. Kwa hiyo, naomba zile hatua tulizofikia, tuziendeleze.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirudi nichangie taarifa ambayo imetolewa leo. Wengi wa Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kuhusu Benki ya Wanawake wanasema haijafika kila mahali, Mikoa yote! Naomba niwafahamishe kwamba ni kweli mtaji wa benki ni mdogo, lakini kwa vile mtaji wa benki ni mdogo, tumejitahidi kuanzisha vituo vya kutoa mikopo kwenye Mikoa mbalimbali. Mikoa kama ya Dar es Salaam ambako tuna matawi mawili, lakini tumefika Dodoma, Pwani, Ruvuma, Mbeya tuko Njombe na tuko Mwanza na tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni katika kujaribu kupeleka huduma karibu kwa wanawake. Ili kufungua Tawi la Benki tunahitaji milioni 300, tumeona ni pesa nyingi. Kwa hiyo, tumeamua kuanzisha vituo ambavyo tunahitaji kama milioni 40 mpaka 45 inakuwa inawezekana kwa sababu ya wafanyakazi na huduma nyingine kama kompyuta. Lakini kuna na *branch* (tawi), ingetupasa tutoa pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa pesa. Tuliahidiwa kwamba tutapata bilioni 10 kwa muda wa kipindi fulani cha miaka mitano mfululizo na mpaka sasa tumeshapata bilioni sita, si haba, na Serikali inaendelea kutoa pesa kwa benki hii.!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, sisi Wabunge tui-*support* hii benki, ni wangapi wana akaunti katika benki hii? Na wote tupo pale Dar es Salaam. Naomba mfungue akaunti moja inayoweza benki kuwa na uwezo ni kuwa na wateja wengi na sisi pia tunaweza kuwa ni wateja. Matokeo yake tumewaachia akina mama wajasiriamali wadogo wadogo ndiyo wamekuwa wateja wakubwa, hapana! Tupeleke na sisi pesa zetu ili hao wadogo wetu waweze kupata mikopo mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia inazungumzia katika uwezeshwaji, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ambao unaitwa WDF. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwa ukali sana kwamba ile *percent* tano haitoki. Ni kweli asilimia tano ambayo inatakiwa itolewe na Halmashauri

5 FEBRUARI, 2015

inamekuwa haitoki. Sasa basi sisi sote ni Wajumbe wa hizi Halmashauri, tuchukue hatua ili Halmashauri zetu ziweze kutenga pesa katika mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu ukatili ambao unaonyesha kwamba umekithiri katika jamii yetu. Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wizara ya Sheria, Wizara ya Elimu, wote tunafanya kazi moja ya kuhakikisha tunapambana na ukatili. Tuna mkakati ambao ni *multi sectrol* unashughulikia masuala ya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ambalo mnaliona sasa hivi, mtoto akibakwa, watu mtaani wanatoka wanapiga kelele, mwanamke amepigwa, mnaona jamii imebadilika ni kutokana na kazi kubwa inayofanya na Maafisa Maendeleo wa Jamii kuhamasisha jamii kukataa ukatili. Lakini sisi jamii wenyewe, malezi yetu tuanze toka watoto kuhakikisha tunakuwa na malezi mazuri, huu ukatili wote utaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna mauaji ya vikongwe, mauaji ya albino, yote haya yanafanywa ndani ya jamii zetu. Sisi jamii tunafanya nini? Serikali imetunga sheria kali sana ya *Sexual Offences Special Provisions Act, (SOSPA)*, imeweka mazingira mazuri sana kwamba unaenda polisi kuna desk (dawati) la kushughulikia masuala ya ukatili. Lakini kama huku kwenye jamii hatukubadiliki, hatubadilishi *mindset* zetu haya mambo itakuwa ni vigumu kuyamaliza. Kwa hiyo, nawasahi sana Waheshimiwa Wabunge tuendelee kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine limesemwa sana nalo ni kuhusu ajira kwa Maafisa Maendeleo wa Jamii.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulize kwa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja zilizo mezani.

5 FEBRUARI, 2015

Lakini pia niwape pongezi nyingi sana Kamati mbili zilizowasilisha pamoja na Wenyeviti waliowasilisha hoja hizo ambao wamewasilisha kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitajikita katika baadhi ya mapendekezo ya Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kuyatolea ufafanuzi na kuacha maeneo mengine ambayo tutayatolea majibu kwa maandishi. Nitazungumzia kuhusu sera mpya ya elimu, pia hoja au mapendekezo kuhusu utoaji wa mikopo wa wanafunzi wa elimu ya juu na suala la ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii mpya ya elimu, ni sera ambayo imekuja wakati muafaka, imepitishwa na Baraza la Mawaziri mwezi Juni mwaka 2014 na sera ambayo inapokea Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, sera ambayo imedumu na sisi kwa miaka 20 na mchakato wake wa sera hii mpya umechukua jumla ya miaka saba. Mchakato umeanza tangu mwaka 2008 na mpaka umefikia mwaka jana 2014 kuukamilisha.

Kwa hivyo, hii sera hii inapokea sera ambayo imedumu kwa miaka 20, tumetengeneza sera ambayo itadumu miaka mingine 20 ama hata 50 ikitutoa hapa tulipo kutupeleka katika eneo ambalo elimu kwa Mtanzania ni elimu bora, elimu ambayo inawaridhisha wananchi na wale ambao wamepata elimu katika nchi yetu. Hoja katika mapendekezo ya Kamati ilikuwa sera izinduliwe haraka, na mkakati wa utekelezaji wa sera uandaliwe mapema na vyombo muhimu vya elimu vilindwe na kamati imetaja vyombo vile kwa majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mchango wangu kwamba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa sera hii tutaizindua mapema, tena tumepanga tuizindue mwezi huu wa Februari kabla ya mwezi haujaisha, sera iwe imezinduliwa. Lakini sera hii tofauti na maandalizi ya sera wakati mwingine, na mkakati tayari tulishaanza kuuandaa. Kwa hivyo, sasa hivi tupo katika hatua za mwisho mwisho wa kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa sera hii.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeamua twende katika Mfumo wa Matukio Makubwa Sasa. Sera pamoja na mkakati wake wa utekelezaji viwe tayari mara moja, ili sera baada ya kupitishwa tu tusichukue muda mrefu wa kuweza kuanza kutekeleza yale ambayo yapo katika sera mpya ambayo tunaipenda sana. Kwa hivyo, haya ndiyo mambo ambayo tukayoyafanya, tutaizindua mwezi huu na tutaanza utekelezaji mapema iwezekanavyo.

Kuna suala hili la kulinda taasisi zile ambazo au vyombo vya elimu. Kamati imependekeza vilindwe. Mimi niseme kwamba katika sera hii mpya, baada ya kupata Sera Mpya ya Elimu kuna mabadiliko kadhaa ambayo yatajitokeza, kwa sababu sera hii imedumu miaka hiyo 20, mambo mengi yamebadilika. Sheria nyingi hazitoendana na sera mpya. Kwa mfano, Sheria ya Elimu yenyewe ni sheria ya mwaka 1978, tangu 1978 mpaka hivi sasa mwaka 2014 ni muda mrefu sana. Ni miaka 36, ni karibu unaenda miaka 40 ya sheria hiyo na mabadiliko yaliyotokea makubwa mno katika miaka hii 36, hamna namna ambavyo Sheria ile ya Elimu inaweza ikakidhi haja na mahitaji ya sera mpya.

Kwa hiyo, sheria mbalimbali zitafanyiwa mabadiliko, marekebisho, ikilazimika zinaweza zikafutwa na kutungwa zingine. Lakini watungaji sheria ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, si suala la mtu mwingine na waamuzi ni Bunge hili. Kama kubadilisha, atabadilisha Bunge hili, kama kufuta itafuta Bunge hili na sio mtu mwingine yeyote.

Kwa hivyo, hili suala tulifahamu kwamba halina mgogoro wowote au mgogoro mkubwa kwa maana ya utekelezaji wa sera yetu hii mpya. Najua kwamba lililopelekea Kamati kutaka kwamba vyombo hivi vilivyotajwa, Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani na Ukaguzi kwamba vilindwe na vihakikishwe kwamba vinabaki vikijitegemea, ni uvumi uliopita kwamba Sera Mpya inafuta vyombo hivi. Sasa Sera Mpya haiwezi ikafuta Baraza la Mitihani, hawa wanafunzi watafanya mitihani upi, wanafunzi katika ngazi mbalimbali, haiwezekani!

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tulilolipata ni kwamba kadri Serikali inavyoeleza lakini yale ya uvumi wa redio mbao ndiyo yanayopokelewa zaidi kuliko yale ya uhakika yanatokana na maelezo ya Serikali. Naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo haya ya Serikali kwamba vyombo hivi ni vyombo ambavyo vitaendelea kuwa vyombo vya elimu ambavyo vina mamlaka kamili na vitabaki kama vyombo ambavyo vinatoa huduma hiyo ambayo ni muhimu sana katika sekta yetu ya elimu. Kitakachofanyika ni kuhakikisha kuna ufanisi katika utendaji wao wa kazi. Kwa mfano, kwa upande wa mitihani, ni lazima Baraza la Mitihani liongee na Taasisi ya Elimu kwa sababu Taasisi ya Elimu ndiyo inayotunga mitaala na Baraza la Mitihani linatahini mitaala ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hawa wawili hawaongei hakuna namna ambayo mmoja anaweza akajua kwamba mwingine ametimiza kazi yake vizuri. Namna gani Taasisi ya Elimu inaweza ikajua kwamba Baraza la Mitihani limetahini kile ambacho Taasisi ya Elimu imekiandaa kama ndiyo mtaala unaotekelezwa katika shule zetu? Kwa hiyo, maboresho yatafanywa kupitia Sera mpya lakini siyo suala la kufuta au kuviondosha vyombo hivi au kuvi-downgrade au kuvifanya ni vyombo ambavyo havina hadhi ile ambayo ilikuwepo hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Ukaguzi. Mapendekezo ya Kamati ni kuwa ukaguzi uimarishwe na ufanywe Wakala. Nilihakikishie tu Bunge lako Tukufu kwamba tumeendelea kufanya hivyo kwa Idara ya Ukaguzi kwani ukaguzi ni uti wa mgongo kwa maendeleo mema ya elimu yetu. Bila ya ukaguzi itakuwa vigumu sana sisi kupata ubora katika elimu. Kwa hiyo, tumeendelea kuimarisha ukaguzi, mwaka huu wa fedha tunatarajia kuipa vitendea kazi zaidi na rasilimali za fedha. Kwa miaka hii ya karibuni kila wakati tumejitahidi, nalishukuru Bunge lako Tukufu limehakikisha linapitisha pesa ambazo ni pesa nyingi zaidi kwa ajili ya ukaguzi, mwaka huu wa fedha tutaboresha zaidi na tutaendelea kufanya hivyo ili ukaguzi

5 FEBRUARI, 2015

uimarike katika nchi yetu kama vile ambavyo Kamati inapendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iliridhia uundaji wa Wakala wa Ukaguzi. Tumeanza mchakato lakini mchakato huu sasa umesimamishwa kwa sababu Serikali imetoa Waraka maalam wa kusitisha michakato yote ya uundwaji Wakala katika nchi yetu ikiwemo Wakala ya Ukaguzi. Kwa hiyo, katika mchakato wa uundaji wa Wakala hapa tutasimama kwa maelekezo ya Serikali na kwa sababu ya changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika uendeshaji wa Wakala, hili limelazimika kwa sababu hiyo.

Hata hivyo, halitadhuru kwa maana ya uboreshaji wa ukaguzi na tumeanza kuona mafanikio hayo ya ukaguzi mzuri zaidi hata ukienda kwenye ofisi zetu ya ukaguzi sasa hivi unaiona ile hamasa zaidi na uelewa pia wa changamoto ambazo tunapambana nazo na kwa maana hiyo usimamizi wao unakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye suala la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kamati imependekeza kwamba tuimarisha mikopo kwa wenye uhitaji kwa maana ya kwamba wenye uhitaji zaidi ndiyo wapate mikopo na tuimarisha pia ukusanyaji wa mikopo na kuingia mikataba na wale wanaonufaika na mikopo ili waweze kutumikia Taifa kwa miaka fulani. Naomba kusema hapa kwamba hili tunalizingatia na Bodi ya Mikopo inazingatia kila wakati na ndiyo msingi wa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa masomo uliopita utoaji wa mikopo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara.

5 FEBRUARI, 2015

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa siku hii ya leo, nikushukuru pia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii niweze kujibu hoja na mapendekezo mbalimbali ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe kwa kuipa Wizara yangu ushirikiano wa karibu kwa namna ya kipekee kwa kufuatilia na kunisaidia katika changamoto mbalimbali zinazokabili Wizara yangu. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika sekta za Wizara yangu na kutoa michango ya namna ya kuboresha Wizara yangu katika kuhudumia wananchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika mapendekezo ya Kamati na hoja mbalimbali toka kwa wachangiaji mbalimbali. Kimsingi hoja mbalimbali kutoka kwa wachangiaji zimejikita katika sehemu nne ama tano kubwa. Kuna suala la Mfuko wa Vijana, kuna suala la jengo la *TBC* na kuna suala la *electronic ticket* na *TFF* kuhusu uwanja wetu wa Taifa, kuna suala la vazi la Taifa lakini pia kuna suala la *percent* tano au kumi ile inayotengwa kwa Halmashauri kama Vijana wetu wanaipata au nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze katika suala la Mfuko wa Vijana, wengi wamezungumza kwa kiasi kikubwa, mpo sahihi. Mimi niwaombe tu kwamba tusitumie muda mrefu sana kulalamikia masuala hasa ya Mfuko wa Vijana kwa sababu kimsingi Wizara inafanya kazi kwa bidii sana pamoja na kwamba pesa ambayo inapatikana siyo ile ambayo tunaiomba. Mwaka huu tumepata shilingi bilioni mbili lakini hata katika hizo pamoja na uhamasishaji mkubwa ambao tumeufanya kupitia Halmashauri mbalimbali, maombi yamekuja machache sana. Naweza kusema kwamba ni Halmashauri 30 tu katika Halmashauri zote zile ambazo tumezihamasisha nchi nzima ambazo zimeweza kuleta maombi Wizarani.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maombi 30 ambayo yameletwa kutoka Halmashauri 30 yana vikundi vya vijana zaidi ya 1,390. Vikundi hivi kama vikipewa pesa yake yote vinagharimu karibu shilingi bilioni kumi. Suala la msingi hapa ni kwamba pamoja na kwamba tunawaona wale vijana wanaotuzunguka kule na matatizo yao mbalimbali basi na sisi kama Wabunge tuchukue nafasi ya kuwahimiza wale vijana na kuwasimamia na kuhakikisha maombi yao yanafika ili kuweza kuutumia huu Mfuko. Katika hizo Halmashauri 30, kimsingi kama tunatoa pesa yote haifiki shilingi milioni kumi lakini bado tunahangaika kwamba hata wale ambao mnatakiwa kuwasimamia waweze kuleta hayo maombi bado hakijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, nawaomba pia Viongozi mbalimbali, tusaidiane na juhudi mbalimbali ambazo Wizara inazifanya. Tumezunguka Mikoa mingi kuhimiza Halmashauri mbalimbali, kwanza kutoa mafunzo lakini pia kuweza kuwaomba waweze kuwakusanya vijana lakini pia kuweza kubadilisha mitazamo yao iwe mitazamo chanya katika kuhakikisha wanajituma lakini pia wanajitolea na wanatambua kabisa kwamba suala la ajira moja kwa moja Serikalini haliwezi kuwepo isipokuwa linawategemea wao wenyewe kuweza kuchukua kero mbalimbali zile zinazowazunguka na kuzifanyia kazi. Hili ni muhimu kabisa sisi kama Viongozi tuhakikishe tunachukua hiyo nafasi ya kuhakikisha vijana wale ambao tunawaongoza, ambao tunawasemea kwa mara nyingine kwa jina kama vile ni bomu wasigeuke bomu, kwa sababu hilo bomu kama bomu tutakuwa tunalitengeneza sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hupenda kukumbusha wenzetu kila siku kwamba hawa vijana tunaowalalamikia kwamba hawana nidhamu au ni bomu, hawana ajira au nini, hawatoki Mars wanatoka katika jamii zetu, wanatoka katika sehemu zile ambazo tumesema tunaziongoza, basi tuhakikishe zile kero zinazotuzunguka pale vijana wasikae hivihivi bila kuhakikisha wanazishughulikia. Kwa kupitia Mfuko huu wa Vijana pesa zile kidogo ambazo tumepata tayari

5 FEBRUARI, 2015

tumeshazifanyia kazi na wale wote ambao wameleta maombi yao *process* bado inaendelea kuhakikisha kwamba wanapata pesa yao inayostahili. Kwa kumalizia nihimize tu kwa kusema kwamba ni vikundi kutoka Wilaya 30 na mnafahamu kwamba tuna Wilaya nyingi sana, kwa sababu siyo lazima pesa itoke katika huu Mfuko kuna ule kuna zile *percent* tano ambazo zinatakiwa zitoke katika Halmashauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *percent* tano za Halmashauri labda nizungumzie kidogo jitihada kubwa ambazo Wizara imejitahidi kufanya kuhakikisha Halmashauri mbalimbali zinapata mwamko wa kuanza kushughulikia masuala ya kutenga hiyo *percent* kumi, tano ya vijana na tano kwa wanawake. Kwa upande huu, Wizara ilianza kufuatilia kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI kwa kufikia Halmashauri mbalimbali na kukumbushana mpaka kiasi cha kufikia kipindi hiki kilichopita Mheshimiwa Rais aliweza kutoa Agizo Rasmi Oktoba 14, 2014 kwamba kila Halmashauri inatakiwa itoe taarifa ya kiasi kilichotengwa *five percent* kwa matumizi ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niliseme wazi hapa kwamba tumeanza kulifuatilia kama Wizara na kwa kiasi naweza nikaripoti kwa harakahara kwamba Halmashauri 38 tu katika Halmashauri 158 ndiyo zinatenga kiasi cha pesa kwa kiwango hicho cha *ten percent*. Hata hivyo, pamoja na kutenga kiasi hicho cha pesa hakitengwi kile kiasi hasa kinachohitajika cha *ten percent*. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kusema wote sisi ni viongozi basi tusimamie Halmashauri zetu mbalimbali tuhakikishe wanatekeleza hili kwa bidii zote. Kwa sababu hili likipatikana basi hata huo Mfuko wa Vijana ambao tumeutenga ambao unakosa pesa za kutosheleza mahitaji makubwa ambayo yanahitajika kwa vijana utakuwa kidogo una ahueni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojitokeza ni kuhusu *TBC* kupendelea CCM wakati wa kutoa huduma zake. Mimi napenda niseme tu kwamba hii si kweli labda kuna waliokuwa wanataka kufurahisha jamii lakini *TBC* inafanyakazi

5 FEBRUARI, 2015

kwa wananchi wote na jamii yote. Chama cha Mapinduzi kikitumia TBC kinalipa na safari hii sherehe zilizopita kililipa. Niseme pia kwamba hata NCCR wamekwishawahi kufanya mkutano wao na TBC ikaurusha live na walilipa. Ndiyo maana nasema basi tujenge hoja zenye tija ndani humu ili kuweza kujenga mtazamo na taswira nzuri katika jamii ya viongozi wetu ambao tupo humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inahusu lugha ya Kiswahili iheshimike na itumike katika ngazi za juu mpaka vyyo vikuu. Mimi nakubaliana kabisa na mchangiaji huyu. Niseme tu kwamba juhudi kubwa inaendelea sasa hivi, kama mnavyofahamu tunayo BAKITA lakini pia tunayo Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki ambayo inasimamia ukuzi wa Kiswahili na matumizi mbalimbali. Lengo kubwa la Wizara pamoja na jamii kwa ujumla na Serikali ni kuhakikisha tunakiangalia Kiswahili kwa ukaribu kama mnavyofahamu tumekiweka pia ndani ya Katiba lakini pia kuhakikisha kwamba Kiswahili kinaangaliwa kama kiwanda kikubwa cha kuweza kutoa ajira. Kwa hiyo, vitu kama hivi ni vizuri kuvichangia, namshukuru sana mchangiaji aliyetoa mchango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyokuja ni kuhusu maeneo ya viwanja vya michezo kuvamiwa na kubadilishwa matumizi. Ni kweli Serikali imeshatoa maelekezo kuhusu suala hili pia Kanuni za Mipango Miji zinasisitiza kuwa na maeneo ya wazi kwa ajili ya michezo na tutahakikisha kwamba Serikali inafuatilia....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii dakika thelathini.

5 FEBRUARI, 2015

MHE. MARGARET S. SITTA-MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii iliyoshughulikia masuala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ruhusa niwataje majina waliochangia, kwa kweli wamefanyakazi, kubwa bila wao tungekosa ya kusoma, naomba ruhusa yako na nitatumia muda mfupi sana.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Ritta Kabati; Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir; Mheshimiwa Kapteni John Komba; Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar; Mheshimiwa Felister Bura; Mheshimiwa Christowaja Mfinda; Mheshimiwa Sara Msafiri; Mheshimiwa Maryam Msabaha; Mheshimiwa Dkt. Gervas Mbassa; Mheshimiwa Joseph Machali; Mheshimiwa Profesa Kahigi; Mheshimiwa Susan Lyimo; Mheshimiwa Salum Barwany, Mheshimiwa Esther Matiko; Mheshimiwa Eugene Mwaiposa; Mheshimiwa Celina Kombani; Mheshimiwa Dokta Seif Rashid na Mheshimiwa Dokta Shukuru Kawambwa ambao amezungumzia kwa kirefu masuala yote yanayohusu shughuli ya siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wapo walioleta kwa maandishi, Mheshimiwa Rebecca Mgondo; Mheshimiwa Diana Chilolo; Mheshimiwa Namelok Sokoine na Mheshimiwa Jitu Soni. Naomba radhi kama kuna yeyote nimemuacha anaweza kuniletea kikaratasi nikamtaja baadaye kwa sababu mmefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Wabunge wote waliochangia kimaandishi na kwa kuongea kwa sababu michango yao imetusaidia sana katika kukamilisha taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo napenda niliweke wazi ni kwamba kwa kweli Serikali imejitahidi kufanya

5 FEBRUARI, 2015

mambo mengi, hiyo tusikatae. Kwa upande wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imefanya juhudi nyingi sana ya kuboresha utoaji wa huduma nchini na hata Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pia imefanya kazi kubwa sana. Lengo la Kamati ni kutoa yale ambayo tunaona yakifanyiwa kazi yataboresha zaidi kazi nzuri ambayo tayari imeshaanza kufanywa na Serikali. Kwa hiyo, tunapongea hapa lengo letu ni kuboresha kile ambacho tayari kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanzia na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuhitimisha taarifa yetu ya Kamati ya Huduma za Jamii. Kwanza tuanzie na suala la MSD. Suala la MSD amelizungumzia pia Dkt. Seif namshukuru lakini Kamati bado inaona kwamba deni la MSD limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka, ndiyo tunajiuliza, nakumbuka tulipoanzia kufanya kazi sisi kama Kamati ya Huduma za Jamii, deni la MSD lilikuwa linakaribia shilingi bilioni 40 limeendelea kuwa shilingi bilioni 76 na sasa hivi shilingi bilioni 93.3. Kwa hiyo, Kamati inaona hapana, hapa kuna tatizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaishauri Serikali kufanya ukaguzi wa deni hili kuona kitu gani kinachopandisha badala ya kupungua linaendelea tu, pamoja na Serikali kupunguza deni lakini bado linaendelea. Naishauri Serikali ichukue juhudi za makusudi kabisa kukagua hii hali ionekane kitu gani kinachopandisha deni hili mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ni kweli, mwaka 2011/2012, bajeti ilifika mpaka asilimia 12.1 ya bajeti katika jitihada ya Serikali kuongeza bajeti ya afya mpaka ifikie asilimia 15 ya bajeti nzima kama walivyokubaliana kwenye Azimio lao la Abuja mwaka 2011. Tunachokiomba sisi kwa upande wa Serikali baada ya kusikiliza kilio chetu sisi kama Kamati tuliomba sana Serikali kuingiza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika *Big Results Now* (Matokeo Makubwa Sasa) na kweli imeingizwa. Ni matumaini yetu sisi sasa kwamba bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itaongezwa.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata taarifa kwamba mwaka huu inaweza ikafika asilimia 10.5 lakini ikumbukwe kwamba ikifika asilimia 15 kama ilivyoahidi kwamba mwaka 2015 ingefikia asilimia 15 mambo mengi sana ya kutoa huduma yangeboreshwa. Kwa mfano, sisi tunaamini kwamba kama bajeti ya Serikali ingeongezwa na kufikia asilimia 15 kama walivyoahidi katika Umoja wa Nchi za Afrika, hospitali ya *Ocean Road* isingekuwa inapata matatizo kama iliyonayo sasa hivi. Kila tunapotembelea hospitali ya *Ocean Road* tunakuta mashine za mionzi hazifanyi kazi. Tumekwenda siku za karibuni katika kipindi tulipokuwa kwenye Kamati tumekuta mashine bado wanahangaika tu, mashine zimekuwa zikiharibika mara kwa mara. Kwa hiyo, tunaona kama bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ingeongezwa, mashine za *Ocean Road* zingekuwa zimefanya kazi kwa sababu zinahitajiwa na wagonjwa wengi sana kutoka nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwa upande wa *MOI*, Mheshimiwa Dkt. Seif amezungumzia kwamba amefanya jitihada kubwa ni kweli lakini bado hospitali ya *MOI* inayoshughulikia masuala ya mifupa na mishipa ya fahamu bado ina matatizo makubwa sana. Jengo ambalo kweli tunaipongeza Serikali limekamilika lakini bado linahitaji vifaa vingi ambavyo ni lazima viwekwe kwanza watapunguza msongamano lakini pia watatibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kipo Kitengo cha Moyo. Kamati inasisitiza kwamba Serikali ikifanye kitengo hiki kuwa taasisi inayojitegemea na kupewa mashine zinazohitajika pale ili wagonjwa ambao pengine wanasubiri na kupata matatizo kwa kuwa hawana uwezo wa kwenda nje au kupelekwa nje waweze kupata huduma katika kitengo hiki ambacho tunakiomba kiwe Taasisi ya Magonjwa ya Moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo pia Taasisi ya Figo ambayo inashughulikia maradhi ya figo na yenyewe ina uhaba mkubwa wa mashine. Mashine hazitoshi lakini pia ina Madaktari wawili tu. Kwa hiyo, tulikuwa tunaishauri Serikali

5 FEBRUARI, 2015

ihakikishe kwamba Madaktari wanapatikana kwa utaratibu wowote ule wenye ubingwa na mafunzo au utaalam unaohitajika ili hiki Kitengo cha Moyo kiweze kufanya kazi vizuri zaidi kwa sababu kitapunguza gharama ya kupeleka wagonjwa nje wakati sisi tuna vifaa vyote. Kama nilivyosema pia, Taasisi ya Figo inahitaji mashine zaidi kwa sababu zilizopo hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina upungufu mkubwa sana wa watumishi na hasa kwenye maeneo ya pembezoni. Sisi kama Kamati tulitembelea Ghana, tukapata bahati ya kujifunza. Wao wenzetu mwanafunzi ambaye amesaidiwa na Serikali kupata elimu ya Udaktari kwa mfano, anapomaliza Serikali inampa mkataba kwamba utakwenda kutumikia maeneo ya vijijini kwa kipindi hicho ambacho watakubaliana lakini pia wanakuwa wamepewa na posho maalum. Tumekuta wenzetu Ghana maeneo ya vijijini hayana matatizo kabisa kwa wasomi yaani Madaktari kwa sababu wanapewa mkataba lakini pia wanapewa na posho na ile posho maalum haiondolewi atakaporudishwa sehemu za mjini. Sisi tulikuwa tunafikiri ni wazo zuri ambalo Serikali nalo ingelichukua na kurekebisha kuendana na mazingira yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama nilivyotoa mfano wa Wilaya ya Urambo kwamba, wafanyakazi katika maeneo ya pembezoni hawatoshi. Nilichukua mfano wa zahanati 20 tulizonazo Wilayani Urambo lakini ni zahanati sita tu ambazo zina *Clinical Officers* na kila zahanati inatakiwa iwe na *Clinical Officer* mmoja ambaye ni Afisa Tabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado tunaishauri Serikali, ione jinsi ambavyo inaweza hata kuwafundisha vijana wenye taaluma inayohusika; kwa mfano vijana waliomaliza Kidato cha IV ambao ndiyo elimu inayotakiwa, watoke hukohuko vijijini ili wafundishwe na kupewa pengine motisha, kama tulivyopendekeza. Ni kweli kabisa Watendaji wa Wizara

5 FEBRUARI, 2015

ya Afya nao wanahitaji motisha hasa wanapokwenda kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la Idara ya Ustawi wa Jamii ambalo limezungumziwa kwa uchungu sana na Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir kuhusu Idara ya Ustawi wa Jamii ambayo imeshindwa kufanya kazi zake kikamilifu kutokana na kuwekwa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambako hata bajeti haitoshi. Matokeo yake ni kwamba, watu wenye mahitaji maalum hawapati huduma wanazostahili. Kwa hiyo, bado tunaiomba Serikali na kuishauri kwamba Idara ya Ustawi wa Jamii ihamishiwe Ofisi ya Waziri Mkuu ambako Ofisi ya Waziri Mkuu inaweza ikatoa maelekezo kwa Wizara mbalimbali kwa namna ambavyo inapaswa kuwahudumia watu wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ni vizuri nihamie upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Tukianza kwa upande wa Sera, mimi neno moja ambalo sikulifurahia ni kwamba, Kamati imefanyia kazi uvumi; siyo kweli! Kamati haikufanyia kazi uvumi, tumefanyia kazi taarifa tuliyonayo na tuliomba tupewe Sera ili tuthibitische au tuhakikishe hatukupewa! Kwa hiyo, Kamati bado inaoimba Serikali iione Sera hiyo pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hapa ningezungumzia kwa kifupi kwa nini sisi tunasema hivyo? Tumeangalia nchi jirani za wenzetu, Uganda, Kenya, Rwanda ambazo ziko kwenye Umoja wa Afrika, bado zina Mabaraza yao ya Mitihani. Sisi tulivyoona mwelekeo wa Sera ya Elimu ni kwamba hivi vyombo vikusanywe. Sisi tunaishauri Serikali, tafadhali sana, vyombo hivi viwe huru. Kama ni maboresho, kama alivyosema vimeanzishwa muda mrefu, yawe ni maboresho ambayo yatawezesha vyombo hivi kufanya kazi kwa uhuru zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba sheria ndiyo zitakuja kuamua; mimi nataka kusema itakuwa

5 FEBRUARI, 2015

tumeshachelewa. Sera ndiyo inayoelekeza mambo yatakayoingia kwenye sheria lakini tukikaa tungoje sheria, sheria inatafsiri kilichomo ndani ya Sera! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunasema kwamba Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo inashughulikia kutunga mitaala, haitungi mitaala tu Taasisi ya Elimu Tanzania, inatunga pia mihutasari, inatunga pia miongozo ya ufundishaji, lakini pia panapokuwa na mabadiliko katika mtaala au muhtasari au mabadiliko ya aina yoyote ndani ya ufundishaji wanatoa mafunzo pia, ndio wanaotunga vitabu hawa. Serikali imewaagiza kutunga vitabu vya kiada ili angalau shule zitoe elimu inayofananafanana pamoja na kwamba watachukua vitabu vya ziada lakini Taasisi ya Elimu imepewa jukumu la kutunga vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulikuwa tunafikiria kuanza kuikusanyakusanya ni kuipunguzia uhuru. Sisi tulikuwa tumependekeza kama Kamati kwamba ifanyiwe maboresho yatakayoweza kufanya kazi vizuri zaidi baada ya kufanya utafiti wa kina. Kwa hiyo, sisi bado tunaisihi Serikali, kuiachia Taasisi ya Elimu Tanzania iwe huru kama ilivyokuwa ila ifanyiwe maboresho ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa upande wa ukaguzi; asubuhi nilitoa takwimu hapa, sasa hivi shule za msingi ni zaidi ya 16,000, shule za sekondari ni zaidi ya 4,000, vyo vya ualimu ni zaidi ya 132 na vyote ni Serikali pamoja na binafsi. Bila kuimarisha ukaguzi siyo rahisi kuangalia viwango vinavyotolewa ndani ya taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali na mimi nilikuwa nafikiri pengine tutaongea sisi kama Kamati kuona jinsi ya kwenda kuwaona Serikali kwa undani zaidi ili hii neno lililozungumziwa kwamba tumesimamisha taasisi zote! Tuiombe Serikali iangalie ukaguzi kwa macho tofauti kwa sababu tunahitaji ukaguzi uliokamilika kutokana na wingi wa taasisi zilizopo sasa kwa sababu lazima kijulikane kinachoendelea ndani ya taasisi hizo kwa upande wa viwango vya elimu.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwa upande wa Walimu; kwa kweli, kama kuna siku ambayo Kamati imefurahi, tulikutana mchana, Kamati imefurahi sana kusikia Mheshimiwa Celina Kombani akisema mwanzo wa mwaka wa fedha huu mpya Tume ya Ajira kwa Walimu au *Teachers Service Commission* itaanza kazi. Kamati imefurahi sana kwa maneno hayo. Mheshimiwa Kombani pamoja na Serikali ya Awamu hii ya Nne mtakumbukwa kwa hilo kwa sababu chombo hiki kilikuwepo kikafutwa! Ndiyo maana tunaogopa, Baraza la Mitihani lipo na lenyewe lisije likafutwa kwa sababu, huwa vinakuwepo halafu vinapotea. Tunaishukuru Serikali kwamba mwanzoni mwa mwezi huu Walimu sasa watapata chombo chao. Kwa msingi huo, matatizo mengi yaliyokuwa yanawapata kutokana na kuhudumiwa na vyombo vingi yatatatuliwa na hatimaye kwisha kabisa. Kwa hiyo, nadhani kuanzia leo Walimu wote nchini wafanye kazi vizuri sana kutokana na Serikali yao kuwajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tulikuwa tunaomba kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa Walimu posho ya mazingira magumu. Kwa sababu kuna maeneo mengine hakuna maji, hakuna barabara kwa kweli, kuna umuhimu wa kuwapa posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mikopo kwa wanafunzi, hivi karibuni Serikali iliamua kuwapa mafunzo Walimu wa Sayansi na sisi Kamati tulifurahi. Jambo ambalo tulikuwa tunahoji Serikali hapa ni kwamba, huenda lilikuja bila kuwa na maandalizi ya kutosha. Ndiyo maana tunasema kwamba, hata vile kuchomekwa hawa Walimu ndani ya Bodi ya Mikopo, Serikali iangalie upya Sheria Mama ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuona jinsi gani haya mabadiliko yaliyofanyika yanaendana na lengo kuu la Bodi ya Mikopo. Sisi tunaamini asili hasa ya kuanzisha hii Bodi ya Mikopo pamoja na mengine ilikuwa ni kuwalenga wanafunzi wanaotoka katika familia zisizokuwa na uwezo. Kwa hiyo, sisi tulikuwa tunaomba kwamba, Sheria ya Bodi ya Mikopo iangaliwe upya kuona kama bado inakidhi kusudio lake la kuundwa.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali kwamba inapokuja na mabadiliko mapya, jambo la kwanza ni kuhusisha wadau halafu pili kuelimisha. Tumeona matatizo yaliyojitokeza hasa yalipotokea mambo ya kutoa alama na upangaji wa madaraja kwa Kidato cha IV ilileta matatizo makubwa sana. Jamii na wadau kwa ujumla walisema maneno mengi kwa sababu hawakushikirishwa pamoja na kupewa elimu ya kutosha. Kwa hiyo, tunaomba Serikali inapotaka kuleta mabadiliko makubwa, ishirikishe wadau, lakini pia itoe elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwa upande wa wanafunzi na hasa hawa watu wenye mahitaji maalum. Kwa kweli kwa upande wa elimu ndiyo kwenyewe hasa kwa sababu kuna masuala ya miundombinu. Bado tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba inapotoa usajili wa shule kuna miondombinu na mahitaji mengine ambayo yatawasaidia watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ugatujaji wa elimu, Kamati bado inaendelea kuiomba Serikali na kuishauri kwamba mafunzo ya ualimu yaendeleo kuwa chini ya Wizara ya Elimu ili kuwe na uwiano katika kutoa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika mafunzo kazini basi yawekewe utaratibu maalum au mpango maalum ambao utawezesha Walimu walioko kazini kupata mafunzo endelevu ili kuwasaidia waende na mabadiliko yanayotokea katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mafunzo ya KKK, sisi tunaipongeza Serikali. Hata hivyo, Serikali kwa kuja na mpango huu wa KKK yaani Kusoma, Kuandika na Kuhesabu lakini pia tunaomba kwamba kuwe na mpango maalum, ule mpango uliokuwapo zamani ufufuliwe na hata kama utakuja mwingine lakini ulenge kuwasaidia Walimu kupata zile *skills* yaani Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kumalizia kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni suala la mafunzo ya ufundi. Suala la mafunzo ya ufundi yanayotolewa na VETA tumeomba na bado tunaomba kuendelea kuishauri Serikali kwamba zile *skills development levy* zinazopelekwa kwa 2%, yaani ile kodi maalum inayoelekezwa kwa upande wa masomo ya ufundi kwa kupitia VETA iongezwe kutoka 2% hadi kufikia 4%. Hii itasaidia VETA kupanua zaidi mafunzo yake hasa kwa vijana ambao wanamaliza Kidato cha IV au Darasa la VII lakini wanashindwa kuendelea na elimu ya juu ili nao wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mengi ambayo tungeweza kuongea. Narudia tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo mmechangia kikamilifu katika kuishauri Serikali lakini naamini kwamba Serikali ni sikivu basi itachukua yale ambayo itaona kwamba yanafaa kwenda kufanyiwa kazi kama tulivyopendekeza ili hatimaye nchi yetu ipate elimu nzuri na bora iendane na wakati hasa huu wakati wa sayansi na teknolojia ili nchi yetu iweze kuendelea kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niwie radhi nimalizie la mwisho, kuhusu lugha ya kufundishia. Ni kweli Waheshimiwa Wabunge mmezungumzia katika michango yenu kwamba lugha za kufundishia ziimarishwe. Tunaingoja hiyo Sera ya Elimu tunaamini kwamba itafafanua zaidi kuhusu lugha zitakazotumika, lakini lugha zozote zitakazopendekezwa, kama ni Kiswahili na Kingereza, ziwekewe utaratibu maalum wa kuimarisha kwa sababu bila lugha hata upatikanaji wa taaluma au kuelewa kwa wanafunzi yale wanayofundishwa inakuwa vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana wewe na ninasema kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na nawashukuru sana Wabunge wote mliochangia. Ahsante sana. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Toa hoja

MHE. MARGARET S. SITTA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, umejibu kwa ufasaha, umejibu vizuri sana na hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa yote yaliyojitokeza na kutufafanulia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina ombi la kufanya nyongeza katika mapendekezo ya Kamati. Napendekeza pendekezo moja la ziada katika kitabu cha taarifa cha mwanzo kulikuwa na pendekezo namba 4.2.7, sasa mimi pendekezo langu nikasema 4.2.7(a) Kwa kutoharibu mtiririko lakini kwa taarifa ya sasa ina maana iko katika pendekezo la namba 7. Kama ni hivyo ili kutoharibu mtiririko pendekezo langu liwe 7(a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu linasema kwamba, kwa kuwa katika Tanzania wafanyakazi wengi wa Serikali wanahudumiwa na Mfuko wa Bima ya Afya lakini kutokana na zoezi la uhakiki linaloendelea sasa hivi, kwa kawaida zamani, mfano kama Mwalimu au Bwana Shamba au mtumishi yeyote wa Serikali akiwa na watoto wa ndugu zake ambao pengine wamefariki anaishi nao pale nyumbani alikuwa na fursa ya kuwaingiza ili mradi waweze kupata fursa ya kupata matibabu kwa sababu yeye wale ni *dependants* wake. Sasa kutokana na uhakiki unaoendelea sasa hivi

5 FEBRUARI, 2015

nimepata taarifa kutoka kwa wafanyakazi mbalimbali wa Serikali wakisema kwamba, wale watoto wa ndugu zao ambao wamekufa ambao walikuwa wanawahudumiwa sasa hivi hawaruhusiwi kuingizwa kama *dependants* wao isipokuwa ni mtoto wa damu au wazazi. Hii imeleta changamoto kubwa sana na sintofahamu kwa wafanyakazi wengi sana wa Serikali ambao sasa hivi wanahakiki data zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilileta mapandekezo yangu kwamba:-

"Kwa kuwa wafanyakazi wengi wanahudumiwa na Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa;

Na kwa kuwa taratibu na maelekezo yaliyotolewa katika kuboresha na kuhakiki taarifa za uanachama kuhusiana na wategemezi kwamba ni watoto wa damu na wazazi wa wanachama na kuwaondoa wategemezi wa wanachama wasio watoto wa kuwazaa au ndugu zao wa karibu kwa maana ya wadogo zao;

Kwa vile wanachama wa Mfuko wa NHIF ni wafanyakazi wanaoishi na wategemezi wengi ambao ni wadogo zao au watoto wa ndugu zao wanaowalea kutokana na mfumo wa maisha katika jamii zetu (extended family);

Bunge linapendekeza kwamba Mfuko wa NHIF usiwafunge au usiwazuie wanachama wa Mfuko wa NHIF kuwaingiza watoto wanaowalea au wanaowahudumia ili kuwanufaisha wanachama wanaochangia michango hiyo kila mwezi katika Mfuko wa NHIF".

Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta pendekezo hilo kwa mantiki kubwa kwamba wafanyakazi hawa ambao wengi mshahara wao ni mdogo na wanaishi na watoto wengine hasa ikizingatiwa tatizo la ugonjwa wa UKIMWI ni kubwa zaidi, kuna *dependants* wengi sana wanaishi na wafanyakazi. Sasa mfanyakazi huyu japokuwa hana watoto

5 FEBRUARI, 2015

aliowazaa lakini ana watoto wa ndugu zake ambao anawalea kwa nini wasiingie katika kunufaika na *NHIF* ambapo wao wenyewe kila mwezi wanachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo pendekezo langu na naomba Bunge hili iliunge mkono kwa sababu hiyo ni mantiki na ukiiangalia ni falsafa pana ya kuwasaidia Watanzania wanyonge, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo, hoja yako nimeiona lakini hili ni suala la kisheria, Waziri wa Afya!

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ina msingi lakini kiuhalisia ni kwamba imo kwa mujibu wa sharia na kinachotakiwa pale ni kwamba lazima uthibitisha kwamba kaya yako hiyo ni ile ambayo imo kwa mujibu wa tafsiri ya kaya. Kwa hiyo, wale watoto hata kama ikiwa ni *dependants* maana yake ni lazima uthibitisha kisheria kwamba hawa watoto kweli ni wale ambao unawahudumia wewe mwenyewe na unaishi nao na wanakula kutoka kwenye sahani au jiko moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinyume cha pale, tukiongeza idadi kwa kusema kwamba usajili, hiyo maana na dhana nzima ya kuwa na bima inapotea. Kwa sababu, msingi wa bima ni *risk sharing* na *risk sharing* maana yake inatoa *opportunity* ya mtu mmoja ambaye amekata bima, yeye matumizi yake kwenye bima hiyo yanakuwa kidogo na kumruhusu yule mwingine ambaye matumizi yake katika matumizi ya hiyo bima yanakuwa makubwa. Hiyo ndiyo tafsiri nzima ya bima na tukiifanya kwa sababu tu yeye amekata bima basi asajili hata mtu ambaye hahusiki na yeye na wala hayumo katika kaya yake, *then* hii itatupa tatizo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ameliweka vizuri lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo na yeye kwa kuonesha uhitaji wa jambo hilo.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, GN. No. 491 ya mwaka 2002 imetoa *definition* ya *dependants* kwenye sheria hiyo inayoongoza Mfuko wa Bima ya Afya. Sasa katika kufanya *definition* ya hao *dependants* ambao wanatakiwa wahudumiwe na Mfuko huo wa Bima ya Afya inaonekana liko tatizo moja ama lingine, aidha la kiutendaji ama la kutoa tafsiri halisi ama la namna wanachama wa Mfuko wanavyoweza kutoa orodha ya hao *dependants*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani Mheshimiwa Waziri kadiri alivyolisema na kuliweka vizuri, sasa hivi Mfuko wa Bima ya Afya na vyombo vingine wanaendelea na suala zima la kufanya *review* ya wanachama waliopo, hao *dependants* kama wapo ni kina nani na wakoje. Kwa hiyo, shughuli hizo zote sasa hivi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Jafo si kwamba Serikali haipendi hili pendekezo lake lakini anaweza kutusaidia kufanya marekebisho kidogo ya kuipa nafasi Serikali kwa sababu wameshaanza kufanya hiyo *review* na tunaona wote kwenye vyombo vya habari, wanapofanya hiyo *review* basi waingize na kipengele hiki kuona kwamba kinafanyiwaje kazi na hasa hii *definition* iweze kukaa vizuri na kuweza kutoa haki sawa kwa wanachama wote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo nafikiri Waziri amejieleza vizuri, uupate upenyo wa kuingia kwa sababu Serikali inalifanyia kazi, wewe tia msisitizo ili sasa kuwe na *win situation* kwako na Serikali na watu wote *of benefit* na Mfuko huu.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na niwashukuru sana Mawaziri wote wawili kwa kuliweka vizuri hili na kwa sababu mchakato huu unaendelea, basi mimi natoa fursa kwa Serikali iangalie kwa upana kwa sababu lengo ni kuwahudumia Watanzania. Ahsante Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ahsante. Haya Mheshimiwa Wenje.

5 FEBRUARI, 2015

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na angalizo kidogo katika hiyo hoja ya Kamati ya Huduma za Jamii kwenye ukurasa wa pili, sasa kama utaniruhusu niendeleo.

MWENYEKITI: Ukurasa?

MHE. EZEKIA D. WENJE: Wa pili.

MWENYEKITI: Unayo *amendment*?

MHE. EZEKIA D. WENJE: Unasema?

MWENYEKITI: Umeleta *amendment*?

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaleta *amendment*.

MWENYEKITI: Basi tafadhali kaa chini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Jafo amekubali, kwa hiyo, sina haja ya kuwahoji, hili ni suala la Serikali na mtoa hoja.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, *sorry*, Mheshimiwa Wenje amenichanganya kidogo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitalihoji Bunge kwamba sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii
pamoja na maoni na mapendekezo
yaliyofanywa kwenye Taarifa hiyo)*

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Mapendekezo yamepita, nawatakia kila la kheri Kamati na wote waliochangia. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti Kamati ya Maendeleo ya Jami, dakika thelathini. *(Makofi)*

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa dakika thelathini ili niweze kufanya majumuisho ya hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge walizichangia wakati wa mjadala wa mawasilisho ya taarifa ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianza kwa kutoa shukrani kubwa kabisa kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu, Mheshimiwa Kapt. John Damiano Mtokambali Chintete Mokomba, Mbunge wa Nyasa. Vilevile nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii kwa namna ambavyo wananipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo orodha fupi sana ya wachangiaji na napenda kuwatambua kwa majina yao. Waliopata fursa ya kuchangia hoja yangu ilikuwa ni pamoja na Mheshimiwa Ritta Kabati; Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Sara Msafiri; Mheshimiwa Felister Bura; Mheshimiwa Eugene Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Salum Barwany, Mbunge wa Lindi; Mheshimiwa Moses Machali; Mheshimiwa Nassib Omar Suleiman, Mbunge wa Mfenesini; Mheshimiwa Kapt. John Komba; Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo; Mheshimiwa Murtaza Mangungu; Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo; Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Profesa Kahigi na wa mwisho kabisa alikuwa ni Mbunge wa Chalinze, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwatambua wachangiaji, nitumie fursa hii pia kusema kwa kuwa Mawaziri

5 FEBRUARI, 2015

wanaohusika na sekta hizi hawajatoa majibu kwa kina kwa sababu ya muda, ningeshauri majibu yote ambayo yaliandaliwa yatolewe kwa maandishi kwa watoa hoja mbalimbali ili waweze kujua ni nini Serikali iliamua au ilipendekeza au ilishauri katika maeneo ambayo wao walichangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijazungumzia maoni ya jumla, nizungumzie maoni ya wachangiaji wachache. Kwanza, wachangiaji karibu wote hawa waliipongeza Kamati yangu kwa kazi na taarifa nzuri ambayo imewasilishwa mbele ya Bunge lako. Kwa hiyo na sisi kama Kamati tumepokea pongezi hizo, tunazikubali na tunastahili pongezi hizo kwa sababu kweli tumefanya kazi nzuri ya kupitia kazi hii ambayo tulikabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili, wazungumzaji au wachangiaji wote wamezungumzia kuhusu ufinyu wa bajeti na hili ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, bado tunaiomba Serikali hasa Wizara ya Fedha pale inapotenga fedha kwa ajili ya Wizara hizi ambazo nimezitaja hapa Wizara tatu tunazozisimamia kutoa fedha hizo kwa wakati ili Wizara hizi ziweze kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana unapoonza Wizara imetengewa shilingi bilioni 16 kwenye bajeti inapata shilingi bilioni 4. Maana yake majukumu mengi ya Wizara hayawezi kufanyika kwa wakati. Hata kutembea kwenye Mikoa Mawaziri wetu watahindwa kwa sababu hata uwezo wa mafuta kwenye magari yao itakuwa tabu. Kwa hiyo, utekelezaji wa majukumu yao utakuwa mgumu kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Felister Bura alikuja na hoja tatu, vazi la Taifa, Mheshimiwa Waziri amelitolea ufafanuzi sina ya kulielezea. Hata hivyo, mchakato wa vazi la Taifa ulianza muda mrefu toka Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi yuko pale hadi leo hatuelewi mustakabali wake. Kama Serikali ina njema na ina hakika kwamba jambo

5 FEBRUARI, 2015

hili ni jambo ambalo ni kipaumbele ni vema sasa tujue hatua gani zilizofikiwa katika kupata vazi hili la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Felister Bura na niwapongeze vijana ambao Mheshimiwa Felister Bura aliwataja walioamua kujijiri wenyewe. Naishauri Wizara ya Habari kupitia Mfuko ule wa Vijana kuangalia namna ambavyo inaweza kusaidia kikundi hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja kwa sababu naamini fedha za Mfuko wa Vijana zipo, bado maombi yanaendelea kupokelewa. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe maoni ya kikundi hiki ili nao waweze kuzingatwa kwa sababu wameonyesha mwelekeo mzuri wa kujijiri na kuweza kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwaiposa alikuwa na ushauri kwamba asilimia tano ambayo inatengwa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya maendeleo ya vijana na akina mama sasa ielekezwe kwenye Benki ya Wanawake ili benki iweze kupata mtaji mkubwa. Kamati yangu imeangalia jambo hili, mawazo ya Mheshimiwa Mbunge ni mazuri lakini kwenye muktadha wa jambo hili hayawezi kuwa endelevu. Bado tunashauri Serikali kutenga zile shilingi bilioni mbili kila kwa ajili ya benki hii na endapo ingefanya hivyo kwa muda wa miaka mitano kusingekuwa na haja tena ya kuendelea kuangalia maeneo mengine ili kuongeza fedha kwenye Benki hii ya Wanawake. Kwa hiyo, wito wetu ni kwamba Serikali iendelee kutoa kiasi kile cha fedha kufikia pale shilingi bilioni 15 ili benki hii ijiendeshe. Benki hii ni ya umma kwa sababu mtaji wake unatokana na Serikali. Ziko benki ndogo ndogo zinajiendesha vizuri, zina mitaji mikubwa iweje benki kubwa kama hii ya Serikali ishindwe kufikia lengo lake kwa kushindwa kupata shilingi bilioni 15? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jengo la *TBC*, wachangiaji wengi wamejaribu kuonyesha mfadhaiko wao kwa namna gani jengo lile ambalo lingetumika kama *Administrative Block* kwa muda wa miaka 20 sasa

5 FEBRUARI, 2015

halijakamilika. Serikali haijatoa majibu hapa na ninaamini kwa sababu ya ufinyu wa muda. Kwa hiyo, Kamati yangu inaendelea kuisitiza kwa Serikali tupate majibu ya kina yanayoridhisha na yanayoeleweka ni kwa nini sasa na ni lini sasa Serikali itaweza kumaliza jengo lile ili kuweza kulinda heshima ya nchi yetu na chombo hiki kikubwa ambacho tunakitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, Kamati yangu inaendelea kuishauri Wizara inayohusika na *TBC* kuanza kubuni vyanzo vipya vya mapato badala ya kuendelea kutegemea ruzuku ya Serikali ambayo kila siku tunapanga haiendi. Kwa hiyo, waweze kuangalia maeneo gani wanaweza kuwekeza, tumekwenda maeneo mbalimbali, Mwanza, Arusha, Morogoro, wanayo maeneo mengi, wanayo ardhi ya kutosha, wanayo majengo ya kutosha, wana miundombinu ya kutosha hata pale Mikocheni, wanao uwezo kabisa wa kuingia ubia na mashirika mbalimbali ili kuweza kuendeleza rasilimali zao na kuweza kupata fedha za kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti inashangaza, kama *ITV, Star TV, Clouds*, zinaweza kurusha matangazo yake kwa uhakika, ni vyombo vya watu binafsi iweje televisheni ya Serikali, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ambayo mimi nina imani nayo ishindwe kusaidia chombo hiki kuweza kutimiza wajibu wake? Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba imeweka fedha zake pale lakini pia *TBC* wenyewe kuandaa mazingira ya kuweza kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usikivu wa *TBC*. Jambo hili limejadiliwa na limeletwa kwa maandishi na Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa, Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mangungu na nitoe wito tu kwa *TBC* kwenda kule Lindi anakotoka Mwenyekiti ili kuweza kuangalia hali halisi ya usikivu wa *TBC FM*, maeneo ya Kilwa kule Kipatimo, Nanjilinji waweze kupata matangazo haya kwa ufasaha zaidi. Nampongeza

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mbunge Mangungu kwa umakini wake na kufuatilia jambo hili mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala zima la ushauri kutoka kwa Mbunge Jitu Soni, Mzee wa Kilimo Kwanza huyu. Yeye anashauri Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kujikita pia kuwekeza katika maeneo ambayo yatatoa fursa kubwa ya kuongeza wigo wa ajira kwa vijana. Mimi na Kamati yangu tunakubaliana kwamba badala ya kuwekeza kwenye majengo tu na miundombinu na madaja ambalo ni jambo jema, Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inapopata fursa iangalie maeneo mengine ambayo inaweza kupanua wigo wa ajira kwa vijana hasa maeneo yanayohusu kilimo, wawekeze kwenye kilimo, maeneo yanayohusu uvuvi, hilo litakuwa ni jambo bora na litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusu pensheni kwa wazee. Hii imekuwa ni kilio na changamoto kubwa kwa Kamati hii. Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge, *Iron Lady*, ameweza kufanya kazi kubwa sana kutetea hili. Leo analiacha jambo hili kwenye mikono ya Mwenyekiti likiwa salama na mimi naendelea kusiondwa kwamba bado wazee wa nchi hii, ninapozungumza wapo ndani ya ukumbi huu kama hawako wako nje ya ukumbi huu wakiwa wanafuatilia kutaka kujua kutoka Serikalini, ni lini sasa pensheni kwa wazee itaandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wana mambo makubwa matatu. La kwanza, huduma ya afya kwa wazee. Serikali inasema kwamba watapewa matibabu bure lakini madawati hayo ya kutoa matibabu bure kwenye hospitali zetu hayapo. Wazee wanasumbuka, vitambulisho vyao bado havitambuliwi kwenye maeneo yale, tunaiomba Serikali kuweka mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nataka niwakumbushe, uzee na kuzeeka havikwepeki. Kwa hiyo, leo mko vijana akina Mheshimiwa Silinde, hampigani

5 FEBRUARI, 2015

jambo hili kwa nguvu zenu zote kesho mtazeeka. Mtakuwa wazee na mtahitaji haya tunayoyasema, Serikali mtusikie kwa masikini sana. Serikali kama imeshindwa jambo hili iseme wazi ili tuachane nalo sasa. Maana imekuwa ni kilio cha muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana wenzetu wa *Health Age International*, wamefanya tafiti nyingi, wamekuwa msaada mkubwa katika kuhudumia wazee wa nchi yetu, tunawapongeza sana wenzetu hao. Hata wenzetu wa *TASAF* sasa hivi kupitia ule mpango wa kutoa ruzuku kwa kaya maskini unawafikia wazee. Kwa hiyo, tunaishuru Serikali pia kwa juhudi hizo lakini bado tunasema wazee hawa wana kilio chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wale ambao walifanya kazi wakastaafu pensheni zao ni ndogo sana. Mwingine anasema anapata shilingi 10,000 kwa mwezi, mwingine anapata shilingi 20,000 kwa mwezi. Kwa hiyo, Serikali tunaishauri twendeni kwenye *international standard* walau asilimia 10 ya mshahara aliyomalizia yule mzee ndiyo sasa itumike kama sehemu ya kumlipa pensheni yake kwa mwezi ataweza kuendesha maisha yake. Hii ni *international standard* siyo hapa tu, duniani kote sasa ni walau asilimia 10.

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, Kamati yetu inawasisitiza Watanzania wengi kujiunga kwenye mifumo ya uchangiaji kwa hiari kwenye Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii (*supplementary scheme*). Kwenye kila Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuna mfumo wa uchangiaji kwa hiari. Utakapomaliza umri wako, utaendelea kupata pensheni yako kwa sababu Waswahili wanasema fainali uzeeni. Kwa hiyo, ni lazima Watanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge tujipange kujiandaa na uzee kwa kuweka michango yetu kwenye Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kupitia *supplementary schemes* ambazo ziko kule. Hata wakulima, *NSSF* wana

5 FEBRUARI, 2015

mkulima *scheme*, wana mvuvi *scheme*, hata wavuvi wanaweza kuwekeza fedha zao na baadaye zikawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunawaomba wenzetu wa SSRA kupitia Serikali na Wizara husika kuendelea kutoa elimu kwa umma ili Watanzania walio wengi wajue nini maana ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii na namna ambavyo watahiriki kikamilifu katika eneo hili. Wenzetu Wachina endapo unatoa asilimia kadhaa kuwekeza fedha yako kwa hiari kwenye Mifuko hii, Serikali ya China huwa inatoa motisha kwa watu hao. Ukiweka Sh.10,000 Serikali inaongeza Sh.10,000 ili kuwapa motisha watu wengi kujiunga na Mifuko ya Hifadhi kwa hiari yao. Kwa hiyo, tunaomba sasa na tunatoa wito Kamati hii kwamba ikiwezekana Serikali ya nchi yetu ifikirie utaratibu huu kwa sababu utatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafanyakazi. Nimezungumza kwa kina kuhusu migogoro hasa maeneo ya makampuni ya ulinzi lakini kwenye migodi yetu na nilitoa mfano wa mgodi wa Bulyankulu kule Kahama. Kila mwaka tunapata ...

MWENYEKITI: Mwenyekiti samahani kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa matumizi ya Kanuni ya 153, naomba Bunge lako litengue Kanuni ya 28(4) ili Bunge hili liendeleo hadi shughuli zilizopangwa katika ratiba ya leo Zitakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Tunaendelea mpaka shughuli za Bunge zitakapokamilika. Mwenyekiti endelea.

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa naelezea kuhusu migogoro ya wafanyakazi hasa kwenye sekta ya migodi. Kamati yangu imekuwa inakutana na changamoto hii mara kwa mara na hata leo tunao wafanyakazi zaidi ya 55, wameachishwa kazi baada ya kubainika kwamba wana matatizo ya kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi kwa uelewa wangu na Kamati yangu endapo mtu ana matatizo ya afya ziko taratibu za kisheria za kumwachisha kazi na kumpa stahiki yake. Kwa hiyo, taratibu hizi hazifuatwi na hao wenye migodi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali na hii naamini kabisa Waziri mhusika yuko hapa atanielewa, atasikia kwamba Serikali sasa jambo hili limekuwa ni la muda mrefu, linajirudiarudia, muende kule. Badala ya wale waathirika 55 kutoka Kahama kuja hapa, ni vizuri sisi Serikali tutoke hapa tuwafuate huko ili twende tukakae na mwekezaji, tukae na hao waathirika ili kuweza kubaini tatizo ni nini ili Serikali iweze kuchukua hatua na kama watu hao wana haki zao waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti nalisema hili kwa sababu inajengeka dhana kwamba sasa hivi wawekezaji hao wanakuwa na nguvu kuliko Serikali. Mheshimiwa Waziri amesema hapa migogoro hii iende OSHA na CMA lakini ziko changamoto katika utatuzi wa hiyo migogoro huko CMA, migogoro inachukua muda mrefu haitatuliwi. Kwa hiyo, hawa wafanyakazi wa migodini wanakata tamaa. Kila siku tukifanya vikao vya Kamati wanakuja kueleza Kamati hapa. Jana tumewapokea, leo tumekuwa nao wafanyakazi 55 na hii si mara ya kwanza. Kwa hiyo, Serikali hili ilichukulie kwa uzito wa hali ya juu. Waziri na Serikali ielekee kule ili kuweza kujua kiini cha tatizo na kuchukua hatua zinazostahili.

5 FEBRUARI, 2015

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ambayo Mashirika haya Hifadhi ya Jamii yanaidai Serikali, kwenye Maoni na Mapendekezo tumependekeza na niliamini Waziri wa Fedha angeweza kusimama kutolea ufafanuzi, maana yeye ndiyo mwenye fedha. Wenzetu wanatuambia mbele ya Kamati kwamba, Miradi yao yote waliyopanga kuifanya hawawezi kuitekeleza kwa sababu Serikali haijatao fedha. Kama Mradi wa Daraja la Kigamboni, Serikali iliahidi asilimia 40, imetoa asilimia sifuri, maana yake asilimia mia moja yote inafanywa na NSSF. Maana yake ni kuwa, fedha za Wanachama wa NSSF sasa ndizo zinazotumika kuwekeza, sasa wanapostaafu wenyewe watalipwa nini? Nia kubwa ilikuwa uwekezaji huu uongeze fedha kwenye Mifuko hii ili wafanyakazi wanapostaafu, Wanachama wao waweze kupata maslahi yaliyo bora zaidi na mafao mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, fedha hizi shilingi bilioni mia nane kumi na moja na kwa kuwa Serikali mliafikiana na Taasisi hizi kulipa bilioni mia tatu na moja mwaka 2014, leo 2015, kuwalipa PPF bilioni 236, nafikiri hatua za makusudi zichukuliwe na Serikali katika kulimaliza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, kwa kujadili Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Naomba nimtambue Mheshimiwa Susan Lyimo, alichangia lakini sikumtambua wakati ninatambua wale wachangiaji. Mheshimiwa Susan Lyimo tunamshukuru kwa mchango wake ambao aliuleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyaeleza hayo, ninaomba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti, umejibu na nakupongeza sana kwa majibu yako.

Sasa namwita Mheshimiwa Halima Mdee!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimeleta mapendekezo ya marekebisho ya Kifungu cha 3(2) cha Mapendekezo ya Kamati, ninaomba yasomeke kama ifuatavyo:-

"Kwa kuwa wanawake ni kundi muhimu sana katika shughuli za kiuchumi hapa nchini; na kwa kuwa Benki ya Wanawake ilianzishwa ili kuwawezesha wanawake kupata mikopo kwa riba nafuu kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara zao; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa ahadi ya Serikali kuchangia jumla ya shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo; na kwa kuwa Benki husika hadi sasa imeshindwa kujiendesha kibiashara kwa sababu haijakidhi matakwa ya Benki Kuu kutokana na kukosa mtaji; hivyo basi, Kamati inapendekeza Serikali itekeleze ahadi hiyo ya Rais kabla ya Mkutano wa Bunge wa kujadili Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2015/2016."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta pendekezo hili kwa sababu Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Maendeleo ya Jamii amezungumza kwamba, ahadi hii ya shilingi bilioni kumi ilitarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano. Sasa taarifa zinatonyesha miaka miwili ya kwanza, yaani 2010/2011 na 2011/2012, ndicho kiasi cha bilioni mbili mbili kilitolewa. Baada ya hapo, miaka iliyofuata, 2012/2013 ilitolewa bilioni 1.3, 2013/2014 ilitolewa milioni 450 na 2014/2015 hakijatolewa kitu. Rais aliyetoa ahadi ndiyo muda wake unaisha. Wakati huo huo Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii ambaye ni Mwenyekiti wa UWT na mimi hapa nikiwa Mwenyekiti wa BAWACHA Taifa, amesema kaulimbiu ya mwaka huu ya Siku ya Wanawake ni Uwezeshaji wa Wanawake Tekeleza Wakati ni Sasa. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Tukiwa katika mchakato huo, naomba *commitment* ya Serikali, kwa sababu katika bilioni kumi, *balance* ni bilioni 4.25 tu, *iji-commit* hapa kwamba, kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha na kabla hatujaanza mwaka mwingine wa fedha, hiki kiasi kiwezeshe kwa Benki yetu ya Wanawake ili iweze kusogea kama ambavyo kaulimbiu ya mwaka huu inasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu nimeyaboresha, yanafanana kabisa na Mapendekezo ya Kamati, ila nimeweka *deadline*, kwa sababu tukiacha ombwe tunawapa fursa kutokutekeleza wajibu wao ipasavyo. Nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimepokea marekebisho yake, lakini na mimi nataka niweke marekebisho. Nakubaliana na unayoyasema kwamba, tunastahili sasa kulipwa, lakini kwenye sentensi inayoanzia hivyo basi Kamati inapendekeza Serikali itekeleze ahadi hiyo ya Rais kabla ya Mkutano wa Bunge. Mimi nasema tuandike hivi; hivyo basi, Kamati inapendekeza Serikali itekeleze ahadi hiyo ya Rais kabla ya kuanza kwa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2015/2016. Hili ni pendekezo lakini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, imekaa vizuri.

MWENYEKITI: Okay, kwa hiyo, sina haja ya kuwahoji wameshaelewana wadau. Ya pili?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaleta mapendekezo ya pili ya kufanya marekebisho ya Pendekezo Namba 3.3 la Kamati. Kimsingi, tunazungumza lugha moja ila nimefanya maboresho ili lieleweke vizuri zaidi, naomba isomeke kama ifuatavyo:-

5 FEBRUARI, 2015

“Kwa kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana ulianzishwa kwa mujibu wa Azimio la Bunge lililopitishwa mwezi Agosti mwaka 1993, kwa mujibu wa Kifungu cha 17(1) cha Sheria ya *Exchequer and Audit Ordinance Cap. 439 (No. 21)* ya 1961, kama mkakati wa kuwezesha makundi muhimu katika kujenga uchumi wa nchi; na kwa kuwa Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge za LAAC na TAMISEMI zimekiri kwamba, azimio hili limekuwa halitekelezwi na Halmashauri zetu kwa kiwango kilichotarajiwa; hivyo basi, Kamati inapendekeza Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) iziagize Halmashauri zote zilizokuwa hazitengi pesa husika, kuhakikisha zinatenga fedha kwa wakati;

(ii) katika kila mwaka wa fedha, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kusimamia Halmashauri ambayo ni TAMISEMI, atoe taarifa Bungeni juu ya utekelezaji wa azimio hilo; na

(iii) Halmashauri zinazodaiwa zilipe malimbikizo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, namba ya kwanza haipo, umeleta *amendment* mbili tu. Umeleta ya hivyo basi, Kamati inapendekeza Serikali ifanye yafuatayo:-

Iziagize Halmashauri zote kila mwaka Waziri mwenye dhamana atoe taarifa Bungeni juu ya utekelezaji wa azimio hilo; na ya pili, Halmashauri zinazodaiwa kulipa malimbikizo ambayo zinadaiwa. *Those are the only two amendments* ambazo umeleta na *much as* una hamu, lakini *I am sorry* ni hizo mbili tu ndizo zitajibiwa na Serikali. Kanuni zetu ndiyo zinavyosema, hata kisheria, wewe ni *lawyer*, hauwezi kupeleka ushahidi ambao tayari umeshafungwa. Kwa hiyo, endelea kwa hizo mbili tu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilifanya maboresho kwa sababu kulikuwa kuna *typing error*, kwa hiyo, hata ukiisoma hiyo ya kwanza inakuwa kama kuna sentensi mbili kwenye moja, ndiyo

5 FEBRUARI, 2015

maana nikazitenganisha ili ziweze kueleweka, lakini *concept* zilikuwa hizo tatu nilizoielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona tutengeneze mazingira ambayo tutailazimisha Serikali iweze kuji-*commit* na Waziri mwenye dhamana anayesimamia masuala ya Serikali za Mitaa, aweze kusukuma na kuzilazimisha Halmashauri ziweze kutenga pamoja na Madiwani vilevile huko chini kuona wana *commitment* ya ziada, kwa sababu kuna taarifa ambazo zitatakiwa ziletwe Bungeni.

Ukiangalia Taarifa ya Waziri wa Vijana, amezungumza kabisa hapa kwamba, kati ya Halmashauri 158, ni Halmashauri 38 tu ambazo zinatenga fedha na hizo Halmashauri 38 hazitengi kwa kiwango cha asilimia kumi. Vilevile Taarifa ya LAAC ilisema, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, makusanyo ya ndani ya Halmashauri kwa mwaka yalikuwa shilingi bilioni 970. Kwa hiyo, asilimia kumi katika hicho kipindi cha miaka mitano, ilitakiwa bilioni 97 ziende kwenye Mifuko ya Vijana na Akina Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeona nilete pendekezo hili kuboresha Mapendekezo ya Kamati, lakini vilevile kuifanya Serikali ione kwamba, inawajibika kufuatilia, hali kadhalika Bunge, Madiwani na Halmashauri zetu. Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Serikali nani anajibu; Waziri wa TAMISEMI au Mheshimiwa Kabaka?

KUHUSU UTARATIBU

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka nijifunze kutoka kwako kuhusu utaratibu, kwa sababu Mheshimiwa Halima anafanya *amendment* kwenye Mapendekezo ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, lakini ukiwahoji Wadau hivi huwa mtoa hoja mwenyewe hatakiwi kuonyesha msimamo wake katika jambo hilo?

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtanda utapata nafasi yako tulia, usiwe na haraka utapata tu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kuhusu utaratibu, lakini najua Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), anayo maelezo ya kutosha katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, jambo moja likishafanyiwa maamuzi haliwezi kurejewa tena kufanyiwa maamuzi. Wakati tukifanya mjadala wa Kamati ya Bajeti, Kamati ya LAAC na Kamati ya PAC, jambo hili lilijitokeza kwa kiasi kikubwa na Bunge lako Tukufu lilishafanya maamuzi kuhusiana na jambo hili la michango ya Halmashauri kwenda kwenye Mifuko ya Vijana na Mifuko ya Wanawake. Tulifanya maamuzi kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Sasa mimi ninaomba mwongozo wako, kama tulikwisha kufanya maamuzi katika jambo hili na tayari Bunge hili lilishapitisha katika Mkutano huu huu maamuzi yake; je, leo tunafanya maamuzi tena mengine kuhusu jambo hilo moja; na kama ndivyo sasa Serikali utekelezaji wa maamuzi hayo utaenda kuyaangalia mapendekezo hayo kwa mujibu wa maamuzi yaliyokwisha kufanywa wakati wa kupitisha mjadala wa mwanzo ama mjadala huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Halima Mdee!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia aliposema Bunge lilifanya maamuzi angesema lilifanya maamuzi *specifically* yapi. Tunazungumzia Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ambayo katika kipengele cha 3(3) ambayo mimi nimependekeza kuboresha tu imesema; Kamati inapendekeza kuwa Halmashauri zote nchini ambazo hazitengi asilimia 5 ya wanawake na asilimia 5 vijana, ziorodhweshwe na zichukuliwe hatua kali.

5 FEBRUARI, 2015

Sasa kama Mheshimiwa Jenista Mhagama anasema, kwa kuwa kwenye Kamati zilizopita tulifanya maamuzi, vilevile aseme katika maandiko yote hapa yaliyoandikwa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii yanayohusiana na asilimia zile kumi; tano vijana, tano wanawake; yafutwe. Mapendekezo hayo yakifutwa mimi sitakuwa na haja ya kuleta maboresho ya mapendekezo.

Nimeleta maboresho ya mapendekezo kwa kuwa mapendekezo yameletwa. Sasa atusaidie aseme tuliamua nini ambacho kina-*conflict* na hiki nilichokipendekeza *then* Kiti chako kitaamua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hebu tusaidie na wewe mwenye hoja.

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui unanitaka nisaidie kwenye jambo gani; Kamati ya Maendeleo ya Jamii inawajibika kuangalia Halmashauri zetu na asilimia 5 za wanawake, asilimia 5 kwa vijana; na kwa kuwa Kamati imejifunza kwamba hakuna fedha hizo, Halmashauri nyingi hazitengi fedha hizo na ndiyo maana tukaja na mapendekezo?

Kwa hiyo, kama Kamati nyingine ilijadili na kutoa mapendekezo juu ya jambo hili, hekima ya kawaida tu, hatuwezi kufanya maamuzi ya namna mbili tofauti katika jambo moja. Kwa hiyo, endapo Serikali ingeieleza Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba jambo hili tayari yameshafanyika maamuzi, Kamati ingeweza kuondoa jambo hili. Kwa kuwa hakuna kitu cha namna hiyo, bado sisi tuko katika mstari ule ule ambao tunaamini tulikuwa katika mstari sahihi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo tatizo lililokuwepo hapa Mheshimiwa Waziri ni *to walk the talk*; maamuzi yamefanywa lakini hayatekelezwi. Sasa hoja ya Mheshimiwa Halima tumwombe huo uliosema ushauri kuwa Serikali ilishafanya maamuzi; sasa lini utekelezaji utanza? Halmashauri hizi

5 FEBRUARI, 2015

haziwasikilizi na kwa vile haziwasikilizi vijana na akina mama hawapati haki ambayo Serikali inataka wapate.

Sasa tueleze majibu ya Serikali, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mapendekezo ambayo anayapendekeza Mheshimiwa Mdee, anataka tuziagize Halmashauri zote kuwa kila mwaka Waziri mwenye dhamana atoe taarifa Bungeni juu ya utekelezaji wa azimio hili. Kutoa taarifa mimi sidhani kama ni tatizo, tutatoa taarifa na suala la Halmashauri zinazodaiwa malimbikizo, kwa sababu hizi pesa zinatokana na makusanyo ya ndani ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha.

Mimi nadhani mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati ya LAAC, naona yanajitosheliza zaidi ambayo yalisema; Kamati inapendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), ichukue hatua za Kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote ambao kwa namna moja au nyingine, walihusika na kutokutekelezwa kwa agizo hili la kisheria la kutenga kiasi cha asilimia kumi ya fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani kuwezesha Mfuko wa Wanawake na Vijana. Badala ya hili la kusema itoe malimbikizo. Tutaziagiza zitalipa malimbikizo yanayotokana na kile walichokikusanya.

Nilichotaka kukisema ni kwamba, sisi kama Wabunge, tuna nafasi katika vikao vyetu vya Kamati ya Fedha, kuhakikisha kila mwezi tunapokwenda kwenye Kamati ya Fedha tuulize pale je, mwezi huu. Kamati ya Fedha ni kujadili mapato na matumizi kila mwezi; je, ni mara ngapi tumeenda kule tukauliza mwezi huu katika hizi tulizokusanya ngapi zinaenda katika Mfuko wa Wanawake na Vijana?

Badala ya kusubiria hapa, mimi nina imani kabisa haya tunayoyasema hapa tungekuwa tunasema kwenye vikao vyetu, kwenye mabaraza yetu, Halmashauri zote zingekuwa zinatoa hiki kiasi kinachotakiwa. (Makofi)

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri, umelieleza vizuri sana. Suala la Halima, Serikali imekubali, taarifa ya kila mwaka kama unataka wataileta. Vilevile wewe na mimi ni Wajumbe wa Halmashauri zetu na hizi pesa siyo za Serikali, hizi pesa ni za *own source*, makusanyo yetu wenyewe ya ndani ambayo Serikali wanawa-*eyes on hands off*. Kwa hiyo, hili suala ni *strictly inhouse issue* ya Halmashauri. Sasa serikali imekubali hilo, wataleta taarifa kutusaidia. Hili la pili nakuomba tu ulifanye liwe *redundant*.

Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, kwa sababu pendekezo ambalo lilipitishwa na LAAC lilikuwa linazungumzia hatua za Kisheria na kinidhamu, mimi sina tatizo nalo kabisa. Kitu ambacho ninakizungumza hapa na ambacho Waziri wa Vijana amekiri na ambacho mimi na wewe tunajua kwenye Halmashauri zetu tunafanya na bado havitekelezeki, ndiyo maana tumesema likitoka agizo la Bunge, Waziri akitakiwa afuatilie kwa Watendaji wake kule chini, tukizitaka Halmashauri ambazo zilitakiwa ndiyo kwa makusanyo hayo ya ndani watoe asilimia tano, tano, lakini hawatoi, maana yake hizi Halmashauri zinadaiwa fedha kwa ajili ya haya makundi mawili.

Kwa hiyo, hoja yangu hapa ni nyepesi tu kwamba; tukizitaka Halmashauri ambazo zilikuwa hazitoi zilipe malimbikizo, wanaweza wakaamua katika kila bajeti ya mwaka, kuangalia miaka kumi iliyopita ama mitano iliyopita, kutegemeana na kiwango kama walikuwa wanatoa asilimia kumi ama laah, waamue ni kiwango gani watalipa kidogo kidogo kufidia lile deni la nyuma ili tuweze kutunisha hii Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo dhana yangu tu. Hilo la kisheria sina tatizo nalo na nakubaliana nalo kabisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Waziri kajieleza vizuri tu, Serikali imetoa Sera kwa Halmashauri, watu wa kusimamia hii ni sisi, mimi na wewe Madiwani. Sisi tunatakiwa tuhakikishe kwenye Kamati ya Fedha (*Finance*

5 FEBRUARI, 2015

Committee), Mkurugenzi kabla ya bajeti, bajeti hii Halmashauri yako imepita na wewe umesema ndiyo; mbona hamkuhoji hili suala la pesa za vijana?

Sasa mnataka kuleta *politics* hapa za kuonyesha *the shortfall* ya Serikali *which I would not agree*.

Mheshimiwa Halima, Serikali imejiweka vizuri tu, wale wote ambao wana upungufu watachukuliwa hatua na yako kwenye mapendekezo ambayo tunayapitisha. Wewe yafuatilie mapendekezo baada ya kupita hapa uwaoneshe wale wote waliozembea na sisi Bunge tutakusaidia.

Sawa Mheshimiwa Halima? Tukubaliane yaishe tuondoke. Nakuomba wewe ndugu yangu wa Dar es Salaam. Limekwisha nakushukuru. (*Kicheko*)

La mwisho Mheshimiwa Halima maana ulikuwa na *amendment* nyingi au na hili nalo limekwisha?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mwisho ni dogo na linaendana na mapendekezo ya Kamati 3.10 na 3.11. Nimeyajumuisha kwa pamoja na lengo ni kupata *commitment* ya Serikali, kwa sababu yamezungumzwa mengi sana kuhusiana na hii Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii; ni kweli inafanya kazi kubwa ya uwekezaji. Sisi kama Wabunge tunataka Mifuko hii iendelee kuwa hai ili iweze kuisaidia Serikali katika uwekezaji, lakini vilevile isaidie pensheni kwa wazee wa sasa na sisi wazee wa baadaye. Sasa ninapendekeza 3.10 na 3.11 zisomeke kama ifuatavyo:-

“Kwa kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa na mchango mkubwa katika shughuli za uwekezaji nchini; na kwa kuwa madeni haya yamekuwa sugu kwa kipindi cha muda mrefu, hali ambayo inatishia uhai wa Mifuko husika; hivyo basi, Kamati inapendekeza Serikali iwe imelipa madeni ya Mifuko kama ilivyokubaliana na Mifuko husika, kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2015/2016.”

5 FEBRUARI, 2015

Ninazungumza haya kwa sababu Kamati imezungumza, kulikuwa kuna *deadline* ya Serikali tarehe 14 Novemba, 2014 haijatekelezwa mpaka sasa. Tusipoweka *deadline* inawezekana mwaka huu wa fedha ukaisha tukaanza mwaka mwingine wa fedha ukaisha. Kwa hiyo, ninachohitaji ni *commitment* ya Serikali ndani ya huu muda ambao muda wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete unaisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha sijakuita bado.

Nami nilitaka kusema kukopa harusi kulipa matanga. Anayesema nani; Waziri wa Fedha au Waziri wa Nchi? Anataka *commitment* hii ya 2015/2016 sijui mtatuambia nini?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Pendekezo la Mheshimiwa Halima siyo baya na amekuwa akionyesha *concern* kama zilivyokuwa zikioneshwa na Wabunge wengine. Kuweka hii *deadline* kwamba, kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2015/2016, nadhani *is just too soon*. Kwa sababu sisi tunaelewa na hili deni lenyewe vilevile *is a concern* kwetu, lakini kuna *process* za kwenda kupeleka likaridhiwa na Serikali jinsi gani italipa haya madeni. Kwa sababu siyo tu kwa *NSSF* na *PPF*, lakini katika Mifuko mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyokuwa imewekwa na Kamati iko vizuri zaidi kuliko Mheshimiwa Halima anavyotuwekea kwamba, lazima tuwe tumelipa kabla ya Mkutano wa Bajeti. Kwa hiyo, tunachukua kwa sababu tuko kwenye *process* ya kuendelea kulipa, lakini *its constrain* ni *deadline* ambayo ametuwekea Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, mimi naomba tuchukue hii ya Kamati.

MWENYEKITI: *Commitment* ya Serikali ni kuwa mndalifanyia kazi, mtazungumza na wahusika na pesa zao mtawalipa.

5 FEBRUARI, 2015

WAZIRI WA FEDHA: Kabisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala lilijadiliwa kwa kina sana wakati wa Taarifa ya PAC. Hili suala limezungumzwa hapa na Kamati ya Huduma za Jamii na wamesema kama ambavyo PAC ilisema kwamba, katika bilioni 811 za NSSF, Serikali iliji-*commit* kulipa shilingi bilioni 301, hali kadhalika kwa PPF ambayo inadai bilioni 236. Serikali ilishakaa vikao na hawa wahusika, ikafanya uchunguzi wote ikasema tutalipa hizi fedha tarehe 14 Januari, 2014.

Sasa hivi ni tarehe 5 Februari, 2015. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisaidie; anasema hii *deadline* ina utata, unadhani muda gani unakutosha wewe kuweza kulipa hizi fedha za hii Mifuko lakini zaidi kuokoa wanaochangia na kulinda Mifuko yetu? Ama uniambie hii Taarifa ya Kamati, ukurasa wa 31, inayozungumzia kikao chenu cha tarehe 14 Novemba, 2014 ni ya uwongo. Ukiambia ni ya uwongo *then* mimi sitakuwa na tatizo.

Aseme muda wake tu hata akisema miaka miwili poa. Nataka nisikie *commitment* yake maana naona anataka kuleta ... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti!

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninanyoosha kwa ajili ya masuala mengine. Kwa kuwa ulimwita Waziri, naomba Mheshimiwa Waziri aendelee.

MWENYEKITI: Kwa hiyo haupo kwenye hili, ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina tatizo na Taarifa ya Kamati kuhusiana na vikao hivyo, vimefanyika. Uamuzi wa Serikali ni kwamba, deni la Mifuko

5 FEBRUARI, 2015

ichukuliwe yote kwa pamoja na twende kuangalia utaratibu gani madeni haya yatalipwa. Basi, huo ndiyo ulikuwa uamuzi wa Serikali na ndiyo maana sasa tuko kwenye *process* kwa ajili ya kuamua sasa hili deni lote la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii litalipwaje. Kwa hiyo, siwezi nikakwambia ni baada ya miaka miwili au mitatu, inawezekana kesho, inawezekana baada ya saa mbili.

Ninachotaka kusema ni kwamba, sisi tuko katika *process* na *commitment* ya Serikali iko pale pale ya kulipa madeni haya ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Halima, Serikali imeshaweka *commitment*, walikutana mwaka jana walitaka kulipa, kama unakumbuka mafuriko, mimi na wewe tuliomba bilioni 50 Dar es Salaam, barabara za kwako ziliharibika, barabara za nchi nzima ziliharibika. Mimi sitaki kuitetea Serikali, lakini ukweli ndiyo huu, *commitment* ya Serikali ni hiyo, *they are ready to pay* na ni lazima walipe. Bunge hili litasimamia haki, kwa sababu hizi pesa siyo za NSSF au Mifuko, ni pesa za Wanachama na Bunge tuna wajibu wa kuwasimamia Wanachama.

Serikali iliingia kidogo katika *act of God* wanaita watu, hawakutegemea mafuriko yale na madaraja kuanguka kule Ununio na maeneo mengine. Kwa hiyo, mimi nafikiri Mheshimiwa Halima tukubaliane na Serikali, *commitment* imeiweka, tuwape muda, tuendeleo kuwafuatilia wote Bungeni kujua lini watalipa ili kila mtu iwe *win win situation* ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Halima, nakuomba na kwa hilo nakushukuru. Nataka watu kama hawa, kidogo ukimweleza anaelewa. Ahsante sana Mheshimiwa Halima. (Kicheko)

Mheshimiwa Jafo!

5 FEBRUARI, 2015

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeleta mapendekezo ya kuongeza pen데kezo lingine baada ya ile 3.11 tupate pen데kezo lingine namba 3.12. Pen데kezo langu hili linasomeka kama ifuatavyo:-

“Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa wafanyakazi wanaopata athari wakiwa kazini katika makampuni ya migodi ya madini hapa nchini, hususan Mgodu wa Bulyankhulu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapen데keza kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge, itakayokuwa na jukumu la kuchunguza mazingira ya kazi na athari mbalimbali walizozipata wafanyakazi walioachishwa kazi kutokana na kupata ugonjwa uliosababishwa na mazingira ya kazi katika Mgodu wa Bulyankhulu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hata Mwenyekiti wa Kamati amezungumzia kwa kirefu sana hapa. Nami nizungumze wazi kwamba na mimi nilikuwa mdau mkubwa sana, nilifika katika Mgodu wa Bulyankhulu na nilifika pia Mgodu wa North Mara, nimekutana na wafanyakazi wengi sana. Ukiachia suala hili kuna suala la kuwa-*blacklisted* watu ambao wameonekana wameathirika na wanaonekana hawawezi kupata kazi sehemu nyingine yoyote.

Watu hawa leo hii kuna wengine wamekuja hapa hata kusikia kwao ni kwa shida wanatumia mashine; hali kwa kweli ni mbaya sana. Kwa hiyo, kama Bunge naomba tuwe sauti ya watu wanyonge. Bunge kama chombo ambacho wananchi wamekipa matumaini makubwa, lazima lisimame katika kutetea haki za hawa. Kwa hiyo, ndiyo maana nimepen데keza kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge, ambayo itaenda kukutana na wafanyakazi kubainisha ni yapi yanayoendelea. Ukiona mfanyakazi mpaka anakuja hapa Bungeni na anahangaika, maana yake kuna makubwa yanawapata huko wanakofanyia kazi. Kwa hiyo, mantiki ya pen데kezo langu ni hilo na ninaiomba sana Serikali ikubaliane nami kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Ahsante. Serikali; Mheshimiwa Waziri wa Kazi!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru na naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo, kwa *concern* yake kubwa sana na wafanyakazi hao wa migodini.

Nilifikiri pia nitumie nafasi hii kabla sijazungumzia hili suala, ninyooshe kitu kimoja tu ambacho Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati alikizungumza pale mwisho, kwa ajili ya kuweka mambo sawa; ni hili suala la uwekezaji ambalo Mifuko inafanya kwamba ni pesa za Wanachama. Hili ni kweli lakini uwekezaji ni lazima katika Mifuko hii, kwa sababu pesa usipowekeza ukaizalisha, *inflation* ikija inaipiga inakwisha. Kwa hiyo, wanawekeza kwa ajili ya kuhakikisha wanalinda *inflation* ya pesa yao. Niwataarifu tu kwamba, katika uwekezaji huu wanapata miongozo kutoka Benki Kuu na kutoka *SSRA* na hawawekezi zaidi ya asilimia walizowekeza katika miundombinu na maeneo mengine.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri unajibu nini?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Nilikuwa naweka hilo sawa. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimeshaliweka sawa naomba niende kwenye...

MWENYEKITI: Tulishakubaliana, Bunge likishafanya maamuzi haturudii tena na ninyi ndiyo Serikali mnasema hilo. Jibu hili la Jafo. (*Makofi*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, ninamshukuru sana Mheshimiwa Jafo, kwa *concern* yake. Naomba niseme hivi; nimesema wafanyakazi hawa kwanza wanatakiwa wapate barua kwamba wamefukuzwa kutoka kwenye migodi. Barua ile wanaenda nayo *OSHA*, *OSHA* inachofanya ni kuwapima, kitu kinachoitwa *exit medical examination*. Wakishapimwa, *OSHA* wanatumia Wataalam ambao wanahusika na masuala ya *occupational health hazards*. Wakishagundua

5 FEBRUARI, 2015

kwamba wamepata matatizo kutokana na ajira zao, inatakiwa sasa mwajiri aanze kuwatibu. Tatizo linalotokea wafanyakazi hawa hawachukui barua kule, wanatumia labda nafasi nyingine na wadau wengine kusema sisi tumefukuzwa kwa sababu tunaumia au tumeumia kazini; lakini ili tujue kama wameumia kazini wapewe barua inayoonyesha kwamba wamefukuzwa kutokana na kuumia kazini. Kwa sababu ni kosa la jinai kumfukuza mfanyakazi kwa kuumia kazini.

Kwa hiyo, nasema hii Kamati inayopendekezwa, kwanza, inasemekana itakuwa inachunguza mazingira ya kazi na athari mbalimbali wanazozipata. Kamati hii ya Bunge haitakuwa na utaalim wa kuwapima hawa wafanyakazi, kwa hiyo, hawawezi kujua athari za magonjwa au maumivu waliyonayo kwa sababu hawana utaalim wa magonjwa haya yanayotokana na kazi. Kwa hiyo, nilifikiri waachie hii kazi iendelee na OSHA na *afferall* sasa hivi tumeanzisha Mfuko wa Wafanyakazi Wanaoumia Kazini. Sasa hivi waajiri wote hawatakiwi kuwatibu, wanatakiwa kuchangia Mfuko huu ambao namshukuru Mheshimiwa Rais, ameshatuchagulia Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji na mimi nimeshachagua Bodi, kwa hiyo, Mfuko umeanza.

Mfuko huu sasa ndiyo utakuwa na kazi ya kuhakikisha unaratibu mahitaji ya wagonjwa wote ambao wanaumia kazini, ikiwemo kufanya hizi kazi ambazo Mheshimiwa Jafo amezitaja. Kwa hiyo, pamoja na *concern* yake, mimi nafikiri kwanza Kamati hii kuingia kwenye mgodi itakuwa siyo rahisi kwenda kuangalia athari na kuangalia mazingira. Kwa hiyo, nashukuru kwa *concern* yake, lakini nafikiri kazi hii OSHA wataifanya vizuri kama wanavyoendelea kuifanya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: *Concern* ya Mbunge ni *very valid* na mpaka ameisema, tayari ameletewa malalamiko ya wadau ambao wamepata athari. Hiyo OSHA inaonekana iko *incompetent*, haifanyi kazi inavyotakiwa ifanye, ndiyo maana Mbunge analeta hoja hii. Nakubaliana na wewe, kuweka

5 FEBRUARI, 2015

Kamati Teule itakuwa *very difficult* kwa sababu Wabunge ni wachache sana ambao wana uwezo wa kutambua taaluma ya kidaktari. Vilevile Mheshimiwa Jafo, labda hili nalo tuiombe Kamati ya Maendeleo nayo iwe *zero distance* na hao OSHA, kuweza kujua maendeleo na maradhi na ugonjwa wa watu wetu; kwa sababu masuala ya migodi kuna *issue* ya *ku-decommission* hii migodi.

Mimi sijaona hata kama mna utaratibu wa kuweka bajeti ya *ku-decommission*, *uki-decommission* mgodi ina maana hata wale wafanyakazi wa migodi wanapimwa na kutibiwa na kupata fursa ya kujua afya zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo, unakubali kuwa hili Kamati watalichukua wenyewe, watakwenda watalifanyia kazi, watakaa na OSHA na kujua na *ku-zero in* kwa wagonjwa ambao wapo na kushirikiana na OSHA kujua hali zao za kiafya na tuhakikishe wanapona.

Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuelezea hayo, lakini naomba kuzungumza machache kwanza.

Naomba kama OSHA, kama nani, kwanza lazima wawe na uchungu na maisha ya Watanzania; hili ndiyo jambo la msingi sana. Kwa sababu inawezekana tunasema tuna taasisi lakini haifanyi kazi kwa kadiri inavyotakiwa. Kuna watu wengine ambao sasa hivi wanatakiwa kwenda India, lakini wako hapo wanakufa na watoto wao wanawaangalia. Hili jambo linatia uchungu. Mmi naomba pendekezo langu nilifanyie marekebisho kama Mwenyekiti utaridhia, kwamba; ikiwezekana sasa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, licha ya kufanyika lakini Kamati ya Maendeleo ya Jamii, iunde kikosi kidogo japo hata kwenda kuwasilikiza *concern*. Tuulizane ni watu wangapi wa Serikali wameenda kuwafuata kule migodini kusikiliza matatizo ya wafanyakazi? Ni wangapi hapa tuulizane au tupo maofisini jamani?

5 FEBRUARI, 2015

Ni watu wangapi ambao tunasema wamekaa ofisini wanakula mishahara wameenda kuwasikiliza wafanyakazi wanaoteseka?

Nalisema hili kwa chungu, kwa sababu kipindi kile nilizungumza suala la *jeotropha* kule wafanyakazi wangu Kisarawe ambao wengine mpaka walipoteza urijali, lakini hakuna vyombo vilivyoenda kufuatilia kule. Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi nina maslahi nalo, nina chungu nalo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunazungumza kwamba, ikiwezekana Kamati ya Maendeleo ya Jamii, iunde timu ndogo ya kwenda kuwasikiliza kujua hizo *concern* kwa undani kabisa lina ukubwa jambo hili kiasi gani. Jambo hili tutakuwa tumewatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hilo, lakini ikiwezekana Kamati ya Huduma za Jamii sasa iende kwa undani, iangalie mikakati yake, halafu Kamati hiyo katika Bunge la Kumi na Tisa ije kutupa taarifa nini walichokiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Nakupongeza sana Mheshimiwa Jafo, umezungumza vizuri sana kutetea maslahi ya watu wako, ni kama sisi Dar es Salaam tunavyotetea wale watu wetu, sisi hatuna migodi wala stakabadhi ghalani pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti!

MHE. SAIDI M. MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kusema maneno mawili, matatu. Nikubaliane kwamba, maoni na mapendekezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Halima Mdee, kimsingi ndiyo yale yale ya Kamati, yeye alichokuwa anakifanya ni kuweka katika lugha ya kisheria na kuweza vilevile kuweka *timeframe*.

5 FEBRUARI, 2015

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ya Halima tena yaache, usianze kuibua mambo, twende hili la Jafo. (Kicheko)

MHE. SAID M. MTANDA: Kuhusu jambo la Jafo, Kamati yangu inakubaliana na ushauri tulioutoa, tulitaka Serikali iende yenyewe kule, kwa sababu yupo Kamishna wa Kazi, OSHA hao wapo na barua za wale wafanyakazi na malalamiko yao yapo hapa na ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, tulichotaka kusema hapa na nitakabidhi kwenye meza yako nyaraka hizi kwamba, Serikali yenyewe kupitia Kamishna na Waziri, wapange utaratibu wa kufika huko mgodini.

Vilevile sikubali kwamba hatuwezi kufika mgodini, huko mgodini kuna nini? Migodi mingi tumeweza kuitembelea na tumeweza kuona hali za wafanyakazi na kuzungumza na menejimenti na wafanyakazi; kwa hiyo, linawezekana na Kamati yangu iko tayari kufanya hivyo. (Makofi)

MWENYEKITI: Sawa. Mheshimiwa Waziri, huna haja ya kujibu, Mwenyekiti ameshasema, mmeshakubaliana na wao watapanga ratiba kwenye kazi zao na hamuwezi kuwazuia ratiba za kazi zao. Mheshimiwa Jafo nafikiri umeridhika hatuna haja ya kuhoji hili. Hili lingine la 3.13? Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI SAIDI JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza pendekezo lingine la 3.13 ambalo linasomeka Mamlaka ya Afya na Usalama Kazini kuendesha zoezi la upimaji kwa wafanyakazi waliobainika kuathirika ili kujua kiwango cha athari ya kiafya kwa wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 27 Februari, 2013 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa na kikao na vyama vya wafanyakazi. Ilionekana kwamba kuna concern kubwa ya wafanyakazi hawa ambao

5 FEBRUARI, 2015

wameathirika kazini na ilitolewa maelekezo kwamba, ufanyike utaratibu wale watu kwenda kupimwa, bahati mbaya mpaka leo hii jambo hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo jipya, ni mwendelezo wa ajenda ileile ambayo hata Mheshimiwa Rais aliona kwamba ni jambo la msingi kwa ajili ya wananchi wake. Kwa hiyo, ndiyo maana nimeleta pendekezo hilo sasa, Bunge lipendekeze kwamba, hivyo vyombo vinavyotakiwa kwenda kupima wafanyakazi, japokuwa Mheshimiwa Waziri mwanzo alizungumza, lakini mpaka leo hii watu walikuwa bado hawajaenda kufanyiwa hiyo *checking*. Sasa nimependekeza hapa kama Bunge litoe kauli kabisa ya kupendekeza kwamba, wanaohusika na kwenda kufanya hiyo kazi, waende kufanya kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge kutoa kauli haina tatizo, lakini jambo hili nalifahamu. Unajua kilichokuwa kinatakiwa ni Chama cha Wafanyakazi *TAMICO*, wafanyakazi hawa wapitie kwa *TAMICO*, *TAMICO* ndiyo anakuwa *coordinator* wao kati ya mwajiri na *OSHA*. *OSHA* walishaandaa utaratibu wa kuwapima hawa wafanyakazi. Inavyoonekana, *TAMICO* na baadhi ya viongozi wa hao ambao waliachishwa kazi mwaka 2007, hawana mahusiano mazuri.

Sasa naomba niseme hivi, wafanyakazi hawa, *OSHA* ipo tayari kuwapima, naomba waende Dar es Salaam wakapime, kwa sababu wanaenda kwa ajili ya kupata sasa uhakiki kwamba walifukuzwa kwa ajili ya magonjwa, ile *exit medical examination*. Naomba waende *OSHA* wakapimwe na *OSHA* wako tayari kuwapima, lakini hata hawa ambao wanasema hamsini waende *OSHA* kwa sababu wengine wameshaenda, waende bila kupitia hata hicho Chama cha Wafanyakazi. Naomba Chama cha Wafanyakazi *TAMICO*

5 FEBRUARI, 2015

kiwe *coordinator* wa hawa wafanyakazi, kusudi isiwe mfanyakazi mmoja mmoja au *group* wanakuja kwa Waziri, wanaenda OSHA, bila utaratibu ambao tumeuzoea. Kwa hiyo, tuko tayari hawa wafanyakazi kwenda kupimwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jafo, nafikiri Serikali imekubali na Mheshimiwa Mwenyekiti ambaye ni Kamati yako pamoja na kutembelea migodi na hili muya-*accommodate* kwenye maazimio yenu na kwenye kazi zenu hizi zinazoanza ili kusaidia. Hii hoja ya Mheshimiwa Jafo ni muhimu sana, kusaidia siyo watu wa kwake tu *in-fact* ni maeneo mengi sana watu hawapati *attention*, mamlaka zipo, taasisi zipo, lakini *business as usual*. Kwa hiyo, nakuombeni basi mfanye hiyo shughuli.

Mheshimiwa Jafo tumeridhika?

MHE. SELEMANI SAIDI JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeridhika kwa ajili ya maslahi ya Watanzania na naomba kazi ifanyike kama tulivyokusudia.

MWENYEKITI: Nami nakupongeza sana kwa kulileta hili, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwamba, Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuanzia Januari, 2014 hadi Januari, 2015 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Nawapongeza sana Serikali kwa majibu yenu mazuri na Mawaziri wote. Nachukua nafasi kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wake, pamoja na wale wote waliotoa *amendments*; Mheshimiwa Halima na Mheshimiwa Jafo, mmefanya kazi nzuri sana. Vilevile

5 FEBRUARI, 2015

tushukuru na tumpungeze Dkt. Dau wa *NSSF*, kwa kuweka Chuo kile ambacho kitapunguza fujo, kitapunguza vijana kuzurura mitaani, watakuwa wanakwenda kufanya mazoezi ili na wao wapate ajira ya michezo.

Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana, najua hii ipo chini yako na wewe ni mdau wa *NSSF*.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo dogo tu hapa; Wabunge wote wanatangaziwa kwamba, kesho jioni, baada ya kuahirisha Bunge, kutakuwa na tafrija ya Wabunge wote kuukaribisha mwaka mpya, itakayofanyika katika eneo la maegesho ya magari. Wabunge wanaoegesha magari eneo hilo, wanaombwa wasiegeshe magari yao siku ya kesho kuanzia asubuhi ili kazi ya kupamba iweze kufanyika na kukamilika kwa wakati. Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28, Fasili Ndogo ya 12, Mheshimiwa Mrema amepewa Kibali cha Spika kutoa taarifa yake Bungeni. Mheshimiwa Mrema, maelezo binafsi!

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nitoe Maelezo Binafsi ya Mbunge wa Jimbo la Vunjo, Dkt. Augustino Lyatonga Mrema na hii Taarifa Binafsi ninaitoa chini ya Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianza kuugua Ugonjwa wa Kisukari tangu mwaka 1982. Mnamo mwaka 2009, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alinipeleka India kwa matibabu na Rais alitaka kujua kama kisukari kimenitafuna kwa kiwango gani. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Niligombea Ubunge katika Jimbo la Vunjo mwaka 2010 nikiwa na Ugonjwa huo wa Kisukari. Nilichaguliwa kuwa Mbunge na baada ya hapo niliendelea kuongoza na kulitumikia Jimbo la Vunjo nikiwa na tatizo la kisukari na

5 FEBRUARI, 2015

nimefanya kazi zangu za Ubunge vizuri. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge, kwa kunipeleka tena nchini India kwa matibabu zaidi ya kisukari mwaka 2013 na 2014, namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 nilirudi India kwa ajili ya vipimo na niligundulika kuwa nina saratani ya mapafu, ambapo Madaktari walinipa matibabu ambayo niliyatumia kwa kipindi cha mwaka mmoja na kujisikia nafuu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 Desemba, 2014, ulinipeleka tena India kwa ajili ya *check-up* ya saratani ya mapafu ili kuweza kujua hali yangu ya kiafya kwa ujumla inaendeleaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukutaarifu na pia kulitaarifu Bunge na Wananchi wa Vunjo kwamba, Ripoti ya Madaktari juu ya afya yangu imetoka na ninayo hapa. Inasema, nanukuu: *"In comparison with the previous pet scan dated on 10th July 2014, there is no recurrent metabolically active disease in the lung or elsewhere in the whole body survey."* Hiyo Ripoti nimeambatisha ipo, anayetaka kuona kuthibitisha ninayosema, Spika anayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 18 Desemba, 2014 nikiwa hukohuko India, nilifanyiwa *check-up* ya kipimo cha UKIMWI, yaani *Aids-HIV Test* na nikagundulika kuwa sina UKIMWI. Mungu ni mkubwa, Spika anayo hiyo taarifa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, nimeambatanisha taarifa kamili ya Ripoti yote ya Madaktari kutoka India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, wakati nikiwa India, Mheshimiwa James Mbatia, Mteule wa Rais, alinukuliwa na Gazeti la Mwananchi la tarehe 9 Desemba, 2014 kupitia mikutano yake ya hadhara katika Jimbo la Vunjo kutangaza kuwa, kwanza, ametangaza

5 FEBRUARI, 2015

Kampeni inayoitwa *Delete TLP*. Akisema ina lengo la kukifuta katika historia Chama cha *Tanzania Labour Party*, kinachoongozwa na Mrema. Nimeambatanisha habari hiyo kwenye gazeti hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Katika dhima yake ya ku-*delete TLP*, akisema ana lengo la kufuta *TLP*, huyu Mheshimiwa James Mbatia na wapambe wake ambao wamehamia kwenye Jimbo mpaka kwenye Kata na Vijiji, walikuwa wanawaeleza Wananchi wa Vunjo na wako tayari kuja hapa Bungeni kutoa ushahidi walionao kuwa, Mrema ni mgonjwa sana na ana UKIMWI, hivyo atakufa wakati wowote, ni marehemu mtarajiwa. *(Kicheko)*

Alikuwa anawaeleza Wananchi wa Vunjo kwanza kutochagua Wagombea wa Vijiji na Vitongoji kwa Tiketi ya *TLP* ambayo Mwenyekiti wake atakufa hivi karibuni. Mheshimiwa Mbatia na Wapambe wake, ambao zoezi wameligharimia kwelikweli, walikuwa pia wakipita kuhamasisha wananchi wakisema Ubunge apewe yeye kwani afya yake nzuri, Mheshimiwa Mrema ni mgonjwa wa UKIMWI na atakufa saa yoyote, hivyo, wachaguliwe wagombea kupitia Chama chake cha *NCCR-Mageuzi*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja aliye hapa ndani anafahamu kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi kwamba, kipindi au muda wa kampeni bado haujafika na wala Jimbo la Vunjo halijatangazwa na Serikali kwamba liko wazi. Sasa inakuwaje Mheshimiwa James Mbatia aanze Kampeni na tena ya kunidhalilisha, kunitukana mimi Mbunge halali wa Jimbo la Vunjo wakati muda wangu haujamalizika? Kitendo chake cha kuvamia Jimboni kwangu na kuzamia huko kwa lengo la kunichafua tu ni kuchochea vurugu Jimboni na pia kunizuia nisifanye shughuli zangu za Kibunge ndani ya Jimbo langu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kwamba, wapo watu wengi hapa nchini ambao ni wagonjwa wameathirika, lakini wanatekeleza majukumu yao ya kila siku. Hivyo, kitendo cha Mheshimiwa James Mbatia kutumia

5 FEBRUARI, 2015

porojo, propaganda hiyo ya uongo, kwa kuwaeleza wananchi nina UKIMWI na ninaweza kufa muda wowote, hii ni wazi kuwa Mheshimiwa Mbatia anatumia maneno haya ya uongo na ya uzushi, kama mtaji wake wa kisiasa; kwani anajua ikiwa nitakuwa hai, hawezi kupata Ubunge wa Jimbo la Vunjo, ndiyo maana anawaeleza kuwa nitakufa muda wowote kwa kuwa nina UKIMWI. Nataka kumwambia hafi mtu hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua wote hapa ndani tunajua kuwa kifo ni mpango wa Mungu. Leo hii Mbunge anakwenda kuwaeleza Wananchi kuwa Mbunge fulani ana UKIMWI na atakufa muda si mrefu; hivi kweli kwanza ni heshima hiyo? Ni jambo linalompendeza Mungu kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako, Wananchi wa Vunjo na Mheshimiwa Mbatia anatakiwa ajue kuwa, sasa kwa ushahidi nilioleta hapa Bungeni, ambao anao Spika, afya yangu ni njema na sina UKIMWI, atafute sababu nyingine. Nilikuwa na Saratani ya Mapafu na hivi sasa nimepona. Nitaendelea kufanya kazi zangu za Ubunge katika Jimbo la Vunjo na ninataka kuwahakikishia kuwa nitagombea tena Ubunge, maana huo ndiyo unaonitoa roho, ili kuhakikisha namalizia kazi zangu nilizokwishazianza kule Vunjo; kwa mfano, kuna lile Soko la Mataifa la Lokolova, Himo, nimeongea na Rai juzi, ameniambia ataweka jiwe la msingi mwezi wa tatu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nitaacha kuwashukuru tena wote waliohangaikia afya yangu. Wa kwanza ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Kikwete. Yule ni Rais, ni binadamu, ana utu. Usione tukimpenda Rais Kikwete bure, wakati wenzako wanangonjea ufe, lakini Rais yule anahangaika na watu kama alivyohangaika na mimi mwaka 2009 wala sikuwa Mbunge, ninamshukuru sana Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2015

Wa pili ni Mheshimiwa Anna Makinda, ni binadamu, ni mama kweli lakini ana utu, kila nilipopewa tarehe ya kurudi India aliniwezesha kwenda. Kwa hiyo, ninamshukuru sana.

Nawashukuru sana Madaktari wa Hospitali ya Dodoma hasa Dkt. Chaula, ni Mtaalamu wa Sukari. Wakati mwingine ameweza kuwashinda hata kule India, kuna Madaktari sawa, lakini nikiangalia nikirudi sukari yangu haipandi, nikiwa India inapanda, wale wameshindwa kudhibiti kwa upande wa sukari. Kwa hiyo, natumia *formula* ya Dkt. Chaula.

Nawashukuru sana Madaktari wa Muhimbili, Madaktari wa Agakhan, pamoja na wale wa Hospitali ya Apollo ya India, bila kumsahau mke wangu, mpenzi wangu, Rose Mrema; walikuwa wanamhamasisha mume wako ana UKIMWI, lakini ameendelea kuwa mvumilivu kipindi chote nilicholazwa India mpaka taarifa hii ilipotoka. Kwa hiyo, alivumilia matusi, kashfa na kejeli, yaliyokuwa yanatolewa kuwa nina UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe taarifa hii mbele ya Mwenyezi Mungu, aliyenisaidia kuwa hapa mpaka leo na wapiga kura wema, wachamungu wa Vunjo ambao wameendelea kuwa na mimi wakati huu mgumu, ninanyanyaswa, wako tayari kutoa ushahidi. Hayo matusi, hizo kashfa, walikuwa wanawapigia wanavijiji wangu kwamba huyo msimchague ni marehemu mtarajiwa na nimeathirika sana. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa yangu juu ya ugonjwa wangu. Naona hata aibu kusema mambo yanayonihsu ya kibinafsi, kutumia muda huu wa Watanzania wana matafizo mengi, lakini sina namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mrema, pole.

5 FEBRUARI, 2015

Kwa mujibu wa Kanuni zetu, maelezo binafsi hayajadiliwa wala hakuna nafasi ya kuyajadili, haya ni maelezo yake. Kwa niaba ya Bunge ninakupa pole, lakini nakuombea uzima na afya, Mungu akujalie, akupe umri mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.37 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 6 Februari, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*